Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 21 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante tukae. Katibu!

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2013 *[The Annual Report of Energy and Water Utilities Regulatory Authority for the Year Ended 30th June, 2013]*.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe.

Na. 95

**Mikataba ya Halmashauri Kuandaliwa kwa Kiswahili**

**MHE. MUNDE A. TAMBWE** aliuliza:-

Mikataba ya *BOQ* za Halmashauri huandaliwa kwa lugha ya Kiingereza hivyo kusababisha kutoeleweka na kuhoji vizuri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kuandaa mikataba na *BoQ* hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Munde Abdalah Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mikataba ya Makadirio ya Gharama za ujenzi *Bills of Quantity* katika Halmashauri huandaliwa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa sehemu kubwa maandalizi ya mikataba hiyo yanazingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 21 ya Mwaka 2004 kama ilivofanyiwa marekebisho mwaka 2011 ambapo Taasisi za Manunuzi *(Procuring Entities)* zinatakiwa kutumia mikataba *(Standard Contracts)* ambayo imeandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Regulatory Authority (PPRA)* na ambayo imeandaliwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa madhumuni ya kuyawezesha Mabaraza ya Madiwani kuhoji na kusimamia vyema mikataba ya Halmashauri. Ni vema mikataba hiyo ikawa inaandaliwa na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka vizuri na kuwawezesha Madiwani kuhoji vipengele mbalimbali ndani ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Mikataba na Sheria ndogo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilishaanza kutekeleza kwa kuanzia na Sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa la tarehe 19 Mei, 2010 kwa barua Kumb. Na. P./P/2/567/59 ambayo iliagiza kwamba Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ziandae Sheria ndogo zote kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) itashirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma *(PPRA)* kuhakikisha kwamba suala hili la Mikataba kuandaliwa na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili linafanyika ili kuwawezesha Waheshimiwa Madiwani kuielewa na kuweza kuhoji vizuri mikataba yote inayohusiana na *BoQ*.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inapeleka mabilioni ya shilingi za walipa kodi katika Halmashauri zetu na kwa kuwa Serikali inatambua uwezo wa Madiwani wa kusoma

lugha ya Kisheria ya kiingereza na lugha ya kitaalamu kwamba ni mdogo na kwa kuwa tumekuwa tukifuatilia suala hili mimi mwenyewe binafsi toka 2012 tukiomba *BoQ* hizi zitafsiriwe Kiswahili na majibu yanakuwa ni haya haya kama tuliyojibiwa leo. Sasa leo naomba *commitment* ya Serikali ni lini sasa itakuwa tayari wamesha tafsiri hizo *BoQ* na zitaanza kutumika kwa lugha ya Kiswahili?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa kwamba huyu Mbunge anayezungumza hapa amekuwa anafuatilia jambo hili kwa karibu sana. Ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kumpongeza sana kwa jitihada hizi. Sasa anachokisema hapa ni kitu ambacho wewe na sisi wote tuliokuwemo humu ndani tunakielewa kwa sababu lugha ya Kiswahili nimemsikia Rais akihutubia Bunge la Afrika kwa Kiswahili.

Sasa leo sisi wenyewe humu ndani halafu tukaanza tena kusema kwamba Kiswahili kisitumike unajua tulikuwa kwenye ukoloni wakati wa Kiingereza na nini. No! Mimi nasema kwamba *credit* hii tunaipeleka kwa Mbunge tunampongeza kwamba amefanya hivyo.

Mheshimiwa wakati alipokuwa anazungumza hapa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angela Kairuki alitoa *statement* ya Serikali hapa ikionyesha jinsi tunavyoshirikiana kuhakikisha kwamba Sheria zetu zote sasa hivi zinaanza kupata tafsiri ya kiingereza.

Akaja *Attorney General* naye akazungumza hapa akatoa *statement* mimi namsikia hapa akieleza jinsi ambavyo na sisi tunastahili kusema wameanzisha Kitengo katika Ofisi yake kitakachofanya kazi hiyo.

Nataka Mheshimiwa Mbunge aniamini tunapomwambia tunafanya nini, hivi tunavyozungumza Sheria zetu ndogo wewe unafahamu hata kule Njombe, Sheria hizi zimeandikwa kwa Kiswahili. Sasa anachozungumza hapa anazungumza habari ya *BoQ* na *BoQ* zile mpaka sasa hivi zinasoma kwa kiingereza, wako Madiwani ambao tunakuwa na bahati, wana *Ph.D.s* na nini inasaidia.

Lakini tunaowatumia sasa hivi ni *municipal* na *district solicitors* ndio wanaotoa tafsiri kwanza kwa sasa kusaidia Madiwani waweze kuelewa Mkataba. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa *Council* hawezi kusaini kabla hajapata ridhaa pia inayotokana na Mwanasheria pale, tutafanya hivyo. Yeye anataka kujua kwamba ni lini. Hii kazi imeshaanza tayari na ndio maana nime-*quote* barua hapa ambayo aliandikiwa mama Celina Kombani wakati huo tukaipeleka kwenye Halmashauri na ninazo zote hizo *documents* hapa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Taarifa, vikao vya Madiwani mfano Kamati ya Fedha mfumo wao utoaji wa taarifa, mapato na matumizi umekuwa hauko wazi na hauwasaidii sana Madiwani.

Je, ni lini sasa mfumo huo wa uwaandaji wa taarifa hizo utabadilika ili kuuwezesha Madiwani kuuelewa na uwe rahisi kueleweka?

**SPIKA:** Zenyewe zinawekwa kwa kiingereza?

**MHE. CELINA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, zinaandikwa kwa Kiswahili lakini mfumo wa uandaaji wake kujua matumizi halisi hauko wazi.

**SPIKA:**Muwe mnaagalia Swali la msingi halafu mnauliza swali la nyongeza. Naomba ujibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kwamba *I will be less than frank* kusema kwamba naelewa *exactly* anasema nini. Lakini nitajaribu kueleza kufuatana na Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inaundwa na Mwenyekiti wa *council* ambaye chini yake wale wenyeviti wa zile Kamati zingine zote wanaingia pale pamoja na Wajumbe wengine wawili ambao wanateuliwa na Baraza kati ya Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi Mtendaji halafu majina yale yanapeleka kule kwenye Baraza halafu ndio wanasema hawa ndio Wajumbe wa hii Kamati.

Kamati hii ndio Kamati inakutana kila mwezi mara moja na inachukua mambo yote yanayozungumzwa katika Kamati hii yanakwenda kujadiliwa *finally* kule katika *full council*. Sasa Mheshimiwa anazungumza kwamba hakuna uwazi, nitaomba mimi uniiruhusu tutakapomaliza Swali hili, niende nikakae nae pale anieleze vizuri hicho anachosema kwamba hakielieweki hauko vizuri, ili mimi sasa nishirikiane na Waziri yupo hapa tuweze kuondoa hilo tatizo kama kuna mahali ambapo inafunikwa. Mimi nilijiandaa kujua kwamba kiingereza ndio tatizo hapa, lakini kama kuna kitu kinafunikwa funikwa tutalitatua.

Kuna jambo moja ambalo nataka niliseme hapa labda ndio anataka kulisema hapa. Kule nyuma walikuwa wanakwenda moja kwa moja, kazi inakwenda kufanyika kwenye *site* kule bila kupitia kwenye hii Kamati.

Lakini iko Sheria imeletwa hapa, tuliipitisha hapa ambayo inasema kama kuna *contract* yoyote inatolewa hapa, hawawezi wakaenda kwenye *field* ukakuta vijiko vinafanya kazi, hivi kabla hawajapitisha hapa kwenye hii Kamati na kwenda kwenye Baraza la Madiwani. Kama ni hilo tutazungumza lakini kama umeruhusu nitakwenda kukaa naye pale halafu anieleze vizuri.

**SPIKA:** Hamna kukaa mtaendeshaje Mikutano miwili? Mheshimiwa Rajabu. Sikuruhusu kukaa kule labda mtoke nje kabisa. *(Makofi)*

**MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Suala la *BoQ* ni suala la kitaalamu, suala ambalo linakuwa na Wataalam wake wanaitwa *Quantity Surveyors* na katika Halmashauri zetu zote nchini tunakuwa tunaajiri tu Ma-*engineer* kwa maana ya *Civil Engineers or Architects* lakini hatuna hawa *Quantity Surveyors* ambao wao ndio wanaodadavua, ndio ambao wanatafsiri zile *BoQ* nilitaka kujua tu kwa upande wa Serikali mna mpango gani sasa kuajiri hawa *Quantity Surveyors* kwa ajili ya kutoa tafsiri halisi ya hizi *BoQ* ambazo wao ndio wenye mamlaka ya kuzitengeneza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi natambua kwamba anayezungumza hapa ni Mwenyekiti wa *Local Content Authority Accounts Committee* hiyo nafahamu.

Kwa hiyo, anaupeo mkubwa sana kuhusu hili jambo. Ni kweli unachosema lakini baadhi ya Halmashauri zetu zipo ambazo *already* zimeanza aina hii ya watu wanaozungumza ambao ni *Quantity Surveyors*.

Kwa sasa hivi ni kweli kuna hilo tatizo lakini mpango tulio nao ni kuhakikisha tunawapata, kwa sababu hii ni *area* ambayo ni *very sensitive*. Ndio inayoleta haya matatizo yote mnayosikia anazungumza hapa. Tunamtegemea zaidi pale *engineer* ambaye ha-*follow* kwenye hii *category* ambayo anazungumzia hapa. Watu wengine wanaoingizwa pale ni Yule Afisa anayeshughulika na masuala ya Manunuzi, wengine wanaandikiwa barua na Mkurugenzi Mtendaji. Mheshimiwa tunalichukua hili.

Lakini nataka nikuhakikishie tu kwamba zipo baadhi ya Halmashari ambazo sasa hivi zina *Quantity Surveyors* na wanafanya vizuri. Lakini ni eneo ambalo nafikiri lina haja ya kufanyia kazi kama Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee* anavyoshauri.

**SPIKA:** Ahsante sana tumechukua dakika kumi suala hili sasa tumwite Profesa Msolla, kwa Swali linalofuata.

Na. 96

**Mji wa Ilula Kupandishwa Hadhi**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA** aliuliza:-

Mji wa Ilula, Wilaya ya Kilolo, umekidhi vigezo vyote vya kufanywa Mji Mdogo na tayari maombi yake ya kupewa hadhi hiyo yalishapelekwa kwenye Mamlaka husika.

Je, ni lini Mji huo utapewa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Ilula?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula katika Wilaya ya Kilolo yalitangazwa kupitia tangazo la Serikali Namba 353 la tarehe 17/9/2004. Mamlaka hiyo inaundwa na eneo la vijiji vya Iliula Mwaya, Ilula Itunda, Ilula Sokoni, Itungi, Ikokoto, Mnafu na Isagwa.

Mheshimiwa Spika, tangu eneo hilo kutangazwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula, Halmashauri haikuendelea na zoezi na uanzishwaji Mamlaka hiyo kiutendaji, kutokana na kuwepo hitaji la kupanua Mipaka ya eneo la Mamlaka husika na kuhusisha pia eneo la Kijiji jirani cha Imalutwa. Pendekezo la kuhusisha kijiji jirani cha Imalutwa lilibuliwa na wananchi wa Kijiji hicho Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ilijadili suala hilo katika kikao cha Fedha, Uchumi na Mipango tarehe 15 Mei, 2014 ambacho kiliazimia kuwa pendekezo la kuingiza Kijiji cha Imalutwa lisifanyike sasa na badala yake litashughulikiwa wakati Halmashauri

ya Wilaya ya Kilolo inawasilisha pendekezo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula kuwa Halmashauri ya Mji wa Ilula kwa kuzingatia taratibu zilizopo. Azimio hili limetolewa kupitia barua ya tarehe 19 Mei, 2014 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Halmashauri inaendelea na taratibu za kuandaa Cheti cha kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula pamoja na kuandaa nembo ya Mamlaka hiyo. Baraza la Madiwani limepanga kukutana tarehe 27 Juni, 2014 ili kujadili na kuridhia mapendekezo ya Nembo ya Mamlaka hiyo katika kukamilisha uanzishaji wa Mamlaka hiyo kisheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Peter Msolla.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa maelezo yake lakini pamoja na hayo maelezo nina Maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwanza, kwakuwa yeye mwenyewe ametamka kwamba Mji wa Ilula ulitangazwa mwaka 2004 takribani miaka 10 iliyopita na Halmashauri nyingi hazijui taratibu masharti ya hatimaye kupewa Halmashauri ya Miji Mdogo ya Wilaya.

Kwanini Serikali haina utaratibu wa kuwajulisha Halmashauri husika taratibu zinazotakiwa kufuatwa kabla ya kufikia ngazi hiyo inayoombwa?

(b)Kwa kuwa utaratibu wa kugawa maeneo ya utawala ufanywe mara moja katika miaka mitano na mwaka huu wa 2014 ndiyo mwaka ambao tunategemea wa kutaka kuona mgawanyo maeneo mapya ya Utawala.

Je, Serikali itakuwa tayari kuupatia Mji mdogo wa Ilula hadhi ya kuwa na Halmashauri ya Mji huo, iwapo itatekeleza hayo masharti ya Nembo na mambo mengine ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatamka?

**SPIKA:** Ahsante! Kugawa mnagawa baada ya muda gani? Siyo miaka kumi, sidhani kama ni miaka mitano, bali kumi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Alisema kwamba muda wa kugawa ni kila baada ya miaka mitano, ndiyo nasema siyo miaka kumi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, naomba niweke jambo hili vizuri tuweze kuelewana hapa. Mheshimiwa Profesa Msolla amekuwa anafuatilia jambo hili kwa karibu sana na mimi naomba nimpongeze kwa ajili ya jambo hilo. Lakini hii nataka niweke vizuri.

Hii Mamlaka tunayozungumza hapa *establishment* yake na GN yake ilishatoka na kila kitu na kama tulivyoeleza hapa tulishatoa hiyo na kazi inayotakiwa kufanyika sasa ni kuhakikisha kwamba jambo hili linakamilika. Hapa ninazungumza habari ya Halmashauri ya Mji Mdogo ni kipindi cha mpito kuelekea Halmashauri ya Mji. Yaani hapo katikati na ndio maana hata sura zinabadilika pale kunakuwa na Wenyeviti wa Kitingoji, Mwenyekiti wa Council na Madiwani wawili ambao wanatoka katika ile Halmashauri mama wanaingia katika hiki kitu kinachozungumzwa hapa.

Hiyo Elimu anayozungumza Profesa Msolla ndio hiyo tunaitoa hapa na Elimu hiyo wanayo pale kilichotokea pale ni kwamba hakuna kazi inayofanyika pale. Sasa katika hili nataka nimthibitishie Mheshimiwa Profesa Msolla kwamba tunayo barua hapa ambayo

tumeiandika Halmashauri na mimi nitampa nakala hiyo ya hii barua, ili aweze kufuatilia vizuri kwa ukaribu.

Sasa hili la pili analo lizungumza hapa, kila mwaka Mheshimiwa wakati inapofika kipindi cha miaka mitatu tunapokwenda kipindi cha Uchaguzi Mkuu kunakuwa na utaratibu huu wa kuanzisha Mamlaka mpya, sasa zipo zinazo *follow after ten years* zingine kabla ya hapo kwa mfano kuna Vitongoji, Kata, Vijiji na kadhalika.

Kwa hii Halmashauri tunayozungumza hapa *issue* ipo kule Kilolo na sisi tumezungumza na Mkurugenzi Mtendaji tumemwambia kule, ili ahakikishe kwamba Halmashauri hii inakuwa Halmashauri ya Mamlaka ya Mji Mdogo na nitampa hii barua na Profesa sisi tumeshazungumza watu wake watuletee vielelezo vyote ili tuweze kupata Nembo, Kitambulisho.

Mheshimiwa Spika, Nembo hii inayozungumza hapa maana yake ndio linalozungumza hapa. Haiwezi ikatolewa hivi hivi na TAMISEMI, lazima itoke kule Kilolo, kama wanataka kuweka Mkungu wa ndizi au kuweka kabichi waonyeshe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali yenyewe marefu kweli kweli. Mheshimiwa Mhita, utasemea nini sasa? Kilolo au wapi?

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa hili tatizo la Kilolo linafanana sana na la Kondoa. Mamlaka ya Mji wa Kondoa nayo pia imekidhi vigezo na tumekwishapeleka maombi yetu katika Mamlaka inayohusika ili Halmashauri hii ipandishwe hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Kondoa.

Je, ni lini basi Halmashauri hii itapandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji mdogo wa Kondoa?

**SPIKA:** Ahsante sana. Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi, muda umechukua mwingi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba niliweke vizuri hapa, ile ndogo inaitwa Mamlaka ya Mji Mdogo lakini hii nyingine ile kubwa inaitwa Halmashauri ya Mji kama vile unavyosema Korogwe pale. Ninadhani anachosema Mheshimiwa Mbunge hapa nafikiri anazungumzia sasa kui-*promote* kuipeleka katika Halmashauri ya Mji ndicho kinachozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, Kondoa inapanuka haraka sana, *essence* yake kwa kifupi sana kwa sababu umeniambia nieleze kwa kifupi, ni kwamba unataka Kondoa na maeneo mengine kama Kibaigwa yasivurugike. Kama unakwenda kule Lamadi unakuta inavurugika tu watu wanajenga halafu kesho ukitaka kuweka nguzo za umeme unaweka wapi, hujui uweke wapi, unataka kuweka mtaro wa maji uweke, watoto wanabembea wakati wa sikukuu za Iddi na Christmas hujui watambembea wapi. Hicho ndicho kinachofanyika hapa ndiyo maana unataka iwe *a planned area*.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa kwamba hao wote walioomba, mamlaka hizi zote, iwe ni mamlaka ya Mji Mdogo na Halmashauri ya Mji wote sasa hivi tunaita zote tunazi-*pack* pamoja ili wakati zitakapotoka zitoke zote kwa pamoja kuhakikisha kwamba kelele hii tunayoisikia hapa ndani haipo tena ikiwa ni pamoja na Halmshauri ya Mji wa Kondoa.

**SPIKA:** Ahsante sana, naomba tuendelee na swali lingine, Mheshimiwa Rebecca Mngodo atauliza swali hilo.

Na. 97

**Watoto Kupewa Maziwa Shuleni**

**MHE. REBECCA M. MNGODO** aliuliza:-

Nchi yetu ina idadi kubwa ya mifugo.

Je, ni nini kifanyike ili watoto wapate maziwa mashuleni.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu ya afya na lishe shuleni unazingatia sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 inayohimiza umuhimu wa lishe bora kwa watoto wakiwa shuleni. Kuanzia mwaka 2007 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani imekuwa ikitoa lishe kwa watoto wa shule za msingi kwa lengo la kuimarisha afya ya watoto, kuinua mahudhurio, kupunguza utoro na kuimarisha usikivu na ufuatiliaji wa masomo darasani.

Mheshimiwa Spika, lishe bora kwa watoto shuleni ni pamoja na kuwawezesha kupata maziwa shuleni kupitia Kamati za shule, watalaam wa chakula na lishe, afya, makampuni ya maziwa, wafugaji, wazazi na viongozi wa Halmashauri inawezekana kuandaa mpango madhubuti wa kuwapa watoto maziwa wakiwa shuleni pale yanapopatikana.

Serikali itaendelea kuwahamasisha wazazi na wadau wa elimu ili kuwa na utaratibu utakaowawezesha watoto wa shule kupata maziwa angalau glasi moja kwa siku wanapokuwa shuleni au nje ya shule.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ningependa kumwuliza Waziri maswali mawili ya nyongeza:-

Katika majibu yake amesema kwamba kuna utekelezaji wa programu ya afya na lishe shuleni unaozingatia sera ya elimu. Ningependa kujua ni kwanini hii sera haitekelezwi na Wizara imekaa kimya?

Swali langu la pili ni kwamba wote tunafahamu kwamba Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, zaidi ya mifugo milioni 20, badala yake sisi Watanzania tunaona kwamba mifugo ni usumbufu badala ya kuitumia kwa manufaa. Ningependa kujua Serikali inatoa mwongozo gani ili wale wadau wanaohusika na maziwa na Halmashauri zote ambazo ziko katika maeneo yale ya ufugaji, maziwa yaweze kukusanywa na watoto wetu wapate maziwa badala ya kuwaacha wanachoka na kushindwa kusoma vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tupo ndani ya Bunge naona wengine wanajisahau kabisa wanafikiri wako peke yao wanaongea mpaka mimi nawasikia.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ingawa kisera tuna azma ya kutoa chakula shuleni na tumeanza katika baadhi ya maeneo hasa maeneo ya wafugaji, sisi kama Serikali na pia maeneo mengine tukishirikiana na *WFP*.

Lakini kinachogomba kuweza kutoa lishe katika shule zote ni uwezo wa kibajeti. Kadiri tutakavyokuwa na uwezo, tutapanua mgango zaidi na ningehamasisha Halmashauri zote nchini na Mikoa yote ambayo ina uwezo basi ianze wala isisubiri kasma ile ya Serikali Kuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maendelkeo ya Mifugo na Uvuvi, unarudia au unaendelea?

**WAZIRI WA MAENDELEO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni nyongeza ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu ile sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Mngodo, ambalo kwa kweli ni la msingi kwa sababu ni muhimu sana vijana kupata maziwa katika hatua zao za makuzi kwa sababu maziwa ni chakula kamilifu na kinajenga sana uwezo wa watoto kukua na kuelewa vizuri hata wanapokuwa madarasani.

Mheshimiwa Sika, sasa nchi yetu uwezo wa kutoa maziwa kwa sasa ni takribani lita bilioni mbili. Lakini maziwa yanayosindikwa kwa sababu watoto ni lazima waewe maziwa ambayo ni salama. Uwezo wa kusindika ni lita laki tatu tu kwa mwaka.

Sasa hiki ni kiwango ambacho bado ni kidogo sana ukilinganisha na idadi ya watoto walioko mashuleni. Kinachotakiwa sasa hivi ni kuhamasisha kwanza wafugaji waweze kuyakusanya maziwa yao, yaweze kusindikwa katika viwanda ili wanapopewa maziwa yawe maziwa salama. Lakini ni swali zuri sana nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mawaziri wawili wakijibu swali wananichukulia muda tayari, kwa hiyo ninaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Michael Laizer.

Na. 98

**Watuhumiwa Wanaokaa Rumande**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Watuhumiwa wengi hukaa au kurudishwa rumande kwa sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa Jaji, Hakimu au kukosa fedha za kuendesha kesi:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo ni kumnyanyasa mwananchi asiye na hatia?

(b) Je, baada ya kesi kumalizika na akakutwa hana hatia, haki zake atalipwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA KATIKA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaongozwa na utawala wa sheria ambapo kabla ya mtu kufikishwa mahakamani na baadaye kuamriwa kwamba apelekwe mahabusu au rumande ni lazima kwanza mahakama ijiridhishe na misingi ya kisheria inayopaswa kuwa imechukuliwa na upande wa mashtaka na hakimu mwenye dhamana ya kusajili hati ya mashtaka. Hatua hizo ni pamoja na usahihi wa hati ya mashtaka, makosa yaliyowasilishwa dhidi ya mshtakiwa na haki ya kisheria iliyopo kwa pande zote kuhusu dhamana na kwa kufanya hivyo, mahakama hufuata taratibu zilizowekwa na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kudhibiti mwenendo wa kesi na kutoa amri inayostahili kwa wakati. Hivyo, inapotokea Jaji au Hakimu ana udhuru au kuna tatizo la kibajeti kama inavyotokea pale mshtakiwa au Wakili wake ana udhuru, Mahakama kwa kutumia sheria na taratibu zilizopo huchukua hatua stahiki kuhakikisha kesi inasikilizwa na kutolewa uamuzi.

Taratibu hizo ni pamoja na zile zinazochukuliwa kwa kusikiliza kesi na pia kuwa na mpango mahsusi wa kumaliza mashauri ya muda mrefu mahakamani. Hatua hizi hutoa haki sawa kwa mshtakiwa na kwa mshtaki ambaye ni Jamhuri.

(b) Mheshimiwa Spika, kesi inapomalizika kwa mshtakiwa kuachiwa huru au kutiwa hatiani, pande zote zinatakiwa kuridhika na matokeo ili mradi mwenendo wa kesi umeleta matokeo ya haki. Pale inapothibitika kwamba misingi ya kufungua mashtaka na kusikilizwa kwa kesi imekiukwa wahusika huchukuliwa hatua na mamlaka za nidhamu zinazohusika na mwathirika anaweza kufungua kesi ya madai kama anao ushahidi wa kuthibitisha kwamba mashtaka aliyofunguliwa dhidi yake yalifunguliwa kwa hila (*Malicious Prosecution*). Upande wa Mashtaka nao pia huwa na haki ya kuwashtaki watu wanaotoa taarifa za uwongo kwa vyombo vinavyochunguza jinai. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, mtuhumiwa anaanza kuwekwa rumande pale Polisi, Polisi wanamzuia kwa muda na baadaye kumpeleka mahakamani na aende tena rumande. Kwa watu ambao hawawezi kujitetea na hawana wafuasi wao wa kwenda kumtafutia dhamana, huoni kwamba kuna mateso kwa baadhi ya watu ambao hawawezi kujitetea?

Swali la Pili, kwa kuwa, wakati mwingine kesi zinachelewa kwa sababu hakuna fedha za kuendeshea kesi na watu kurudnikana mahabusu, huoni kwamba watu kukaa na kuteseka rumande kwa ajili ya Serikali kutotoa fedha za kuendeshea kesi huoni kwamba huu ni unyanyasaji kwa watu ambao hawana hatia, ambao baadaye wanakuja kuachiwa, wamekaa miezi kadhaa hawana hatia.

Je, huoni kwamba ni unyanyasaji na kukiuka haki za binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuhusiana na watu wasioweza kujitetea, kupitia sheria ya huduma ya msaada wa kisheria kwa makosa ya jinai ambapo tunatoa huduma ya msaada wa kisheria kupitia Serikali katika makosa ya uhaini

na mauaji, ndiyo maana hivi sasa tumeamua kuifanyia marekebisho sheria hiyo ili kuja na sheria mahsusi kabisa inayohusiana na huduma ya msaada wa kisheria kwa makosa yote kwa watu wasiokuwa na uwezo. Lengo ni kuhakikisha kwamba watu wa aina hii wanaweza kutetewa na kuweza kupata uwakilishi na haki zao mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba hatuoni ni unyanyasaji kwa kesi hizi kuchelewa. Napenda kumuarifu Mbunge kwamba Serikali kupitia sheria ya Mwenendo wa makosa ya jinai, kupitia kifungu cha 125 cha sheria hiyo ililiona hili na ndiyo maana iliweka hatua mbalimbali. Anapokuja upande wa mashtaka au upelelezi haujakamilika kunatakiwa kuwa na cheti cha Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa ambapo shitaka linaweza likaahirishwa kwa siku 60. Baada ya hapo pia Wakili wa Serikali naye anaweza akaja kuweka ahirisho kwa siku zisizozidi 60.

Mwisho kupitia kifungu cha 225 kifungu kidogo cha Nne, Mkurugenzi wa Mashtaka naye anayo mamlaka ambayo Mahakama ikiridhia anaweza akaahirisha shitaka hilo kwa siku kwa miaka isiyozidi miwili.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mahakama ikijiridhisha kwamba kumekuwa na ahirisho ambalo halina sababu, mahakama inaweza ikatupilia mbali na kumwachia huru mshtakiwa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri napenda nimwulize kama ifuatavyo;

Hoja ya msingi katika swali lililoulizwa ni kurundikana kwa watuhumiwa ndani ya magereza kwa kusubiri kesi. Mimi ni miongoni mwa watu waliopata fursa au bahati ya kwenda kutembelea magereza, hali ni ya kutisha sana.

Je, kwa sababu watu hawa wanaokaa kule miaka na miaka bila ya kesi zao kusikilizwa kwa kisingizio hicho cha kuwa hakuna pesa, angalau Wizara ya Sheria imejiwekea utaratibu gani wa kuwapeleka Majaji kutembelea magereza haya ili wawasikilize wale washtakiwa na watuhumiwa waone ni namna gani watawasaidia, vinginevyo watu wataendelea kutumia pesa za Serikali, hizi za 1500, au 500 wakati kumbe wangeweza kwa kesi angalau za kuiba kuku tu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza kwa ziara zake mbalimbali katika Magereza na nitoe wito pia kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kwani sisi wenyewe kama Wizara hatuwezi kutembelea na kumaliza Magereza yote ingawa tunao utaratibu wa kila Jaji Mfawishi wa Mkoa husika wamekuwa wakitembelea magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito basi kwa watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria waendelee kuongeza kasi ya kutembelea magereza haya mara kwa mara. Mimi mwenye binafsi toka nimeteuliwa katika Wizara hii nimeshatembelea takribani mikoa mitano nabado nimekuwa nikiendelea kufanya hivyo.

Vilevile Mwanasheria Mkuu amekuwa akitembelea mara kwa mara, Naibu Mwanasheria Mkuu, Jaji Kiongozi, Jaji Mkuu, vilevile Mkurugenzi wa Mashtaka wamekuwa wakitembea na mara kwa mara tumekuwa tukigundua watu waliobambikizwa kesi lakini pia wale ambao wamekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, natambua na tunapokea rai yako na tutazidi kuongeza kasi hii.
**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nimepata bahati mbaya ya kuwekwa mahabusu mwaka 2011 pale Arusha na niliongea na baadhi ya watuhumiwa wengi wana kesi za wizi wa kuku, uzembe na uzururaji, kutumia lugha chafu na mambo kama hayo.

Kwa nini Serikali isiandae utaratibu ambao unaweza ukafanya usuluhishi zaidi wa kesi ndogo ndogo kama hizi badala ya kusubiri mahakimu ambao ni wachache wakati watuhumiwa kama hawa wanateseka kwa mambo ambayo yanaweza yakamalizwa kwa muda mfupi kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kupitia mahakama tumekuwa tukitumia taratibu mbali mbali na kutoa wito kwa mahakimu na waheshimiwa Majaji kutumia zaidi adhabu mbadala. Ukiangalia sasa hivi ziko adhabu ambazo unaweza ukatumikia kifungo cha nje, kufanya huduma mbalimbali katika jamii. Vilevile tumekuwa tukiajiri Watumishi mbalimbali ambao wanasimamia mpango huu.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hilo tu, kupitia Mahakama kama mtakuwa mmeona katika hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka huu, tunaanzisha kitengo maalum sasa kitakachoshughulikia masuala ya usuluhishi. Tunapokea wito huo na tutajitahidi kuzingatia wakati wa utekelezaji wa mpango huo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Naomba tuendelee na Wizara ya Viwanda na biashara, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, atauliza swali hilo.

Na. 99

**Mpango wa Maendeleo Kanda ya Kusini**
***(Southern Corridor)***

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Mpango wa Maendeleo ya Kanda ya Kusini Lindi, Mtwara na Ruvuma (*Southern Corridor*) imekuwa ni kauli ya muda mrefu:-

(a) Je, Bunge limesharidhia kuwepo kwa mpango huo?

(b) Je, Azimio hilo lililetwa llini katika Bunge?

(c) Je, utekelezaji wake ukoje hadi sasa?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa nani, Mheshimiwa Waziri jibu swali la Viwanda. Waziri Majibu ni yale yale niliyokuambieni, ninyi mnaongea wakati mimi nauliza. Haifai namna hiyo, siyo vizuri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, unisamehe sana.

**SPIKA:** Mawaziri wote wenye maswali wanakaa *front line,* inakuwaje ninyi mnakaa nyuma?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna watu bado, samahani.

**SPIKA:** Haya endelea.
**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, nchi za Malawi, Msumbiji, Tanzania na Zambia ziliingia mkataba wa ushirikiano katika Nyanja za kiuchumi, kibiashara na kijamii tarehe 25 Disemba, 2004. Mkataba huo ulilenga kuanzishwa kwa Kanda ya Maendeleo na programu zake ili kuhakikisha kuwepo kwa Miundombinu ya uhakika baina ya nchi husika kwa lengo la kufungua uwekezaji na biashara. Hivyo, kwa kuzingatia kuwa mkataba huo wa ushirikiano wa kiutendaji zaidi suala hili halijawahi kuletwa Bungeni ili kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, suala hili halijawahi kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mpango huu, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), ilishaanza kutekeleza miradi mbalimbali ambayo imeibuliwa katika Kanda za maendeleo hususani inayohusika na uanzishwaji wa viwanda mama. Miradi ya kiuchumi ambayo imeanza kutekelezwa hadi sasa chini ya msukumo wa Kanda za Maendeleo ni pamoja na Mchuchuma na Liganga, ujenzi wa barabara kuanzia Mtwara hadi Mbambabay ambayo ujenzi wake unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ukanda huu utanufaika pia na mradi wa kuzalisha na kusafirisha umeme utakaowekwa kwenye gridi ya Taifa, mradi wa ujenzi wa barabara na reli kutoka Ziwa Nyasa hadi Mtwara na mradi wa *Petro-chemical Platform* unaoainisha matumizi sahihi ya gesi ya Mtwara, vikiwemo viwanda mbalimbali vitakavyojengwa kutokana na gesi kama vile kiwanda cha mbolea na vituo vya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi.

Aidha, uendelezaji wa mradi wa kivuko kutoka *Mbambabay* Tanzania kwenda *Nkatabay* Malawi umefanyiwa upembuzi yakinifu. Ukanda huu pia umeanza kunufaika na ujenzi wa viwanda vya saruji vya *Dangote Cement Co. Ltd,* uliopo Mtwara Mikindani, *MEIS Cement Company* uliopo Lindi, pamoja na umeme wa gesi unaotumika katika Mji wa Mtwara.

**MHE. SALUM K. BARWANY:**Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amekiri katika majibu yake ya msingi kwamba Bunge halijawahi kuridhia wala kujadili mpango mzima wa maendeleo ya *Mtwara Corridor.* Atakubaliana na mimi kwamba mpango huo haupo? Swali la kwanza hilo.

Swali la pili, kwa kuwa kulikuwa na tamko la Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwamba itahakikisha kwamba maeneo yote ambayo yako nyuma kimaendeleo yatapewa kipaumbele. Kwa kuwa mpango huo umeshindwa kutekelezwa Serikali haioni ni mwendelezo ule ule wa kuyafanya maeneo haya ya Mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara, kuwa nyuma kimaendeleo?

**SPIKA:** Ahsante sana. Lakini huwa hatusomi maswali. Mheshimniwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, miradi ambayo nimeitaja ni miradi ambayo inatendeka sasa hivi, inaendelezwa sasa hivi. Kwa hiyo, tayari mpango huu unatekelezwa na unatekelezwa kwa kiasi cha kasi sana kama mnavyofahamu. Mradi wa Mchuchuma na Liganga tayari uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mradi wa migodi wa makaa na ya chuma tayari iko katika utekelezaji wa hatua mbalimbali. Mradi wa ujenzi wa mgodi wa Ngaka ya Kusini uliyo chini ya Kampuni ya Tanzu ya *Tamco* katika ya *NDC* na *Inter Energy* tayari umeanza kufanya kazi na makaa yanayochimbwa tayari yameshaanza kuuzwa katika viwanda mbalimbali nchini.

Kwa hali hiyo, na kwa sasa hivi tayari kuna Kampuni ya *Kitanzania S and M Agro Enterprises* ambayo imeingia mkataba juzi juzi na wawekezaji kutoka Korea ambao wana *MOU* ya kuendeleza masuala ya Kilimo na *Agro Processing* katika Kanda hii ya *Mtwara Corridor* hususani Lindi na Mikoa mingine ya jirani pale. Kwa hiyo, kwa kweli mradi huu imeshaanza kutekelezwa. Kwa hiyo, siyo suala kuwa haitekelezeki, imeshaanza kutekelezwa Mheshimiwa Barwany na tutakukaribisha ukajionee mwenyewe. *(Makofi)*

Kuna mradi wa *SAGOT* ambao nao pia uko mbioni kutekelezwa kwa kiasi kikubwa tu na tayari fedha imeshaanza Kutolewa kwa ajili ya miradi hiyo. Kwa hiyo, hii ni miradi Mheshmiwa imeshaanza kutekelezwa kwa vipindi mbalimbali. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kayombo swali la nyongeza.

**MHE. GAUDANCE C. KAYOMBO:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, katika miradi hii ya *Mtwara Corridor* kuna ujenzi wa reli kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay* hii nayo Serikali inasemaje, umefikia wapi mradi huu?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mradi wa *Mtwara Corridor* kuna ujenzi wa reli kutoka Mtwara *Mbamba Bay*. Kilichofanyika sasa hivi ni tenda hii kutangazwa na Wizara ya Uchukuzi na yameshajitokeza makampuni mbalimbali kuonyesha *interest* ya kuwekeza katika mradi huu. Tunasubiri matokeo yatakayotokea kutokana na *interest* inauyoonyeshwa na makampuni haya ili utekelezaji wake uanze na baada ya kampuni hizo zingine zinatoka *South Africa,* nyingine Canada na kadhalika. Tunasubiri matokeo yake. Lakini kweli mradi huo upo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba tuendelee muda wenywe umekwisha, maswali bado sita. Muda umebakia hata nusu yake umeshapita. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, atauliza swali.

Na. 100

**Utafiti wa Magonjwa ya Mikorosho**

**na Minazi**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kufanya utafiti wa magonjwa yanayosumbua mikorosho na minazi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mazao ya korosho na minazi katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Utafiti wa zao la korosho umekuwa ukifanyika tangu miaka ya 1970 ambapo utafiti ulikuwa unafanyika katika Kituo cha Nachingwea na baadaye kuhamia Kituo cha Utafiti Naliendele Mtwara.

Mheshimiwa Spika, utafiti katika zao la korosho umebaini magonjwa yanayoathari uzalishaji wa zao la korosho ni pamoja na ubwiri unga na *Blaiti* yaani *leaf and nut blight*. Utafiti wa kina juu ya madawa mbalimbali ya kudhibiti magonjwa ya korosho umefanyika na kupendekeza madawa ya Salfa ya unga, Zolfo ventilato, Bayfidan, Anvi, Bayieton na Topas ambayo ni baadhji ya madawa yaliyosajiliwa kutumika kuzuia ugonjwa wa ubwiri unga.

Aidha, kwa upande wa kutumika kuzuia ugonjwa wa ubwiri unga. Aidha, kwa upande wa ugonjwa wa Blaiti dawa za *Flint*, *Nativo, Score* na *Acanto* ni kati ya madawa yaliyosajiliwa kwa ajili ya kuzuia ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, zao la nazi limekuwa likiathiwa na ugonjwa wa kung'onyea minazi unaojulikana kitaalam kama *Coconut Lethal Disease (CLD)* ambapo hapa nchini mara ya kwanza ulionekana huko Bagamoyo mwaka 1905 na Ras ya Msimbati, Mtwara na Kunduchi Dar es Salaam mwaka 1912. Katika kukabiliana na kufa kwa minazi Serikali ilianzisha m pango wa Taifas wa uendelezaji minazi *(National Coconut Development Program-NCDP)* mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa zao la minazi, umeonesha kuwa minazi mingi hapa nchini imekufa kutokana na ugonjwa wa kunyng'onyea minazi *(Coconut lethal Disease)*. Matokeo ya utafiti wa muda mrefu uliohusisha aina mbalimbali 46 za minazi ya kigeni na aina 30 za minazi mirefu ya asili yameonyesha kuwa aina zote zinashambuliwa na ugonjwa huo lakini kwa viwango tofauti.

Hata hivyo, minazi mirefu kutoka katika maeneo ya Vuo, Mwambani na Kituo cha Uzalishaji wa mifugo Mkoani Tanga na kutoka Songosongo mkoani Lindi imeonekana kustahimili ugonjwa huu kwa kiwango kikubwa zaidi ukilinganisha na minazi kutoka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utafiti wa muda mrefu, ugonjwa huo bado umeendelea kuwa tishio kubwa hapa nchini kutokana na ukweli kwamba magonjwa yanayosababishwa na vimelea vya *phytoplasma* yanahitaji utafiti wa muda mrefu na endelevu. Aidha utafiti uliofanyika pia unaonyesha kuwa matokeo ya matumizi ya Sayansi na Teknolojia ambayo

yamefikiwa kwenye maeneo mengine ya kilimo yatahitajika kutumiwa kwenye ugonjwa huu wa minazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha ushirikiano na nchi ya Sri-Lanka ambayo yapo katika hatua za mwisho ili kuingia makubaliano ya ushirikiano (MOU) katika utafiti wa zao la Minazi kwa kuzingatia kuwa nchi ya Sri-Lanka imepiga hatua katika utafiti wa magonjwa ya minazi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa nimwulize maswali matatu ya nyongeza.

Kwanza, kwa kipindi cha kutokea mwaka 1905 mpaka sasa ni zaidi ya miaka 100 na bado inaonekana utafiti haujapata muda wa kutosha.

Je, tuwape muda gani miaka 300 hadi 500 au miaka mingapi ili utafiti huu uweze kufanyika na Serikali sasa inazo mbinu gani mbadala katika kuhamasisha na kuwasaidia wananchi hawa ambao wengine maisha yao yanategemea kutokana na kilimo cha minazi na mikorosho? *(Makofi)*

Swali la pili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, usiulize maswali marefu sasa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Ni kweli. Swali la pili, ni sababu zipi za msingi na zisizo za msingi ambazo Serikali imekuwa ikitoza ushuru wananchi hawa bila ya kuwapa ruzuku ya pembejeo kama mazao mengine inavyopewa. Lakini bado mnaendelea kuwatoza ushuru kwamba mnashirikiano kulima, mnashirikiana nao kutunza, au mnashirikiana nao kuvuna? Swali la tatu.

**SPIKA:** Wee acha utani. Mheshimiwa Naibu wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mangungu yeye mwenyewe ameuliza maswali mengi. Maana yake swali la kwanza lilikuwa na utafiti wa zao la korosho na utafiti wa zao la minazi. Kwa hiyo, kwa vyovyote lazima majibu yangekuwa majibu marefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tupewe muda gani kwamba umechukua muda mrefu kwa ajili ya utafiti. Naomba niseme kwamba vyuo vyetu vimeendelea na utafiti kwa muda mrefu na Mheshimiwa Mangungu kama Mbunge anayetoka maeneo hayo anajua kabisa ya kwamba Chuo chetu cha Naliendele ni moja ya Vyuo vya Utafiti ambavyo vinaheshimika sana duniani katika utafiti na vimekuwa vinaendesha zoezi hili kwa muda mrefu. Lakini tatizo ni kwamba ugonjwa wenyewe unakuwa unabadilikabadilika na kila utafiti unapofanyika magonjwa mengine yanatokea.

Hata hivyo, utafiti unaendelea bado na sasa tunataka kuingia mkataba kama nilivyosema muda siyo mrefu tutasaini *MOU* na Serikali ya Sri-Lanka ambayo wenzetu wame-*advance* sana katika masuala ya utafiti. Kwa kushirikiana na chuo chetu cha Utafiti cha Naliendele nina hakika kwamba siyo muda mrefu sana tutapata matokeo mazuri na

tutawashauri wakulima mbegu ambazo wanaweza wakatumia kwa ajili ya kuendelea kuzalisha zao la minazi.

Lakini sehemu nyingine Mheshimiwa Spika, aliuliza kwamba mbinu mbadala ambazo tunaweza tukazitumia. Moja, kwanza lazima tuwashauri wananchi kwamba waende watumie pia walime mazao mengine. Kwa sababu kama unaweza ukang'ang'ania zao moja ambalo linaonyesha kukabiliwa na magonjwa mara kwa mara haitatusaidia.

Ushauri ambao tunautoa kwa wananchi wanaweza wakapanda pia na mazao mengine kwa mfano machungwa, maembe, ambayo yanaweza pia yakawa tija pale ambapo zao hili kwao linaweza likawa linakabiliana na magonjwa.

Mheshimiwa Spika, aliuliza maswali matatu. Napenda nijibu hayo mawili. Asante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, ndiyo utaratibu. Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman. Hayupo, nyote mmekaa hapa hamjui Suleiman. Mheshimiwa Said Mtanda.

Na. 101

**Sheria Inayoruhusu Biashara ya Ranchi kwa Wanyamapori**

**MHE. SAID MTANDA (K.n.y. MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN)** aliuliza:-

Je, kuna Sheria gani ama Kanuni gani inayoruhusu biashara ya Ranchi kwa Wanyamapori, kama ilivyo katika Wilaya ya Meatu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 kifungu namba 89 kinaruhusu uanzishaji na ufugaji wanyamapori kama bustai *(Zoo)* shamba *(farm)* na *ranch.*

Aidha, ili kuanzisha ranchi au mradi unaofanna na huo kanuni zinazosimamia miradi ya namna hiyo ni Kanuni za mwaka 2013 *(TheWildlife Conservation, Wildlife Ranching, Farming, Breeding Sites, Orphanage Centers, Sanctuaries and Zoos Regulations, 2013)*. Kanuni hizo zimechapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 379 la tarehe 4 Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizi zinaelekeza mambo ya kuzingatia ili kuanzisha ranch ya wanyamapori au miradi inayofanana na hiyo. Maelekezo hayo ni pamoja na:-

Moja, eneo kuwa umbali wa zaidi ya kilometa 20 kutoka maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni kwa mujibu wa kanuni Na. 3 (1) (b) ya Kanuni ya uanzishaji wa mashamba ya wanyamapori hai ya mwaka 2013.

Pili, eneo kuwa na uhaba wa wanyamapori kama ilivyoelekezwa na kanuni Na 3 (4) ya kanuni ya uanzishaji wa mashamba ya wanyamapori ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo hivyo, hakuna ranchi iliyosajiliwa katika Wilaya ya Meatu.

**MHE. SAID MTANDA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa niulize swali dogo la nyongeza. Nilitaka kufahamu kwa niaba ya Mheshimiwa Suleiman Nchambi Wizara iko tayari kwenda Meatu ili kwenda kuupatia ufumbuzi migogoro inayoambatana kati ya wakulima na wafugaji inayotokana na ranchji hizi? Wizara, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kule kwa sababu ya migogoro hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali ni kweli tuko tayari kwenda Meatu kwa ajili ya kwenda kutatua migogoro hiyo na nataka nimwambie tu kwa sasa hivi tumejikita na tunaendelea. Lakini kuna mambo ya kusikitisha kuna baadhi ya viongozi wa Serikali nao wanakuwa ni sehemu ya migogoro. Lakini nataka nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kutatua migogoro hiyo.

Na. 102

**Wanafunzi Ambao Hawajapata Matokeo kwa Kutolipa Ada**

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Je, ni wanafunzi wangapi wa kidato cha nne ambao hawajapata matokeo yao kwa sababu yakutolipa ada za mitihani?

**WARIZI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne Mwaka 2013 yalitangazwa tarehe 21 Februari, 2014 ambapo matokeo ya watahaniwa 31,518 kati ya watahiniwa 404,083 waliofanya mtihani huo yalizuiwa kwa sababu ya kutolipa ada. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 7.79 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Matokeo ya mtahiniwa yaliyozuiwa hufunguliwa mara moja baada ya mtahiniwa husika kulipa ada yake ya mtihani. Hadi tarehe 8 Mei, 2014 jumla ya watahiniwa 7,314 wameshawasilisha ada zao na kufunguliwa matokeo yao na hivyo idadi ya watahiniwa ambao bado hawajawasilisha malipo ya ada ni 24,204,

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahimiza wazazi na walezi wa watahinikwa ambao matokeo yao yamezuiliwa kwa kutolipa ada ya mtihani, kulipa ada hiyo mapema ili matokeo hayo yaweze kufunguliwa na hivyo kutoa fursa ya wanafunzi hao kuendelea na kozi zao mbalimbali kulingana na matokeo yao.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Majibu kidogo yananisikitisha. Lakini Mheshimiwa Spika kwa kuwa miaka ya nyuma Serikali ilikuwa na tabia ya kutambua watoto ambao hawana uwezo na wa kuwalipia ada kwa ajili ya masomo na ada za mitihani. Lakini kwa sasa Mheshimiwa Spika, imekuwa kinyume, Serikali imekuwa na tabia ya kutumia Watendaji Kata na *Ma-DC* kuwapeleka wazazi Mahakamani ambao hawana uwezo wa kuwalipia ada watoto wao. Hatima yake watoto ndiyo hao ambao wanakuja kushindwa kupata matokeo kwa kukosa ada.

Je, Serikali kweli ina mkakati gani wa kuwasaidia watoto ambao hawana uwezo kabisa ambao wanatambulika?

Swali la pili. Mheshimiwa Spika, majibu yanaonyesha ni watoto 24,000 mpaka sasa hawajapatiwa matokeo yao ya mtihani kwa ajili ya kutolipa ada ya mtihani.

Nini hatima ya watoto hao 24,000 wa kimaskini kwa sababu watoto hao watakuwa wamesoma kwenye shule za Kata. Siyo watoto wanaosoma shule za watu ambao wana uwezo. Nini hatima ya watoto ambao hawajapata matokeo yao katika kujiendeleza kimaisha. Tunawasaidia au tunazidi kuwafanya wawe maskini? Ni nini hatima yao?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, moja ni utambuzi wa wanafunzi ambao wana uwezo mdogo wa kuweza kulipia gharama hizi. Serikali ina mpango maalum kupitia Halmashauri kuweza kuwatambua wanafunzi wa aina hiyo mapema sana katika masomo yao tangu wakiwa katika ngazi za chini na wao wanaorodheshwa na kila mara Halmashauri kufuatana na pesa walizokuwa nazo wana-*support* katika masomo yao na kulipia gharama zao.

Pamoja na ada hizi za mitihani. Kwa hivyo, siwezi kusema kwamba wale wote ambao ni asilimia 7 ya wanafunzi wote watahiniwa wote ambao mpaka hivi sasa hawajalipa ada za mitihani yao kwamba wote hawa ni wale maskini.

Lakini katika wale ambao ni wa hali ya chini ambao wanalipiwa na Halmashauri bila shaka watakuwa wamelipiwa. Lakini wale ambao hawalipiwi na Halmashauri sisi wote tuna wajibu wa kuweza kuendelea kuwasaidia na kuwatambua na naomba Halmashauri zifanye kazi ya kuhakikisha kwamba wanawatambua katika kundi hili wale ambao labda wameshindwa kabisa ili waweze kuwasaidia na sisi Waheshimiwa Wabunge na Wahisani mbalimbali tufanye kazi hiyo hiyo ili hii asilimia ndogo 7 ya wanafunzi hawa waweze nao kuweza kupata matokeo yao.

Lakini la pili kuhusu hatima. Hatima ni kwamba tutajitahidi kila namna ili kuweza kuhakikisha hawa ambao wameshindwa kulipa ada zao za mitihani waweze baadaye kuweza kulipa. Lakini natoa wito kwa wazazi, walezi, Halmashauri na sisi Waheshimiwa Wabunge kuweza kuhakikisha kwamba tunawanusuru watoto hawa wachache ambao wameshindwa kulipa ada zao.

**SPIKA:** Haya majibu yamekuwa marefu. Tunaendelea Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Devotha Likokola atauliza swali hilo.

Na. 103

**Uhamasishaji Kuwekeza na Kuanzisha Benki ya Jamii**

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali Kuu ina wajibu gani katika kuhamasisha, kuwekeza na kuanzisha Benki za Jamii, *Community Bank,* katika Wilaya zote nchini?

(b) Je, wajibu huo umetekelezwa kwa Wilaya ngapi hadi sasa na itafanya nini kuwahamasisha wananchi wa kipato cha chini kuwekeza katika vikundi *(Investment Club)*?

(c) Je, Serikali inaweza kukamilisha zoezi la kuhamasisha, kuwekeza na kuanzisha hizo Benki za Jamii kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2012 - 2014?

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge si mnaona *time*?
Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.
**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU M. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi wa Tanzania kupata huduma za kibenki vijijini. Kwa kutambua hilo serikali inaendelea kuweka mazingira bora ya Sheria, Kanuni, Sera na Mikakati, ili kuwezesha wadau wanaokusudia kuanzisha benki na kutoa huduma za kibenki kwa wananchi na pale ambapo huduma hizo zinaweza kujiendesha. Hivyo, Serikali haiingilii moja kwa moja maamuzi ya wapi benki zitaanzishwa na huduma hizo kwa kuwa maamuzi hayo yanategemea utashi wa wadau hao.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Taasisi Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000 na baadaye kutunga Sheria ya kusimamia Taasisi na Asasi hizo kuziwekea Miongozo pamoja na Kanuni za kusimamia uanishwaji na uendeshaji wa Taasisi hizo na kulinda maslahi ya wananchi wanaoongezeka kwenye benki hizi. Ikiwa ni pamoja na wawekezaji katika vikundi.

(c) Mheshimiwa Spika, aidha Serikali iko katika hatua za mwisho za kuandaa mkakati wa kuboresha huduma za kifedha vijijini. Lengo la mkakati huu ni kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa mtu mmoja mmoja, kaya na wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati, ili kuongeza kasi ya ukuaji wa ucbhumi na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, ndani ya mkakati huo kuna mkakati mdogo wa *SACCOS* ambao unakusudia kutoa mwongozo kuhusu upungufu uliopo katika muundo wa *SACCOS* ili kuzijengea uwezo wa usimamizi wa mitaji.
Mkakati huo unalenga kuweka *SACCOS* katika ukubwa wa muundo imara, ili kuboresha na kuziongezea ufanisi wa kutoa huduma kwamaeneo ya vijijini ikiwa ni pamoja na kuunganisha baadhi ya *SACCOS* zilizopo, ili kufikia ukubwa unaokubalika na kuanzisha mtandao wa *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kutoa elimu na kuhamasisha uwekezaji na uanzishaji wa benki za jamii na taasisi nyinginezo za kifedha ni endelevu, halitakoma katika kipindi cha miaka mitatu tu. Kwa sasa Serikali inaandaa mkakati wa Kitaifa wa elimu ya kifedha nchini. Lengo la mkakati huo ni kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha kwa kumwelimisha haki zake na wajibu wake. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiuliza Serikali. Kwa kuwa, wadau wakubwa wa *Community Bank* ni Halmashauri zetu pamoja na wananchi.

Je, Serikali, iko tayari kuziagiza Halmsahauri zote nchini zifanye kama Halmashauri za Dar-es-Salaam zilivyoweza kununua hisa nan a kuanzisha *Community Bank* ya Dar-es-Salaam na baadaye kuwauzia hisa wananchi na kuendeleza vizuri *Community Bank* ya Dar-es-Salaam?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali haiziamini *Community Banks;* kwa nini haifanyi kazi na biashara na *Community Bank* hata maeneo ambapo *Community Banks* zipo kama vile kule Mbinga na Serikali inaendelea kufanya kazi na *NMB* tu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Devotha Likokola, kwa jinsi anavyofwatilia hii Sekta ya *Micro-Finance* na jinsi ambavyo anawawezesha wajasiriamali wadogo wadogo hasa akinamama.

Niseme tu wazo lake ni jema la kuagiza Halmashauri zote ziweze kuiga mfano wa Dar-es-Salaam pamoja na Mbinga. Sisi hilo tutalichukua na tutalitolea maelekezo, isipokuwa tunawashawishi na tunawahamasisha pia wananchi wa maeneo mengine yale na wenyewe wawe tayari kwa sababu, kwa maeneo haya aliyoyataja na wananchi na wenyewe walikuwa tayari kushiriki katika zoezi hilo, ili wawe na *ownership* ya benki hizo kama jina linavyosema ni za wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu hili la pili la Serikali je, haiziamini? Hapana. Serikali inaziamini na kwa namna moja ama nyingine ambavyo inajenga mazingira ya benki hizi kuimarika ni moja ya hatua ambayo inaziimarisha benki hizi na baadaye itaanza kusbhiriki kikamilifu katika kufanya kazi pamoja, ili na zenyewe ziweze kuwa katika mitaji. *(Makofi)*

Na. 104

**Huduma za M-Pesa na tiGO Pesa Kutumika Kulipa Mishahara ya Awamu**

**MHE. SARA M. ALLY** aliuliza:-

Watumishi wengi wa maeneo ya pembezoni mwa nchi (Vijijini) hucheleweshewa mishahara yao na kulazimika kuifuata mbali na vituo vya kazi:-

Je, ni kwa nini Serikali isitumie njia za kutuma fedha kwa njia ya simu za mkononi kama vile *M-Pesa* na *tiGO* Pesa, ili kuwasaidia Watumishi wa Vijijini kupata mishahara yao kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo na umuhimu wa huduma za M-Pesa na tiGO Pesa katika kutoa huduma za kifedha kwa wananchi kwa kutumia mtandao wa simu za mkononi. Vilevile Serikali inatambua kuwa huduma hizo kwa sasa zimeunganishwa na ma-benki yanayotoa huduma hapa nchini. Mojawapo ni kama Benki ya *NMB, CRDB* na Benki ya Posta.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo Serikali kupitia Wizara ya Fedha, huwalipa watumishi wa umma mishahara kwa kupitia akaunti za watumishi zilizopo kwenye mabenki mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, malipo ya Walimu yanapitia katika mabenki na kwa kuwa, huduma za M-Pesa na tiGO Pesa kwa sasa zimeunganishwa na mabenki Serikali inashauri kuwa, Walimu wajisajili kwa huduma za kimtandao za mabenki wanakopitishia mishahara yao, ili nao waweze kutumia huduma hizo muhimu.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, halafu naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, watumishi wengi sana ambao wanakaa maeneo ya vijijini wanashindwa kuendelea na kazi kwenye maeneo yale kwa sababu kunakuwa na huduma ambazo haziridhishi, zikiwemo huduma za mawasiliano, ikiwemo huduma ya simu kwa hiyo, huwa wanaacha kazi.

Kwa hiyo, basi nilikuwa nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, anaonaje Serikali sasa ikikaa na wadu wa simu ambao ni wamiliki wa Makampuni ya simu, ili waweze kuona namna ya kutumia mnara mmoja wa simu kuunganisha huduma zao, ili nchi nzima mitandao ya minara ya simu iweze kuwafikia watumishi hao waweze kujiunga na hizo huduma za kibenki ambazo Mheshimiwa Waziri ameziongea hapo awali?

Mheshimiwa Spika, na Mheshimiwa Waziri ni shahidi; hata kwenye Makampuni ya kwenye ma-benki siku hizi mtu una kadi moja, unapata huduma za pesa kupitia ma-benki yote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wakati Serikali ikiendelea na juhudi zake za kusambaza mitandao ya simu na mawasiliano nchi nzima.

Je, kwa nini Serikali sasa isitoe motisha kwa watumishi wanaofanya kazi maeneo ya vijijini kwa kuwalipa gharama wanazotoka kwenye vituo vyao vya kazi kufwata malipo yao ya fedha kwenye ma-benki ambayo mara nyingi yako kwenye Halmashauri na kwenye Wilaya?

Serikali inaonaje sasa kuwalipa nauli, ile gharama, ili waendelee kukaa kwenye vituo vya kazi na waweze kutoa huduma kwa wananchi? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nimpongeze Mheshimiwa Sara Msafiri kwa kuwajali watumishi wanaoishi vijijini na kutambua umuhimu wa mahitaji ya simu.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya simu sio anasa ni mahitaji ya lazima katika maisha ya mwanadamu. Kwa kulitambua hilo, Serikali imekuwa ikipata changamoto kutoka kwa waanzishaji ama makampuni ya simu pindi inapowataka wapeleke mitandao katika baadhi ya

maeneo na wao kuona kama maeneo yale hayatawapa faida. Kwa kutambua hilo, Serikali inatazamia, kupitia mkopo, kujenga mitandao katika baadhi ya maeneo ambayo makampuni haya yalikuwa yanayaona hayana tija na hatua hizo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwa na mtandao minara ambayo inatumia mitandao yote, jambo hili pia linahitaji kwanza mtandao ule uliojengwa uwe umejengwa kwa kusudi la kuweza kuunganisha makampuni yote ama mitandao yote katika mnara mmoja. Kwa hiyo, katika minara hii ambayo, Serikali inakusudia kuijenga katika maeneo ambayo wafanyabiashara walikuwa wanaona hawana biashara jambo hilo litazingatiwa, ili mtambo ule au mnara ule ukishajengwa makampuni yote yaweze kutumia mnara huo na yaweze kulipa ushuru kwa Serikali, ili wananchi waweze kupata mitandao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la kuweza kuwapatia motisha kidogo wananchi ama watumishi wanaokaa mbali. Kama nilivyosema mwanzo kwamba, maadam watumishi hawa wanalipwa mishahara yao kwa kupitia mabenki na mabenki ambayo yameunganishwa kwenye simu, tukishaweza kuwaunganishia simu, maana yake litakalotokea ni lipi; mtumishi atakuwa ana uwezo wa kuangalia salio la mshahara wake kama umeshaingia kwa hiyo, hataweza kwenda kubahatisha mjini kama mshahara wake umeshaingia ama la. Akishajua kwamba, mshahara umeingia atakuwa na uwezo wa kuichukua ile fedha kama ni *M-Pesa* kama ni *tiGO* Pesa kama ni *Airtel Money* kutoka kwenye benki na kuiweka kwenye simu yake na kuitoa katika *agent* aliyeko karibu wa simu hivyo, haitamlazimu tena kutoka kijiji cha mbali kwenda mjini kutafuta benki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumetumia muda zaidi wa maswali kwa hiyo, naomba kwanza nitambue wageni tulionao.

Wageni ambao wapo Ukumbini hapa, kwanza kuna Mheshimiwa Balozi wa Tanzania katika Ubalozi wetu wa Geneva nchini Uswis, Mheshimiwa Modest Jonathan Mero. Mheshimiwa Balozi karibu; hukutuambia kama utakuwa *around.* Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi tukienda kwenye Mikutano yetu Geneva, huwa anatupa msaada sana sana katika *delegations* zetu. Watu wote tukienda huko hujisikia nyumbani sana. Hasa *delegation* ya *IPU* na *delegations* nyingine zilizowahi kwenda Geneva. Yaani yeye na *Staff* yake yote wanafanya kazi kubwa sana ya kutusaidia katika kuona mazingira ya hoja zetu zinazofanyika kule. Ndio maana nikasema mbona sikujua yupo kwa sababu, kwa kweli, amekuwa msaada sana kwa Wabunge wangu wakienda kufanya safari hizo. Ahsante sana Mheshimiwa Balozi, nadhani tutatafuta nafasi ya kukuona. *(Makofi)*

Halafu nina wageni wangu mimi. Ninao Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Uganda. Hawa ni Mheshimiwa Chris Bayomusi, *Member of Parliament.* Yupo Mheshimiwa Theopista Sendongo na yeye ni *Member of Parliament.* Halafu wameongozana na Afisa wao, Katibu ambaye anaitwa Ndugu Emmanuel Nsima. Karibuni sana. *(Makofi)*

Hawa wamekuja kama *delegation* ya Bunge la Uganda, wanakuja kufanya utafiti wa mambo yanayohusiana na mambo ya uchaguzi. Tunavyoshuhudia Muswada wa Gharama za Uchaguzi, kama watu wanafanya Kura za Maoni. Kwa hiyo, wana kasafari ka-utafiti namna hii.

Kule kwao, Bunge lao Kubwa lina Wabunge Binafsi, *Independent Candidates,* wengi sana. Kwa hiyo, wanajaribu kuona hivi ni nini kinachosababisha watu waondoke kwenye vyama vyao wakaingia kwenye *independent candidate.* Kwa hiyo, wako hapa kwa shughuli hiyo, watakuwepo na sisi kwa muda wa siku chache. *(Makofi)*

Halafu, tuna wageni wa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ambao ni Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na Msajili. Wahandisi kutoka Taasisi mbalimbali za Wizara ya Ujenzi, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Eng. Mussa Iyombe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia na Naibu Katibu Mkuu Eng. Nyamuhanga. Ahsante sana. Hawa hatujawataja kwa majina kwa sababu leo ndio Wizara yao, wote wako hapa na tutakuwa nao kwa siku nzima ya leo. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Yuko mgeni wa Mheshimiwa Rose Kamili.

Huyu Rose Kamili sikuhizi ni Waziri Kivuli wa Wizara ysa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo, yuko Mheshimiwa Richard Ambrose, huyu ni Hakimu wa Mahakama ya Ardhi na Nyumba kutoka Morogoro; Mheshimiwa Hakimu yuko wapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, ambaye ni Ndugu Ajuaji Marios Ajuaji, kutoka Mkuranga; Ndugu Ajuaji Marios yuko wapi huyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Abusalam Ameir, ambao ni Wenyeviti 22 na Makatibu wa vyama vya wakulima wa miwa wa Bonde la Luembe la Kilombero. Wakulima hao wako wapi wasimame huko waliko. Ahsante sana. *(Makofi)*

Hawa ni wakulima wa miwa katika mabonde ya Kilombero na Luembe. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Wageni waliofika hapa Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wapo wanafunzi 200 kutoka Shule ya Sekondari Kikuyu, Dodoma. Naomba wasimame Wanafunzi wote na Walimu wao. Ahsante sana, karibuni sana, nyie mpo hapa hapa karibuni sana hapa ni kwenu mnaweza kuja kututembelea wakati wowote. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi wanne kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanne hao wako wapi? Ahsante sana, karibuni na tunawaomba mwendelee na kusoma vizuri. *(Makofi)*

Halafu nina Matangazo ya Kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Magret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana, watakuwa na Kikao chao Chumba cha Msekwa C, saa saba mchana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 9.00 mchana kutakuwa na Kikao chao katika Ukumbi Namba 125, Hazina Ndogo. Saa 9.00, halafu saa 10.00 Mkutano, sijui!

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa 7.00 mchana watakuwa na Kikao. Kwa hiyo, nasikia Kamati hiyo ya Uchumi Viwanda na Biashara pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Jamii watakuwa na Kikao chao Saa 7.00 mchana, Hazina Ndogo, Chumba Namba 136. Pia, ninalo Tangazo hapa kwamba, tuna mwenzetu, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mbunge wa Kojani, amefiwa na Mama Mkwe wake leo alfajiri na inabidi aende kuzika Pemba.

Halafu, wale Waumini wa Kanisa la *Roman Catholic*, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Selasini, wa Jumuiya hiyo, anasema leo Ibada ipo kwa muda mnaopangiwa saa 7.00.

Baada ya hayo, Katibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mnyika, inakuwaje?

Ooh, nimekuita John Mnyika, *I am sorry*. Nilikuwa namwangalia Mchungaji Msigwa, lakini namwita John Mnyika, nimemzoea. Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa?

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kifungu cha Kanuni ya 68 (7) ambacho kinasema: *"Hali kadhalika,"* sijui nikisome au nisipoteze muda? Kinajulikana. *"Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo."* Ninaunganisha na 63 (1), ambacho kinasema: *"Bila kuathiri Masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni. Kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba, anatoa kauli na maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na sio jambo la kubuni au la kubahatisha tu."*

Mheshimiwa Spika, siku ya Ijumaa…

**SPIKA:** Naomba uwe *brief* eeh?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, sawa. Siku ya Ijumaa wakati Bajeti ya Mambo ya Ndani inajadiliwa, Mheshimiwa Ritta Kabati alitumia msemo ambao ninapenda kuunukuu wa: "Akili ndogo isitawale akili kubwa". Aliutumia msemo huo kwamba, mimi nilisababisha Wamachinga Iringa Waandamane na akasema mimi nilisababisha gari la Zima Moto liharibiwe na niliji-*commit* kwamba, nitalipa lile gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maneno hayo mwanzoni nilitaka niyapuuze kama ambavyo huwa ninampuuza. Lakini yamekuwa yakiaminisha watu kwamba, hizo habari ni za kweli na kwamba mimi niliji-*commit* kwamba, nitaandika. Kwa hiyo, kwa sababu, haya maneno ni ya uwongo na la pili, haya masuala yako Mahakamani na Spika huwa unasema masuala ya Mahakamani tusiyalete hapa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Kiti chako kimlazimishe afute hayo maneno au athibitishe mahali ambapo mimi niliandika kwamba, nitalipa hilo gari ambalo nimelivunja. Kwa sababu, haya ni mambo ambayo ni ya kubuni na amekuwa na tabia mara nyingi anabuni mambo ambayo si ya kweli. Na…

**SPIKA:** Mwongozo sio Hotuba jamani, kila siku tuelewane, Mwongozo sio Hotuba. Umesema unaomba yafutwe maneno yale, si ndio maombi yenyewe? Ndio Mwongozo?

**MHE. MCH. PETER MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, umeombwa Mwongozo, lakini ni vizuri ninaona tumeanza kufanya vitu ambavyo pengine ni kinyume na Kanuni. Katika Uongozaji Bora wa Shughuli za Bunge, Kanuni ambayo Mheshimiwa Mchungaji Msigwa amerejea, ile Fasili ya (7), inazungumza kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema. Katika tafsiri ya aina yoyote haiwezekani Ijumaa ikawa ni mapema…

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipaza sauti ya kuzomea kuonyesha kutoridhika )*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hebu tuelewane kidogo.

**SPIKA:** Naomba tusikilizane, msubiri kwanza, halafu tuna utaratibu wetu.

Msubiri tuelewe, jamani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Aliyeombwa mwongozo ni Spika, mimi namshauri Spika na kazi yangu mimi ni kutafsiri, ndiyo kazi niliyosomea; maneno yaliyotumika pale ni kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema. Kwa nini inakuwa hivyo? Ili tusirejee mambo ambayo yalitokea zamani yakachelewesha shughuli za Bunge, ndiyo maana kifungu hicho kipo. Ninasema naomba tuheshimiane kidogo, walau kidogo. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwamba, mwongozo ulioombwa siyo wa kikanuni.

**SPIKA:** Unajua kuna watu hapa wamesema tufuate taratibu za Bunge na kufuata taratibu za Bunge toka mwanzo niliwaambieni, maswali ya mwongozo siyo suala la kuunga mkono, ni yule yule aliyekuwa na suala lake anataka aongozwe na Spika, hamuungwi mkono na watu wengine kama mnavyofanya. Sasa naendelea na mwongozo wa Mheshimiwa Msigwa na mkisoma vizuri kanuni ya mwongozo ni kwamba, Spika ataamua wakati wowote atakapoona inafaa na ndivyo ninavyofanya. *(Makofi)*

Katibu, hatua inayofuata!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Ujenzi

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana namshukuru Mwenyekiti, alifanikiwa kuwaita Wenyeviti na Wasemaji wa Kambi ya Upinzani kutoa Hotuba zao. Kwa hiyo, sasa tunaendelea na mjadala. Nitamwita Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Said Jafo. Naomba Mheshimiwa Faith kama yupo; hayupo? Mheshimiwa Mendrad Kigola yupo.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa, napenda kuunga mkono Hotuba ya Waziri wa Ujenzi, ambayo imeleta maana sana. Tunajua kabisa katika uchumi ili Uchumi wa Tanzania uweze kuendelea lazima tuimarishe miundombinu. Miundombinu kama hatutaiimarisha vizuri, maana yake hata uchumi utashuka.

Nataka niseme kwamba, Waziri wa Ujenzi na Wizara nzima kwa ujumla, imefanya kazi nzuri ambayo inaonesha taswira nzuri sana kwa Watanzania. Mwaka huu tumepata bahati mbaya, barabara nyingi sana zimeharibika kutokana na mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu. Kwa kuwa ni suala ambalo lina sababu, hatuwezi kumlaumu sana Waziri kutokana na uharibifu huu wa mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tena nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kutusikiliza sisi Wabunge kwa yale tunayoyasema hapa Bungeni. Nilimpelekea Mheshimiwa Waziri maombi ya barabara zangu za Jimbo la Mufindi Kusini ambazo zimeharibika, nataka niseme kwamba, namshukuru kuona kwenye Kitabu cha Bajeti ya mwaka huu ameweza kuzipangia bajeti. Nimeona kuna barabara inayotoka Igowole – Kasanga – Nyigo, kilomita 54, ameshaipangia shilingi milioni hamsini; nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Barabara ya kutoka Mbalamaziwa - Kwatwanga umeipangia bajeti ya shilingi milioni mia moja; nakushukuru sana.

Barabara ya kutoka Nyololo – Igohole – Kibao itafanyiwa *feasibility study and detailed design*. Sasa hivi imeratibiwa kuwekwa kiwango cha lami, naona umeipangia milioni sabini kwa *detailed design*. Hapa nitaomba ufafanuzi kidogo, kwa sababu mwaka jana ulifanya *detailed design* kwa Barabara ya Nyololo kwenda Igohole mpaka Mgololo kwa kiwango cha lami na Serikali ilikubali kwamba ile barabara lazima iwekwe kiwango cha lami. *Detailed design* ya mwaka jana ulibajeti milioni 65 na ninakushukuru watu walifika kule na waliona. Walianza kufanya mikutano na Wajumbe wa Serikali ya Kijiji walifika na wakafanya kazi nzuri. Mwaka huu tulikuwa tunategemea kupata majibu kwamba unaanza ujenzi wa barabara kiwango cha lami kwa sababu *detailed design* imeshapita.

Nashukuru imepangiwa tena fedha, labda kuna kazi hazijaisha, lakini ninachokuomba Waziri, ili Wananchi wale waweze kuelewa vizuri, tunajua kabisa hii barabara imeshapangiwa kwenye kiwango cha lami na *detailed design* umeanza kufanya, lakini Wananchi ambao wako jirani na barabara na wale ambao wanastahili kulipwa, mpaka sasa hawajui lolote. Mheshimiwa Waziri uliahidi kwamba, utakuja kule Mufindi na hujafika Mufindi, miaka miwili umeahidi; sasa nakuomba leo uwaambie Wananchi wale utakwenda lini.

Mheshimiwa Spika, lingine, Barabara ya Nyololo sasa hivi imeharibika sana na ukitaka kuangalia Uchumi wa Tanzania, unatoka katika Wilaya ya Mufindi hasa Jimbo la Mufindi Kusini; kwa mfano, viwanda vikubwa sana ambavyo vinaingiza pato kubwa la Taifa katika nchi hii vipo Mufindi pale. Kwa mfano, kile Kiwanda cha Chai sasa hivi hata Wakulima wa Chai wanapopeleka chai kwenye kiwanda kile, wanashindwa kuyafikisha kwa sababu magari yanakwama njiani. Kuna Kiwanda kikubwa kile cha Mgogololo cha Karatasi, wale wanasafirisha malighafi kwenda nje na barabara ile kutokana na mvua imeharibika, magari yamekwama karibu miezi miwili pale, wameshindwa kusafirisha malighafi

Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, hii Barabara ipewe kipaumbele cha haraka sana itengenezwe kiwango cha lami. Nimeona umetengeneza kiwango cha lami kwenye barabara nyingine ambako hata uchumi haupo; kwa mfano, hapa Dodoma, nimeona kuna sehemu nyingine umeshaweka barabara za lami, kwa mfano huko milimani kuna lami. Una-*target* wawekezaji, wawekezaji pale hawapo, sisi kule walishawekeza siku nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri apeleke barabara za lami kwenye viwanda ambavyo vipo tayari. Wawekezaji walishawekeza tayari, kwa hiyo, tunawakatisha tamaa wasiwekeze zaidi. Naomba hilo liangaliwe sana. Kwa kazi yako nzuri naamini kwa kuwa umeshaanza kufanya *detailed design,* mwaka wa fedha huu utaanza kuweka kiwango cha lami barabara ile.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara nyingine inatoka Mafinga inakwenda Mtili – Sawala – Mgololo. Barabara ile ni muhimu kwa sababu wafanyabiashara wengi wanatokea kanda ile. Bahati nzuri hapa nimeona umeipangia milioni mia nane, nakushukuru sana, lakini ninataka nikwambie kwamba, zile barabara ni muhimu. Umesema utatupatia kilomita mbili, nakushukuru kwa kupewa kilomita mbili, lakini Wilaya ya Mufindi siyo ya kilomita mbili; Wilaya ya Mufindi ni ya kupewa kilomita nyingi tu za lami, kwa sababu uchumi mkubwa unatoka pale; kwa nini tunapewa kilomita mbili hapa?

Nakuomba Mheshimiwa Waziri barabara ya kutoka Mafinga ambayo inaenda Mtili – Sawala, tunaunganisha mpaka pale Zilozilo Mtwango na tutaunganisha na ile ya Nyololo, kwa hiyo, barabara mbili zitakuwa za kiwango cha lami. Ukifanya hivi Uchumi wa Tanzania utakua bila matatizo na wawekezaji wale watafurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya *survey* kidogo, nikamwuliza mwekezaji wa Mgololo, amesema kwa mwaka anachangia *1.2 billion,* kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami. Sasa kama anachangia *1.2 billion* kwa ujenzi wa barabara za lami; kwa nini tusipewe barabara ya lami haraka na ukizingatia kwamba pale Mgololo kwenye mteremko kilomita nane zimeshajengwa tayari?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kazi yako ninavyokufahamu na sisi tupo nyuma yako, tunakuomba ufanye haraka sana ujenge barabara kiwango cha lami, ukizingatia Wilaya ya Mufindi ni Wilaya ya mvua sana; kwa hiyo, ukiweka kifusi hata mwaka jana niliongea, unaweza ukawa unaweka kifusi kila mwaka na barabara ambazo zinaharibika kila mwaka tunatumia fedha. Ukijenga kwa kiwango cha lami unaweza kukaa hata miaka kumi hujajenga tena, kwa sababu unakuwa umeshatibu kabisa ugonjwa.

Jambo lingine ambalo napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kuna barabara moja ya Hawaga – Kiyowela – Mgololo, umeitengea shilingi milioni 192; nakushukuru sana. Barabara ile imeharibika sana, kwa sababu wafanyabiashara wengi wanaotoka Magunguli, wanatoka Bonde la Mgololo, wanapeleka mali Makambako, wanapita hii barabara. Hivi sasa imeharibika sana magari kule hayapiti. Nadhani hata Meneja wa *TANROAD* ananisikia na sasa hivi kule mvua zimeshaharibu kabisa. Ninatoa pole kwa Watu wa Mufindi, ni wavumilivu sana ilitakiwa waandamane, lakini tukasema Serikali yetu ni sikivu na mimi nakuamini Mheshimiwa Waziri kwa kazi yako na tunakuona unafanya kwenye Mikoa mingine. Wanachosema, wanasisitiza tena Mheshimiwa Waziri bado hujafika Mufindi ukafanya mkutano, siku ile ulipita Mafinga pale kwa ajili ya barabara uliyoleta Mafinga kwa dakika tano tu, kwa hiyo, uli-*beep* tu.

Tunakuomba sasa Mheshimiwa Waziri ukafanye mkutano kule wa siku nzima tukuone pale. Tunakuona tu unaenda Kaskazini, unaenda wapi, sasa tunataka tukwambie, Uchumi wa Tanzania hii unatoka Wilaya ya Mufindi ambako wewe bado hujafika ukafanya mkutano.

Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru tena nimeona umeipangia Barabara ya Nyololo – Igowole – Mtwango shilingi milioni 495, lakini hapa nitaomba utoe ufafanuzi kidogo; hizi ni tayari kwa kiwango cha lami au ni milioni 495 kwa ajili ya kuweka kifusi? Nitaomba wakati unatoa ufafanuzi hapa utueleweshe vizuri. Kuna Stendi ile ya Nyololo, magari mengi sana yanasimama ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Selemani Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa hii asubuhi ya leo na mimi kuwa mchangiaji wa pili katika Wizara hii muhimu. Nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi ya mimi kuwa mchangiaji wa pili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, mimi huwa napenda kusema anayefanya kazi lazima umsifie. Lazima tuzungumze ukweli, kama kuna mtu anafanya kazi mpe haki yake anafanya kazi, halafu tuchangie palipo na upungufu tuweze kuboresha zaidi. Waziri wangu wa Ujenzi unafanya kazi kubwa sana, japokuwa kwangu barabara za lami hazijaanza lakini kiujumla unajitahidi kweli kweli mpaka unakonda kwa kufanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tunataka watu wanaojituma kwa ajili ya Taifa letu hili. Tanzania itapata sifa sehemu yoyote, Tanzania unazunguka barabara za lami kutokana na ujenzi unaofanyika na kazi kubwa inayofanyika; hongera sana Mheshimiwa Waziri. Sambamba na kukusifia huko, naomba nikujulishe kwamba, katika Wilaya yangu ya Kisarawe kuna barabara mbili muhimu, barabara inayotoka Kisarawe inayoenda mpaka Vikumburu lakini inaishia Maneromango pale ambayo ipo katika ahadi ya kilomita 54 ujenzi wa barabara ya lami. Kingine ina urefu wa kilomita 148, inaanzia Makofia Bagamoyo inakuja Mlandizi inaishia mpaka Vikumburu. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa sababu mwaka jana baada ya kupiga kelele katika barabara inayoanzia Kisarawe mpaka Maneromango, ulifanya *fesibility study;* nashukuru sana hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru mwezi uliopita hapa baada ya kukwambia kwamba, *detailed design* haijafanyika na watu bado tunapiga kelele kwa nini barabara hii haijengwi kwa lami; hivi sasa Wakandarasi wako *site* kule wanafanya *detailed design.*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ile ahadi yake ya kusema barabara ya lami itaanza sasa, Wanakisarawe wanasubiri kwa hamu kuona barabara ya lami inaanza kutoka Kisarawe kwenda Maneromango. Hili naona kwake haliwezi kushindikana, kwa sababu najua kwamba ni mchapakazi.

Nimeona katika bajeti ya mwaka huu, hela ndogo iliyotengwa hapa, lakini kwa kutumia Ofisi yako utajua utafanya nini, na kwa sababu hata mwaka jana Mheshimiwa Rais alipokuja kule Kisarawe, alisema barabara hii itajengwa na wewe mwenyewe umesema barabara hii itajengwa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, *speed* yake ile ile anapotengeneza miundombinu ya barabara katika maeneo mengine, juhudi ile ile basi mwaka huu tuanze kuiona inaenda Kisarawe kwa kasi. Wale watu wanaofanya *detailed design* pale, kazi iende moja kwa moja, Wanakisarawe mwaka huu waone ujenzi wa barabara ya lami unaanza katika Jimbo lao la Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Barabara ya kutoka Mlandizi – Mzenga – Maneromango. Barabara hii niliposoma Kitabu cha Mipango ipo katika ile *Big Results Now (BRN)*. Nashukuru sana barabara hii kuipa kipaumbele. Naomba tufahamu vilevile, bahati mbaya simwoni Waziri wa Uchukuzi humu; katika eneo la Kisarawe kuna suala zima la ujenzi wa bandari kavu. Leo hii tunapozungumza kwamba, Dar es Salaam kuna msongamano wa magari, Bandari Kavu ya Kisarawe ingeimarika hata haya malori yote yasingekuwa yanaingia pale Dar es Salaam. Kwa hiyo, *automatically* ungeweza kupunguza kiwango cha malori yanayoingia Dar es Salaam, maana yake ungeweza kupunguza kiwango cha foleni ya magari yanayoingia Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, bahati nzuri barabara hii mwaka huu umeitengea milioni mia nne na umenieleza kuna *feasibility study and detailed design* inafanyika mwaka huu. Naomba hilo lifanyike ilimradi ujenzi wa lami uweze kutengenezeka pale, mwisho itaweza kusaidia hata ujenzi wa bandari kavu ambapo katika bajeti ya mwaka huu imeonesha Bandari Kavu ya Kisarawe itajengwa, kwa kuanza kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, suala zima la miundombinu ya barabara ni jambo la msingi kwa ajili ya kuweka uchumi wa Wananchi. Naomba niwaeleze, bahati nzuri Kisarawe tuko karibu kabisa na Jiji la Dar es Salaam. Mimi nina imani, unapozungumza suala zima la msongamano wa Dar es Salaam kama tungeweza kuiimarisha Kisarawe hata Wakazi wengine wa Dar es Salaam wangekuwa wanaishi Kisarawe na kufanya kazi Dar es Salaam; kwa hiyo, *automatically* ungeweza kupunguza kiwango cha foleni katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala zima la nyumba ambazo zimewekwa X. Kuna maeneo mbalimbali hivi sasa barabara zinakopita watu hawajui hatima yao ni nini. Naomba hapa leo katika kuhitimisha Mheshimiwa Waziri aeleze nini hatima ya watu waliowekewa X, maana hivi sasa wako katika sintofahamu; hawajui nini kitakachoendelea katika hilo. Wewe ndiyo mfumbuzi wa hilo swali, naomba utupatie majibu hapa nini ufumbuzi wa zile nyumba zilizowekewa X.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kupunguza msongamano wa Jiji la Dar es Salaam, naomba kutoa ushauri; kuna barabara inayotoka Maili Moja inapita Kisarawe pale, barabara hii inatumika sana watu wanaoishi Gongolamboto, Chanika mpaka Banana. Barabara hii ingeweza kuimarishwa kuwekwa kiwango cha lami, watu wanaotoka Mikoani wengine wangekuwa wanashukia maili moja pale, wanakata barabara ya kati na kuingia Jiji la Dar es Salaam barabara hii ni fupi sana.

Naomba Wataalamu wako, tusifikirie kwamba mpaka lazima tuanzie Mbezi, wakati mwingine watu wanakwama hata kabla hawajafika Mbezi. Inawezekana barabara hii ingeweza kuimarika, mtu akifika pale Kibaha tunaanza kupunguza msongamano wa watu katika Jiji letu la Dar es Salaam. Hili nina imani likifanyika, tutahakikisha basi maeneo yetu haya ambapo tunaona Dar es Salaam sasa hivi inazidiwa, wakazi sasa hivi wanataabika sana, wakazi wataweza kupata fursa ya kuhakikisha wanaingia katika Jiji la Dar es Salaam mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo napenda kuizungumzia ni barabara inayotoka Vikumburu mpaka Mloka Rufiji. Barabara hii naona mwaka huu imetengewa fedha chache sana. Barabara hii inatuunganisha sisi Wakazi wa Mkoa wa Pwani, kwamba, ukitoka huku Kisarawe unaingia Rufiji. Bahati nzuri sana angalieni janga la mwaka huu lililotokea, pale sasa hivi ukiangalia daraja la Rufiji hali ilikuwa mbaya, lakini inawezekana kama tukiwa na *alternative road* ambayo ukitoka huku Rufiji unakata unatokea Kisarawe, tena ni njia fupi kuliko nyingine yoyote. Kuunganishwa kwa barabara hii kutasaidia sana, wakati mwingine watu wanaotoka Mikoa ya Kusini badala ya kuingia Jiji la Dar es Salaam wanapita Rufiji, wanaingia Kisarawe, wanaingia Mlandizi, wanaendelea na safari nyingine. Naomba sana, Wataalamu wetu wanaweza kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kuijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile kwa sababu Wizara ya Uchukuzi bado haijafika, niwaombe sana hizi Wizara zifanye kazi kwa ukaribu kabisa. Nina imani sana tukiweka mawazo ya pamoja hasa hii barabara ya kutoka Mlandizi mpaka Mzenga mpaka Maneromango na tukiweka nguvu za Wizara ya Ujenzi, barabara hii itatengenezwa haraka kwa sababu tuna kila sababu ya kufanya hivyo. Tuna ujenzi wa bandari kavu, tuna kilimo kikubwa cha michikichi huko na sasa hivi

tunataka kuinua uchumi wa nchi. Ndugu yangu Waziri Kigoda, juzi alizungumza, suala la kilimo cha michikichi linaingia Kisarawe ambapo hivi sasa tunataka kufanya uwekezaji mkubwa katika suala hilo. Kwa hiyo, lote linahitaji miundombinu ya barabara.

Mimi nina imani sana, kwa *speed* mnayoondoka nayo, naomba msiniangushe. Nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri, ndiyo maana nimesema kwamba, mtu anapokuheshimu na wewe mheshimu; ninakuheshimu sana Mheshimiwa Waziri. Nina imani heshima hii ninayokupa, Watu wa Kisarawe wataona fursa sasa kwamba kweli Magufuli ni jembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze hayo machache, mimi yananitosha, kwa sababu watu wanasema maneno machache yanatoa tija katika mustakabali wa taifa. Naomba tija hii Mheshimiwa Waziri sasa ile *speed* yetu twende kwa kasi, Wanakisarawe waanze kuona sasa lami inajengwa kuanzia Mkuyani pale kwenda Maneromango. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Madabida, atafuatiwa na Mheshimiwa Pamba!

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru sana kwa kunipa nafsi hii na mimi nichangie. Mimi ni Mwanakamati wa Miundombinu, kwa hiyo, naunga mkono pia yale ambayo yamezungumzwa na Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpe pole Mheshimiwa Magufuli, mtani wangu, kwa ajali ya ndege aliyoipata, lakini naona alikata rufaa tupo naye. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe pia pongezi kubwa sana Mheshimiwa Magufuli, pamoja na Watendaji wote wa Wizara yake, kwa kazi kubwa na nzuri sana ambayo waliifanya Dar es Salaam wakati tulipokumbwa na mafuriko na madaraja yote yalipokata barabara, tukawa tumekuwa *cut off* kabisa na Tanzania yote. Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa sababu walifanya kazi nzuri sana usiku na mchana kufungua mahali hapo; nasema asante sana.

Mnafanya kazi nzuri kwa sababu hata Hotuba ya Kambi ya Upinzani imekusifia sana na ukiangalia katika ukurasa wa pili, wamesema tokea mwaka 2003, umeweza kupandisha kiwango cha barabara nzuri kwa asilimia 25. Asilimia 25 katika miaka kumi wakati miaka 40 tulikuwa na asilimia 13 tu, nakupongeza sana. Wakiipa Serikali ya Chama cha Mapinduzi miaka mingine ishirini, tutapandisha kwa asilimia 50; endelea, piga kazi, usirudi nyuma na asikukatishe mtu tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme kwamba, katika kuzifungua Barabara za Dar es Salaam, nimeona Wizara imeweka mipango mizuri sana ingawa mvua imetuharibia sana, barabara nyingi zimeharibika. Kwa hiyo, ninaomba atuambie jinsi gani watatusaidia tena hasa kutengeneza zile barabara za *TANROADS* na nyingine kama ninavyoomba sasa hivi. Niwaambie wale wengine kwamba, zile barabara ambazo za Mikoa, msimwambie yeye kwamba hakutengeneza kama ilivyokuwa imeandikwa kwenye Kitabu cha Upinzani, zile za Mikoa ni za Madiwani na sisi kama Wabunge ni Madiwani, ila ombeni kama mnataka kama hivi ninavyomwomba mimi, naomba kwa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam amezungumza sehemu nyingi sana na mimi ninaafikiana na yeye kwa utatuzi wa msongamano. Amezungumzia madaraja ambayo nilikuwa nimeyasema, lakini leo ninataka kujikita katika sehemu moja kubwa ambayo na yeye anaijua, Selander Bridge. Nimesoma kitabu hiki leo usiku kucha tokea mwanzo mpaka mwisho, hakuna hata mahali pamoja ambapo ameitaja Selander Bridge. Sasa mimi nasema, sikatai

hiyo boti ambayo inanunuliwa ambayo itakuwa inatoka Feri mpaka Bagamoyo, lakini siyo ufumbuzi wa foleni na msongamano ambao uko Selander Bridge. Ametanua sehemu nyingine zote na kweli unaiona ni mpango mizuri; vipi utazidi kuongeza unatanua lakini mdomo bado uko vilevile haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sijui kama ndugu yetu, mtani wangu anatukejeli, sijui ametudharau, sijui anatuona hamnazo! Watu wa Dar es Salaam wananisikia wanaotumia Selander Bridge sasa hivi kwamba, hakuna kwenye kitabu hiki hata sentensi moja inayohusu Selander Bridge. Huku siyo kutudhihaki; hivi kweli ile foleni inayopita Selander Bridge twende tukangoje feri kuvuka na hiyo boti? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mimi ninaomba hilo niambiwe, kinyume chake leo ni mara ya tatu ninasimama kuhusu Selander Bridge.

Lingine, nataka nizungumzie kidogo kuhusu Ndundu – Somanga, kusema kweli hakuna majibu sasa hivi ya kuwaeleza Watu wa Kusini kwa nini Ndundu - Somanga haijamalizika. Haiwezekani, Miaka 50 ya Uhuru, Ndundu – Somanga, kilomita 15! Huku nimeiona, sielewi hizi hela zinatosha pale Ndundu – Somanga? Ninataka watuambie lini Ndundu - Somanga inamalizika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara zinajengwa mara ya pili na ya tatu, Ndundu - Somanga kwa nini isimalizike? Siyo kweli, leo hakuna majibu ya Ndundu - Somanga zaidi ya kutuambia ni lini itamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali inisikilize, ninataka niongelee kuhusu madeni ya wakandarasi. Haya madeni ya wakandarasi yako zaidi ya bilioni mia nne na kitu. Sasa hizi hela pengine ndiyo maana hawamalizi hizi barabara madeni makubwa sana. Ninataka nipate kauli ya Serikali; hizi hela zitalipwa kabla ya tarehe 30 Juni; kwa sababu ama sivyo hizi hela zingine zinakuwa kiini macho kwamba hazitokwenda kujenga zingine inabidi zikalipie madeni, sasa akilipia madeni hizi zingine zilizoandikwa humu si itakuwa kiini macho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, hizi hela za misaada za kutoka nje. Mimi nimesema hapa nimekubaliana na mipango mizuri sana, ambayo ameweka kwenye kitabu chake kwa Dar es Salaam, pamoja na *flyovers,* kuna barabara zile za juu. Nimeangalia hizi *flyovers,* kaziweka kwenye hela za nje, lakini hizo hela za nje zenyewe hazikuoneshwa *donor* nani au tunaanua ngoma juani; maana yake isije ikawa tumeandika tu humu lakini hakuna kitu kinachoendelea. Mimi nataka nijue, hizi *flyover* zitajengwaje kwa sababu hela nyingi ziko kwenye hela za nje, lakini huyo *donor* anayetoa hela za nje hakuelezwa hapo. Sasa mimi ningependa kupata kauli ya Serikali *donor* ni nani kwenye huo Mradi wa *Flyover?*

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi sana kwa Wakala wa Ujenzi wa Nyumba, wamejenga nyumba vizuri sana kule Magwepande ambako wanasema watakopesha wafanyakazi. Mimi nawapongeza sana na nimeona wamenunua viwanja 10,000 na mwaka huu watajenga nyumba 10,000.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja nikishapata habari za Selander Bridge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Saleh Pamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga!

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda na mimi niungane na wengine, kutoa pongezi kwa Wizara yetu ya Ujenzi, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2010, nasema hongereni sana. *(Makofi)*

Kikubwa kinachofurahisha katika Wizara hii na katika Serikali yetu ni kwamba, barabara zote hizi ambazo zinajengwa, kwa asilimia kubwa, karibu asilimia 70 ya fedha za barabara hizi ni fedha zetu wenyewe; nasema hongera sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Kitabu cha Waziri, utaona kwamba kuna mambo mengi yamefanyika na barabara nyingi zimetengenezwa; kuna barabara ambazo zimekamilika, kuna barabara ambazo ziko katika *feasibility study,* kuna madaraja ambayo yamejengwa na kadhalika. Kwa hiyo, hiyo ni kazi nzuri ambayo inafanywa pamoja na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *TANROADS* na wote ambao wanahusika katika masuala ya barabara.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie masuala mawili ambayo yako katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Suala moja ambalo amelisema katika ukurasa wa 12 wa Hotuba yake, ni utaratibu mpya wa kujenga barabara. Amezungumzia suala la Barabaraya Dar es Salaam - Chalinze Express Way na huu ndiyo utaratibu mzuri unaotumika Duniani kote, kwa sababu Serikali nyingi Duniani hazijengi barabara, isipokuwa ni *private sector* ndiyo zinazojenga barabara.

Upo utaratibu wa kujenga na kukabidhi, *Build, Operate and Transfer, Build Own and Operate* na kadhalika. Hii itatusaidia Serikali yetu sisi kwamba, badala ya kuhangaika na kujenga barabara, zile bilioni 600 tunazotumia katika kujenga barabara, fedha hizo zingekwenda katika huduma nyingine muhimu, kwa mfano, elimu, huduma za jamii pamoja na afya. Kwa hiyo, ninapenda kuishauri Wizara hii kwamba, kwa sababu wameanza utaratibu huu sasa, waanze utaratibu huu kwa barabara nyingine pia ambazo zipo kwenye *pipe line*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani. Napenda niishukuru Serikali, wamekamilisha *detailed design* na *feasibility study.* Tunachoomba kwa Serikali sasa, waharakishe kuhakikisha fidia inalipwa haraka na *tender documents* zinatoka haraka na pengine katika miezi sita ijayo na kabla hatujaenda kwenye uchaguzi, angalau ujenzi uweze kuanza. Kwa sababu tunaamini kwamba, barabara hii itasaidia kufungua mtiririko wa usafiri kutoka Kaskazini hadi kufika sehemu za Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu la Pangani, mvua imenyesha sana na wakati huu ninavyozungumza, mvua inaendelea kunyesha. Tumeathirika sana hasa kwenye zile Barabara za Mikoa; sasa hivi katika Jimbo langu barabara ya kutoka Pangani hadi Mkaramo, ambayo ni barabara muhimu inayounganisha Wilaya haipitiki. Wananchi hawawezi kufika hospitalini, hawawezi kufanya kazi zao, lazima wapite Handeni ambapo ni zaidi ya kilomita 200. Kwa hiyo, naiomba Wizara na namwomba Mheshimiwa Waziri, kwamba, katika hili nadhani hatua za dharura zifanyike haraka sana kuhakikisha tunawaokoa wale Wananchi ambao wamekuwa *cut-off* kabisa pamoja na Wilaya yetu na Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ambalo nataka kulizungumzia, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri, anafahamu nimekuwa nikimlalamikia sana juu ya kivuko. Kivuko cha pili cha Pangani. Jiografia ya Pangani ni kwamba, Wilaya yetu imekatwa na Mto Pangani, kwa hiyo, kama hatutakuwa na kivuko cha uhakika, ni wazi kwamba, nusu ya Watu wa Pangani hawawezi kufika kwenye Makao Makuu ya Wilaya.

Nimeona katika bajeti yake kwamba, kuna ununuzi wa vivuko, nitapenda atapokuja ku-*wind up* aniambie katika *procurement of ferries;* je, kile Kivuko changu cha Pangani One kimo? Kama kimo basi kwa niaba ya Wananchi wa Pangani, napenda nichukue nafasi hii, nimshukuru sana, kwa sababu tumepata Kivuko cha Pangani Two, lakini kivuko kimoja kikiharibika tunakuwa na matatizo makubwa sana, Wananchi hawawezi kuvuka na ule mto ni mkubwa sana, kwa hiyo, hawawezi kutumia mitumbwi kwa kuvuka mto, siyo salama.

Kwa hiyo, ninashukuru *in advance* kwamba, Pangani One kama ni kweli imo, basi kwa niaba ya Wananchi wa Pangani, napenda nichukue nafasi hii nimshukuru sana. Ninakuhakikishia kwamba, fedha hizi zikipatikana, pale tuna uzoefu wa kujenga pantoni, kwa hiyo, nadhani kwa haraka zaidi mtatusaidia tuhakikishe kivuko hiki tunakitengeneza haraka.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo, nilitaka niyaseme. Wizara hii inafanya kazi nzuri sana, endeleeni kuchapa kazi, tengenezeni barabara kwa sababu hizo ndiyo zinazo-*open up* nchi yetu kwa ajili ya maendeleo yote mengine ya kiuchumi, ya kijamii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja, hongereni sana Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Suzan Kiwanga!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia juu ya Wizara hii. Nami nianze kwa kuwashukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa ujumla, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kujenga barabara katika nchi yetu ya Tanzania. Wako watu ambao pia wanaweza kumlaumu, mimi niseme kwamba, ni sawa na unapomlea mtoto wa kambo, hata ungemsaidia kiasi gani atalaumu tu; kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, chapa kazi, baba ni baba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri yangu ya Njombe na Makambako, pale Makambako nimejaribu kupitia, Halmashauri ya Mji wa Makambako, Waziri Mkuu alituahidi kujenga kilomita tano na wewe Waziri nilikwambia wakati fulani nilileta na barua. Niombe sana kwa mwaka huu fedha, angalau ukitupa kilomita mbili zinazotoka na *TANROAD,* utakuwa umetusaidia sana kutengeneza miundombinu katika Mji wetu wa Makambako.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kwamba, Halmashauri ya wilaya ya Njombe ni Halmashauri iliyotoa Halmashauri nne ambayo sasa imebaki Halmashauri Mama ya Wilaya ya Njombe. Zipo barabara ambazo tunaomba Wizara hii izipokee ili Halmashauri iondokane na mzigo mkubwa ambao inao katika Barabara za Wilaya hiyo ya Njombe na Makambako. Barabara hizo tulijadili katika vikao mbalimbali, hivi sasa ziko kwako Mheshimiwa Waziri, ni barabara ya kutoka Makambako – Mlowa – Kifumbe mpaka Kitandelilo; Barabara ya kutoka Mtwango – Kichuwa, Ihegi Kuu – Nanyombo na kwenda Lupembe inakwenda kutokezea Madaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Kibena kwenda Lupembe mpaka Madeke, ambayo tumeizungumzia kwa muda mrefu na sasa imetengewa bajeti; nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru sana hata kama ni kidogo, hela ambazo umezitenga kwa mwaka huu wa fedha kama ulivyotenga, barabara itangazwe kwa hela hizi hizi ianze. Kushukuru ni kuomba tena, kwa hiyo, naomba wakati unaendelea na barabara hizo, basi uendelee kututengea fedha ili barabara hii sasa iweze kujengwa kwa lami. Katika Mji wa Lupembe kuna viwanda vya chai, kuna uchumi mkubwa na kuna wawekezaji wengine ambao hivi sasa wanataka kuweka viwanda pale, akiwemo ndugu mmoja anaitwa Msambwa na

wengine na makampuni mengine. Tatizo kubwa ni barabara; kwa hiyo, tukiweka barabara hizi za lami zitatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie mizani iliyopo pale Makambako. Sijajua Serikali ina mpango gani, kwa sababu mizani hii iko mjini na magari yanakuwa mengi, foleni inafika mpaka njiapanda ya kwenda Njombe na Mbeya, kwa hiyo, imekuwa vilevile ni kero. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, aniambie Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanaondoa mizani pale mjini, waweke mahali pengine ili Wananchi wa Makambako waepukane na kero hiyo ya msongamano wa magari.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Dar es Salaam linalohusiana na *parking.* Imefika mahali imekuwa ni kero kubwa sana; kwa mfano, mtu anapopata pacha anaanza kutengeneza pembezoni mwa barabara, anakamatwa na kutozwa faini, hela nyingi. Wale mawakala ambao wamepewa kibali na *TANROAD,* wanakamata wanatoza faini shilingi 250,000 na unatakiwa ulipe kwenye Jiji shilingi 250,000. Jamani hizi hela watu watazitoa wapi na gari limeharibika! Hebu Wizara angalieni namna ambavyo mnaweza kuweka miundombinu vizuri na kuwasaidia hawa watu ambao wanaharibikiwa na magari au wanasimama kwa ajili ya kuangalia magari yao na kadhalika. Suala hili limekuwa ni kero sana kwa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kukushukuru kama nilivyosema, ukipata kidogo ni lazima ushukuru lakini naomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda umefika, wewe umeshindwa kuzungumzia Barabara za Makao Mkuu ya Njombe, vipi Mwenyekiti? *(Kicheko)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ameshasikia Waziri kwamba, pale ndiyo Makao Mkuu.

**SPIKA:** Muda umeisha! Mheshimiwa Suzan Kiwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga.

**MHE. SUZAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika masuala ya barabara. Mimi natokea Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro unaonekana ni Ghala la Taifa, lakini kuna barabara nyingi ndani ya Mkoa huo, kutokana na mazingira yake na hali ya mvua, barabara nyingi mara kwa mara hazipitiki. Pamoja na jitihada za Waziri husika wa barabara, Mkoa huo unatakiwa uangaliwe kwa jicho la karibu sana.

Mheshimiwa Rais Kikwete, alitoa kauli kwamba, ule Mkoa ni ghala la chakula. Kwa hiyo, huwezi ukautazama Mkoa wa Morogoro sawasawa na mikoa mingine. Hali halisi inaonesha, lakini kwa kuwa muda ni mchache, nijikite katika Wilaya ambayo mimi ninatoka na familia yangu na ninakaa kule. Hali ni mbaya, mpaka leo ninavyosema, Wilaya ya Kilombero, barabara zake zote hazipitiki. Tumepata ahadi nyingi kwamba, barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami na Wilaya hii ni ghala la chakula, ni *SAGCOT*, lakini barabara hazipitiki! Kwa hiyo, ni hali mbaya na Wilaya hii inaungana na Mkoa Mpya wa Njombe. Wananchi wa Njombe wanaweza wakapita barabara itakayotengenezwa kuanzia Kidatu – Ifakara, Ifakara – Mlimba, Mlimba – Madeke – Njombe kuja Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine, kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri mwenye dhamana, afanye ziara kwenye hiyo Wilaya aone namna ya kuunganisha Wilaya ya Kilombero na Mkoa wa Njombe. Mkoa wa Morogoro tumeshapeleka maombi, tumepitisha kwenye *RCC* kwamba, tunahitaji Mkoa Mpya wa Kilombero. Kwa hiyo, ni vyema sasa mkaiboresha Wilaya hiyo. Mimi naomba nipate majibu, kwa kuwa kuna wafadhili wengi wanafadhili Barabara za Wilaya ya Kilombero, Wilaya hii imepata ufadhili kwa *USAID* Marekani, lakini mpaka leo Halmashauri imeshapeleka maombi Mkoa, Mkoa, Wizarani, *USAID* wanataka wafunguliwe akaunti maalum ya nane ndani ya Wilaya ya Kilombero waingize hela ili wajenge barabara; Mpanga - Ngalimila, Namawala - Mofu, Mgudeni - Mofu, Kilometa 38. Wana mpango pia wa kujenga barabara karibu kilometa 200, lakini mpaka leo Wizara inatoa kigugumizi kufungua hiyo akaunti. Tatizo liko wapi? Naomba Wizara husika ione umuhimu wa hawa wafadhili kufungua akaunti maalum kwenye Halmashauri, waingize hela ili barabara hizo zijengwe. Kigugumizi kiko wapi? Naomba kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ifakara – Mlimba, walisema watajenga kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Waziri unakumbuka maswali mengi kutoka kwa Wabunge wa Wilaya ya Kilombero, umejibu hapa mwaka 2013/2014 kwamba, utajenga kwa kiwango cha lami kutoka Ifakara mpaka Mlimba na Mlimba mpaka Madeke - Njombe Changarawe. Bajeti hii inaisha kesho kutwa, ulipanga shilingi milioni 60 zimefanya kazi gani? Naomba kupata majibu.

Sasa hivi hii bajeti tunayojadili hapa umepanga shilingi milioni 90; zinaenda kufanya kazi gani? Kwa hiyo, naomba Barabara za Wilaya ya Kilombero zijengwe.

Mheshimiwa Spika, Kivuko cha Kilombero. Umesema jana katika Hotuba yako kwamba, kazi inaendelea; iko wapi Mheshimiwa nenda katembelee Kilombero sasa hivi ni bahari? Kuanzia Lipangalala mpaka kule kilometa mbili ni bahari. Sasa najiuliza, mlipotoa ahadi za Serikali, Desemba mwaka huu hilo daraja litaisha; je, hilo ni kweli? Naomba uwajibu Wananchi wa Kilombero na Wananchi wa Ulanga. Kweli hii bajeti mliyotenga mwaka huu itaenda kumaliza hilo daraja, wakati mpaka yule msimamizi alijinyonga kwa sababu ujenzi ulioanza ulizolewa na maji? Kwa hiyo, ile kazi iliyofanyika mwanzo ni sawa sawa na sifuri.

Je, mna mpango gani kama Serikali kwenda kuangalia upya lile daraja na kuanza upya ili liishe mwezi wa kumi na mbili kama mlivyoahidi? Naomba Mkoa wa Morogoro muungalie kwa umakini kwa sababu ni Mkoa pekee, ni ghala la chakula, maji mengi, kila wakati madaraja na barabara zinabomoka, kuna haja ya kutenga pesa nyingi ili kuufadhili Mkoa wa Morogoro uingie katika dulu na sisi tujisifu kwamba, sasa na sisi tuna barabara. Miaka 50 ya Uhuru na sisi tujivunie.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kipindi kile cha uzinduzi wa Daraja la Kilombero aliendа Naibu Waziri na alisema ataenda mara kwa mara; naomba sasa Waziri mwenye dhamana, aende akafanye ziara katika Mkoa wa Morogoro hususan Wilaya ya Kilombero na Ulanga, aone hali halisi, hata anapokuja kupanga bajeti anajua kabisa hali ngumu. Ninataka kupata majibu ya Serikali ni lini mtaruhusu Wilaya ya Kilombero ifungue akaunti ya nane ili kuingiza hela za wafadhili tupate kujengewa barabara Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali!

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunijalia na mimi nikaweza kusimama mbele yako na kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Ujenzi, inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa Lwenge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ningependa niongelee msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Msongamano katika Jiji la Dar es salaam ni picha halisi ya tunakoelekea katika miji inayokua kwa kasi, ukiwemo Mji wa Mwanza, Mji wa Arusha, Mbeya na Miji mingineyo.

Mheshimiwa Spika, ninafikiri tukienda kwa mpango huu anaokwenda nao kaka yangu Mheshimiwa Pombe Magufuli, kusubiri mpaka mji uelemewe ndiyo akubali kuchukua Barabara za Halmashauri, atakuwa amechelewa, huenda atakuwa yeye si Waziri tena na atakuwa amemwachia mzigo Waziri atakayekuwepo kwa wakati huo. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, nafikiri Kikao cha Bodi ya Barabara ndiyo kikubwa cha mwisho katika Mkoa. Kikao cha Bodi ya Barabara kinapotoa mapendekezo kumpa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, wanaona kutengenezwa kwa barabara zile ni kufungua Mkoa wao. Mheshimiwa Waziri anapokwenda kutengeneza barabara ambazo hata Mkoa haukumwagiza, nikichukua mfano mdogo katika Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mwanza, kwa miaka mitatu mfululizo tumeomba kutengenezwa kwa Barabara ya Sabasaba, PPF kutokea Busweru, kwa sababu barabara hii Halmashauri haina uwezo nayo na ndiyo maana Bodi ya Barabara ya Mkoa ikaiomba barabara hii aichukue Mheshimiwa Magufuli na alikubali.

Cha ajabu, Bodi ya Barabara ndiyo kikao kikubwa ambacho kinapokea ushauri kutoka Halmashauri. Alichonishangaza Mheshimiwa Waziri, aliwaita Madiwani wa Wilaya ya Ilemela, akaikataa Barabara hii. Haikuwa mahala pake, alipaswa kuiarifu Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mwanza kwamba, Barabara hii nawarudishieni. Kwa kuitisha Madiwani na kuwaambia Barabara hii haitaki kwanza ni kinyume na taratibu na hapa niseme wazi, Mheshimiwa Waziri amechemka. Tulidhani kwamba, kama aliona ni muhimu badala ya kuwaita Madiwani angetuita wenyewe Wajumbe wa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mwanza akatueleza haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Magufuli kwamba, barabara hii mwaka huu tumekurudishia, huu ni mzigo wako uondoke nao. Kama huwezi, basi tunaomba ile asilimia 30 unayowapa Halmashauri waongeze iwe 40 ili waweze kufanya shughuli ya barabara hii. Hii ni kwa sababu hakuna kikao chochote tulichokaa Bodi ya Barabara tukatengua maamuzi haya. Kwa maana hiyo, ilikuwa ni vizuri zaidi kikao hiki, kwanza, nafurahi kabisa kinasimamiwa na Mwenyekiti wa Mkoa wa Chama cha Mapinduzi, akiangalia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Diallo, anaingia kwenye kikao hiki. Alikubaliana na sisi kutekeleza Ilani yenu ya Chama cha Mapinduzi; kwa maana hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aweke hata heshima kidogo kwa Mwenyekiti wake wa Mkoa anayetekeleza Ilani ya Chama chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa niongelee suala moja; Mheshimiwa Magufuli, baada ya kuikataa ile barabara amekwenda kuchukua barabara nyingine kabisa ya Mwanza - Nyanguge Bypass; sawa. Kwa kuwa Mji wa Mwanza unakua kwa kasi, kwa barabara ile uliyochonga ni majanga. Barabara umechonga nyembamba, madaraja barabara haina, moramu uliyomwaga ni ya kishikaji na bado hata kwenye kona ambapo magari makubwa yanatakiwa yaingie kwa sababu ile barabara ni ya kibiashara, inakwenda mpaka Kayenze ambapo Kayenze umepatelekeza.

Barabara ya kutoka TX - Kayenze umeitelekeza, haina matengenezo na wala hauijali kwa kitu chochote. Trunakuomba hebu tekeleza barabara zako vizuri na zile unazopewa

uzichukue uzifanyie kazi, ili Wananchi waweze kujiendeleza kiuchumi. Aangalia sehemu yenye uchumi, kwa mfano, hii barabara uliyokwenda kuichonga, *semitrailers* zinapita, lakini kama umeenda kuweka madaraja ya kishikaji, watu wanachukua samaki, wanachukua dagaa, yanapita pale malori ambayo yamefunga mtoto nyuma, unategemea yatapita kwenye barabara hiyo? Mji wa Mwanza unakua, tunaomba ututengenezee barabara ili zisije zikaanza bomoa bomoa zisizokuwa na manufaa kama ambavyo umewafanyia Mikoa mingine kama Dar es Salaam na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Magufuli, pia katika barabara hiyo uliyoichukua napenda nikwambie kwamba, barabara hiyo hawakulipwa ipasavyo!

**SPIKA:** Nasema unatumia Waziri siyo majina ya mtu!

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa mwongozo wako. Wananchi hawakulipwa ipasavyo, mtu anaenda kuchukuliwa ardhi yake analipwa shlingi 5000. Kwa hiyo, utaratibu haukufuatwa, sheria za kuchukua ardhi ya mtu haikufuatwa. Tungependa sasa mkae chini mfikirie, wale ni Wananchi maskini, wameilinda ardhi hiyo kwa siku nyingi, walikuwa na mashamba yao, muwalipe kitu kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika Kikao cha Bodi ya Barabara tuliongelea barabara inayoanzia Sengerema inakwenda Bukokwa, Nyehunge hadi Nkome. Tulisema barabara hii itengenezwe, lakini haijatengenezwa. Hata Rais wa nchi ameshasikika akisema kwamba, barabara hii ni mbaya kuliko barabara zote nchini. Barabara hii ni ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi, tulitaka pia iwe na matengenezo lakini mpaka leo haipitiki, haina matengenezo, kule watu wanalima, wanashindwa hata kufikisha bidhaa zao mahali husika wakauza wakaweza kujipatia kipato.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, barabara hii aiangalie na aitengeneze bila kujali ipo kwa nani, mimi ni Mbunge wa Mkoa wa Mwanza, atengeneze barabara hii kwa manufaa ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa niongelee kidogo kuhusu matuta ya barabarani. Barabara nyingi zimekuwa na matuta makubwa na kila siku kukicha kunaongezwa mengine. Barabara hii ukiangalia kutoka Morogoro kuja Dodoma kuna mifereji mikubwa katikati ya njia. Ukiangalia kutokea Mlandizi kupitia kwa Matia kuna mifereji mikubwa ambayo imesababisha ajali nyingi sana. Mimi ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri, kuliko kuongeza matuta kwenye barabara, ni vyema basi ile gharama unayotumia kuongeza matuta, kama huna pesa za kufanya ukarabati mkubwa, uzibe ile mifereji iliyo katikati ya barabara, kwa sababu unapokuwa upande mmoja kuhama upande mwingine ukiwa na gari ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante lakini naomba Mheshimiwa Waziri azingatie kwa sababu na yeye ana familia na nyumba huko.

**SPIKA:** Amezingatia. Mheshimiwa Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Hokololo!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie Hotuba ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza, nijielekeze kwenye ukurasa wa 135, ambapo kuna barabara ambazo mara nyingi sana napenda kuzizungumzia kutokana na ahadi ambazo zimekuwa zinatolewa kwamba itajengwa.

Kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Magufuli, naona ametenga fedha kwa kiasi cha shilingi bilioni kumi kwa ajili ya barabara inayoitwa Kidawe - Kasulu – Kibondo – Nyakanazi, kilometa 310 ili iweze kujengwa. Kutenga fedha ni jambo moja, lakini utekelezaji kwa maana ya

fedha kutolewa ni suala lingine. Kibaya zaidi ambacho labda kidogo naona ni tatizo na nafikiri Watendaji wake wamemdanganya Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, kwamba, Mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu na nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, hakuna mkandarasi ambaye yuko *site* akiendelea na kazi ya ujenzi wa barabara hii. Hizo kilometa 50 ambazo zitaanzia upande wa Nyakanazi kuja Kibondo na kilometa 50 kutoka Kidawe kuja Kasulu, hakuna Mkandarasi *site*. Maomba Mheshimiwa Waziri pengine ucheki na Wasaidizi wako, kwa maana ya watu wa *TANROAD,* wakueleze huyu Mkandarasi ameenda lini. Kwa sababu tunafanya mawasiliano sisi na watu wakiwa Kigoma. Kwa kweli tuna kiu kuona barabara hii inaanza kujengwa. Kwa hiyo, tutashukuru sana kuona Mkandarasi yuko *site*, lakini sasa hivi hajaenda *site.*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, historia ambayo ilikuwa imejengeka ya barabara hii kuweza kutengewa fedha, mwaka huu sasa utakuwa ni wa tano mfufulizo. Isipojengwa barabara hii kwa kweli naomba wakati mwingine tutakapokuja kutumia lugha zenye ukali, msije mkatulaumu kwa sababu wakati mwingine kama binadamu una nyongo ni lazima utakasirika na unaweza ukajikuta unatumia lugha ambayo haimpendezi binadamu yeyote yule. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Magufuli ufuatilie barabara hii huyo Mkandarasi tumwone *site*.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika barabara hii, ninegependa nipate *commitment* ya Serikali, zile fedha za tangu mwaka juzi, shilingi bilioni 3.5 nazo zitatumika katika ujenzi wa barabara hii. Zile shilingi bilioni kumi za mwaka jana nazo zitaingizwa katika barabara hii na hizi shilingi bilioni za mwaka huu, kiasi kwamba walau tutakuwa na shilingi bilioni 23.5, kama zote zitakuwa *invested* na kila mwaka zikawa zinatengwa kidogo kidogo, ni imani yetu kwamba, Wakazi wa Mikoa ya Kigoma na Mikoa ya Kagera ambayo sisi ni majirani, tutakuwa watumiaji wakuu wa barabara ile zinaweza walau zikasogeza na kuharakisha kwa barabara hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nitaomba nipate ufafanuzi, ninashukuru kuona inatengewa fedha ila tunataka kuona kazi zikifanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ame-*suggest* kwamba kuwe na chombo kinachoitwa *Rural Roads Agency*. Ni muhimu sana kuwa na pengine Wakala wa Barabara Vijijini, kwa sababu barabara zilizo nyingi huko vijijini zina hali mbaya na ukijaribu kuangalia uwezo wa mamlaka za Serikali za Mitaa kuweza kuzihudumia barabara hizi ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tukubaliane kwamba wazo hili tulione ni wazo zuri na ni jema, kama kutakuwa na Wakala wa Barabara Vijijini litakuwa ni jambo zuri kama ilivyo kwa *TANROADS*. Tunaona *TANROADS* wakati mwingine kama fedha zipo wanafanya kazi nzuri. Naomba tupate ufafanuzi baadaye juu ya wazo hili, ulichukue na ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni *issue* ya malori, malori ambayo wakati mwingine yametajwa na Waziri Magufuli amekuwa anayapigia kelele yanabeba mzigo mkubwa. Ajabu Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amediriki kutofautiana na Waziri na Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Ujenzi ambaye ameamua kusimamia matakwa ya Sheria na siyo matakwa yake. Sheria ile Namba 30 ya Mwaka 1973, pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2001, ime-*specify* malori yabebe mzigo kaisi gani. Sasa leo pengine Waziri Mkuu atusaidie, kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alivyosema, kama Waziri Mkuu hana malori barabarani au ya rafiki zake au ana *share* kwenye makampuni haya, atuambie ni kwa nini ametoa agizo ambalo linakwenda kinyume cha sheria kwamba malori yaruhusiwe?

Ni wazi uamuzi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu haukuwa mzuri, ulikuwa ni uamuzi wa kifisadi, kwa sababu unafisadi barabara zetu na barabara zetu zinazidi kuharibika. Tutaomba tuweze kupata kauli ya Serikali, kwa kweli halikuwa jambo la afya kwa mtu yeyote mwenye akili nzuri. Barabara zinajengwa kwa gharama kubwa, lakini pia upatikanaji wa fedha hizi ni kidogo.

Mheshimiwa Magufuli, naomba niseme tu kwamba, usife moyo kuhusiana na *issue* hii, hata kama ni kiongozi wako amekupinga, lakini endelea kumwambia apende kuheshimu misingi na matakwa ya kisheria. Haiwezekani tukawa tuna-*rely* kwenye *opinion* za watu tu kwa sababu ni viongozi. Leo kilomita moja ya lami kuijenga tunaambiwa ni kati ya shilingi milioni 600 mpaka biloni moja. Sasa tuna-*invest* pesa nyingi kama Taifa kwa ajili ya ujenzi wa barabara halafu anakuja kiongozi mmoja kwa sababu ana mamlaka ya Uwaziri Mkuu, anatumia mamlaka yake vibaya; hili jambo halikubaliki, halikubaliki, hata kidogo. Waziri Mkuu anawajibika kuwaomba radhi Watanzania, ambao kodi zao zinatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara halafu wao wanatoa maagizo ambayo hayapendezi. Hii kwanza nafikiri imemfedhehesha hata Waziri wa Ujenzi.

Waziri wa Ujenzi hawezi kusema kwa sababu ni bosi wake, lakini watu ambao tunatathmini unaweza ukafanya *situation analysis* unaona kabisa ile ilikuwa ni *insubordination* na ilikuwa ni udhalilishaji kwamba huyu Waziri wa Ujenzi anachokifanya hakina akili, kitu ambacho siyo kweli. Amesimamia misingi ya kisheria, Waziri Mkuu ajisahihishe katika hili, tunataka tuone misingi na matakwa ya kisheria inaheshimika.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo, haya mambo matatu; la kwanza hilo la barabara yetu ya Kidawe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi, tunaomba tupate majibu ya Serikali kuhusiana kwa sababu Mkandarasi yuko kule *site* basi baadaye aweze…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Agness Hokololo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile; sijui kama yupo!

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na niipongeze Serikali kwa ujumla, kwa namna ambavyo imefanya, hasa katika kuhakikisha Tanzania sasa inakaribia kuwa kijiji. Kwamba, imeunganishwa katika Mikoa yote, naipongeza sana Wizara na Serikali yagu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye maeneo ambayo inahitajika kasi ya ziada katika kuhakikisha nayo pia yanakuwa kijiji kama ambavyo maeneo mengine yamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Madabida ameongea sana kuhusu Barabara ya Ndundu - Somanaga, lakini mimi nikumbushe, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amekiri kwenye Kitabu chake kwamba, Barabara ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi, ya kilomita 468, kwanza, ninaishukuru Serikali kwa sababu huko nyuma tulikuwa tunachukua hata mwenzi mzima ili kufika sisi nyumbani kwetu Masasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo hoja, mimi ni shahidi, mimi ni mdau; kilomita 60 za Ndundu - Somanga wote tunazijua, lakini tangu nimeimgia hapa, mimi siyo wa zamani, lakini 2011 nilisikia kuna fedha ziliwekwa, 2012, 2013, kila mwaka kuna fedha zinatengwa kwa ajili ya hii barabara.

Leo nimeona pia kwamba, baada ya Wananchi wanaotoka Tunduru, Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi, wote wanaohitaji kuja Dar es Salaam, wamenyeshewa siku kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kama mama ninaamini kabisa hata wewe machozi yangekutoka. Swali langu kwa Wizara, hizi kilomita 60, Mradi huu ulianza 2008, itatuchukua miaka mingapi kukamilisha? Barabara hii kilomita 468 ilianza mwaka 1900 na sasa naona ni takribani miaka 20 na fedha zilizotengwa ni bilioni 5.2, nina uhakika kile kipande kilichobaki sasa cha kilomita 12 kwa bilioni tano haiwezi kukamilika. *(Makofi)*

Sasa, hata yale matumaini, Naibu Waziri alipotembelea kule, kwamba barabara hii ingeweza kutengenezwa na kiuhakika kwa sababu nilikuwepo, kwamba zingechukua takribani siku 130 kukamilisha, bilioni 5. 2, ina maana inalala. Ina maana Wananchi wa Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara tuendelee kulala pale kwenye zile kilomita 12. Inasikitisha, akina mama wajawazito wanapotembea pale, wanaponyeshewa, adha zinazopatikana pale; hivi ni kweli athari zinazotokana na kumalizika kipande hiki cha Ndundu - Somanga, hizi kilomita 12 hazieleweki?

Sisi wenzenu Watu wa Mtwara, tunanunua boksi la *tiles*, lile linalounwa Dar es Salaam shilingi 7,500 kwa shilingi 32,000. Gharama za vitu tunavyovinunua madukani, vifaa vya ujenzi, inapanda mara nne, ni kwa sababu ya kilomita 12. Nauli zetu, mimi mwenyewe nimepanda basi kuthibitisha, nauli hata zile zinazotolewa na *SUMATRA* hazitekelezeki, kwa sababu ya kile kipande. Vilevile hata begi la kilo kumi tunatozwa nauli!

Jamani adha hizi, ninaiomba Serikali yangu, Mheshimiwa Magufuli, pamoja na jitihada zote na pongezi zote, tuhurumie sisi wajukuu zako. Tafadhali, inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa hilo linaeleweka na litafanyiwa kazi. Bilioni 5.2 haitutoi pale, lazima tufanye kitu kingine cha ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi, kilomita 209. Mwaka jana ilitengewa bilioni 3.2, mwaka huu bilioni tatu. Inatengewa fedha za upembuzi yakinifu, huu upembuzi yakinifu mbona hatuoni Wataalam wakipita kule unafanyikia mezani! Utakwisha lini na ujenzi wake utaanza lini! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi, kilomita 200; ninaipongeza Wizara, upembuzi yakinifu umekamilika, lakini tunaambiwa fedha zitakapopatikana, ukarabati utafanyika. Yale maroli ya mabomba ya gesi, jamani mnayajua uzito wake. Sasa barabara ile ninavyoona, badala ya kufanyika ukarabati hapo fedha zitakapopatikana ajaliwaye, pengine sasa itakuwa ni kujenga upya. Jamani, tukarabati kwanza, tuzibe ufa kabla hatujajenga ukuta.

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna Barabara ya Masasi – Mpeta – Newala, kwa kweli ilianza vizuri na ile lami imeishia pale kwenye Kijiji kile cha Mchaka. Mradi huu ulikuwa unaelekea ufike kule Lupaso kwa Mheshimiwa Rais Mstaafu, Mzee Mkapa. Mimi niiombe sana Serikali yangu, kwa kweli ni heshima, siyo tu kwako Mheshimiwa Magufuli, ni heshima kwa Serikali, huu Mradi ukikamilika. Ninaomba sana, tutafute namna ya kuwezesha ili barabara hii ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara zetu sasa za kutoka Mtwara – Newala – Masasi – Nachingwea, kwa kweli ilivyo sasa, Watu wa Nachingwea hawawezi kufikiwa, wa Liwale ndiyo kabisa. Mimi niombe sana, nimeona kuna kilomita 11 huku ambazo hizi ni za kiwango cha changarawe, zile za kutoka Nachingwea - Lukuledi, lakini, Mheshimwia Waziri nikuombe na kule unaweza ukapata vitu vizuri vipo kule, mbaazi na samaki nchanga; hebu tembelea ukajionee hali halisi kule ilivyo sasa. Ule Mto Lukuledi unaendelea kukua na mabadiliko ya tabianchi hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, nikiamini kabisa, Serikali inakwenda kuyafanyia kazi haya na majibu yatakuja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile; hayupo! Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Brigadia General Hassan Ngwilizi!

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, ila niombe ingefaa sana ungekuwa unatutaja mapema, kwa sababu nilikuwepo lakini ndiyo nasikia.

**SPIKA:** Nimemtaja aliyefuatia hakuwepo, ndiyo maana nikakuita anayefuatia. Nilikuwa nimeorodhesha lakini hawakuwepo, kwa hiyo, ndiyo maana unafuatia wewe. Anayefuatia Mheshimiwa Brigadia General Ngwilizi, halafu atafuatia Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi naomba nichangie Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu yake nzima, kwa kazi kubwa sana wanayoifanya ya kufanya mapinduzi ya kuiunganisha nchi yetu kwa barabara nzuri za lami kwenye maeneo yaliyo mengi.

Ukisoma Kitabu chake naamini, pengine ni Kitabu cha Hotuba kikubwa kuliko vitabu vyote ambavyo hadi sasa vilishasambazwa hapa Bungeni. Hii ni kuonesha tu kwamba, kuna kazi nyingi zinazoendelea.

Ninaushauri kwenye maeneo machache; la kwanza, inavyoonekana suala la vipaumbele linaanza kuwa tatizo katika utekelezaji wa Miradi ya Barabara, kwa sababu Kitabu hiki kimesheheni barabara nyingi sana na nyingi zimepewa fedha kidogokidogo sana. Mbaya zaidi, kuna baadhi ya barabara muhimu sana Kitaifa, hazimo kabisa.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015, imeweka ahadi ya kuunganisha Mkoa wa Shinyanga kwa barabara mpya za lami, kuunganisha Mkoa huu na Mkoa Mpya wa Katavi, kuunganisha Mkoa huu na Mkoa wa Tabora, pamoja na kuunganisha Mkoa huu na Mkoa wa Geita. Kwenye Ilani ya CCM tuliahidi kwamba, katika kipindi hili tutaanza upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kahama kupitia Mgodi wa Bulyang'hulu hadi Geita. Vilevile tuliahidi kuanza upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kahama, kupitia Bukene - Mambari hadi Tabora. Vilevile tukaahidi kutakuwepo barabara ya lami inayotoka Kahama kupitia Kaliua hadi Mpanda. *(Makofi)*

Huu ni mwaka sasa wa tano wa kibajeti katika utekelezaji wa hayo tuliyoyasema. Kitabu hiki pamoja na ukubwa wake, pamoja na umuhimu wa barabara hizo ambazo zinaunganisha Mikoa, hakijaonesha fedha nyingi ukiacha fedha kidogo kama milioni 200 tu kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa Barabara ya Kahama - Geita, barabara zingine zote nilizozisema hazijatajwa wala kuwekewa fedha.

Ukiangalia kwenye Kitabu hiki, kuna barabara zingine za kata, nisingependa kutaja kwa heshima ya kila Mbunge ambaye ameomba fedha hizo. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kwamba, barabara hizi ambazo zinaunganisha Mikoa ni vizuri sana zikapewa kipaumbele. Ninaamini bado tuna bajeti moja mwakani, lakini pia hata sasa hivi bado hatuja-*conclude budget process* kwa sababu Bajeti Kuu ya Serikali haijapita. Niombe katika hatua zinazoendelea, kufanyike marekebisho yatakayowezekana ili kuweza kurekebisha barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nizungumzie Barabara ya Kahama – Geita. Barabara hii imekuwa ni tatizo la muda mrefu sana na hoja ya msingi hapa ni matumizi ya barabara hii, ambayo inaunganisha Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga, lakini inaunganisha maeneo makuu ya uchumi; Mgodi wa Bulyanhulu na Mgodi wa Geita. Matumizi ya barabara hii katika kuhudumia migodi hii, inahusisha kupitishwa magari makubwa yenye mzigo mkubwa na inatimua vumbi sana kwa Wananchi na wengi wanaathirika kiafya.

Kumekuwepo mazungumzo yakihusisha Serikali, Wananchi pamoja na Mwekezaji wa Mgodi wa Bulyanhulu na Geita. Nimekuwa nikimshauri sana, kaka yangu Mheshimiwa Magufuli, nakujua na nakufahamu vizuri sana, na ni mtu wa kuchukua ushauri, niliwahi kukufahamisha kwamba, sisi kama Wananchi wa Kahama, tulishafanya mazungumzo na Mgodi wa Bulyanhulu na wakaonesha utayari wa kuweka *juice* ya miwa *(molasses)*, ambayo ingesaidia ku-*suppress* vumbi kwenye maeneo ya makazi.

Niliwahi kuuliza swali hapa na kwa bahati mbaya inavyoonekana teknolojia hii bado haijafika kwenye Wizara yako, lakini ukifika maeneo ya Kidatu, maeneo ya kule Kagera, ambako kuna mashamba ya miwa, wanatumia sana teknolojia hii na Mgodi ulishaahidi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, suala hili ulitilie maanani, Mgodi ulikwishakuahidi toka mwaka 1997, waliposainiana mkataba na Serikali wa kuanza uchimbaji pale Bulyanhulu, ni upande tu wa Serikali kuwasukuma ili watekeleze wajibu wao.

Sisi kama Wananchi tuna waibu wa kukukumbusha na tunaamini tunakukumbusha kwa njia za kiungwana sana, lakini uungwana nao una ukomo. Najisikia vibaya sana kufika mahala nikasema kwambam sasa ninasita kukubali bajeti yako, kwa sababu ninajua kazi ambazo umezifanya, ninaamini unaweza. Ninakuomba tusifike huko, tafadhali kaa na Mgodi wa Bulyanhulu na Geita, wekeni mkakati wa kujenga barabara hii katika hatua za awali angalau kuondoa vumbi ambalo linawasumbua Wananchi na baadaye kupitia Bajeti ya Serikali na Wadau wengine, muweze kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni suala la uharibifu wa barabara. Nizungumzie kwa kifupi sana; barabara zinaharibiwa kwa kuzidisha mizigo, si kwa ile asilimia tatu ya nyongeza ambayo imekubalika kwenye mazungumzo yaliyotokea miaka ya nyuma, lakini kwa kiasi kikubwa ni kutokana na rushwa. Magari yanayopita yanakuwa na uzito mkubwa sana. Kwa hiyo, nataka nikuombe sana, pamoja na kazi nzuri uliyofanya na umesema kuna watumishi zaidi ya 400 kwa jinsi nilivyosikia jana, ambao wamechukuliwa hatua, naomba uendelee kuchukua hatua. Nilikuona mara moja tu, ulikwenda pale Kibaha na lile pama usiku na ukaweza kupata mambo makubwa.

Sasa naomba undelee kufanya hivyo, nenda mizani mingine mingi zaidi kuna matatizo makubwa. Ukifanya hivyo, mkaendelea kudhibiti mianya ya rushwa itasaidia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni suala la ulipaji wa wakandarasi wanaofanya kazi kwenye barabara hizi. Serikali imeji-*overstretch,* lakini pia fedha zinazotoka ni kidogo sana. Wakandarasi wadogo hawa ambao ni Watanzania, tunawahimiza wajiunge katika vikundi waweze kupata kazi kubwa kubwa, wengi wao mitaji yao wanaikopa kwenye mabenki. Sasa hivi ukisikiliza karibia kila eneo, kila *Regional Manager,* anadaiwa fedha nyingi kweli kweli, hasa hawa wakandarasi wadogo, tunapowakopa, kwa sababu wao wanapofanya kazi, wanakopa mafuta, wanakopa vitu mbalimbali. Serikali si vizuri ikawa inawakopa wakandarasi, iwalipe haraka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Brigadia General Ngwilizi kama yupo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Shah kama yupo.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naomba nimshukuru *Allah Subhanahu Wataala,* kwa kunipa afya njema asubuhi ya leo ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Aidha, naomba nimpe pole Mheshimiwa Waziri Magufuli, kwa ajali aliyoipata alipokuwa kwenye helikopta wakati akiwa kazini, Mwenyezi Mungu, ataendelea kukunusuru kaka yangu. *(Makofi)*

Vilevile naomba nikushukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kutupatia kilomita moja ya lami pale Kondoa Mjini; nashukuru sana. Hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, nashukuru. *(Makofi)*

Sasa naomba nianze kwa barabara yetu ya Dodoma – Mayamaya. Mwaka jana mwezi wa Aprili, niliuliza swali la msingi, je, Barabara ya Mayamaya - Dodoma itakamilika lini kwa kiwango cha lami? Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu kwamba, ifikapo mwisho wa mwezi Septemba, Barabara hiyo itakamilika. Sasa ni miezi minane Barabara hii haijakamilika; je, itakamilika lini ili magari yaweze kupita bila usumbufu wowote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, Mheshimiwa Waziri, naomba tena leo ni siku tofauti sana, nikushukuru tena, kwa sababu tarehe 2 Desemba, 2013, ulitualika katika hafla ya uwekaji saini kati ya Serikali yetu na Makandarasi ambao wamepatikana kukamilisha Barabara ya kutoka Dodoma mpaka Babati. Ulieleza kwamba, *mobilization* itakuchukua miezi mitatu na sasa miezi mitatu imeshapita sana. Pamoja na kwamba, makandarasi hawa nimepita nimeona wameshajenga makambi, wameshaleta vifaa mbalimbali, mashine na mambo mengine, wameweka mpaka mchanga, lakini kazi ya ujenzi wa barabara haijaanza.

Tunaomba tuone kazi ikianza, kwa sababu makandarasi hawa wamepewa miezi 33 kukamilisha kazi. Sasa kama hawataanza mapema, maana yake ni kwamba, miezi 33 itafika na barabara yetu hii itakuwa bado haijakamilika. Je, wanaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile makandarasi hawa naomba wafahamishwe kwamba wawachukue wenyeji wa maeneo yale, wafanye kazi ambazo wanaweza kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokwenda kwenye Kambi ya Kolo, walinifuata Wananchi, wakasema mbona tunaona watu wanachukuliwa kutoka maeneo mengine, wakati sisi tupo! Mheshimiwa Waziri, tafadhali, Wananchi hawa nao waweze kunufaika na ujenzi huu wa barabara. Hii ndiyo nafasi pekee ya Wananchi hawa nao kuweza kupata kazi ambazo wanazimudu, waweze kufanya na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, jambo hili nimelizungumza mara nyingi, mwaka 2010, Mheshimiwa Rais wetu, alipokuwa katika Kampeni za Uchaguzi, alipokuwa pale Huruwi, aliahidi kwamba, barabara ya kutoka Ntundwa kuja Huruwi mpaka Kashi, itapandishwa hadhi na itachuliwa na *TANROADS*. Hatua zote zimeshachukuliwa, imepita ngazi mbalimbali, lakini hadi ninapozungumza leo, barabara hii bado haijachukuliwa na *TANROADS*. Tangu mwaka 2010 ahadi hii Mheshimiwa Waziri, naomba basi, tuheshimu ahadi za Mheshimiwa Rais wetu jamani. *(Makofi)*

Vilevile tunazo barabara ambazo tumekwishaziombea zipandishwe hadhi na barabara hizi zinatoka Wilaya ya Kondoa zinakwenda katika Mkoa wa Manyara; kwa hiyo, zinakidhi vigezo. Barabara moja inatoka Mnenia - Kikore, inaingia Galapo, tumeshaiombea, bado haijapandishwa hadhi. Barabara nyingine inatoka Serya inakwenda mpaka Bereko, haijapandishwa hadhi.

Barabara nyingine inatoka Kinyasi Majengo - Chubi mpaka Babati. Mheshimiwa Waziri, tumeshaziombea zaidi ya mara mbili, hazijapandishwa hadhi, tunaomba basi zipandishwe hadhi. *(Makofi)*

Vilevile, tunalo Daraja la Munguli, ambalo lilifunguliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais. Lipo katika barabara inayotoka Mtilyangwi mpaka Kondoa. Barabara hi tayari imekwishachuliwa na *TANROADS*, nashukuru sana, lakini lile daraja sasa pale lilipo, mchanga unakaribia sasa kufunika hata daraja na hili nimeshaliombea, tumeliombea kwa maandishi kwamba ule mchanga uondolewe.

Mimi naamini mvua itakayokuja sasa mchanga utafunika daraja na ukifunika daraja, daraja hili litakuwa katika hali mbaya sana, litabomoka. Tukizingatia kwamba, daraja hili halina tatizo lolote, isipokuwa tu huo mchanga ambao unazidi kuja juu na limefunguliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, hebu tumpe heshima yake basi Mheshimiwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Itakuwa ni aibu iwapo mchanga utafunika daraja na daraja lile livunjike katika muda mfupi kabisa.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni ni aibu iwapo kama mchanga utafunika daraja na daraja lile livunjike katika muda mfupi kabisa. Mheshimiwa Waziri mimi nasema hivi, mimi nakuamini, nakuamini sana. Na pia nimeona pesa ambazo mmezitenga katika hizi barabara zetu mbili; Mela - Bonga, Mela - Mayamaya, nimeona pesa imetengwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, ndiyo maana nikasema leo nitakuwa tofauti sana ndugu yangu. Kwa hiyo, naomba nimalizie, nisipigiwe kengele, nikushukuru sana wewe, nimshukuru Naibu Waziri, nimshukuru Wakaii**,** Katibu Mkuu, na nimshukuru meneja wa TANROADS wa hapa Dodoma. Ahsanteni kwa kazi nzuri mnayofanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Kwanza kabisa na mimi naomba niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kusimama hapa na kuyasema haya kwa niaba ya wananchi wa Mafia. La pili nikusukuru wewe Mheshimiwa Spika, usione tabu kwa niaba ya Wabunge wote, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Wafanyakazi kwa jinsi mlivyokuja kunipa pole na kuwepo katika maziko ya mama yangu mzazi, nawakushukuru sana na Mwenyezi Mungu atawalipa mema wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niseme upande wa Wizara hii ya Ujenzi kwangu mimi nina mambo matano ambayo nitaomba Mheshimiwa Waziri ayaangalie sana tena kwa huruma. Wala siwezi kutamka kwamba naondoa shilingi au kufanya lolote, isipokuwa, la kwanza kabisa, kwa heshima zote, Mheshimiwa Spika nakuambia wewe utupe kibali cha Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Waziri wa Maji, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Uvuvi pamoja na Wenyeviti wa Kamati na ikiwezekana pamoja na Wenyeviti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya TANROADS. Naomba sana, siku ya Jumamosi utupe kibali, mimi niko tayari kuweka rehani hata kitu changu chochote nipate usafiri wa ndege kutoka Dodoma au Dar es Salaam kwenda Mafia wakaone wenyewe hali ilivyo na kushuhudia jinsi mvua ilivyotuathiri na sisi tuko Kisiwani. Kwa hiyo naomba hili la kwanza, Mheshimiwa Magufuli nakuomba sana siku ya Jumamosi tuandae ziara ya kwenda Mafia asubuhi na jioni utarudi, wala hutopoteza muda katika kuhangaika, maana naona mna kazi nyingi ambazo zinasababisha pengine hamupati muda wa kuweza kutembelea maeneo ya kwetu. Kila siku tunasikia ziara, mnakwenda huku, mnakwenda huku. Lakini hebu keshokutwa Jumamosi, kwa gharama zangu kama ninyi mtakuwa hamna fungu katika Wizara yenu au

katika mifuko ya TANROADS au Road Funds kuweza kwenda Mafia. Niko tayari kupata gharama hizo hata kwa deni, lakini twendeni mkaone hali halisi ya mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru barabara ya Utende – Kilindoni imetengewa shilingi bilioni 2.4. Lakini kwa taarifa ambazo nimezipata leo asubuhi, wale wajenzi Chicco mpaka hivi sasa wanadai shilingi bilioni 3.4.

Kwa maana hiyo, hizi fedha zikienda wanalipwa na bado watakuwa wana deni na kazi italala, na hali mbaya, tufanye nini? Sasa ili tukayaone haya ni bora ndiyo maana nikakuomba Mheshimiwa, twendeni kule tukakae na viongozi wenzangu wa Wilaya pamoja na wakandarasi na wale washauri ili tuweze kujua ni jinsi gani ya kuweza kutatua tatizo hili na barabara hii iweze kujengwa.

La pili, katika ujenzi huu wa barabara kuna miundombinu ambayo ilikuwepo, *okay*, wenye nyumba baadhi yao wamelipwa wengine wako katika mchakato wa kulipwa. Kuna watu katika maeneo ya Utende wameomba kulipwa minazi yao ambayo ilipandwa zaidi ya miaka 70, lakini utaratibu unasema haukubaliki kwa sababu wako ndani ya barabara. Kwa kuwa ilitumika sheria ya 1932, Mafia kipindi hicho, pengine barabara hizo zilikuwa zikiitwa barabara za miguu, hata neno Wilaya halikuwepo.

Sasa nashangaa sheria ile kutumika katika maeneo ambayo hata Wilaya Mafia ilikuwa kama Tarafa katika Wilaya ya Rufiji, na minazi ilipandwa kipindi hicho. Kwa hiyo naomba muangalie wale wananchi ambao wanashughulika na hilo.

La tatu, Mheshimiwa, kwa heshima zote, nakuomba sana, ulinipa milioni 300. kwenye tuta lile. Lile tuta limengwa limeishia nusu, kwa hiyo hali ilivyo ni mbaya zaidi. Nakuomba sana utuongezee milioni 350 likamilishwe. Halafu hii ni ahadi ya Rais, naona haya kusema, wenzangu wamesema hapa kwamba Rais ametoa ahadi lakini watu hawashughulikii. Mimi nasema ulijitahidi, lakini tumalizie ili tukamilishe na tuondoe tatizo hili ambalo lipo sasa hivi linawakabili wananchi wa Kijiji cha Jojo na Banja wavuke katika kisiwa kikuu cha Mafia maeneo ya Jimbo. Kwa hiyo nakuomba sana katika hili uweze kuliangalia na tuweze kuona ni jinsi gani ya kuweza kututatulia.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lile la kukatika shimo, nafikiri taarifa unayo. Nashukuru sana wataalamu wako wamefika, lakini hali ni mbaya. Mheshimiwa, wakati nilipokuwa nikiwaambia mwaka wa jana, gharama yake ilikuwa haifiki hata milioni 30 au 50. Leo si chini ya bilioni moja kwenda kulifukia shimo lile, na kila tunavyozidi kukaa athari yake inakuwa kubwa, uwanja unaondoka.

Sasa ndiyo maana naomba tena, siku ya Jumamosi, naomba tuandae safari ya kwenda Mafia Wizara zote hizi kama nilivyozitaja, ya kwako, mawasiliano, na wengine wale twende tukaangalie mambo mengine ili tukirudi tuyaamue yote kwa pamoja na kuona ni jinsi gani ya kuweza kuyafuatilia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, mwaka wa jana nilikuomba kwa heshima zote Mheshimiwa Magufuli. Tunaomba kivuko, Mafia ni Kisiwa, biashara hizi za wananchi wa kawaida, akina Said Salum Bakhresa kuja kule ni mtihani. Sasa kama ulivyoweza kusaidia vivuko katika maeneo mengine, hebu na sisi Mafia tuangalie, na sisi pale kuna watu zaidi ya 60,000, lakini wapo Watanzania Bara ambao na wao wanakwenda. Kwa hiyo Mheshimiwa tunakuomba, hili suala la kivuko hebu mwaka huu, sijui kama itakuwaje, naona kamati ya Bajeti tutakwenda kukaa na kujadili katika mapitio. Tunaomba uanze kutuangalia na kutuandalia ujenzi wa kivuko kati ya

Mafia na *Mainland* huku, kwa maana ya kati ya Kilindoni na Nyamisati. Hili naomba sana uliangalie na sasa tuanze.

La mwisho kabisa, sisi abiria wengi wa Mafia tunatumia Bandari ya Nyamisati. Maeneo ya Nyanjate kwenda Nyamisati Bandarini pamevurugika kabisa. Kwa pesa hizi za milioni 16 hazitofanya lolote. Kwa hiyo naomba hili mtuangalie, na hii Mheshimiwa ndiyo barabara yetu kuu. Kwa heshima zote naomba sana pale pakitengenezeka, na lile eneo la kina cha maji zinapokuja kufungia meli pakitengenezwa, tuna mpango na watu wa TPA, wamesema watatusaidia tuweze kupata usafiri wa kwenda na kurudi.

Mheshimiwa kwa heshima zote naunga mkono hoja hii na Mungu atakubariki.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza niseme dhahiri hapa kuwa naunga mkono hoja ya Wizara hii, na ninampongeza sana Mheshimiwa Magufuli, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Bodi hii ya *TANROADS,* Wakandarasi wote, na hasa Meneja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa namna kwa kweli wanavyotoa ushirikiano mzuri sana kwa viongozi, Wabunge wote wa Mkoa huu kujaribu kuboresha miundombinu hii.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nichukue nafasi kuwapongeza wakandarasi wazalendo ambao kwa kweli wameonesha uwezo mkubwa sana. Wako wengi; yuko Scoll, ndugu Vicent, wako wengine Estine na wale ambao sijawataja basi nimewaongeza katika orodha ya wakandarasi wazalendo ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam ni Mkoa ambao ndiyo unaoingiza mapato ya kitaifa zaidi ya 80%. Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam ikifa, uwezo wa Dar es Salaam kuweza kuisaidia Mikoa mingine utakuwa ni mdogo sana.

Mimi naiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Mheshimiwa Magufuli, tuwe na mpango maalum kama vile ilivyofanywa kwenye Mkoa huu wa Dodoma, mkopo maalum kwa miundombinu kwenye Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mkopo huu unalipika na Mkoa wenyewe wa Dar es Salaam. Tukipatiwa kupitia Wizara hii, au Waziri mwenyewe Mheshimiwa Magufuli asimamie, tupate bilioni 400 za mkopo, *dollar* takriban 250, tuboreshe miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam, pesa hizi zitajilipa kutokana na *property tax (kodi za majengo)* katika Mkoa wetu huu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tukiboresha miundombinu kwenye mitaa, kwenye nyumba, wananchi wataweza vile vile kuongeza kutozwa ada zaidi ya kodi za majengo baada ya kuona miundombinu imeboreka.

Kwa hiyo kitu hiki kinawezekana kabisa, hatuhitaji hata Serikali kulipa deni hili, deni hili litalipwa na wakazi wenyewe wa Dar es Salaam. Tukiboresha Dar es Salaam tutaweza sasa kusaidia kuboresha maeneo mengine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Uhuru. Naipongeza Serikali, kutoka Mandela mpaka Malapa wameshatengeneza vizuri, zimebaki kilometa labda tatu tu kutoka daraja la Malapa mpaka kufika *Clock tower*. Hii barabara imekufa. Najua jana Mheshimiwa Magufuli kaahidi kuwa ameiwekea, wekea lakini barabara hii sasa inataka iwe *resurfaced* upya.

Mheshimiwa Spika, ukifika pale kipande cha Shule ya Uhuru, juzi nilikuwepo pale, magari yananasa, huwezi kuamini, barabara ya mjini, kwenye jimbo la Ikulu barabara zinanasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba, na juhudi zote hizi ambazo Mheshimiwa Magufuli anazo na Mkoa waitazame upya suala hili la barabara ya Uhuru.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye Jet Kona – Davis Kona – Temeke. Barabara hii tunasukuru sana ilikuwa kilometa 13, zimeshajengwa kilometa 10, bado tatu tu. Hizi tatu zikimalizwa italeta sura nzuri sana kwenye Mkoa huu na kuwapa watu imani kuwa Wabunge wao na Serikali yao inawatazama.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara hukohuko Temeke eneo la Mashine ya Maji ambayo nayo vile vile nataka itazamwe.

Mheshimiwa Spika, lingine, maeneo ya Kinondoni, eneo la Mapipa, wananchi wengi wanafikiri eneo la Mapipa limeachwa kwa sababu eneo la Mapipa ni barabara ya Halmashauri, na uwezo wa Halmashauri ni mdogo. Kwa hiyo Mapipa na maeneo mengine haya yote yataingizwa katika huu mpango aliosema wa kuboresha Dar es Salaam kama mkakati uliofanywa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, leo ukiingia Dododma na ndege inapendeza, kwa sababu kuna maeneo zimewekwa lami hakuna nyumba, ni viwanja tu, na huu ndiyo mkakati mzuri wa Serikali kuweka *utilities*, kuweka miundombinu halafu mwananchi akija kununua kiwanja unaweza ukamuuzia kwa gharama kubwa kwa sababu miundombinu pale tayari inakuwa imeshawekwa. Kwa hiyo mimi nilikuwa naomba, naweka mkazo kabisa kuhusu suala hili la *project* maalum ya Mkoa wa Dar es Salaam, na deni hili litalipwa.

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Magufuli, Dar es Salaam sasa hivi ina uwezo wa kuchangia kodi za majengo shilingi bilioni 25 kwa mwaka. Sasa shilingi bilioni 25 kwa mwaka kwa mikopo hii ambayo tunapewa na Serikali ya China na benki kubwa, tunahitaji siyo zaidi ya miaka 15, tunaweza tukalipa deni hili na ukaiona Dar es Salaam inapendeza kwa barabara, kwa madaraja, kwa mitaro, ili sasa tuweze ku-*generate revenue* zaidi kuzipeleka kusaidia Mikoa mingine ya wenzetu nje ya hii Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi hoja yangu ilikuwa ni hiyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri kuhusu barabara ya Uhuru, lakini barabara ya Uhuru imeachwa siku nyingi sana. Naomba, nimezungumza na Meneja wa *TANROADS,* imeanza tangu jana usiku, leo anaishughuilikia, na labda kesho itakuwa imekwisha.

Kwa hiyo mimi nakushukuru sana, nakuunga mkono, nakuombea kila la heri, lakini hili suala la mkopo huu kwa *project* ya Dar es Salaam naomba wewe na wenzio.

Lingine vile vile, mnaweza mkaanzisha *road toll*. Tunapoteza pesa nyingi sana, tuna magari hapa yanapita barabara hii ya Dodoma – Morogoro, ni zaidi ya magari 150,000 kwa siku. Hivi magari haya yakichangia 5,000 tu tunajipatia si chini ya bilioni 300 kwa mwaka. Barabara hizi tukikuachia wewe peke yako na Serikali hamuwezi, ni lazima wananchi wenyewe wachangie barabara hizi, na njia ni hiyo ya wao kulipia *road toll*.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam leo kuna magari yanazunguka kutoka Tegeta mpaka mjini ni magari 50,000 kwa siku. Waingereza wenzetu wameweka *congestion fee.* Mwingine anatoka Tegeta anakuja mjini kuzurura tu, wanaleta foleni kuja kupiga mizinga mjini. Kwa hiyo

mimi nilikuwa nafikiri hawa wangewekewa *congestion fee,* watakuwa hawaji kujaza barabara hizi. Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Desderius Mipata, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis. *(Kicheko)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Na mimi naungana na wenzangu kumpongeza sana Waziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri zinazofanyika nchi nzima. Kwa kweli kazi ni nzuri, lakini nina changamoto zifuatazo:- Ninaanza na barabara ya Sumbawanga – Kanazi, Kanazi – Kizi Kibaoni na Kizi – Starike – Mpanda.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zimeanza kujengwa muda sasa, na zinatengewa pesa kidogo kidogo, mwanzo zilikuwa bilioni nne ikaja bilioni sita sita, leo ni nane nane na zinakwenda kama mapacha, lakini maendeleo kwa kweli yamekuwa siyo mazuri sana. Najua chanzo cha fedha hizi ni sisi wenyewe, vyanzo vya ndani havina nguvu sana lakini basi tuwe wakweli kwa wananchi tuwaambie, hizi barabara zinakamilika lini? Kwa sababu wanakuwa wanatuambia hawaelewi; hawaelewi barabara hizi zinaisha lini, na sisi tunawapa ahadi kwamba zitakwisha, lakini kazi zinasimama kila wakati. Namuomba Mheshimiwa Waziri azitilie mkazo barabara hizi, ni muhimu sana kwetu sisi na wananchi wanaamini, na kazi yako inaonekana.

Lingine muhimu katika barabara hizi, tunadhani ututembelee. Bajeti iliyopita nilikuomba ututembelee na ukatuahidi. Unapotembelea kasi inaongezeka kwenye barabara, kwa hiyo utusaidie kwa kututembelea.

Katika ujenzi wa barabara hii pia kuna mgogoro pale Chala. Mgogoro ule nilijaribu pia kuzungumza mbele ya Mheshimiwa Rais, akiwepo Naibu Waziri, na Naibu Waziri akaagizwa kwamba angalieni, kwa nini mgogoro wa Chala uwe wa peke yake peke yake tu, sehemu zote mmeangaliwa vizuri!

Kwa hiyo mimi naiomba Wizara ione umuhimu wa kulimaliza. Tume nyingi sana zimeundwa na Mkoa kuhakikisha kwamba changamoto hii inaondoka, lakini bado majibu hakuna. Mara ya mwisho tumefanya kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa, tukaangalia *option* mbalimbali ambazo zilikuwa zimeandaliwa na TANROADS, na tukapendekeza *option* ya tatu kwamba pengine hii ingeweza kusaidia, na tukaleta mapendekezo. Mpaka sasa wananchi wa Chala wanasubiri bila kupata majibu; naomba majibu yapatikane.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ahadi za Mheshimiwa Rais. Ahadi za Mheshimiwa Rais kwenye barabara ambazo ziko kwenye jimbo langu. Iko barabara ya Kitosi – Wampembe kilometa 67, barabara ya Nkhana – Kala Kilometa 68. Alipokuja Mheshimiwa Rais mwaka 2010 aliahidi kwamba barabara hizi zitapitika mwaka mzima; na kwa kujua hilo Halmashauri kila ikipendekeza pesa zinakuwa hazipatikani. Waliomba tuweze kuzipandisha hadhi zihudumiwe na Mkoa. Mkoa ulikubali kupitia Bodi ya barabara na tukapeleka kwenye Kamati ya Kitaifa ambayo pia ilikuja ikakubali kwamba ina vigezo vya kutosha, tukawa tunasubiri huko juu.

Mpaka ninavyosema hivi, barabara hizi ni changamoto kubwa, na juzi alipokuja Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM alikwama kwenye barabara hizi, na akaniahidi kwamba nitakuwa Mbunge wa pili kuzungumzia barabara hii, na barabara hizi zimechukua muda mrefu na mimi zimenichukulia muda mwingi kuzisema mara kwa mara katika Bunge hili. Kwa hiyo naiomba Serikali, wekeni utaratibu wowote zipitike, hatuwezi kueleweka tunapofika kwenye uchaguzi. Hazipitiki leo, Katibu Mkuu amekwama saa sita kwenye barabara hii na vyombo vya habari vyote vilionesha, na akahangaika sana, na akaahidi wananchi wale kwamba kwa kweli

hii ni changamoto na nimeipata, naenda kuwaona watu wenye dhamana ili waweze kuziangalia.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ukiziacha kwenye Halmashauri hazitaweza kujengwa, ni ngumu sana, zina mazingira magumu sana. Lakini kule zinakokwenda kuna watu wananishi katika hali ya umasikini, wanategemeana, ni ukanda ambao uko tofauti, wanazalisha kitu kingine na hawa wanazalisha kitu kingine, wanategemeana sana, ni za muhimu Mheshimiwa Magufuli. Niliwahi kukona, pia ukanishauri niweze kuwaona watu wa TAMISEMI, ni kweli niliwaona, namshukuru Katibu Mkuu alinipa hela kidogo. Katika makisio yaliyowekwa ya bilioni moja moja kwa barabara, tumepata milioni 400 kwa barabara moja na nyingine milioni 400. Kwa hiyo hata baada ya matengenezo yaliyofanyika bado tunakwama, magari yanashindwa kupita. Naomba nizisemee barabara hizi kwa hisia za juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni barabra hii ya Tunduma. Kutoka Laela kuja Sumbawanga ujenzi wake siyo mzuri sana. Yule Mkandarasi anaenda taratibu, ni kweli kuna pesa, lakini utaalamu hasa ndiyo shida yangu, viraka ni vingi kupita kiasi. Ninahisi kama mngekuwa mnatemebelea hii barabra hizi chanamoto zisingekuwepo. Ninaomba mtuahidi, mtutembelee ili tuweze kupata ufanisi unaotakiwa.

Mheshmiwa Spika, mwisho niungane na wenzangu wanaosema kwamba barabra za vijijini ni muhimu sana. Hizi barabara zinazoenda kwenye uzalishaji na kusogeza huduma kwenye barabara kuu, zinakuwa hazihudumiwi ukiziacha kwenye Halmashauri. Naomba Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini. Wakala huyo atatusaidia na kuwasaidia wakulima. Wapo wakulima katika maeneo mengi wanakosa huduma hii na kwa maana hiyo hatuwezi kuboresha kilimo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pale kwangu, kutoka Kasu kwenda Katani, kutoka Katani kwenda Chonga, Chonga kwenda Myula, ni barabra inayounganisha wakulima wengi sana, lakini inahudumiwa na Halmashauri na Halmashauri haina nguvu ya kutosha. Kwa hiyo, unakuta inakata, kama mwaka huu ilikata karibu kipindi chote cha masika, wananchi hawawezi kusafiri kwenda huku wala kule na Halmashauri haina pesa. Kwa hiyo, pangekuwa na Wakala inayoshughulikia Barabara za Vijijini, msisitizo na utendaji ungekuwa umeboreka zaidi. Kwa hiyo na hili mliangalie, sijashauri peke yangu, nimeona wenzangu wameshauri, bajeti ya mwaka jana pia nilishauri.

Mheshimiwa Spika, mnapoanzisha Wakala wa Barabara tunaona kabisa jitihada zinakuwa kubwa. Wakala wa Mkoa wanafanya vizuri kwenye barabara zote za Mkoa, ni nzuri kabisa hata hapa mimi sina sababu ya kuzisemea sana. Isipokuwa Barabara ya kutoka Chala kwenda Kirando kwenda mpaka Namanyere – Kirando, hapo tuna changamoto ya kutosha. Penyewe pale mmetutengea fedha, mimi naziona zile fedha pengine zinaweza kuwa kidogo. Lakini, zikisimamiwa vizuri zinaweza kufanya kazi nzuri. Kipindi kilichopita pametusumbua, hapajawa pazuri sana, pamekuwa pakitusumbua, hapapitiki vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ningeomba nikusifu kwa utendaji wako mzuri, lakini sasa utusikilize hasa sisi tunaokusemea mazuri. Haiwezekani barabara zikachukua muda mrefu sana bila kutekelezwa. Sasa hivi inakuwa mwaka wa sita tunaenda, barabara hazikamiliki na wananchi wana hamu ya kuona kwamba wanaleta mabadiliko makubwa sana katika suala zima la barabara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja. Asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Khamis Shamsi, halafu atafuatia Mheshimiwa Malocha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimwia Spika, nashukuru. Kwanza, nianze na hoja aliyoimalizia mzungumzaji aliyepita juu ya umuhimu wa Serikali kuangalia kwa umakini sana suala la Wakala wa Barabara za Vijiini. Na hili kama Kambi ya Upinzani, tumekuwa tukitoa ushauri kwa Serikali huu ni mwaka wa tatu sasa. Ni muhimu barabara zetu za vijijini zikiboreshwa, hata uwezo wa wakulima wetu kusafirisha bidhaa zao utakuwa ni wa rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi hii inaagiza vyakula kutoka nje, lakini tunaambiwa Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi, imekuwa ikizalisha ziada ambayo inaozea kwenye mashamba kwa sababu tu imeshindikana kusafirisha bidhaa zao. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba ni muhimu Wizara ianze kuliangalia na Serikali kwa ujumla, kwa sababu kama tuna uwezo wa kusamehe kodi kwa mwaka trilioni 1.8 sawa na 27% ya makusanyo ya TRA. Tafsiri yake ni kwamba tukiweza kupunguza kiwango tukaenda sawa sawa na wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, maana yake ni kwamba tukifika asilimia moja na tukikubaliana kwamba katika hizi fedha asilimia kama 50 zinaenda kwenye barabara tunaweza tukajikuta tukafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo mimi nilikuwa nadhani ni suala la muhimu, na ni muhimu Serikali ikaanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile barabra ambayo imetoka kuzungumzwa ambako pia Mheshimiwa Arfi anatoka huko ya Sumbawanga – Kanazi – Kibaoni, ilitakiwa ikamilike mwaka 2012. Sasa miaka miwili imepita, sasa hivi tuko 2014. Sasa nilikuwa nindhani ni suala la busara kabisa Waziri wa Ujenzi akatuambia hii barabara itakamilika lini.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya Barabara ni muhimu tu-*focus* kwenye Mikoa ambayo tunatoka pia zaidi. La kwanza, nitambue kazi nzuri ambayo inafanywa na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam, amekuwa akaitupa ushirikiano mzuri, na nitambue *project* kubwa ya kujenga mfereji mkubwa sana kwa ajili ya kuondoa, mafuriko eneo la Bonde la Mpunga, eneo la Kwa Warioba, *project* ambayo inakaribia shilingi bilioni sita. Kwa hiyo niishukuru Wizara kwa hilo. Niaamini kwamba Wakandarasi ambao wamepewa hiyo dhamana watafanya kazi hii ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi niungane na Mheshimiwa Hokororo kwamba Mheshimiwa Magufuli umekuwa ukitutengeneza ma-*book* makubwa sana. Lakini haya ma-*book* makubwa haya unayotutengeneza, haya mavitabu licha ya kwamba umepewa sifa, lakini mengi unatengeneza kutuchanganya tu. Ukikuta babara ambazo zinaelezewa hapa ni barabara ambazo zimekuwa zikielezewa miaka mitano/sita/saba iliyopita. Unachofanya wewe unajaza barabara zote za nchi nzima, halafu kila kibarabara unaweka kilometa mbili, ama unasema umbembuzi yakinifu. Sasa matokeo yake watu wanapata matumaini, halafu kumbe hayo matumaini ni matumaini hewa, halafu unapata sifa unajaza makaratasi mengi hapa, kumbe haya makaratasi vilevile hakuna, kitu. Naheshimu kazi yako baba yangu, lakini ni muhimu kuwa *realistic*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hapa tunaambiwa umetengewa shilingi trilioni 1.2, lakini ni kweli hizi trilioni 1.2 ndiyo pesa ambazo unaenda kuanzia kufanya kazi, ama katika hizo trilioni 1.2 kuna bilioni 700 ambazo ni madeni ya makandarasi, lakini kumbe mwaka huu wa fedha, fedha ambayo inaenda kule ni milioni ama 400 ama 500. Kwa hiyo, haya mambo ni muhimu kuwa wakweli ili Wabunge wakienda kwenye majimbo yao wakati huku wana matumaini makubwa, wanashangaa mwaka unakatika halafu chenga, mwaka unakatika vumbi. Kwa hiyo ni muhimu siku nyingine uje na kitabu hata chembamba hivi lakini kiwe kitabu chenye tija, lakini siyo unakuja na kitabu kinene huku.

Mheshimiwa Spika, mimi nina barabara jimboni kwangu za kupunguza foleni Mkoa wa Dar es Salaam. Kuna barabra ya Tegeta Kibaoni – Goba, kuna barabara ya Tankibovu – Goba, kuna barabara ya Chuo cha Ardhi – Goba, kuna barabara huku Jimbo la Ubungo ziko; Kibamba – Kisopo, Kimara – Kilungule, Baruti – Msewe. Yaani hizi barabara Mheshimiwa Magufuli, nikiangalia hotuba zako wewe za miaka mitatu/minne iliyopita na wengine waliopita, hizi barabara zipo, zinatengewa fedha kila mwaka, lakini barabara hazijengwi!

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nadhani ni muhimu mtuambie, kwa sababu ninyi mkisema, wananchi wakituuliza mbona tulisikia, tunawambia barabara zinajengwa, barabara hazijengwi! Kwa hiyo ninaomba Mheshimiwa Waziri ukija katika kuhitimisha hoja yako, utuambie kiukweli kabisa, hizi barabara za kupunguza foleni Mkoa wa Dar es Salaam ambazo ziko kwenye majimbo yote ya Dar es Salaam, lakini hususani majimbo haya ya Kinondoni; Jimbo la Ubungo, Jimbo la Kawe, Jimbo la Kinondoni, zinaanza ujenzi rasmi lini? Kwa sababu imeifikia kipindi mimi siamini tena hizi unazoziandika, yaani haya maneno unayoyaweka huku, siyaamini kwa sababu umekuwa ukiyaweka kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, Dar es Salaam imekumbwa na mafuriko makubwa kama yalivyokumba maeneo mengine. Kitengo cha Maafa cha Waziri Mkuu, ambacho kina jukumu la kuhakikisha kwamba masuala ya dharura kama haya yanashughulikiwa na kitengo hicho, hakina fedha kabisa. Barabara za Manispaa ya Ilala, Temeke, Kinondoni zimeharibika, zinahitajika fedha za dharura zisizopungua bilioni 20 ili kuweza kurekebisha ile miundombinu. Sasa ninataka nipate majibu hapa, hizo fedha zipo? Na tuna haki ya kupata kwa sababu Dar es Saalaam ndiyo inaochangia asilimia 80 ya mapato ya nchi hii. Kwa hiyo, ni lazima Wizara ya Ujenzi kwa sababu barabara zetu, madaraja yetu ndiyo yameharibika, mtuambie kuna mkakati gani wa dharua wa kwenda kutatua hilo tatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi kupitia kikao cha RCC, Mkoa wa Dar es Salalam, tulifanya tathmini ya kujenga mfereji mkubwa wa chini maeneo ya Bunju kuelekea Boko ili kuzuia mafuriko makubwa sana ambayo yamesababisha maafa makubwa sana kwa wananchi yasiweze kutokea tena. Sasa walikuja watu wa TANROADS Mkoa, wakafanya tathimini, inatakiwa takribani shilingi bilioni saba. Sasa ninajua kwamba hayo mambo yako kwenye mchakato, lakini kwa kuwa ndiyo tuko kipindi cha bajeti, na hii taarifa ilikuwepo tokea mwaka 2013, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kawe, ningelipenda kujua kwa sababu tukitengeneza ule mfereji mkubwa tutazuia mafuriko kabisa ukanda mzima wa Kunduchi, tutazuia mafuriko kabisa ukanda mzima wa Bunju. Kwa hiyo ile hasara ambayo Serikali inapata kwa masuala ya dharura, kipindi cha mafuriko hayatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni suala la DARTS (Mabasi ya Kwenda Kasi). Hizi mvua zilivyotokea hivi karibuni zimetuonesha kwamba tuna kazi kubwa ya kufanya, kwa sababu barabra mpya ambazo zimejengwa, ukipita pale Jangwani kwa Mheshimiwa Zungu, ilifika kipindi kwamba mvua ikinyesha, daraja la Jangwani pale, linafungwa, wananchi inabidi walazimike kupita hii barabara ya *Sellander.* Sasa nilitaka nijue…

**SPIKA:** Asante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Nilisema namuita Mheshimiwa Haroub Shamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Malocha.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Pamoja na kukupa shukrani, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema mwenye kurehemu.

Mheshimiwa Spika, na mimi nichangie kama walivyosema wenzangu waliotangulia, kwa sababu mambo mengi ni hayo hayo. Lakini kuna mambo ambayo mwili wa binadamu una viungo vingi, lakini tunavyoambiwa na wanazuoni kwamba kiungomuhimu ni uso. Sasa ukisikia kama mtu uso wake ndiyo anoutumia kuupigia *polish* viatu vyake, basi huyo mtu huhesabiwa kwamba hana akili.

Mheshimwia Spika, Dar es Salaam ndiyo uso au sura ya nchi hii. Kila mtu atakuwa haijui Mikoa mingine, lakini atakuwa anaijua Dar es Salaam, na umuhimu wa Dar es Salaam kila mtu anaujua, wameeleza wenzangu walionitangulia, Mheshimiwa Zungu na Mheshimwia Mdee, kwamba uchumi mkubwa unakusanywa Dar es Salaam. Lakini hali ya mazingira ya Dar es Salaam ilivyo, miundombinu yake haistahiki kuambiwa ndiyo Mji Mkuu. Pamoja na kwamba tunaambiwa Mji Mkuu sasa ni Dodoma, lakini kiuhalisia Makao Makuu ya Serikali yako Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Uhuru kama walivyosema wenzangu haistahiki kuitwa barabara ya uhuru kutokana na hali yake ilivyo. Pamoja na kwamba tunaona imetengewa fedha za matengenezo, lakini tunachosisitiza ni kwamba, wakandarasi hawa wafanye ile kazi inayostahili, *value for money* ionekane, wasiondoshe njiani. Sitaki kuamini kama hakuna wataalam katika wizara hii, wataalam kwa kweli wapo wazuri. Maana wataalam waliopo katika Wizara hii walisoma enzi zile ambazo na mimi nilikuwa niko shule, ilikuwa mambo haya ya vyeti *fake* bado, na pia walipata fursa ya kwenda kusoma zaidi nje ya nchi, kwa hiyo namini uwezo wao. Lakini sasa ufanisi ni kitu muhimu. Lazima waoneshe ule uwezo wao, kivitendo, kiuhalisia, isiwe kuandika tu, lakini watu waone *impact* yake. Vijengwe vitu vizuri vinavyohili au vinavyolingana na thamani halisi.

Mheshimiwa Spika, nataka kidogo nizungumzie juu ya barabara mpya za Dar es Salaam za kupunguza msongamano zinazojengwa sasa. Hili jambo huwa tunalisema mara nyingi kwamba barabara hizi zilivyojengwa hazikuachwa nafasi pembeni, zimewekwa…wanaita wenyewe kitaalam *gable stone*. Hazina nafasi ya mchepuko kama gari likitokezea dharura kuhabika, kwa hiyo itasababisha msongamano mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka Mheshimiwa Waziri akija hapa atupe ufafanuzi maana ndiyo wao makandarasi, ma-*engineer* huko wanajua, utaalam wa mambo haya. Kwa hiyo ujenzi huu tunaona kidogo una upungufu, sijui kwa sababu sisi siyo ma-*engineer,* lakini wakitueleza, wakitufahamisha, kwa sababu zile *gable stone* zinasababisha hata kama gari itakwenda mbio kidogo tu, basi itazidisha *speed* kama ikigonga kule inaweza kusababisha hatari kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni juu ya tatizo la makandarasi au hao wahandisi kufanya kazi ambayo hailingani na kazi waliyopewa, halafu hatua zinazostahiki hatuzioni. Ingawa Mheshimiwa Waziri huwa anatuambia kwenye Kamati kwamba wanafutiwa usajili, wanasimishwa ukandarasi wao. Lakini hizi siyo hatua sahihi. Mtu ikiwa unaharibu mali ya umma, halafu wewe uwe umesimamishwa ukandarasi, iwe ndiyo basi. Tunahitaji kuona hatua zaidi za kinidhamu zikichukuliwa au hatua kali zikichukuliwa juu ya makandarasi au ma-*consultant.*

Mheshimiwa Spika, hapa tumeona katika hotuba ya Mheshimwa Waziri ukurasa wa 65, kuna barabara inayojengwa kutoka Bagamoyo – Makurunge, inakweda Saadani – Pangani mpaka Tanga kilometa 178.

Mheshimwia Spika, Mheshimwia Waziri ametuambia hapa kwamba *consultant* aliyekuwepo hapa amesimamishwa kufanya kazi au kashindwa kufanya kazi. *Consutant* alikuwa anaaitwa *Unitech,* kashindwa kufanya kazi, kaeleza katika kitabu chake, kashindwa kufanya kazi, kazi imemshinda. Sasa mtu kapewa kazi, kwa nini kapewa kazi ambayo haiwezi? Haya ndiyo tunayosema hawa wataalam wa Wizara wanafanya kazi gani? Ilikuwaje wakampa mtu *tender* ambayo haiwezi, alipeleka vyeti feki. Na hawa kwanini wakapokea vyeti ambavyo ni vya mtu ambaye hana uwezo? Hawa waliopokea hatua gani wamechukuliwa, na huyu aliyepeleka vyeti ambavyo havistahili kufanya kazi hii, hatua gani kachukuliwa zaidi ya kusimamishwa tu, kwamba basi acha kazi hii, anapewa mshauri mwingine ambaye ni kutoka *South Africa?* Hili jambo linatusikitisha, kwa sababu fedha nyingi zinapotea badala ya kufanya kazi ya kusaidia nchi, zinafanya kazi za kuliwa na watu wachache.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la *CCTV Camera* ambalo tumelisema sana kwenye Kamati kwamba hizi lazima ziwekwe katika vituo vya mizani. Hii itapunguza urasimu, itapunguza ubadhilifu, itapunguza rushwa na itaongeza ufanisi na pia itazuia barabra zetu zisiharibike zaidi kwa kupitishwa mizigo mizito ambayo inakuwa na uzito kuliko uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna tatizo la matuta barabrani ambayo huwa yanasababisha pia hasara au hatari mbalimbali. Hata magari ya mizigo, huwa mizigo inasogea na kwa hiyo ukipimwa katika mizarani, unaambiwa mzigo umesogea katika *excel* moja, lakini katika *total weight* unaonekana mzigo ule ni sahihi. Sasa mtu anapigwa faini wakati kosa siyo lake, kosa ni la mwenye barabara Mheshimwia Waziri Magufuli. Hapa Mheshimiwa Magufuli mara nyingi umekuwa ukituambia kwamba matuta yataondolewa, lakini kila siku yanaongezwa mapya.

Mheshimiwa Spika, juzi wakati nikija Dodoma hapa, nilipita Visiga, nikakuta matuta mapya yamejengwa, ukubwa wake kama mgongo wa punda. Sasa tunaambiwa matuta yanaondoshwa, halafu matuta yanaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi duniani imeweka matuta katika *high way.* Lazima elimu itolewe watu wajue matumizi ya barabara. Lakini kujenga matuta kila mahali katika *high way,* haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwia Spika, kwa hiyo tunataka tujue au unazuiwa kuondosha haya matuta, kama ulivyozuiwa kuzuia magari yasizidishe mizigo? Tunataka utuambie hapa. Mheshimiwa Waziri atuambie kama anazuiwa kufanya hizi kazi kwa sababu tunapiga kelele kila siku katika Bunge. Sasa inaonekana hili Bunge limekuwa ni Bunge la nyimbo tu, hakuna ufanisi, hakuna utekelezaji unaofanywa. Hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kulisema hapa linahusu TEMESA. Hii TEMESA ni Wakala wa Matengenezo ya Magari ya Serikali. Lakini katika kitabu hiki cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* upungufu mwingi ameuainisha juu ya TEMESA, na Mheshimiwa Waziri tumeona katika Bajeti yake amesema katenga fedha. Lakini tunaona magari ya Serikali yanatengenzwa kiholela barabarani, hakuna ukaguzi unaofanywa kwa magari ya Serikali, hakuna udhibiti, fedha zinapotea bure, wanapewa watu wenye gereji bubu mitaani. Sijui hizi gereji ni za nani zinazotengeneza magari ya Serikali kwa gharama kubwa? Ambapo kuna Wakala wa Serikali huu ambao unatengeneza magari kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Spika, hii *Report* ya *CAG* inaeleza upungufu mwingi juu ya TEMESA. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atueleze upungufu huu ulioelezwa na CAG, umeufanyia kazi vipi kivitendo, siyo kimaandishi katika makaratasi. Tunasisitiza mambo haya

yafanyiwe kazi kivitendo. Watalamu kama hawapo waongezwe na magari haya ya Serikali kama ilivyoelezwa katika *Report* ya CAG, yaorodheshwe.

Mheshimiswa Spika, nakushukuru. Ahsante.

**SPIKA:** Asante sana. Sasa nimuite Mheshimiwa Aloyce Malocha, atafuatiwa na Mheshiwa Highnes Samson Kiwia.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote katika ofisi yake kwa namna wanavyosimamia barabara zetu nchi nzima. Lakini nisiishie hapo, nimpongeze vile vile Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Rukwa anakuwakilisha vizuri na timu yake, kwa kweli wanawajibika vizuri. Ikitokea barabra daraja limebomoka, wanatafuta namna ya kupitisha magari ili yaweze kupita kwa haraka. Nawapongeza sana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie daraja la Mto Momba. Daraja hili limekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya na Rukwa, ni kiunganishi kizuri sana katika suala la kiuchumi na usafiri. Lakini, niishukuru Serikali mwaka jana mlitoa shilingi bilioni mbili na mwaka huu mmetupa shilingi bilioni mbili. Tunachosisitiza hapa ni kwamba usanifu ukamilike mapema ili daraja lianze kujengwa haraka, hilo ndiyo tunaomba lifanyiwe uharaka. Tunashukuru Serikali imeshatenga fedha tayari, kilichobakia hapa ni usimamizi wa karibu kumpata mkandarasi anayeweza kusimamia kwa uhakika na kutengeneza daraja zuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda niongelee barabara ya Kiliamatundu – Kasansa – Kibaoni – Stalike. Barabara hii ni ya muda mrefu, ilikuwepo toka wakati wa ukoloni, kutokana na umuhimu wake kiuchumi ndiyo maana ilikuwepo toka wakati wa mkoloni. Sasa ninachoomba Serikali kwa umuhimu wa barabara hii, inapaswa kabisa kufikiriwa kuwekewa lami, ni barabara muhimu kiuchumi, na nikupe mfano, hata mwaka 2008 alipokuja Waziri Mstaafu Mheshimiwa Edward Lowassa alisema hii barabara ikitengenezewa miundombinu mizuri na miundombinu mizuri ya kilimo, ina uwezo wa kulisha nchi tano za Afrika Mashariki hasa kwa zao la Mpunga, aliona.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 Mheshimiwa Mbatia aligombea urais, maneno aliyoyatumia katika ukanda ule alisema, kwa nini eneo hili limechelewa pamoja na umuhimu wa namna hii, hili eneo lina uchumi mkubwa. Naye akarudia maneno yaleyale aliyozungumza Mheshimiwa Edward Lowassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachozungumza hapa ni kwamba viongozi wetu mjaribu kutembea upana wote wa nchi nzima msikalie eneo moja, kuona ni kujifunza na ni kukupa hamu kwamba eneo hili nilifanyie kazi gani. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Mawaziri mjaribu kuweka mtandao wa kutembea maeneo yote ya nchi ili muone nchi hii maeneo mengine ambavyo yamesahaulika pamoja na kuwa na vigezo vingi sana vinavyoweza kuongeza uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii niishukuru Serikali, katika bajeti ya mwaka huu imetenga kulima tuta kutoka Mto Wisa mpaka Ilemba, lakini hiyo haitatosha. Lile eneo ni eneo la mvua nyingi na maporomoko mengi, hii barabara nataka muifikirie sasa kuiwekea lami. Ina madaraja mengi, naomba Serikali ianze kufikiria hilo, ina uzalishaji mkubwa. Yapo maeneo mengine mnatengeneza barabara kwa sababu ya *interest* labda ya viongozi, hili ni suala la kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri atafute muda wa kwenda kupita eneo lile atajionea yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie suala la barabara ya Ntendo –Muze. Barabara ya Ntendo – Muze ni barabara inayounganisha watu wa ukanda wa Ziwa Kaskazini na Mji wa Sumbawanga, lakini barabara hii ni ya TANROADS. Muda wa masika barabara hii inatusumbua sana, inakuwa na utelezi mwingi na fedha zanazotolewa ni kidogo. Tunaomba Serikali kwa sababu ni kilomita 37 tu iweze kuichukua barabara hii iweze kuiwekea lami.

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie barabara za Halmashauri; Barabara ya Kamazit – Ilemba, Miangalua - Chombe. Hizi barabara ni za Halmashauri, lakini Halmashauri haiwezi kutengeneza zinahitaji fedha nyingi, na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba atazitengeneza kwa kiwango cha lami. Naomba Serikali mtekeleze ahadi za Mheshimiwa Rais. Ninashukuru kweli mwaka huu mmetenga fedha kidogo hata mwaka jana mlitenga fedha, lakini haitoshi, ni lazima muongeze nguvu, ahadi ya kiongozi kama yule inatakiwa itekelezeke kwa uhakika, waseme kweli ni kiongozi aliadhidi katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ambalo mwezangu Mheshimiwa Mipata alilizungumzia ni barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga na Sumbawanga - Mpanda. Tunashukuru kwamba mlishaamua kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami, lakini muda unakuwa mrefu sana mpaka unakuta hata kipande kile kilichotengenezwa kinaanza kuchakaa hata kabla barabara haijaisha, kinapoteza umaana na Mkoa ule muda mrefu umekuwa nyuma.

Sasa kama mmeamua kuutengenezea lami, hebu kazeni uzi ili iishe haraka, muanze kutufikiria katika mambo mengine, tulichelewa sana, mtusaidie tunataka kusonga mbele kama Mikoa mingine. Sasa mmeamua kutengeneza, lakini mnakwenda kwa kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kweli nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi unavyofanya kazi. Ni haki yako kupongezwa wala si unafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Highness Samson Kiwia atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Filikunjombe, kisha atafuatia Mheshimiwa Njwayo.

**MHE. HIGHNESS SAMSON KIWIA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia tatizo la msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Changamoto tunayoiona leo pale Dar es Salaam kama hatutaitumia kama shule kama taifa na tukaweza kujipanga katika kuangalia miji mingine katika Taifa letu, tutakuwa ni watu ambao tunaendelea kupanga mipango kutokana na matukio na siyo kupanga mipango kutokana na mahitaji ya muda mrefu na muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika miji yetu mingi hususani kwa mfano Jiji la Mwanza na Arusha, tayari kumeshaonekana dalili za msongamano wa magari na foleni. Na ni ukweli usiopingika kwamba tatizo la ongezeko la watu mijini siyo tatizo la Tanzania peke yake, ni tatizo la dunia yote. Kila unapokwenda utakuta watu wanatoka vijijini wanakimbilia mijini kwa sababu mijini kuna fursa.

Lakini wenzetu katika nchi nyingine wanafanikiwa kwa kuandaa mazingira yanayotosheleza kulingana na ongezeko na kasi ya kukua kwa miji, jambo ambalo naliona hapa kwetu halichukuliwi kwa umakini unaotakiwa, na ndiyo maana kesi za kuvunjwa nyumba

katika maeneo mbalimbali ambayo yako karibu na barabara haziishi kila siku kwa sababu hakuna mipango ya muda mrefu, tunapanga mipango kutokana na matukio.

Mheshimiwa Spika, na suala hili kwa ujumla si suala la Wizara ya Ujenzi peke yake, ni suala ambalo linapaswa kutazamwa na Serikali yote kwa ujumla, kwa sababu kama tutaendelea kuwa tunachukua huduma zote za msingi tunazipeleka mjini katikati, maana yake ni kwamba hatutaweza kuondoa tatizo hili. Kwa hiyo, pia ipo haja ya kusambaza hizi huduma mbalimbali za msingi katika miji yetu. Tunapofikia mahali kwamba hospitali za msingi zote zinakwenda mjini, vituo vya Polisi vipo mjini, Wizara zipo mjini na Mahakama ipo mjini, maana yake ni kwamba hatutaweza kutatua tatizo hili.

Kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba tatizo hili si la Wizara ya Ujenzi peke yake, kama Taifa iko haja ya kuangalia mkakati wa pamoja wa namna ya kukabiliana na changamoto hii ili kuokoa miji mingine ambayo sasa inaonekana inakua kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie hali ya barabara katika Mkoa wa Mwanza hususani Jimbo langu la Ilemela. Jiografia ya Mji wa Mwanza hususani Jimbo la Ilemela, tumezungukwa na milima, na kimsingi milima hii ni ya mawe na bahati mbaya au bahati nzuri milima hii ninayoizungumza ambayo imezunguka Jimbo langu ina makazi ya watu wengi sana, kwa hiyo mvua zinaponyesha kama mvua za mwaka 2012/2013 na 2013/2014, maana yake ni kwamba maji yote yanayotoka milimani yanakuja kwenye barabara za Mkoa, barabara za Manispaa na kuzigeuza kuwa makorongo na njia za kupita maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchanga wa Manispaa ya Ilemela ambayo imezaliwa na Jiji la Mwanza, ni ukweli usiopingika kwamba Manispaa ya Ilemela haina uwezo wa kuweza kuzijenga hizi barabara. Nimezungumza katika Wizara hii hata mwaka jana, nikasema kwamba tayari tumeshaleta maombi maalum na nikaomba kwamba suala ili liangaliwe kwa udharura wake kwa kutambua uwezo mdogo wa Manispaa ya Ilemela katika kuzikarabati zile barabara. Lakini mara mbili mfululizo Wizara imeshindwa kutazama suala hili kwa udharura wake, na hapa ndipo ambapo nashangaa na niungane na Mheshimiwa Halima Mdee kwamba, hivi kazi ya pesa za mfuko wa dharura kazi yake ni nini? Kwa sababu kila mara tunakuja hapa Bungeni, tunaomba tusaidiwe kulingana na changamoto ambazo zinakabili Majimbo yetu, lakini tunageuzwa kuwa ombaomba ombaomba.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Mbunge ni kuishauri Serikali na kuisimamia, siyo kuwa ombaomba. Tunaoishauri Serikali tunaomba tusikilizwe na mahitaji ya wananchi yaweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba nizungumzie hali ilivyo sasa ya barabara za Mkoa. Kutokana na hali hii ya kijiografia ya jimbo, barabara nyingi ambazo zinatengenezwa na TANROAD hazidumu, na bahati mbaya zaidi barabara hizi zinatengenezwa kwa kiwango cha moramu. Sasa ukijumlisha maji haya yanayotoka milimani, halafu yanaelekea kwenye barabara, matokeo yake tutaendelea kuwa tunatumia fedha ndogo kila siku bila tija.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimshauri Waziri kwamba aangalie barabara hii ya msingi na hasa barabara hii inayotoka *Airport* kwenda Kayenze angalau tujenge kwa kiwango cha lami. Lakini pia tuangalie barabara hii inayotoka *National* kwenda Muhonze Keyenze pia tuijenge kwa kiwango cha lami, na barabara hii ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuniongezea kilomita nyingine 18 kuzipandisha hadhi ya Mkoa; barabara ya kutoka Nyakato kwenda Buswelu - Muhoze mpaka Kayenze. Lakini matokeo ya barabara hii yamezalisha changamoto nyingine

kubwa sana na kupelekea Waziri kuiondoa barabara ya awali ambayo ilikuwa ikihudumiwa na *TANROADS* na kurudisha kwenye Halmashauri.

Huu siyo uungwana kwa wananchi wa Ilemela! Barabara hii kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo imekuwa ikihudumiwa na TANROADS na uchanga wa Manispaa ya Ilemela hatuna uwezo wa kuihudumia barabara hii. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwa kukushukuru kwa nyongeza ya barabara hii ya Nyakato, lakini nikuombe barabara hii ya Kiseke - Buswelu muendelee kuihudumia mpaka pale mtakapokuwa na uwezo wa kujenga kuwa barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumzie ahadi ya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu alipofanya ziara Jimboni mwaka 2012 Novemba, aliahidi kiasi cha shilingi milioni 800 kwa ajili ya barabara ya mawe na Mheshimiwa Waziri kipindi hichohicho uliahidi barabara ya mawe Wilaya ya Nyamagana, lakini Wilaya ya Nyamagana tayari barabara ya mawe imekamilika, ahadi ya Waziri Mkuu haijatekelezwa. Sasa hapa wananchi wa Mwanza wanashindwa kuelewa huyu ni *boss* wa nani na huyu ni *boss* wa nani.

Mheshimiwa Waziri, nikuombe umuondelee aibu hii Waziri Mkuu kwa kutimiza ahadi ya shilingi milioni 800 aliyoahidi kujenga barabara ya Nyamanoro – Kawekamo, kwa sababu ni miaka miwili sasa na hakuna ambacho kimefanyika na ukweli ni kwamba namuheshimu sana Waziri Mkuu, ninaamini malengo yake yalikuwa ni mazuri na changamoto ya barabara za Ilemela anazifahamu kama ambavyo unafahamu.

Niombe kwamba basi ahadi hii ya Waziri Mkuu ya shilingi milioni 800 aliyoahidi kujenga barabara ya Nyamanoro - Kawekamo basi iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nikuombe Mheshimiwa Waziri, tunayo barabara ya Buzuruga - Pasiansi na Buzuruga - Sagakiloleni ambayo imejengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 6.5 kwa kiwango cha lami, hii ni mara ya pili nazungumza. Mheshimiwa Waziri nikuombe, kabla ya kukabidhiwa kwa barabara hii, ufanye ziara ya kwenda kuiangalia, ina matatizo mengi, ina changamoto nyingi, hata kabla hatujakabidhiwa, imeishaanza kuonekana ina mmomonyoko.

Mwisho nikuombe Mheshimiwa Waziri, barabara yetu ya kutoka *Airport* kwenda Kayenze uitazame. *TANROADS* wanachelewa kuitengeneza na sasa hali yake ni mbaya sana. Tuangalie uwezekano wa kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango. Mheshimiwa Filikunjombe atafuatiwa na Mheshimiwa Njwayo.

**MHE. DEO H. FILIKUJOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini mimi kabla sijaanza kuchangia naomba kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kuwa nami katika kipindi kigumu, kwanza cha kumuuguza na pia kumzika baba yangu mzazi Mzee Filikunjombe ambaye alifariki wiki tatu zilizopita. Naomba pia nitumie fursa hii kuishukuru sana ofisi yako, wewe mwenyewe, kumshukuru Dkt. Kashillilah pamoja na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mama Tunu Pinda ambao mara kwa mara walikuwa wanakuja hospitali kumwona, mara nyingine Mama Tunu Pinda anabeba uji kuja kumletea Mzee Filikunjombe wakati amelazwa. Namshukuru sana Mama Tunu Pinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kila mmoja kwa nafasi yake kwa michango yenu ya hali na mali katika kuhakikisha kwamba mazishi ya Mzee Filikunjombe yanakamilika na anapumzika salama katika safari yake uzima wa milele.

Mheshimiwa Spika, waliomzika Mzee Filikunjombe ni wengi, siwezi kumshukuru kila mmoja lakini naomba niseme nawashukuru sana ndugu, jamaa na marafiki na kipekee niwashukuru sana wananchi wa Ludewa kwa kuwa pamoja nami katika kipindi hiki kigumu. Kwenu nyote kwa ujumla wenu nawashukuru sana kwa sala zenu, dua zenu na matashi yenu mema. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wizara ya Ujenzi niwe mkweli, wakati tunasherehekea miaka 50 ya Uhuru siku ile mimi na wananchi wa Ludewa tulikuwa kwenye majonzi na tulikuwa kwenye masikitiko kwa sababu tulikuwa tunafanya sherehe kwenye vumbi, Wilaya nzima hakuna barabara hata moja iliyokuwa na lami.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumesahauliwa, lakini baada ya mimi kusema Bungeni, baada ya mimi kuililia Serikali, baada ya mimi kunung'unika, hatimaye taratibu jitihada zimeanza.

Hivi sasa ninavyozungumza Ludewa Mjini tuna kilomita moja ya lami imekwishajengwa na sasa hivi ninavyozungumza kuna mkandarasi Ludewa Mjini anajenga kilomita 11 za lami na hivi ninavyozungumza wakandarasi wapo *site* wanafanya upembuzi yakinifu na *detail design* ya barabara ya lami kutoka Njombe - Ludewa mpaka Manda.

Kwa moyo mkunjufu naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu wake, naishukuru sana Serikali sasa kwa kuwatazama wananchi wa Ludewa. Nimesoma hili buku nimesoma kwenye kitabu hiki nimeona kwamba pamoja na kwamba upembuzi yakinifu unaendelea lakini mwaka huu tumetengewa fedha za kilomita nyingine 50 za lami kutoka Njombe kwenda Ludewa.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi sasa ninavyozungumza pia wakandarasi wako *site* na Serikali imetoa fedha shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kupanua barabara ile kuifanya iwe imara zaidi kwa maandalizi hayohayo ndiyo inayokwenda kwenye migodi, ndiyo inayokwenda Liganga na Mchuchuma, lakini mimi naamini watakaonufaika na barabara ile ni wana Ludewa wote kwa sababu tutapitisha mazao yetu na bidhaa zetu mbalimbali kwenda kwenye soko kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kawaida huwa sipongezi, mimi kwa kawaida huwa sisifii, lakini ukiona nimesimama ninapongeza ujuwe ninamaanisha hivyo. Napenda nitumie fursa hii kabla sijasahau, kuunga mkono hoja kuwa bajeti hii ipite ili Ludewa tuwe na barabara ya lami na nampongeza sana Mheshimiwa Magufuli kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako wanaosema kuna Mawaziri mizigo, lakini mimi napenda nitumie fursa hii kumtoa Mheshimiwa Magufuli katika kundi hilo, Magufuli huko hayumo, wewe unafanya kazi vizuri, wewe ni mchapakazi na Ludewa sisi tunakupenda. Endelea hivyo hivyo! Wangetokea Mawaziri watano, watano tu wawe kama wewe tungekwenda mbali sana.

Mheshimiwa Spika, wako wanaolia humu ndani wanaomba tujenge barabara Kawe peke yake, tujenge Goba peke yake, wewe siyo Waziri wa Kawe, wewe ni Waziri wa nchi nzima kwamba umegawa barabara mafungumafungu kidogokidogo ili iweje? Leo hii tuna kilomita 50 Ludewa, katika miaka 50 tulikuwa tunajenga kilomita hamsini hamsini kila mwaka tungekuwa

mbali. Ni lazima tupendane, ni lazima tukubali kugawana kidogokidogo kinachopatikana. Ni marufuku na kwa kweli itakuwa haipendezi kujenga barabara za Mkoa mmoja peke yake, tujenge nchi nzima na tujenge kila mahali, kila mmoja apate. Wewe ni Waziri wa wote na Ludewa ni wananchi wako na sisi tunakupenda. (*Makofi*)

Wananchi wa Ludewa wamenituma wananiuliza, ndiyo na Kawe mnampenda, lakini siyo Waziri wenu peke yenu, wanasema Mheshimiwa Magufuli njoo ututembelee Ludewa, salamu zako zimeshafika na kazi yako inaonekana. Mbona kwingine unafanya ziara lakini Ludewa hufanyi ziara? Njoo wananchi wale mimi najua wanataka uje kule wakifurahi kule wanakukamatia hata kuku wanakupatia na ukija Ludewa kwa kazi hii unayofanya watakubadilisha jina wewe utakuwa siyo Magufuli, tutakuita Kayombo au Mtweve, tunakufanya uwe mwananchi wa kule. Habari hii ni njema kwa wananchi wa Ludewa nawombeni sana muwe na subira. Mimi ni Mbunge miaka mitatu kazi imeanza kuonekana, barabara ipo. Barabara kutoka Njombe kupitia Uwemba - Ludewa mpaka Manda, ujenzi wa lami unaanza na fedha zimetengwa. Nawaombeni sana wananchi wa Ludewa muwe na imani na mimi Mbunge wenu, hayo ninayoyasema hapa ni kauli thabiti nawathibitishieni, *Eng.* Mfugale siyo wa TANROADS yuko makini. Na nitumie fursa hii pia kusema bayana kwamba tunakushukuru sana, Meneja wa TAANROADS Mkoa wa Njombe, *Eng.* Mazana ni Meneja makini, ni mwadilifu, mcha Mungu na mchapakazi. *(Makofi)*

Mna shida moja ninyi Mawaziri, mtendaji akisifiwa huwa mnamhamisha mnampeleka sehemu nyingine. Mazana usimuhamishe ili asimamie ujenzi wa barabara ya lami kutoka Njombe - Ludewa mpaka Manda. Na uzuri wake barabara hii ndiyo barabara ya upande mwingine wa Spika, kwingine ni kwa Mheshimiwa Filikunjombe. Sasa usimtoe Mazana aweze kusimamia. Sisi Ludewa pamoja na mimi mwenyewe tunakuombea Mheshimiwa Waziri pamoja na CEO wako na Naibu wako na Meneja wa TANROADS muwe na afya njema na uzima ili muweze kutekeleza na kusimamia haya ambayo mmeandika kwenye kitabu hiki ili na sisi Ludewa tuweze kuwa na barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Magufuli, Mungu akusimamie awe pamoja na wewe. Wanaokupinga na kukubeza ni kazi yao hao huwa hawakosekani lakini Ludewa sisi tunakupenda na karibu sana Ludewa. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, utakapokwenda Ludewa usiende kwa helkopta, uende kwa barabara, maana ukienda kwa helkopta utaruka Njombe bure. (*Kicheko*)

Ahsante Mheshimiwa Filikunjombe na ninashukuru kwa kunisemea pia. Nilisema ninamuita Mheshimiwa Njwayo, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Natse.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza wana Mtwara na Lindi wamenitumia *messages* nyingi leo asubuhi wakitaka niiulize Serikali kupitia kwako na nianzie na Waziri wa Ujenzi kwamba, hivi kuna tatizo gani la watendaji wa nchi hii dhidi ya Mikoa ya Mtwara na Lindi? Kwa sababu kila mradi unaopangwa Mtwara haukamiliki kwa wakati unaopangwa. Unacheleweshwa, unaenda polepole, Watanzania wa Mtwara na Lindi hawaelewi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mifano iko mingi; Mheshimiwa Hokororo asubuhi ametaja mradi wa Ndundu – Somanga uliotuchukua muda mrefu bila sababu. Mheshimiwa Lwenge, juzi

ameshinda pale siku mbili anahangaika pale, alikuwa anakula mihogo ya kuchoma pale kwa shida. Hivi lile ni jambo zuri? Tumalize matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani! Wakati mwingine wananchi wanaamua kuchukua hatua zisizo nzuri sana kwa sababu ya kuchelewa chelewa huku kwa ahadi tunazowapa. Mimi naomba ieleweke kwamba, sijapenda sana kwa sababu natambua kipande kile kinahitaji shilingi bilioni 45, lakini leo tumeambiwa hapa na tumeona kwenye bajeti shilingi bilioni 5.2, dah! Hii ni wazi kwamba tutaendelea kukesha tena mwaka ujao pale hapajamalizika. Ndugu zangu tumalize tatizo lile pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli alitembelea barabara ile akaahidi ndani ya siku 180, kwa hesabu ya kawaida ni miezi sita, hatukufanikiwa! Waziri akaahidi tena Machi mwaka huu, hatukupata kitu. Jamani inachosha, mnatuchosha Wabunge tunaotoka maeneo ya huko, Serikali badilikeni na Mtwara na Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia iko barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi. Barabara hii kwa wana Mtwara sisi tumeiita Barabara Uchumi Namba Moja. Mheshimiwa Rais, aliahidi wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2010 kwamba, kabla hajatoka atazindua kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Masasi – Tandahimba – Newala – Mtwara vijijini. Lakini cha kusikitisha mpaka hapa tunapoongea mwaka jana ilitengewa shilingi 3,200,000,000/= mwaka huu nimeona kuna shilingi 3,000,000,000/= lakini anasema usanifu unaendelea. Ukweli ulio wazi ni kwamba, hatujawahi kuwaona wataalam kwenye *field* ama kwa kutumia ndege au njia za kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunaulizwa sana, sasa ifikie mahali mambo haya yakamilike. Mimi niliomuona Mheshimiwa Rais, na bahati nzuri nimemaliza tu kumuona nikakutana na Mheshimiwa Magufuli nje pale tunatoka kwenye jambo hili. Rais alisema amemuita na bahati nzuri kwa sababu nilikuwa natoka yeye ndiyo anakuja, mimi naamini Rais alimuelekeza kumaliza jambo hilo. Hili jambo la barabara hii tulimalize liishe, haiwezekani! Inakuwa aibu, mnatupa kazi ngumu kusema kule kwa wananchi. Ahadi gani zisizoisha hizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu mmoja akanitumia *message* hapa anasema Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba, vipi ahadi ya mkuu wa nchi kuhusu Barabara ya Ukanda wa Korosho Mtwara – Tandahimba – Newala - Masasi? Mbona inaonekana kuna kila dalili za kutowezekana kabla Rais hajatoka madarakani? Sasa huyu mmoja tu aliyejua namba yangu, wako wengi wanaojiuliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi kwenye kikao cha RCC, pia kwenye kikao cha *Road Board*, tuliomba ombi maalum kwa Wizara ya Ujenzi kwamba waangalie kwa macho mawili barabara ya kutoka pale Mangamba kwenda Madimba kwa sababu ya umuhimu wake. Kule ndiko kuna gesi, kule ndiko kunakojengwa mtambo wa kuchakata gesi pale Madimba. Sasa nimeangalia kwenye bajeti pamoja na kupeleka ombi hilo hakuna kitu. Ndugu zangu, barabara hiyo ndiyo itakayosaidia kuchochea uchumi wa nchi hii, ni lazima tuweke macho huko. Wawekezaji wetu wanaokwenda kule watapitaje kwenye barabara ya vumbi, ya hovyo? Ni lazima tutengeneze mazingira yanayofanana na uwekezaji ulioko kule. Halafu ni kilomita zisizozidi hata 50, kweli Serikali inaweza kushindwa mahali ambapo patatusaidia sana kujenga uchumi wetu, kilomita 50 tu?

Mheshimiwa Magufuli wewe ni rafiki yangu, mtani wangu, tuliwahi kukutana Mkwawa wakati fulani unajua, mimi naingia wewe unatoka pale Mkwawa, hebu tuache *legacy* nzuri kwa wananchi wa Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iko pia barabara ya uchumi namba mbili. Mama Anna Abdallah wakati wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi alisema sana. Ile barabara yetu ya ulinzi, ile barabara ni ya uchumi maana kilimo kikubwa kinafanyika huko, kilimo cha kiangazi na kilimo cha kawaida, barabara hiyo licha tu ya kusaidia kwenye uchumi kwa njia ya kilimo lakini ni ya muhimu sana kwa ulinzi wetu.

Mheshimiwa Spika, nataka niwakumbushe hapa kama mmesahau, majuzi tu walikutwa watu kule Nanyumbu wakifanya mazoezi ya mambo ya hatari, mazoezi ya Uboko Haramu Boko Haramu hivi. Wametumia nafasi hiyo kwa sababu kule kumekaa hovyo na kumesahauliwa. Naomba Waziri ashirikiane na Jeshi la Ulinzi kuitoboa ile barabara iwe inapitika, itusaidie, maana ndugu zangu huwezi kujua wakati wa hatari ni lini. Mahusiano yaliyoko sasa na Msumbiji siyo lazima yawe hivi, siku nyingine yanaweza yakatugeuka, mambo yakawa mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kueleza kidogo….

*(Hapa kengele ya pili ililia)*

**SPIKA:** Mbona hamniambii? Nashukuru. Ahsante sana. Nilisema ninamuita Mheshimiwa Natse.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mimi kuchangia machache katika Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza niseme kwamba, barabara kwa maendeleo ya nchi ni jambo muhimu sana kama ambavyo mishipa ni muhimu katika mwili wa mwanadamu.

Nianze kwa kusema kwamba, Waziri wa Ujenzi anafanya kazi yake kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. Nimesikia Wabunge wengine wakisema uchaguzi unakaribia, ile barabara yangu! Nafikiri *mindset* hii siyo nzuri. Serikali inafanya kazi kwa sababu ni wajibu wake kwa wananchi wake na siyo kwa sababu tu uchaguzi unakaribia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba nimpongeze Waziri pia katika bajeti hii, amekumbuka barabara ambayo mara nyingi nimekuwa nikiipigia kelele, inayounganisha Mkoa wa Arusha – Singida - Simiyu sasa na Shinyanga, barabara ya kutoka Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Mang'ola mpaka *junction*. Imetengewa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, jambo moja nimuombe Waziri katika hili kwa umuhimu wa barabara hiyo basi litekelezwe si tu kwa kuandikwa katika kitabu chake cha bajeti.

Jambo la pili ni barabara ya Karatu – Mbulu ambayo Mheshimiwa Rais pia alipokuja kule aliizungumzia. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara. Sasa hapa nimeona imetengewa fedha kwa kiwango cha changarawe. Nimuombe Waziri aone umuhimu wa barabara ile kujengwa kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Mheshimiwa Rais aliisema tulipokuwa naye Karatu tarehe 22 Aprili, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa lami kilimota mbili ndani ya Mji wa Kitalii wa Karatu. Mji ule unakua. Nyakati za mvua udongo wake unaleta shida kubwa. Mheshimiwa Rais, alikazia kwa kusema kwamba tutaanza na hizo kilomita mbili, lakini naahidi kujenga kilomita 10 za lami ndani ya mji ule. Nimuombe Mheshimiwa Waziri,

sijaiona kwenye bajeti yake hata zile kilomita mbili za kuanzia. Ana mafungu mengi, pia kilomita mbili za lami ndani ya Mji wa Karatu, Mji wa Kitalii ambao katika ukanda huu wa Kaskazini unakua kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mkakati gani ambao Serikali inaweka kuhusiana na kubomoka mara kwa mara kwa daraja la Kirurumo? Nafikiri wanahitaji kufanya uchunguzi wa kina, kwanini daraja lile kila mwaka linavunjika na barabara ile inapitisha watalii wengi! Moja ninalofikiri ni kwamba, muangalie mkondo wa maji wa asili katika daraja lile. Najua mliupindisha kitaalam mkaweka mkondo, lakini mkondo wa maji unafuata ile njia yake ya asili. Kwa hiyo, nafikiri muangalie kwa umakini kwanini kila mwaka daraja lile linavunjika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu mapendekezo ambayo yametolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani hapa ya kuwa na Wakala wa Barabara Vijijini. Nafikiri Serikali ione umuhimu wa kuchukua wazo hili la kuwa na Wakala wa Barabara Vijijini. Ni imani yangu hata tukitengeneza huku kwingine juu kama kule chini kwenye *grass root* mambo siyo sawasawa, bado matatizo yataendelea kuwa makubwa. Kwa hiyo Wakala ukiwepo utatusaidia sana kuhakikisha kwamba, nchi hii inapitika kwa mwaka mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa kwamba ukanda ule wa Rukwa – Katavi – Kigoma, ujenzi wa barabara ni muhimu sana kwani wanazalisha sana lakini namna ya kupata chakula kutoka kule inakua ni shida kubwa sana kwa wafanyabiashara. Kwa hiyo, bado tunasisitiza kama nchi Mikoa ile ya Rukwa, Katavi na Kigoma, Morogoro wanasema, ni kweli tuangalie kwa pamoja ujenzi wa barabara maana ni kwa nchi nzima ni lazima nizungumzie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumuomba Mheshimiwa Waziri, katika jimbo langu la Karatu kuna barabara mbili muhimu ambazo nafikiri zitafungua sana jimbo lile, baada ya hii ya kutoka Oldian njia Panda – Mang'ola – Matala – Lalago na kule Kolandoto, kuna barabara ya Njia Panda ambayo ni mpakani mwa Mkoa wa Arusha kwa Karatu na Manyara na kwenda Bonde la Eyasi. Barabara ile ni muhimu sana kwa ajili ya biashara inayofanyika katika bonde lile. Mheshimiwa Spika, asante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukirudi saa kumi, wafuatao wajiandae:-Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Hasnain Mohammed Murji, Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Slyvestry Koka, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Seleman Bungala. Kwa hiyo, hawa ndiyo watakaokuwa wachangiaji wetu baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Tulipokuwa tunasitisha shughuli za Bunge nilikuwa nimewataja wa kuzungumza. Sasa nawaona Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, Mheshimiwa Mntangi.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza, napenda niwashukuru timu nzima ya Wizara ya Ujenzi kwa juhudi zao zote wanazofanya kuhakikisha kwamba Tanzania yetu inabadilika hasa katika Sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu muda ni mchache, niende moja kwa moja katika hoja yangu, hoja yangu kubwa napenda niseme tu, kama alivyosema Mheshimiwa Halima Mdee kuwa, kitabu ni kikubwa na mambo ni mengi sana. Ukiangalia hapa kuna bajeti ya bilioni moja, bilioni mbili, bilioni tatu, miradi ni mingi ambayo ukiangalia kiuhalisia haitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye eneo la Mkoa wangu wa Katavi na Rukwa. Ukikifungua hiki kitabu, ukaangalia ramani ya Tanzania iliyochorwa, hata ulingano wa kuangalia ni pande zipi zenye barabara za lami na pande zipi ambazo hazina barabara za lami inaonekana. Labda niiulize Serikali wananchi wa Mkoa wa Katavi, wananchi wa Mkoa wa Rukwa ambao ni wazalishaji wamewakosea nini?

Mheshimiwa Spika, naongea kwa uchungu sana, wamewakosea nini? Ni wananchi kama Watanzania wengine, wanavuta hewa hii hii tunayovuta, lakini kwa nini, kwa mfano, toka tumeingia naongelea barabara ya Tabora-Kogwa-Inyonga-Mpanda ina tataizo gani? Hawa watu ni wazalishaji, nimekulia huko, nimesomea huko, kwa rasilimali zile zile zinazopatikana kule, ni kwa nini mnawatesa wananchi wa Katavi, Kigoma na Sumbawanga kwa nini?

Mheshimiwa Spika, tulichokosa ni kitu gani katika hii nchi mpaka tujione kama sisi ni wakimbizi ndani ya nchi yetu? Je, hatuna haki ya kupata lami, miaka hamsini ya uhuru hii? Leo ni mwaka wa tatu, tunakwenda mwaka wa nne Bungeni hapa tunaongelea haya haya, tumekosa nini?

Mheshimiwa Spika, mpaka inafika wakati naanza kuhoji, Mkoa wetu tunashukuru ni mpya, sawa, lakini bado tunahitaji maendeleo, lakini ulikuwepo toka miaka hamsini ya uhuru huko nyuma, sasa niulize, je, ni kwa sababu labda maana nashindwa kuelewa, kuna tatizo gani hapa kati ya Meneja wa *TANROADS* labda na Wizara kwa mfano, kama inaonekana Meneja wetu wa *TANROADS*, hawezi kazi mlituletea wa nini? Kwa sababu inasemekana alikuwa benchi kule Dar es Salaam, Makao Makuu sasa mnatuleteaje mtu ambaye hawezi kutusaidia Mheshimiwa?

Mheshimiwa Spika, Filikunjombe pale kamsifia Meneja wake wa *TANROADS* namna anavyofanya kazi kwa bidii. Kwa nini sisi mnatuletea mtu ambaye ukiangalia kutoka Tabora mpaka Inyonga, hata kama ni changarawe lakini ni pazuri. Anzia Inyonga kuja Mpanda yule Meneja wa *TANROADS* kule anafanya nini? Niliwaomba toka kwenye Kamati, mimi natoka Kamati ya Miundombinu, nimewaomba toka kwenye Kamati fanyeni ziara, mwende mkaangalie hata kwa macho ulinganisho.

Mheshimiwa Spika, kuwa na barabara ya changarawe haimaanishi kuwa isipitike. Mama Tunu, Mke wa Waziri Mkuu alikwama pale mara tatu na vyombo vya habari vilionesha toka mwezi wa Kwanza mwaka jana pia alikwama. Kuanzia Inyonga kuja Mpanda kuna tatizo gani? Kama yule Meneja anatuchakachua mtoeni, tuleteeni wachapakazi kama wale wanaofanya kazi kule kwa Mheshimiwa Spika Njombe na kwa Mheshimiwa Filikunjombe.

Mheshimiwa Spika, kwa nini mnatuletea watu, sisi tunataka maendeleo? Ndiyo maana Mheshimiwa Rais akaona umuhimu wa kutupatia Mkoa, ni kwa sababu anaelewa kuwa tulibaki nyuma. Kwa nini msitoe *priorities* kwa Mikoa hii mipya au hii ya pembezoni ambayo toka

zamani hatujui lami, lami sisi tunakuja kuiona Tunduma au ukifika Tabora Mjini ndiyo unaweza kuiona lami na tunaona lami sasa hivi kwa sababu treni hazifanyi kazi, lakini zingekuwa zinafanya kazi wala msingesikia tunawapigia kelele na hizo barabara. Sasa kwa sababu Serikali ya Awamu hii imeamua kupitia mpango wake wa kuiboresha barabara basi na sisi tupewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye namna inavyoweza itafute pesa kwa ajili ya barabara ile, hakuna reli, hakuna nini tunazalisha mazao, tunapeleka wapi? Tupeni ruhusa tupeleke Burundi, tupeni ruhusa tupeleke Zambia na sisi hatujalima kwa ajili ya kuweka kwenye maghala, tunalima ili tuuze ili watoto wetu waende shule. Sasa kama mnatufanyia hivi kwa kweli itakuwa ni ngumu kupitisha hii bajeti kwa upande wangu, itakuwa ngumu kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka niongelee suala la Mto Kavuu, humu mmeandika kwamba shughuli zinaendelea. Sasa hivi kama mtu anaweza kupiga simu Katavi pale akaulizia, hakuna kinachoendelea pale kwenye Mto Kavuu na Mto Kavuu ni kiungo sasa cha kutoka Majimoto, Tarafa ya Mpimbwe kuja Tarafa ya Inyonga ambako ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele mpya. Kumtesa mwananchi kutoka Mpimbwe mpaka Mpanda Mjini ni lazima alale pale siku mbili ndiyo aende Makao Makuu ya Wilaya, Inyonga. Kwa hiyo, ukimrahisishia ile njia pale. utakuwa umemrahisishia shughuli zake za maendeleo. kwa nini hili daraja linasuasua? Kwa nini linakwama?

Mheshimiwa Spika, nawaomba timu ya Wizara, nendeni mkatembee kule mkaone kuna matatizo gani? Kama mnaona kwamba, mimi sielewi, maana sielewi yule mkandarasi mmetuma kuja kufanya nini, sioni anachokifanya miaka yote toka amekuja pale, na ni Meneja wa *TANROADS* ambaye anaitwa Isack Kamwele, sioni anachokifanya kule, ni kukimbizana tu ofisi za CCM, Ofisi ya Chama, Maofisi ya nini. Sasa kama ameletwa kule kutekeleza Ilani za Chama, lile Jimbo ni la Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo, anatekeleza Ilani yake, bado Jimbo lile ni lake, haliko tupu sasa kama ameletwa kule kuja kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza Ilani za Chama, aseme nami ndiyo nawaeleza, hawezi kufanya kazi mbili kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawaombeni sana mkamwangalie na Mheshimiwa Magufuli, uliwaahidi mwaka jana, niliuliza swali hapa kwamba, utakwenda na wananchi wa Mpanda, Mkoa wa Katavi, wanakuita wanasema wamemwambia na Mheshimiwa Kinana mbele ya mkutano pale Inyonga, wamekuomba uende.

Mheshimiwa Spika, sasa, namwomba twende hivyo hivyo na barabara ya vumbi akaongee na wananchi, tusisubiri siku ya kufungua barabara kuwa imepata lami kwa sababu hapa hata nikiangalia katika ndoto hizi hakuna, nitasema lakini mlichoandika hapa ndicho mimi niwaombe tu mfanye juhudi za ziada jitihada za ziada kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi, tuna haki sawa zilizoainishwa kwenye Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Spika, leo Wabunge wengine wamesimama humu wanaongelea barabara za Dar es Salaam wakati wana Majimbo yao wakati wana Majimbo yao, yamesheheni barabara, yamesheheni rangi nyeusi anajisemeaga Mheshimiwa Magufuli kwamba sisi hatujawahi kuona rangi nyeusi barabarani, ni kweli, katika Mkoa wetu zaidi ya tule tu lami tuwili twa kilomita nne, twa mjini pale ambazo tunashukuru, lakini tunataka ya kufungua Mkoa. Tufungulie Mkoa tuingie Tabora, nikiangalia hapa hiyo lami mliyotenga ni kilomita thelathini tu ka Sikonge.

Mheshimiwa Spika, naomba wafanye jitihada za ziada kwa kweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mntangi atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Pia naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara hii ya Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo wanafanya, kwa hakika wanafanya kazi. Mchanganuo ambao umeoneshwa hapa ni dhamira ya kuzitengeneza hizo barabara ambazo kweli ni nyingi, lakini kikubwa ni upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, fedha zipatikane kwa viwango ambavyo wanakusudia, lakini vile vile ni usimamizi kwa Makandarasi. Sasa kwa Makandarasi, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri ameonesha mfano mzuri pale Dar es Salaam, amekataa kupokea barabara zile kubwa za *Kilwa Road* kwa sababu hazikuwa katika kiwango.

Mheshimiwa Spika, naomba aendelee na utaratibu huo katika maeneo mengine mengi, Wahandisi wanakuwa ni wavurugaji, wanaharibu barabara zetu, tuwachukulie hatua na kwa kweli pale zinapokuwa chini ya viwango, Mheshimiwa Waziri asikubali kuzipokea.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru kwa msimamo huo, amenisaidia sana pale Muheza; alikuwepo Mkandarasi mmoja simtaji jina kwa barabara ya kutoka Boza kuja Muheza na Muheza kwenda Amani, kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja hakufanya kazi licha ya kwamba alilipwa hela nyingi sana, lakini maamuzi yalifikiwa na akaachishwa kazi na akanyanga'nywa sehemu kubwa ya barabara zikiwemo barabara zote za upande wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo yanayotakiwa na leo nataka nimhakikishie, Mkandarasi ambaye amechukua nafasi yake, amefanya kazi nzuri kweli kiasi ambacho wananchi pia wanafurahia sasa hivi barabara ya kutoka Boza kuja Mkuzi, Kilulu mpaka Muheza, safi. Barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani kwa kiwango cha changarawe imetengenezwa vizuri na Mkandarasi huyu mpya, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo maeneo mengine muhimu, kwa kweli zipo ahadi nyingi za Mheshimiwa Rais na leo ni lazima niseme. Nasema hili kwa sababu ya kutaka kumjengea heshima Mheshimiwa Rais. Amekuja mwaka 2005 ameahidi kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani, haikufanyika. Mwaka 2010 ametoa ahadi hiyo tena.

Mheshimiwa Spika, Mwaka huu mwezi Machi, 2014 Mheshimiwa Rais amekuja tena Muheza na amefanya mkutano katika barabara hiyo hiyo ya Muheza-Amani. Wananchi walipojua Rais yupo walijaa kweli kwa sababu hakuja katika mpango wa barabara, alikuja katika mpango wa kuzindua maji, lakini walijua Mheshimiwa Rais atazungumzia habari ya barabara na kweli akasema barabara hii itatengenezwa kwa kiwango cha lami na akataja mpango wa mwaka 2014/2015 ambao ndiyo huu tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, sasa usipoiona barabara hiyo inatengenezwa, hivi wale watu wa Muheza waliomsikia juzi tu miezi miwili, watamuonaje na watamzungumzaje Mheshimiwa Rais? Ni vizuri tukapanga tukawa na sekta maalum inayosimamia hizi ahadi za Mheshimiwa Rais, vinginevyo Rais anapokuja katika ziara anakuja kudhalilika tu, kwa sababu kila anapokwenda maswali ni hayo hayo ahadi yako, ahadi yako, ahadi yako!

Mheshimiwa Spika, hapo Muheza vile vile kulikuwa na ahadi ya maji ya Mheshimiwa Rais, kwa macho yangu na kwa masikio yangu, Rais alikaa pembeni akampigia simu Waziri, akampigia pia na Waziri mwingine wa Ardhi na wote wakampa majibu na majibu hayo waliyoyatoa ndiyo aliyoyazungumza katika mikutano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mategemeo ya wananchi ni ahadi hizo kutekelezwa, ni imani yangu kuwa nitapata jibu kwamba barabara hiyo ya Muheza – Amani sasa itajengwa kwa kiwango cha lami na wala siyo barabara ndefu, ni kilomita 34 tu, lakini kule ndiko inakotoka chai, inauzwa kwa Dola nje ya nchi, Taifa linapata fedha za kigeni; kuna wazalishaji wakubwa wa miwa, kuna sekta kubwa ya utalii, watu wanakwenda kule na fedha zinapatikana, leo watu wanashindwa kwenda, chai inashindwa kufika sokoni katika soko la mnada Mombasa kwa sababu barabara haipitiki. Sasa kweli tunalipenda Taifa hili? Tunapenda uchumi wa Taifa hili kweli? Naomba hilo tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulisema ni kwamba, nawashukuru viongozi na namkumbuka kiongozi wangu wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga. Mimi niko Dodoma hapa Bungeni, lakini greda ikiingia kwenye barabara ya *TANROADS* Mkoa, Wilayani Muheza kukitokea tatizo lolote, wananchi wananitumia *message* na ninapopata *message* ile nai-*forward message* yangu moja kwa moja kwa Mkurugenzi nyumbani, anaipokea, ananijibu na anaifanyia kazi. Huyu nampongeza ni mtendaji mmoja mzuri katika Mkoa wetu wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia mmoja ambaye kila mahali atatuma *message* kama barabara ina matatizo, kijana wangu moja *boxer*, mpiganaji anaitwa Muhiru, *message* zake zote pamoja na wengine wananiletea na ninazituma kwa Mhandisi wa Mkoa, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni muhimu kwangu pia ni upandishaji wa barabara za Wilaya kuwa za Mkoa. Tulileta maombi miaka minne iliyopita, Wakaguzi walikuja wakatoa vigezo fulani kwa barabara mbili, lakini nyingine zikapitishwa hii ya kutoka Mbaramu-Misozwe kwenda mpaka Maramba, ile ikapitishwa. Barabara mbili ni kwamba zilikuwa zina urefu, lakini hapo katikakati palikuwa hapajatengenezwa, kwa hiyo, wakatutaka tutengeneze ili vigezo vile vikamilike. Naomba kusema kuwa tumekamilisha utekelezaji huo wa vigezo hivyo, sasa barabara zile ziko katika hali ambayo naomba zikakaguliwe tena ili tuweze kuzipandisha daraja.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ni ya kutoka Kilulu ya kwenda Mtindiro, kwa Bada halafu inatokea kwa Fungo Bagamoyo na inakutana na barabara kubwa ya lami, hiyo inayotoka Segera kwenda Tanga. Ya pili ni barabara ya Mkoa, lakini yenyewe imekwenda nusu tu ya barabara kutoka Bombani hadi Kimbo. Sasa kutoka pale Kimbo, hiyo barabara imeishia katikati na siyo utaratibu wa barabara za Mkoa, ilitakiwa iende moja kwa moja ikaungane na barabara nyingine labda ya Mkoa au barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, sasa hapo pia kukawa na matatizo, kwa hiyo, tumefungua kutoka Kimbo tumekwenda mpaka Potwe, Mpirani mpaka barabara inayokwenda kuunganishwa na barabara kubwa, inayokwenda Wilaya ya Korogwe ambayo pia ni barabara ya Mkoa. Kwa hiyo, hizo barabara mbili naomba tena wawapeleke wataalam wao wakafanye ukaguzi, tuna matarajio watazipokea na kuzipandisha daraja.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nilikuwa nina hofu kwamba pengine sitapata nafasi, basi nasema naunga mkono na nawapongeza tena. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Mikidadi, na baadaye Mheshimiwa Mkono.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii ya Ujenzi kwa muda huu wa dakika saba, kwa hotuba yenye kurasa zaidi ya 309. Naweza nisiweze kuchangia masuala yote, hivyo, mengine nitayachangia kwa

maandishi. Kwa hiyo, naomba nichangie mambo machache ambayo kwa kweli nitaomba majibu kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere aliandika katika kitabu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania na namnukuu:

"Kwa maana moja sasa hatuna Serikali tuna Mawaziri tu, Serikali ni timu, ni timu halisi ina dira na rubani, mkusanyiko wa Mawaziri bila ya mwelekeo, bila mwongozo, bila mshikamano na bila uongozi, kila Waziri na lake, hauwezi ukaitwa Serikali."

Mheshimiwa Spika, nimeanza kwa maneno haya kwa sababu katika Wizara hii ya Ujenzi kumekuwa na migongano ya kauli kati ya Waziri Mkuu na Waziri mwenye dhamana ya Ujenzi juu ya upitishaji wa malori na viwango vya uzito wa mizigo kwenye barabara zetu. Kauli hizi za kugongana kati ya Waziri na Waziri Mkuu zinaashiria maneno haya ya Mwalimu Nyerere kwamba, kwa kweli hatuna Serikali na katika hili katika majumuisho tupate kauli ya Waziri Mkuu, ni kwa nini uharibifu wa barabara hapa nchini uendelee katika hali ya sasa kutokana na maagizo ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kauli kama hizi, maamuzi kama haya ya Waziri Mkuu, ni wazi yanachangia siyo tu katika uharibifu wa barabara, bali pia katika msongamano wa magari, kwa sababu yanatoa fursa ya kuchelewesha ujenzi wa reli na kuchelewesha ujenzi wa njia mbadala. Nayazungumza haya kwa sababu barabara ya Morogoro ambayo inapita Jimbo la Ubungo, katika Kata mbalimbali Kata ya Makurumla, Kata ya Manzese, Kata ya Ubungo, Kata ya Saranga Kimara, Kata ya Msigani Mbezi, Kibamba, Kwembe na Kata zingine, zinaathiriwa na foleni kutokana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nina jambo la ziada ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri anipe kauli, nimepitia vitabu vya hotuba ya Waziri kiwango cha bajeti ya fedha za ujenzi wa barabara, lakini hotuba ya Waziri imerudia kwa sehemu kubwa ahadi zilezile ambazo toka 2005, nimekuwa nikizisikia kuhusu barabara za pembezoni za kupunguza foleni, Jijini Dar es Salaam; barabara zinazotengenezwa ni zile zile; barabara ya Goba, barabara ya Mama wawili barabara zinazotengenezwa ni zilezile.

Mheshimiwa Spika, lakini kiwango cha matengenezo hakilingani na pesa ambazo zimetengwa miaka mbalimbali. Sasa hivi ninapozungumza pamoja na ahadi ya mwaka jana ya Rais, pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwamba, barabara ya Goba ingekuwa imeshaanza kujengwa kwa kiwango cha lami mpaka tufikie tarehe hii.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninavyozungumza sasa hivi pamoja na fedha kutengwa na Bunge, barabara hizi hazijajengwa kiwango cha lami. Natambua mikataba imesainiwa, lakini kusainiwa kwa mikataba ni jambo moja kwa sababu wananchi wamekuwa wakisikia kauli za namna hii kwa Serikali. Naomba katika majumuisho ataje tarehe, barabara ya Goba, Mamawawili, Kilungure, Msewe; barabara hizi ambazo zina mchango kubwa wa kupunguza foleni katika Jiji la Dar-es-Salaam, tarehe ngapi au ni lini Wakandarasi wanaingia *site* kwa ajili ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lisipokuwa na majibu ya maana sio tu kwamba tutaondoa shilingi, bali tutawaambia wananchi wa Dar-es-Salaam pale, wafanye maandamano ya magari na miguu kwenda kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu jambo hili linatokana vile vile na ahadi za Rais za mara kwa mara, ahadi za mwaka 2005 na 2010. Kwa hiyo, Wizara hii isipochukua hatua, naelewa kiwango cha pesa kilichotengwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya Kasma hii hakitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa Maendeleo ulisema, katika kipindi hiki kinachozungumzwa, ilipaswa jumla ya fedha ambazo zingetengwa kwa barabara za pembezoni kuwa shilingi bilioni mia moja yaani milioni elfu moja. Kiwango ambacho mwaka jana hakikukamilika, mwaka juzi na mwaka huu vile vile hakikukamilika. Kwa hiyo, jambo hili nitaomba sana Mheshimiwa Waziri alitolee kauli.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa barabara nilizozisema ambazo tayari zimetengewa pesa kiasi na mikataba imesainiwa, tuna tatizo kubwa zaidi. Kuna barabara ambazo ni muhimu kwenye kupunguza foleni ambazo hazipo kabisa kwenye orodha hii; barabara ya kutoka Kimara Mwisho kupitia Bonyokwa kwenda Mavurunza, kule inaunganisha na Ilala. Barabara ya kutoka Mama wawili kukatizia Kifuru, mmeweka kipande kidogo cha kutoka Kisokwa kwenda Kibamba, ungeunganisha na barabara ya Mama wawili kupitia Kifuru kwenda mbele huko kukatiza Kwembe mpaka kutokezea hii barabara ambayo mmeitengea hapa kwa sababu ya Chuo cha Muhimbili, ni wazi tungefungua nje mbadala za kupita.

Kuna barabara ambayo imetajwa kwa miaka mingi sana na Serikali, ambayo katika bajeti hii, imetengewa fedha ndogo sana za matengenezo ya kawaida tu, haiko katika mpango wa kujenga katika kiwango cha lami, barabara ya kutoka Mbezi kupitia Msakuzi kwenda Mpiji Magohe inaunganisha mpaka Boko mpaka Mabwepande, ni wazi hizi barabara zote zingejengwa kwenye mkakati wa maana wa kujenga barabara tungeinusuru Taifa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la msingi kwa uchumi wa nchi. Sasa hivi Dar-es-Salaam, Serikali inataja takwimu za chini za hasara inayotokana na foleni, hasara ya mafuta, muda wa barabarani, fedha za umma, fedha za wananchi, ukijumlisha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Mikidadi atafuatiwa na Mheshimiwa Mkono!

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyopo mezani petu leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa jina, kwa kazi nzuri anazofanya Tanzania, pamoja na kwamba amepata ajali, wamemtikisa lakini anafanya kazi nzuri Mr. John Pombe Magufuli, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nina mawili, matatu ya kuzungumza. Kwanza, kuhusu kuunganishwa kwa barabara kati ya Mkoa na Mkoa, Ilani ya uchaguzi, 2005 tunaomba na sisi Mkoa wa Lindi kuunganisha barabara kati ya Mkoa na Mkoa, zizibuliwe barabara kati ya Mkoa na Mkoa. Nina barabara mbili; kwanza barabara ya kutoka Liwale kwenda Morogoro, sasa nikitaja Mpigamiti watu wanacheka! Unatoka Liwale inakwenda Mpigamiti inakwenda Mbunga, Wilaya wa Ulanga kwenda Morogoro.

Mheshimiwa Spika, ikifika Morogoro pale utakwenda hapa kilomita mia moja, utakuta Mikumi ambayo pale sasa hivi unaweza kwenda popote, Mbeya, Iringa, Dar-es-Salaam, Ruvuma. Sasa hii ni barabara muhimu, ina Mbuga za wanyama, ina utalii ina kila kitu, mbao! Tunaomba hiyo ifunguliwe.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ya kutoka Liwale kwenda Tunduru, Ruvuma. Wenzetu barabara ya Mikumi, Ifakara, Malinyi kwenda Songea tayari wametengenezewa, wamezibuliwa Mkoa kwa Mkoa. Sisi Mkoa wa Lindi, tunaomba barabara hizi ziwekwe

changarawe kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Iwekwe kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine watu wamezungumzia sana suala la Kibiti Lindi. Kwa kweli sasa hivi inaleta matatizo. Mimi mwenyewe nimeshuhudia mwezi uliopita, watoto wetu wamekaa pale siku tatu, barabara imejaa maji, barabara imeharibika. Pamoja na kwamba kiwango kikubwa cha barabara tayari kimekwisha, lakini bado kidogo tu sijui kinasubiri nini? Bado kipande kidogo tu, lakini kipande hiko ni jasho. Ikinyesha mvua kidogo tu tayari umezama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba barabara hii kile kipande ambacho kimebaki kimaliziwe. Sehemu kubwa imekwisha, tunashukuru hongera sana. Sasa hivi bajeti ya kumi sasa inatungiwa habari ya Kibiti Lindi, Kibiti Mingoyo, Kibiti nini. Sasa tunaomba barabara hii iishe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni migogoro ya barabara, Serikali wakati mwingine inatengeneza barabara inaacha ile barabara ya asili inakwenda maeneo mengine, kisiasa tu. Kwa mfano, kuna barabara ya asili kutoka Milola kwenda Mandawa kupitia Milola, Namkongo, Mchichili, Mputwa, Kiwawa, Mandawa, hiyo ndio barabara ya asili, hiyo ndio barabara ambayo wananchi wanaitaka, kuna zahanati, shule, mazao na kila kitu, lakini barabara imeachwa sasa na kutengwa barabara nyingine inaanzia Milola, Nahoro na Mwandawa. Vijiji vitatu tu, wananchi hawaitaki.

Mheshimiwa Rais pale alikwenda tarehe 2 Desemba, walimwomba, waitengeneza hii barabara ya zamani ya asili kuliko hii mpya ambayo imezushwa haina shule, Zahanati, mazao, jamii hakuna. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa uelekeze Mkoa kutusaidia hili suala la barabara hii, lipitie Milola, Namkongo, Mchichiri, Mputwa, Kiwawa na Mwandawa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kupandisha hadhi barabara kutoka Wilaya kwenda Mkoa. Sheria ya barabara iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2007, Sheria namba 13 ilisema, kwamba barabara zinaweza kupandishwa hadhi pale inapobidi. Sasa sisi tuna barabara zetu ambazo kwa kweli tunaomba zipandishwe hadhi. Barabara ya Nyengedi-Rondo-Mwandawa ya kwanza. Ya pili nanukuu; Mchinga-Kijiweni-Jiwe la Mzungu. La tatu; Liwale-Kilimarondo-Tunduru. Ya nne; Nachingwea-Chilola-Ruangwa. Barabara hizi zina hadhi kubwa, madini, utalii, mbao, *gypsum*, gesi na kila kitu pamoja na korosho humo. Tunaomba hizi barabara zikakaguliwe zipandishwe hadhi.

Mheshimiwa Spika, barabara za Liwale kutokuwa na pacha. Liwale kuna Kata 21. Liwale hakuna barabara zinazounganisha Kijiji na Kijiji, lazima kwanza uanze Liwale ndipo uende Makata. Uanze Liwale uende Kijijij kingine Mkunya, Liwale kwenda Mihumo, Liwale na kwingineko na kadhalika, Kata 21. Huu ni ukoloni! Zamani tulifanya hivyo kwa sababu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, mpaka nieleweshe suala la Kibiti-Lindi ndipo nitaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkono, atafuatiwa na Mheshimiwa Lwanji!

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii ambayo ni ya msingi sana, Jimboni kwangu. Kwa miaka 13 nimekuwa Mbunge nazungumzia suala la barabara.

**SPIKA:** Naomba unyanyue kidogo *microphone*, hatukusikii vizuri. Ahsante.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nazungumzia suala moja tu, suala la barabara ya kutoka Makutano kwenda Serengeti, miaka 13. Bajeti ikija hapa naambiwa maneno yale yale upembuzi yakinifu, mara wamejenga kidogo mpaka sasa kipindi kipya kinakwisha. Hakuna kinachoendelea pale ni porojo tupu. Kutoka Makutano kwenda Nata ni kilomita 80, miaka mitano imepita wanazungumzia hiyo sehemu tu, bado wanafanya upembuzi yakinifu, ama wana *clear the road*. Ukiona watu ambao wako barabarani na wewe unashangaa, ni kundi la watu kama wahuni tu wapo pale na greda za zamani, mbovu, haziwezi kufanya kazi lakini wanatumia fedha za Serikali kufanya kitu kama hicho.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa Tatu tulikaa Kimkoa *RCC*, tukaazimia watu hawa wafukuzwe maana hawafai, tuliazimia wafukuzwe! Bado wapo pale wanarambaramba barabara, lakini hakuna kinachoendelea. Sasa wananchi wamechoka wanasema kama Serikali imeshindwa kujenga barabara inayopita kwa Mwalimu waseme, watuambie kwamba hii barabara haijengeki, ni siasa tu, lakini haina maana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili kuna barabara ya kutoka Musoma kwenda Busekela. Nimekuwa napiga kelele na wenzangu Wanamara na Wabunge wa kutoka Mara walikuwa wanazungumzia hili suala. Ahadi zinatolewa, Rais wa kwanza, Rais wa pili, Rais wa tatu, mpaka Rais wa nne, hakuna kinachoendelea pale, isipokuwa ni porojo tu Bungeni, kila mwaka majibu yapo. Niliwahi kuambiwa na Waziri mmoja kwamba, Mkono unaweza kuuliza maswali, lakini sisi tuna majibu kabla hujauliza swali, ndio ninachokielewa.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, Serikali iko *serious* ama haipo *serious* na wananchi wangu wananisikiliza. Wamenituma niseme, kama haiwezekani mtuambie, sisi wenyewe tuanze kujenga, angalau kuanzisha sisi wenyewe, pengine itawezekana ama mtafute mtu mwingine atufanyie.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kipande kidogo cha kutoka Musoma kwenda Busekela, ambacho nasoma hapa! Wameanza upembuzi yakinifu, najua itachukua miaka mitano bado wanafanya upembuzi yakinifu. Sasa tatizo ni nini? Mkoa wa Mara hakuna kinachoendelea kwa miradi mikubwa, hakuna mradi mkubwa ambao unakwenda, hatuna reli, uwanja wa ndege wala barabara, lakini sisi ndio tuna *link* na watu wa Kenya na watu wa Uganda. Ni nini kinatokea katika Serikali hii ya kwetu, kwa nini hawajali pale?

Mheshimiwa Spika, mara nyingine naambiwa wewe ulikuwa na Rais mmoja angefanya hayo, sasa hakufanya hivyo kabla hajafa nani atakufanyia. Hiyo ndiyo sababu, kwa kuwa Nyerere alitoka kule na hakufanya, kwa hiyo, basi sisi tuna laana hatutajengewa barabara hiyo. Nasema siungi mkono kwa sababu hizi nilizozisema.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi, mwaka jana rafiki yangu Mzee Magufuli alikuwa ananiambia, kaka nitafanya hicho, yapo wapi leo? Mbona hakuna kinachoendelea? Baada ya kusema, nataka majibu mazuri vinginevyo siungi mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Mtanda, halafu Dkt. Haji. Mheshimiwa Lwanji!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie, juu ya bajeti ya Wizara hii. Naunga mkono hoja hii kwa sababu ndugu zetu hawa na hasa Wizara hii kwa ujumla katika maeneo yetu wamejituma vizuri tu. Kwa hiyo, sina sababu ya kupinga na wananchi wamenituma pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya na mara kwa mara wameonekana katika *site* hizo wakiwahimiza Makandarasi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna barabara ya lami, kitu ambacho kilikuwa ni ndoto. Wewe mwenyewe ni shahidi ulivyoniona hata katika Bunge la Tisa nilivyohangaika sana kuhusu barabara hii kuweza kuiomba Serikali iweze kutuona na kuijenga kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, barabara hiyo sasa hivi imejengwa kutoka Manyoni mpaka Itigi. Huwezi kuamini ni raha tupu, imejengwa barabara nzuri sana kwa kweli naipongeza Serikali kwa hilo na sasa hivi lami inamwagwa kutoka Itigi kuelekea Chaya kwenda upande wa Tabora na juzi Katibu Mkuu wa Chama chetu ameshuhudia mwenyewe jinsi Ilani ilivyotekelezwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza kwa kweli pale ambapo wanafanya vizuri, basi tutoe shukurani za wananchi na tuwaunge mkono. Sasa kutokana na muda, nitaongelea barabara moja tu na hii wanaifahamu sana, hii ni barabara inayotoka Mkiwa kwenda Itigi inakwenda Rungwa hadi Makongorosi. Upande ule mwingine kutoka Mbeya barabara hii inajengwa, lakini ahadi ya muda mrefu, nadhani ilianza hata toka Bunge la Tisa kwamba barabara hii nayo ijengwe kwa kiwango cha lami. Iunganishe Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya, lakini kwa bahati mbaya barabara hii imesuasua na mpaka sasa ujenzi wake haujaanzwa.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ipo katika Ilani na pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais amefika Itigi mara mbili wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2010 na pia alifika wakati anakuja kuweka jiwe la msingi la barabara hii ambayo nimeizungumza na akaahidi kwamba barabara hii itajengwa kabla ya uchaguzi wa 2015.

Mheshimiwa Spika, sasa nikiangalia muda uliobaki nadhani hii ahadi itakuwa ngumu au labda itatekelezwa katika hali ambayo itakuwa muujiza. Sasa nawaomba wenzangu basi watueleze ni nini, kwa sababu pamoja na kwamba ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini Mkoa ulipendekeza katika mipango yake kwa kushawishiwa kwamba kila Mkoa upeleke Mradi mmoja utakaoingizwa katika *Millennium Challenge Compact II* na barabara hii ikaingizwa humo. Sasa nilipopitapita nikakuta barabara hii na nilivyosoma nikakuta barabara hii haipo katika mpango huu wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba kupata maelezo, naomba kwa sababu mara nyingi tumezoea wenzetu wanapotoa majibu, wanajibu upande wa wenzetu kule Upinzani. Ndio majibu yao yanatolewa kwa ufasaha lakini sisi tunaambiwa majibu tutayakuta kwenye bango kitita. Sasa tunaomba na wananchi wasikie hayo majibu, hii barabara ni muhimu sana, kwa upande wangu tu mimi tuna Vijiji na Miji midogo kama 20, ukitoka Mkiwa mpaka Rungwa. Nikitaja hapa orodha ni ndefu na ni ***brad*** *basket* ya Mkoa huu wa Singida. Mazao mengi yanalimwa pale, mazao ya mbao na mazao mengi yatokanayo na misitu na chakula ni sisi ndio tunaojaza maghala ya Manyoni na Shinyanga, kuna chakula kingi sana kutoka eneo lile. Wanasema kigezo kimojawapo kwa nini barabara hizo zilizochaguliwa, zilizoteuliwa kuingia katika *MCC II* ni maeneo ya uzalishaji wakati sisi tunazalisha!

Mheshimiwa Spika, cha ajabu katika Miradi hiyo tisa, au saba ambayo ilikuwa imependekezwa katika *MCC* inatoka yote sehemu moja ya nchi upande wa Kusini tu. Siwaonei wivu, lakini kwa nini yote iwekwe kule, wakati na sisi tuna mahitaji yale yale. Kwa hiyo,

ningeliomba Wizara iweze ku-*review* uamuzi wake. nisingependa kutaja maeneo hayo barabara ambazo *MCC II* inafadhili, lakini naomba waangalie uwezekano wa kuiweka barabara hii muhimu katika Mradi huo ambao Mkoa unapendekeza ili na sisi ujenzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, nia ya wananchi ni kuona kwamba, azma yao ya kujipatia maendeleo haraka iwezekanavyo tunapata. Cha ajabu maeneo haya ninayozungumza, kwa mfano, unapotoka Itigi kwenda mpaka Mwamagembe kwenda mpaka Mitundu kuna umeme. Unaweza ukaona jinsi maendeleo yanatofautiana, mahali ambapo kuna umeme taa zinawaka, barabara vumbi tu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ingekuwa inapendeza zaidi kunapokuwa na barabara za lami pamoja na umeme, ni sawa na kuweka umeme kwenye nyumba za nyasi, tulifikiri kwamba umeme ungewekwa kwenye nyumba za bati. Sasa naomba uwiano uende, waangalie yale maeneo ambayo maendeleo mengine yamepelekwa, basi na wao waweze kuharakisha. Kwa hiyo, namwomba ndugu yangu Waziri wa Ujenzi na mwezake watufikirie juu ya suala hilo ili tuweze kuona wananchi wanaboreka zaidi katika mambo hayo ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja kati ya watu wanaoishi katika nyumba 300 hapa mjini Dodoma, nyumba hizi ni za Wizara ya Ujenzi, lakini hatuna barabara, ni ajabu. Ni michepuko tu tunapita hatuna barabara kabisa, mara unakwenda, unakuta kuna nyumba ya mtu mbele, basi inabidi upinde uende sehemu nyingine na tunalipa gharama kubwa sana. Sijui wana utaratibu gani, nadhani wangetueleza tuwe na barabara na zinaponyesha mvua hapa Dodoma huwa zinakuja mara nyingine upande ule, huwa kuna mafuriko tunashindwa kupita.

Mheshimiwa Spika, siku moja nimelala nyumba ya wageni hapa, kwa sababu ilinyesha kiajabu sana, ni fupi lakini ilinyesha mpaka barabara ikashindwa kupitika. Naomba hizi nyumba angalau ziwe *accessible*, tulipe lakini ziwe *accessible,* tuishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kugongewa kengele ya mwisho, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, imegonga. Mheshimiwa Mtanda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mponda halafu Mheshimiwa Selemani Bungala.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nami nakubaliana na Wajumbe wenzangu kwamba Wizara hii kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakifanya kazi zao vizuri na tumpongeze Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili leo nina mambo mawili tu, jambo la kwanza, Rais alifika katika Kijiji cha Milola na wananchi walimwomba Mheshimiwa Rais wapate ufafanuzi ni kwa nini nyumba zao zimewekwa *X* na barabara hiyo ilikuwa ni kichochoro tu kuanzia mwaka 1960, ilipopandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa ni wajibu wa Serikali kuwalipa wananchi wale fidia ili waweze kupisha upanuzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu wananchi wale wamewekewa alama za *X* kutoka Rutamba-Ng'apa, Rutamba mpaka Milola na Rais aliagiza kwamba tathmini ifanyike na wananchi wajulikane ni akina nani wanastahili kulipwa. Nimekuwa nikifuatilia miaka miwili sasa toka Rais alipoagiza hakuna majibu, kila unapokwenda hakuna majibu, jambo hili linanisikitisha

sana. Naomba sasa tuweze kuelewa ni kwa nini, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo na maelekezo yake haya hayafanyiwi kazi.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu hata wananchi wa Mchinga kwenda Kilangala mpaka Kitomanga pale ninapoishi wamewekewa *X* wanauliza ni lini barabara hiyo inapanuliwa hakuna majibu. Hivyo wananchi wangu akiwemo ndugu Ngandala, Abdallah Moshi, Seleman Ngomba, Sharifa Mzee, Mzee Nyenga, Hamad Kilimo, wote hawa sasa wanashindwa kuendeleza nyumba zao kwa sababu ya alama *X* na hawaelewi hatma yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni kero kubwa na tunaomba Serikali ichukue hatua na wananchi wapewe majibu, hata kama yakiwa yale ambayo hawayapendi wananchi, lakini wapatiwe majibu. Tumekuwa tunalalamika sisi Viongozi wao, kila mahali tunakwenda hakuna ufafanuzi. Naomba hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, barabara ile ya Ngongo kuelekea Milola hadi Mandawa, mwaka jana ilitengewa fedha shilingi milioni 250, lakini ukweli ni kwamba fedha hizi hazikufika, barabara hiyo haikutengenezwa, mwaka huu tunaambiwa imetengewa fedha milioni 230. Najiuliza mwaka jana milioni 250 haipo, maana mimi ndiyo Mbunge wa eneo lile, hatukuona ukarabati wa barabara kwa kiwango cha changarawe, leo tunaambiwa tumewekewa milioni 230, jamani! Waoneeni huruma wananchi wa Kusini na hii ni haki yao siyo kuhurumiwa tu. Kama sisi sote Watanzania tunalipa kodi kwa nini fedha hizi sasa haziwasaidii hawa pia.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ililenga pia ipitie Kiwawa, Mputwa ili iende Mandawa, lakini *TANROAD* kwa kuwa wanajua yapo madaraja ya kutengeneza pale wameipindisha na badala yake wanaielekeza sehemu nyingine njia hii kwenda Mandawa, hili halikubaliki. Wananchi wa Kiwawa-Namputwa wanataka barabara hii ipite kwenye mipaka ile ile ili na wao waweze kurekebishiwa barabara yao.

Mheshimiwa Spika, niendelee na hoja yangu ya pili, mradi ule wa Ndundu-Somanga wenye urefu wa kilomita 60, kwenye bajeti hii imetengwa shilingi bilioni 5.2, lakini huu ni kama vile danganya toto hakuna kitu hapa. Hakuna kitu kwa sababu bilioni tano mradi ule una urefu wa kilomita 60 umeanza kutengenezwa miaka sita iliyopita hadi leo miaka sita kwa kilomita 60 zimebaki kilomita 12, maana yake kila mwaka Serikali wanatengeneza kilomita 10. Leo tumetengewa bilioni tano, lakini kutengeneza barabara ile ya lami kwa kipande hicho cha kilomita 12 ni shilingi bilioni 16, unatutengea bilioni tano hii ni kwa ajili ya *commitment* lakini siyo kumalizia ule mradi.

Mheshimiwa Spika, inafadhaisha sana, inasikitisha, inatia huruma kwa miaka sita barabara ya Mkoa *highway*, barabara kutoka Dar es Salaam kwenda Kusini itakakovunwa gesi, ambako tunatoa korosho, tunachangia uchumi mkubwa wa Taifa hili, lakini barabara hii haiishi kwa miaka sita. Jambo hili ni udhalilishaji mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema nitaunga mkono hoja hii kama Serikali itakubali kuongeza fedha hadi bilioni 21…

**SPIKA:** Mheshimiwa Ahsante muda wako umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mponda ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Seleman Bungara!

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja hii. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia leo uzima wa afya, kusimama na kuongea katika Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa pongezi, nawapongeza Mawaziri wote wawili, Waziri Magufuli na Naibu wake, Watendaji wa Wizara nzima na taasisi zake kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli jamani wote tunaona inaridhisha, mengine ni maneno tu. Naomba pongezi hizo pia zimfikie Meneja wa *TANROAD,* Mkoa wa Morogoro Mhandisi Sanga, Mama huyu ni mchapakazi. Tunaomba Mheshimiwa Magufuli kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Filikunjombe kwa sababu ya utendaji wake wa kazi tunaomba umweke Mkoa wa Morogoro miaka kumi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi nyumbani, Ulanga ni kisiwa ambacho hakijazungukwa na bahari wala ziwa, kisiwa kwa maana ya miundombinu kule ni migumu, miundombinu ya daraja na barabara. Ili ufike Ulanga ni lazima uvuke Mto mkubwa wa Kilombero, Mto ule una maji yanayokwenda kwa kasi, una maji mengi, una mamba. Kwa hiyo, maisha ya wakazi wa Ulanga, mtuonee huruma kipindi cha masika kuanzia Januari mpaka mwezi wa Tano tunaishi maisha magumu na maisha ya hatari.

Mheshimiwa Spika, ugumu wake ni kwamba mfumuko wa bei unakwenda *digital* tatu. Mpaka sasa hivi kilo ya sukari ni shilingi elfu nne, lita moja ya mafuta ya taa ni shilingi elfu sita, dozi moja ya kutibu ugonjwa wa *malaria ALU* kama haipatikani kwenye hospitali ya Serikali, ukienda sekta binafsi dozi moja ni sh. 3,500/= mpaka 4,000/=, haya ni maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, maisha ya kule Ulanga ni hatari kwa sababu tunatumia kivuko kile ambacho masika kinafungwa mara nyingi, watu wanatumia mitumbwi ambayo ni *risk*. Mwaka 2010 tumepoteza wenzetu 100 walizama na kivuko kile na juzi hapa tumepoteza wenzetu wawili, matukio haya yanajitokeza mara kwa mara kwa akinamama na wagonjwa wengine wanapovuka pale usiku, kwa sababu kile kivuko kinafungwa usiku, ni hatari, wananchi wanapotea.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali inaonesha jitihada, wanatujengea daraja la Kilombero, lakini naomba niseme wazi daraja lile ujenzi wake unasuasua unatutia wasiwasi kama kweli litakamilika kwa sababu mbili; sababu ya kwanza ni ule ugoigoi wa Mkandarasi, tunahoji huyu Mkandarasi kweli ana uwezo? Mkandarasi huyu ambaye ni Mchina, mkataba wake ni miezi 24, maana yake ni miaka miwili, toka wameanza kujenga daraja lile mwaka jana na daraja lile linatakiwa liishe mwaka huu mwezi Disemba, hadi sasa hivi amefikia asilimia 10 tu na imebaki miezi nane.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kusuasua kwa Serikali kupeleka hela kule, thamani ya daraja lile ni milioni 53, lakini mpaka sasa hivi, asilimia 75 ya muda, hela walizozipeleka Serikali haifiki bilioni 11 na bajeti ya mwaka huu wametenga bilioni saba na nusu, kwa hiyo, bado bilioni 35 na imebaki miezi nane.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali mtuonee huruma jamani, maana wengine wanalalamika hawana viatu, sisi tumezidiwa hata huo mguu wa kuvalia kiatu hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri atakapokuja hapa atueleze ukweli, hiyo miezi minane wanayotueleza wana uwezo wa kumaliza daraja? Wametueleza hapa wanataka kukarabati kivuko cha *MV* Kilombero *II*, kile Kivuko kimechoka, ndiyo maana nasema mnatuweka kwenye hatari, kile kivuko kimechoka, tunaomba sana mbadilishe hiyo dhana ya kukikarabati kwa sababu chenyewe kimeshachoka, mtakikarabati mpaka lini? Tunaomba mtuwekeee kivuko kingine kipya kama vivuko vingine ambavyo tumependekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna barabara inayoanza Ifakara, tunashukuru na tunaipongeza Serikali kwamba tayari wana jitihada za dhati za makusudi kwamba barabara ile kuanzia Ifakara kwenda Lupilo, Malinyi, Kilosa Mpepo, Londo Lumecha mpaka Namtumbo hadi Songea kwamba inatakiwa iwe na hadhi ya lami, lakini tumesikia muda mrefu na tumeona kweli jitihada zipo, lakini tunaomba kuuliza hiyo *no objection* ni mpaka lini? Maana yake mara ya mwisho, mwaka jana nilimuuliza swali Naibu Waziri alisema kwamba hatua imefikia pazuri na tayari wameshapata *no objection,* kwa hiyo mkataba unakamilika, hiyo ilikuwa mwaka jana mwezi wa Tisa. Leo wanaeleza katika bajeti yao bado suala la *no objection, no objection* sijui ndiyo mtoto gani, sijui ni mtu gani huyu *no objection* mpaka leo wanamzungumzia kila siku.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba barabara ile ni muhimu sana, barabara ile siyo muhimu tu kwa wakazi wa Ulanga, bali ni muhimu pia kwa watu wa Songea na Mikoa ya jirani kwamba wanaweza wakaitumia barabara ile wata-*save* masaa manne badala ya kupitia Njombe. Vile vile barabara ile inapita kwenye ukanda wa uzalishaji wa mazao ya nafaka. Tumesema hapa *FAMOGATA*, tumesema *SAGCOT* ndiyo barabara hii inayo-*feed* ukanda huo ambao kama utatumika vizuri itaondoa kabisa tatizo la chakula ambalo linatukabili mara kwa mara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wanafanya utaratibu wa kurekebisha au kumaliza daraja, lakini bado kuna changamoto kwenye kivuko kinachotumika sasa hivi. Wameeleza kwamba wanarekebisha ile gati, lakini tunaomba waharakishe, ile gati inatusumbua sana, ukienda kule, Mheshimiwa Waziri unakwenda mara kwa mara, naomba uende kipindi hiki sasa, ndiyo mambo yamechanganya, pale zinavuka gari karibu 200 kila siku, zikiwa zimebeba mizigo ya nafaka, matokeo yake pale kuna usumbufu wa foleni, madereva wanakaa pale pengine mpaka siku tatu, ndiyo wavuke kwa sababu ya ile gati ambayo mmetuahidi kwamba mtairekebisha, tunaomba hiyo ahadi itimizwe.

Mheshimiwa Spika, ili uunganishe sasa Wilaya ya Ulanga na Kilombero, upande wa pili kule Mlimba, kuna Kivuko kinaitwa Kikove. Tumependekeza kupitia *RCC* na maombi yamepelekwa Wizarani, tunaomba ombi lile la Kivuko cha Kikove likamilike ndani ya bajeti ya mwaka huu, kama imeshindikana basi bajeti ya mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Spika, nilisema leo nipate nafasi ya kuongea moja kwa moja jambo linalohusu Wilaya ya Ulanga, lakini naomba kwa sababu muda unaruhusu, nimalizie kuwapa pongezi Wizara…

**SPIKA:** Muda haukuruhusu, ni kengele ya pili.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nilifikiri ni kengele ya kwanza, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Selemani Bungara atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu na tatu nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Kilwa Kusini.

Mheshimiwa Spika, leo nitaongea mambo machache kidogo. Kwanza simpi lawama Mheshimiwa Magufuli wala simsifu Mheshimiwa Magufuli na wala siamini kwamba katika Baraza la Mawaziri kuna Waziri mzigo, wote ni Mawaziri wasafi tu isipokuwa nafikiria Serikali ya CCM ndiyo Serikali mzigo.

Mheshimiwa Spika, naanza na barabara ya Kibiti-Lindi hususan Nyamwage-Somanga, miaka hamsini ya uhuru Serikali ya CCM imeshindwa kuitengeneza barabara ya Kusini kuwa ya lami na ipitike kifukwe na kiangazi. Baba yangu alikuwa Mbunge miaka 15, Said Ali Bungara, wakati huo Mbunge mwenzake Mheshimiwa Kawawa, walisemaaaa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mpaka wakaamua tuchange fedha watu wa Kusini, lakini napenda sana kumkumbuka sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, marehemu Sokoine, akasema msichange kazi hii ni ya Serikali. Namwombea dua Mungu amweke mahali pema peponi Mheshimiwa Sokoine. Vilikuja vifaa Nangurukuru kutoka Japan, kama vingetumika vizuri basi hata bahari ya Hindi ingefukiwa kwa wingi wa vifaa hivyo, lakini hata kilomita kumi havikujenga.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli mwaka jana kwenye kitabu chake cha bajeti ukurasa wa 90, alitenga bilioni tano milioni mia mbili themanini na saba pointi saba mbili, mwaka huu tena ametenga katika ukurasa wa 127, bilioni tano laki mbili themanini na saba elfu zile zile. Alichokisema mwaka jana na alichokisema mwaka huu ndiyo vilevile. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuseme anawafanya watu wa Kusini watoto wadogo kama hawaelewi! Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Baniani mbaya kiatu chake dawa. Gesi miezi kumi na nane tu imefika Dar es Salaam, barabara miaka hamsini haijafika popote, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, baniani mbaya kiatu chake dawa, gesi mnaitaka, lakini watu wa Kusini hamuwataki, acheni hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba barabara iishe. Miaka minane ya utawala wa Kikwete kilomita 60 mnashindwa kumaliza ninyi? Wala si mzigo wewe, wala siyo mzigo mwingine, mzigo ni Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusidanganyane hapa, nawaomba sana, mimi kama Mbunge wa Kilwa Kusini, nilipanda basi siku moja tukanasa Somanga, wananisema Bwege wala siyo Mbunge, barabara hii wala haiishi, Mbunge si Mbunge Bwege, nawaambia watu wa Kilwa Mzee Bungara alikuwa Mbunge kashindwa, Kawawa alikuwa Mbunge kashindwa, Kingunge alikuwa Mbunge kashindwa, watu wote Wabunge wa Kusini Mheshimiwa Nanjalau, Mheshimiwa Hasnain, wote wa Kusini wanashindwa. Wabunge siyo wabaya, wabaya ni Serikali ya CCM. Serikali ya CCM ni mzigo, kama hawakumaliza barabara hii watu wa Kusini ipigieni kura *CUF*.

Jambo la pili, tarehe 29 Julai, 2012 niliuliza swali kuhusu barabara, ahadi ya Rais kwa Mkocho-Kivinje barabara ambayo inakwenda katika Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Rais aliahidi ataitia lami, Mheshimiwa Magufuli akasema milioni 350 ipo tayari kilomita moja itajengwa. Tukimaliza Bunge hili twende akaiangalie hiyo kilomita ya lami kama imejengwa kwa Mkocho-Kivinje haijajengwa. Kama alitoa hela ishatafunwa huuuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Magufuli wala si mzigo, Mzigo Serikali yake, mzigo Serikali yako isipokuwa inawezekana yeye ndiye anaifanyisha iwe mzigo, lakini Serikali ndiyo mzigo. Namwomba aje, Kilwa jambo la pili hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu tarehe 27 Agosti, 2011 nilimwambia watu wa Mandawa, Kiwawa, Kilanjelanje hawajalipwa hela zao katika kupisha barabara, akasema wameshalipwa. Nikamletea barua nikamwonesha wasiolipwa na nikamwomba aje Kilwa ili aje aonane na watu wasiolipwa. Akasema nitakuja, huuuu mpaka leo, hujafika. Namwomba na unanisikia Mzee Nalinga huko Mandawa, namwambia tena Mheshimiwa aje Kilwa aonane nao kama hakuja akili kichwani mwako, kasema Msondo Ngoma 2015 inakuja, vijiji vinakuja, *wamandharaba nafsi laa yabuki*, anayejipiga mwenyewe haliii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama CCM wanajipiga wenyewe wasilie. Aje Kilwa uje kuwaona watu ambao mpaka leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuna *X* za kijani katika nyumba. Hizi *X* za kijani…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya bwana, usanii tumeuona.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Aje.

**SPIKA:** Haya ahsante. Mbona umemsahau Mzee Nabahani bwana wewe? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Na Mzee Nabahani.

**SPIKA:** Mzee Nabahani alilia humu ndani halafu alipochanga zilikuwa shilingi 97. Siyo tisini na saba elfu, tisini na saba. Ndiyo Marehemu Waziri Mkuu akasema aaa jamani hebu acheni, kwa hiyo nilikuwepo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Abdallah Mtutura atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Koka.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ukiondoa maneno mengine yote ya kejeli, ya mzaha, ya ndugu yangu mwanangu, Bwege namwunga mkono kuhusu kipande hiki ambacho Serikali yetu haijakimalizia. Naamini kwa sababu bahati nzuri niko Kamati ya Miundombinu, mikakati iliyopo hiki kipande nadhani mwaka huu hautakwisha. Kwa hiyo, suala la wananchi wa Kusini kuipigia *CUF* nadhani ni ndoto ya alinacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la barabara kuu za Mtwara *Corridor*. Kipande hiki ambacho hakijakwisha kutoka Mangaka kwenda Tunduru, Tunduru-Namtumbo. Niwatie matumaini wananchi wa Kusini kwamba mwaka huu wa fedha tunamshukuru Mungu na hivi ninavyozungumza Makandarasi wa Makampuni matano wameshaanza kujikusanya kwa ajiili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi wa kipande kutoka Mangaka hadi Lumesule hadi Nakapanya tayari ameshaanza kujikusanya. Kutoka Nakapanya hadi Tunduru Mjini Mkandarasi yupo. Kutoka Tunduru Mjini hadi Matemanga Mkandarasi yupo. Kutoka Matemanga hadi Hulia Mkandarasi yupo na kutoka Hulia hadi Namtumbo Mkandarasi yupo. Kwa wananchi wa Tunduru endelezeni uzalishaji ili mazao yenu yaweze kusafirishwa kwa urahisi kwenda kwenye masoko mbalimbali ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nikijikite kwenye barabara za mkoa. Napenda kuwatia matumaini wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini hususani katika kijiji kile cha Mbesa. Kilio chetu cha muda mrefu, Mbunge wenu nimekifikisha Serikalini na Serikali mwaka huu wa fedha imetenga shilingi milioni mia mbili kwa ajili ya kuanza kujenga daraja katika eneo lile la Mbesa maarufu Maulela. Kwa hiyo, rafiki yangu Mwenye Gwaya uliniambia kwamba unataka kushangilia ushindi wa 2015, ukipita juu ya daraja kwa hiyo sasa anza kujiandaa ili kusherehekea ushindi huo wa 2015 ukiwa unapita juu ya daraja wewe na wenzio akina Mwenye, akina Mzee Chimbalanga. Kwa hiyo, mjitahidi kuweka maandalizi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie barabara ya kutoka Nalasi-Mchoteka hadi Mtwara Pachani katika Wilaya ya mwenzangu ya Namtumbo. Barabara hii ni ya Mkoa na miaka yote wamekuwa wakitenga fedha, lakini matengenezo yamekuwa yakianzia Mtwara Pachani kabla hawajafika Mchoteka, barabara hii fedha zinakuwa zikiisha. Namwomba sana rafiki yangu, kaka yangu Mhandisi Kisimbo safari hii kwa fedha ambazo tutazipata badala ya ujenzi kuanzia Mtwara Pachani kuelekea Mchoteka hadi Nalasi, safari hii waanzie Nalasi wafike Mchoteka na kuendelea hadi Mtwara Pachani ili angalau na wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini na wao waweze kupata unafuu wa barabara yao. Kwa sababu safari hii barabara hii ilikuwa karibu ijifunge na ni barabara ambayo inatumika na Kata nyingi sana katika Wilaya ya Namtumbo na Wilaya ya Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naiomba Serikali, tutaleta pendekezo la kupandisha daraja barabara ya kutoka Tunduru Mjini hadi Misechela. Hii ni barabara ya usalama na vile vile ni barabara ya uzalishaji. Kiasi kwamba kutokana na mazingira ya eneo lile ya barabara inapopita uwezo wa Halmashauri yetu kuijenga ili iwe imara na iweze kupitika mwaka mzima umekuwa mdogo. Kwa hiyo, naiomba Wizara kwamba, tutakapoleta hayo mapendekezo yetu, basi tunaomba myapokee kwa mikono ili barabara hii iwe imetengenezwa na Mkoa kwa sababu Tarafa zingine zote tatu zinazounganisha na wenzetu wa Msumbiji wanazo barabara za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Lukumbule kuna barabara ya Mkoa kutoka Tupendane, Lukumbule, hadi Azimio. Tarafa ya Nalasi wanayo barabara ya Mkoa kutoka Wenje-Nalasi hadi Azimio mpaka Tunduru Mjini. Kwa hiyo na hii Tarafa ya Namasakata nayo ni lazima tupate barabara ya Mkoa kwa ajili ya usalama wa nchi yetu na usalama wa wananchi wa Tunduru kutoka Misechela-Namasakata hadi Tunduru Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaomba, tuliweka mapendekezo yetu kwa Mheshimiwa Rais alipokuja kuhusu uwezekano wa kujengewa daraja inayounganisha wananchi wa Jimbo la Tunduru kwenda Msumbiji. Ikumbukwe kwamba Tunduru pamoja na wenzetu wa Namtumbo tumepeleka mapendekezo ya kuomba Mkoa, Mkoa wa Selous. Sasa itakuwa ni gharama kubwa sana kwa wananchi wa Tunduru ambao tunatarajia kupata Mkoa hivi karibuni kutoka Tunduru twende Songea au twende kwa wenzetu Nanyumbu ili tuweze kuwasiliana na wenzetu ndugu zetu wa Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile wenzangu wemeomba sana Wahandiso wao wa Mkoa waendelee kuwepo katika Mikoa yao na sisi tulishapeleka maombi yetu kwa Mhandisi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sasa namwita Mheshimiwa Sylvester Koka, atafuatiwa na Mheshimiwa Katagira na atamalizia Mheshimiwa George Teu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Koka hayupo, niongee mimi? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hapana, hapana, Mheshimiwa Katagira!

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii iliyo mbele yetu. Nianze kwa kusema naunga hoja mkono kwa kuwa Wizara hii ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri inafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyaka-Bugene. Nashukuru Wizara kwa kutenga pesa za kuendelea kuweka lami barabara hii ya Kyaka-Bugene, lakini suala muhimu ni kwamba pesa hizi zitoke haraka zipatikane na uwekaji lami uweze kuendelea ili barabara hii iweze kusaidia katika maendeleo hasa ya kibiashara ya Wilaya mbili za Kyerwa na Karagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene-Nkwenda-Murongo, Mheshimiwa Waziri anakumbuka alikuja na Mheshimiwa Rais katika ziara. Tukawapokea vizuri sana pale Nkwenda na baada ya maombi ya wananchi kwamba barabara hii ya kutoka Bugene kupitia Nkwenda kwenda Murongo iwekwe lami. Mheshimiwa Rais aliridhia na akaifanya iwe ahadi yake. Kwa hiyo ni muhimu kwamba ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni barabara muhimu sana. Inabeba biashara na inatuunganisha na nchi jirani ya Uganda. Pia wakati ule ule Mheshimiwa Waziri alisimama baada ya vigelegele vikubwa sana na akatamka kwamba wakati ule ule anaagiza kwamba upembuzi uanze.

Mheshimiwa Spika, lakini katika bajeti ya leo ile pesa ya upembuzi yakinifu siioni mle. Namsihi Mheshimiwa Waziri ajitahidi ahakikishe kwambam shughuli za barabara hii ya Bugene-Nkwenda-Murongo ili ijengwe katika kiwango cha lami aishughulikie ahakikishe kwamba inaanza katika bajeti hii ya wakati huu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilima-Chorwabunuka. Nashukuru kwamba pesa zimetengwa sasa za kuendelea kujenga kwa kiwango cha lami Kilima-Chorwabunuka. Suala la muhimu pia hapa ni kwamba pesa hizo zipatikane haraka, ziende ili wajenzi waendelee kuweka lami katika kilima hiki ambacho ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mgakorongo-Kigarama-Murongo. Naishukuru Serikali kwamba sasa imeshatenga pesa za kuendelea na upembuzi yakinifu wa barabara hii ili iweze kujengwa pia katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru tena Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano wake mkubwa, lakini pia nimhimize kwamba ahadi ile ya Rais ya barabara kutoka Bugene kwenda Nkwenda kwenda Kaisho kwenda Murongo ajitahidi ili ishughulikiwe katika bajeti hii ambayo tunawapa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, napenda nishukuru tena na nizidi kusema kwamba naunga hoja mkono, isipokuwa nimwombe tena Mheshimiwa Waziri kuangalia barabara hizi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa George Teu.

**MHE. GEORGE G. TEU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini kabla ya yote ningependa nisahihishe kidogo jina, naitwa Gregory George Teu. George ni baba yangu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nataka tu nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, siku za usoni wakati anawasilisha Bajeti yake aweze kuainisha matengenezo ya barabara ambazo zinajengwa kutumia Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu amejaribu sana kuainisha barabara ambazo zinafadhiliwa na Wahisani zaidi na barabara zile ambazo kwa mfano ziko ukurasa wa 39 ambazo zimefadhiliwa mpaka ukurasa wa 70 ni nzuri sana na watu tumeelewa. Barabara zile ambazo zinatengenezwa kwa kutumia Mfuko wa Barabara hazikuanishwa kwenye bajeti yake

hii. Nimepokea simu nyingi sana kutoka Jimboni kwangu wanauliza sasa sisi wa Mpwapwa mambo yanakuwaje, mbona hatumo?

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba tumo na zimeoneshwa katika Jedwali Namba mbili basi, lakini kwenye hotuba hazikuoneshwa na hii imetupa tabu sana baadhi ya Wabunge kwenye Majimbo yetu kwa sababu tumepokea simu nyingi sana wakiuliza kwamba sisi mbona hatumo. Hapo hapo naishukuru Serikali sana na nataka niwahakikishie wananchi wangu wa Jimbo la Mpwapwa kwamba, ingawaje hawakusikia lakini Mheshimiwa Waziri ametenga fedha za kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kupitia Wizara hii kwa kutenga fedha tangu mwaka 2013/2014, kwa kutengeneza barabara ambayo inaanzia Mbande-Kongwa *Junction* pale Mpwapwa kilomita 53 kwa kiwango cha lami. Tangu uhuru wananchi wangu walikuwa hawajaona lami, sasa kwa mara ya kwanza kabisa kiwango cha mwanzo kabisa ambacho kimeanza lami imeshawekwa na watu wameshaanza kuona lami. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna matengenezo ya daraja la Gulwe utengenezaji wake nao umeshaanza. Nashukuru sana na hili daraja la Gulwe litasaidia sana barabara ya kwenda Kibakwe hadi Chipogolo ambayo inatengenezwa kwa kiwango cha changarawe, nayo nashukuru sana imo katika mwaka huu wa fedha. Matengenezo maalum yaani *Periodical Maintenance* ya barabara kuzunguka Panda Mbili, Mlali, Suguta, Mpwapwa hadi Mhambi nayo inatengenezwa.

Matengenezo ya sehemu korofi yaani *Sport Improvement* ya barabara ya Mpwapwa pale makutano *junction,* Pwaga hadi Lumuma nayo inatengenezwa kwa kiwango cha changarawe, nashukuru sana. Vile vile Gulwe, Mpwapwa Gulwe, Kibakwe, Luhudi hadi Chipogolo nayo inatengenezwa. Kwa hiyo, wasiwasi wa kwamba hawakusikia chochote kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wakati anatoa hotuba yake imeleta mashaka, lakini nawatoa mashaka kwamba kazi inaendelea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile iko barabara ambayo tumepata msaada wa Wahisani wa kutoka Japan, barabara hiyo ni kutoka Chigochangula, pale Msufini, inapita Gumila kupitia Pasua jiwe maarufu sana la utalii ambalo kwa miaka mingi lilisahaulika. Sasa hivi tumeshapata msaada wa barabara hii mpaka Tubugwe. Wenzetu wahisani kutoka Japan wametusaidiana sana kwa kutuwezesha kutengeneza barabara hii ambayo ilisahaulika kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba tu sasa ni kwamba, Wizara ya Fedha ijaribu sana kusaidia Wizara hii ipate pesa ya kuweza kufanya kazi hii nzuri ambayo wameanza kuifanya. Wizara kwa ujumla pamoja na Taasisi zake zote. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Waheshimiwa wote ambao walikuwa wameomba na walikuwepo, wamepata nafasi.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Waziri wa Ujenzi kwa uzalendo wake wa hali ya juu na mapenzi yake kwa Watanzania wenzake. Mheshimiwa Magufuli ni Waziri mchapakazi ambaye Serikali yetu anaiinua juu katika macho ya Watanzania

wote. Mwenyezi Mungu katika Yeremia 3 anasema; "Ukiniamini nitakuonyesha mambo makubwa usiyoyajua bado."

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli yeye ni mmoja wao wale wanaomtegeme Mungu. Hebu angalia ile ajali alivyokuokoeni na kulinda maisha yako na viongozi wengine. Tunaendelea kukuombea, Mungu akupe maisha marefu yenye heri na furaha na mwisho akupe mambo makubwa ili Tanzania kupitia wewe iwe na neema na ifanikiwe katika mambo yote.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze ujenzi wa *flyovers* na daraja la Kigamboni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mradi wa barabara za juu *(flyovers)* umekuwa unatajwa kila inapofika wakati kama huu. Nashauri Wizara isimamie sasa ujenzi wa barabara hizi ili kuondoa kero ya msongamamo wa magari katika Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake. Daraja la Kigamboni litasaidia sana wananchi wanaoishi maeneo ya Kigamboni na vitongoji vyake hivyo nashauri kasi ya ujenzi isimamiwe kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie umuhimu wa kufunga CCTV *cameras* katika mizani katika barabara zetu kwani baadhi ya watendaji siyo waadilifu. Fedha nyingi zinapotea kutokana na rushwa zinazotolewa na wenye malori makubwa yenye uzito uliopindukia kwa macho yangu, nimeshuhudia udanganyifu ukifanywa katika mizani ya Kihonda - Morogoro, Mikese na Kibaha. Watendaji wasiofaa wachukuliwe hatua kali za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua Serikali itaijenga lini barabara ya Nzega - Kagongwa kupitia Igusule (Nzega) na Isagehe? Barabara hii ni muhimu kwa wazalishaji wa mpunga na mazao mengine ya biashara waliopo Mahene na Bukene wanaotumia soko kubwa la Kagongwa (Kahama).

Mheshimiwa Spika, kwa vile nchi yetu imeshuhudia mafuriko makubwa katika maeneo mengi ya nchi yetu, nashauri madaraja yote yafanyiwe ukaguzi ili kuhakikisha ubora na madaraja yote nchini. Uhakiki huu utasaidia kubaini umadhubuti na kama hitilafu zozote zimetokea ili hatua mujarabu zichukuliwe na hivyo kuweza kuepusha madhara yanayoweza kutokea na kuhatarisha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua vilevile ni makandarasi wangapi wanaoidai Serikali na hivyo utendaji kazi wao umeathiri na kutolipwa stahihi zao. Sambamba na hilo napenda pia kujua ni makandarasi wangapi wamefukuzwa na Serikali kutokana na utendaji kazi wao kuwa chini ya viwango ni hasara kiasi gani wamelisababishia Taifa letu. Serikali imewafungulia kesi wangapi ili kudai fidia ya hasara waliyolisababishia Taifa na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na pia na naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. John Magufuli, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanayofanya naomba kupata ufafanuzi kwa masuala yafuatayo kuhusu barabara ya Kamanga – Katunguru - Sengerema (km 35) ambayo mmeitengea shilingi milioni 200 za *feasibility study& detailed design*:

(i) Je, ni lini *feasibility study and detailed design* itaanza na lini inatarajiwa kukamilika?

(ii) Je, lini mnatarajia kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami baada ya *feasibility study and detailed design*?

(iii) Kwa uzoefu mlionao, je, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii (km 35) unaweza kuchukua miaka/miezi mingapi?

(iv) Barabara hiyo kwa sasa imeharibika sana, je, ni lini mnatarajia kuikarabati wakati mchakato wa *feasibility study and detailed design* ikiendelea?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri inayofanywa. Naomba yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete. Katika kampeni za Rais mwaka 2010 Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Vunjo atajenga barabara ya kilometa moja kutoka Himo Mjini kwenda Himo Sokoni kumbe ahadi hiyo haikuorodheshwa, baadaye Mkoa wa Kilimanjaro wameandika kuikumbusha Serikali. Ninaomba ulisemee hili kwa sababu wananchi wa Himo wanangoja kwa hamu kubwa.

(ii) Barabara ya Himo - Himo Hospitali Kata ya Kilema Kusini ambayo inapita kwenye makanisa na taasisi nyingi za Serikali.

(iii) Kukamilisha ujenzi wa barabara za:-

(a) Marangu Mtoni kwenda Kilema Sokoni kilometa tano.

(b) Kawawa - Nduoni Kata ya Kirua Vunjo Magharibi.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana kama utasema neno lolote.

Mheshimiwa Spika, kule Vunjo unatengeneza barabara mbili za kwenda vijiji:-

(i) Marangu - Kilima Sokoni.

(ii) Kawawa - Nduoni Kata ya Kirua Magharibi.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya Himo - Kilema Hospitali. Barabara hii inapita kwenye taasisi muhimu za kidini na shule. Nimeambiwa kwa maandishi DED ameiombea fedha kutoka *Millenium Challenge Account* nisaidie kujua kama hizo zinaweza kupatikana maana itakuwa ni mwokozi wetu.

Mheshimiwa Spika, natoa hongera sana kwa Wizara kwa kazi nzuri na utumishi uliotukuka.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na kuwapongeza Mawaziri na watendaji wa Wizara kwa kutimiza wajibu wao kwa ukamilifu licha ya changamoto za ufinyu wa Bajeti unaowakabili.

Mheshimiwa Spika, daraja la Kilombero kwa mujibu wa mkataba ujenzi wake umebaki muda wa miezi nane tu, lakini maendeleo ya ujenzi unakatisha tamaa kwani utendaji hadi sasa umefikia 10% tu. Aidha, utoaji wa fedha za ujenzi wa daraja hilo unasuasua sana kwani hadi

bajeti hii Serikali itakuwa imetenga shilingi bilioni 18 tu kati ya gharama yote ya shilingi bilioni 53. Je, Serikali ni lini itakamilisha mgao uliobakia wa fedha shilingi bilioni 35 kumalizia daraja hilo? Tunaomba kauli ya Serikali (Wizara) katika mikakati halisi ya kumalizia ujenzi wa daraja la Kilombero kabla ya kipindi cha mkataba.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ikamilishe mkataba na kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ujenzi wa kiwango cha lami katika barabara ya (T16) Lupiro – Malinyi – Londo - Lumecha/Songea. Baada ya kumalizika kwa kazi ya upembuzi yakinifu kwa barabara hii, je, ni nani atafadhili ujenzi wa barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Ujenzi, kwa Waziri pamoja na wote katika Wizara hii na hasa kwa *TANROAD* kwa kazi nzuri wanayofanya na Watanzania wote naamini wanaiona, pamoja na pongezi naunga mkono hoja hii.

Napenda tu kutoa ushauri wangu wa muhimu sana kwa mtu yeyote makini atanielewa, nchi yetu imekuwa ikitengeneza na kufungua njia zote muhimu kwa kasi kubwa na mfano ni barabara ya Iringa - Dodoma km 260. Barabara hii inaunganisha Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Rukwa, Mbeya na Dodoma. Vilevile na nchi za Kusini mwa Afrika na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa vile tayari njia kuu nilizozitaja pamoja na nchi za jirani zinaunganishwa na Mkoa wa Dodoma, ushauri wangu sasa Wizara hii iangalie uwezekano wa kutengeneza barabara ya Gairo – Kilindi - Handeni kilometa zipatazo 250 kwa kiwango cha lami, barabara hii ni muhimu sana kuliko inavyofikiriwa. Kwa vile tayari Tanga – Korogwe - Handeni barabara ni ya lami kilichobakia ni Handeni – Kilindi - Gairo, barabara hii itaunganisha na Mkoa wa Dodoma ambao ni kilometa 132 kutoka Gairo.

Mheshimiwa Spika, ikiungana ina maana ukaribu wa Mikoa ya Kusini na nchi za Kusini mwa Afrika na Dodoma na Tanga zitakuwa karibu sana na vilevile Wilaya nilizozitaja zitakuwa zimeungana na ni pamoja na Mikoa tofauti kabisa na barabara ambazo tayari zipo katika hatua ya kutengenezwa kama Mikumi - Kilosa - Dumila Dumila - Handeni na kuunganisha kwa karibu na wingi wa Wilaya ambazo zitapata huduma ya barabara kama barabara hii ya Gairo - Kilindi - Handeni ambayo vilevile itatuunganisha na makao makuu ya nchi yetu na kuunganisha uchumi kwa kutumia Bandari ya Tanga na kwa faida ya vijiji vingi ambavyo vitafaidika na barabara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napongeza Waziri kwa pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata maelezo kuhusiana na barabara ya Iringa - Msembe *(Ruaha National Park)*, barabara hii ni muhimu sana kwa kukuza utalii nyanda za juu. Kwa masikitiko makubwa barabara hii imetengewa fedha kidogo kwa ajili ya matengenezo tu, mwaka jana tulielezwa kwamba upembuzi upo mbioni ili kujengwa kwa kiwango cha lami. Nataka kufahamu ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami ili wananchi wa Mkoa wa Iringa waweze kunufaika na utalii na hatimaye kuongeza kipato chao?

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru Waziri kwa kuingiza barabara ya Musoma - Makoyo - Busekela kuingizwa katika mpango wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni kiungo muhimu cha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Mwanza hususan Wilaya ya Ukerewe. Pia biashara ya samaki inategemea barabara hii na kwa maana hiyo magari makubwa yanapita barabara hii. Hivyo naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa barabara hii ambayo imekuwa ni kilio cha wakazi wa Tarafa ya Nyanja kwa miaka nenda rudi pamoja na kwamba Marais wa Awamu ya Tatu na hii ya Nne waliahidi wananchi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa napenda kujua upembuzi utakamilika lini ili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, Mji wa Njombe kuna barabara nyingi ikiwemo barabara iendayo Magereza - Kambarage na barabara ya NHC kupitia msikiti na nyingine za mji huu, ieleweke kwamba udongo wa mji huu ni wa tope na utelezi, tunaomba barabara hizi zijengwe ikizingatiwa kwamba ndipo Makao Makuu yenye mradi mkubwa ikiwemo machimbo ya makaa ya mawe, mashamba ya chai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba haya niliyosema yatazingatiwa na kupewa kipaumbele. Nawasilisha.

**MHE. CYNTHIA HILDA NYOYE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Ujenzi kwa kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Katumba - Lwangwa - Mbambo - Tukuyu kwa kiwango cha lami. Tayari mkandarasi amekwishapatikana kuanza utekelezaji kutoka Lupaso mpaka Bujesi. Wananchi wa Rungwe wamefarijika kwa hatua hiyo. Tunaomba Serikali iendelee kutufikiria kutokana na hali ya mvua nyingi sana inayonyesha katika Wilaya hii, barabara hii sasa imeharibika sana na yenye mashimo mengi. Mwaka huu, Wilaya ilipata mm 2,900 za mvua hali ya barabara nyingi ni mbaya sana, tunaomba ifanyiwe matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kikao cha *Road Board* Mkoa wa Mbeya tuliomba kuchepusha barabara kuu kuanzia Mlima Nyoka kupitia barabara ya zamani hadi Uyole Kati mpaka Mbalizi kwa kiwango cha lami. Lengo ni kuepusha magari makubwa kama malori na matrekta yasipite katikati ya Jiji la Mbeya ambako kuna msongamano mkubwa sana. Ombi hili pia liliwahi kufikishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mkoa wa Mbeya, pia kwa barua kwa lengo la kulifikisha kwa Waziri wa Ujenzi. Tunaomba kufahamu walau ni hatua gani imefikiwa hadi sasa kuhusu ombi hili.

Mheshimiwa Spika, nawatakia heri na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka mpya 2014/2015.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, mimi siungi mkono bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sababu ambazo nashindwa kuunga mkono bajeti hii ni kushindwa kukamilisha barabara ambazo zipo Mkoa wa Katavi. Najiuliza sana sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi hatuna haki na nchi? Ni sababu zipi ambazo zimefanya barabara ya Sumbawanga - Kanazi - Kizi haijakamilika na sasa ni mwaka wa nne hakuna dalili za kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Kizi - Kibaoni - Stalike mpaka Mpanda barabara hii haionyeshi dalili kuwa itakamilika kwa muda uliopangwa. Nakuuliza Mheshimiwa Waziri watu

wa Mpanda una kitu gani cha kutuelezea juu ya barabara hizi ambazo zilitolewa ahadi na Mheshimiwa Rais na wewe mwenyewe kutoa maelezo juu ya utekelezaji wa barabara hizi kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpanda - Mishamo Uvinza, barabara hii ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.5 ambazo hazikufanya kazi ya aina yoyote ile, cha ajabu tena mwaka huu mmetenga kiasi hicho kama cha mwaka jana. Mimi nashindwa kuiunga mkono bajeti hii kwa sababu watu wa Mpanda wamechoka kudanganywa.

Mheshimiwa Spika, barabara zote zinazounganisha mikoa mitatu kwa maana Mkoa wa Rukwa, Kigoma na Tabora. Hakuna barabara iliyokamilika, niiombe Serikali ielekeze nguvu kwenye barabara hizi zilizopo Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, barabara ambazo zipo *TANROAD* barabara hizi zinatengo dogo la fedha ambazo haziwezi kufanya matengezo ya barabara ambazo zimeharibika sana na mvua zilizonyesha. Naiomba Wizara iangalie umuhimu wa aina yake juu ya kuongeza fedha kwa barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, barabara zinazounganisha Wilaya na Mkoa katika Jimbo langu nina barabara mbili ya kwanza ni barabara ya Kagwila - Karema tengo la fedha ni ndogo, naomba atizame upya sambamba na barabara ya Kibo - Mwese ninaomba barabara hizi zitengenezwe.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hii nikipata majibu ya barabara zote zinazounganisha barabara.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa uwezo wake nami nipo mahali hapa kuniwezesha kuchangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya bajeti imeandaliwa kwa ustadi mkubwa hivyo napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya bajeti imelenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha miundombinu ya nchi hii inakuwa katika hali nzuri kila kona ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara ni muhimu sana katika Taifa lolote lile ambalo linataka maendeleo ya haraka, ujenzi wa barabara za Tanzania katika kiwango cha lami kumesaidia kuinua usafirishaji mikoani na uchumi wa nchi yetu, wasafirishaji na wataalam wa uchumi wanalitambua hilo. Dira ya Serikali ya Taifa letu ya mwaka 2025 imelenga kuzijenga barabara za nchi yetu kwa kiwango cha lami, kukuza biashara na kurahisisha gharama za usafirishaji nchini. Ujenzi huo utasaidia uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa sana, nchi yetu hivi sasa imetangamana zaidi na maeneo mengine, uwezo wa kwenda mahala popote umekuwa mkubwa na usafirishaji umekuwa mwepesi, kwa kulinganisha na vile tulivyokuwa miaka kumi baada ya uhuru au hata miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa mfano watu wanasafiri kutoka Mwanza hadi Bukoba na kuwachukua kiasi cha saa tano hadi sita jambo ambalo halikuwa hivyo hapo kabla. Hapo mwanzo ulikuwa unapaswa kusubiri meli na ikiwa safari yako haiendani na ratiba ya meli, safari hiyo hiyo ingelichukuwa siku tatu. Barabara kuu ambazo zimewekwa lami ni pamoja na njia ya Dar es Salaam - Morogoro - Iringa - Mbeya ambayo inaunganisha Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo; njia ya Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma - Shinyanga - Kagera ambayo inaunganisha Uganda, Rwanda na Burundi; njia ya Dar es Salaam - Lindi - Mtwara

ambayo inaunganishwa na Msumbiji na njia ya Dar es Salaam - Kilimanjari - Arusha ambayo inaunganisha Kenya na Sudan Kusini.

Mheshimiwa Spika, barabara mpya zimepunguza gharama za uendeshaji na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa kwa nchi jirani kama vile Rwanda, Burundi na Jamhuri za Kidemokrasi ya Kongo. Hata hivyo, bado barabara ndogo na za mikoani zinaweza kuwa changamoto ambayo Serikali lazima ikabiliane nayo. Serikali inapaswa sasa kugeukia barabara za ndani jambo ambalo litaepusha msongomano wa magari Jijini Dar es Salaam wakati wa kwenda na kurudi kazini.

Mheshimiwa Spika, kuziweka lami barabara zote kubwa kunatoa fursa kwa mataifa ya jirani yasiyo na bahari kama vile Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Malawi na Zambia kuitumia Bandari ya Dar es Salaam. Bidhaa zao zitasafirishwa kwa wakati na kwa gharama ndogo. Hapo mwanzoni, abiria alikuwa analazimika kulipa shilingi 80,000/= ($51) kutoka Dar es Salaam hadi Bukoba, lakini sasa nauli imeshuka hadi shilingi 57,000/= ($36). Hii ni tofauti kubwa sana, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuongeza fedha za ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma wakati Tanganyika ilipopata uhuru mwaka 1961, haikuwa imeunganishwa hata kidogo, lakini sasa Serikali imefanikiwa kuiunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Ikumbukwe ilikuwa inawachukua abiria siku sita kusafiri kutoka Dar es Salama hadi Bukoba na masafa ni kilometa 1500 tu. Sasa inachukua saa 18 kwa safari hiyo hiyo, Serikali imefanya kazi ya kusifika.

Vilevile napenda kuipongeza Serikali kwa kujenga sehemu ya mwisho ya barabara kuu ya Kaskazini kati ya Iringa na Dodoma. Barabra hiyo yenye urefu wa kilometa 260 ilikuwa ni barabara pekee kuu nchini Tanzania ambayo haijawekwa lami. Barabara hiyo inafika hadi Cape Town - Afrika Kusini hadi Cairo - Misri.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pamoja wa ujenzi wa barabara kati ya Tanzania na Kenya umeingia dosari kutokana na wakazi kwa upande wa Tanzania kuilalamikia Serikali kwamba imeshindwa kuwalipa fidia ya nyumba na mali zao. Mradi huo wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 242 unatarajiwa kuanzia nje kidogo ya Mji wa Arusha na kupitia Moshi hadi Holili. Kwa Kenya barabara hiyo itapita Mji wa mpakani wa Taveta hadi Voi. Ujenzi huo ambao mkataba wake ulitiwa saini Aprili mwaka 2013 unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambayo imetoa mkopo wa dola za Marekani milioni 300. Mradi wote utagharimu kiasi cha dola za Marekani milioni 560.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi huo umepangwa kuanza mapema nchini Kenya utazinduliwa na viongozi wakuu wa nchi husika wa mradi ambao ni Rais Jakaya Kikwete (Tanzania) na Uhuru Kenyatta (Kenya). Kwa Arusha barabara hiyo itaanzia eneo la Ngaramtoni Wilayani Arumeru na kupita Magereza - Kisongo - Njiro - Usa River ikiwa na urefu wa kilometa 42. Ila kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuhusu kulipwa fidia zao, wananchi zaidi ya 1,000 waliopo katika orodha ya kulipwa fidia za nyumba na mali zao wakati ujenzi unatarajiwa kuanza muda mfupi ujao Serikali ya Tanzania bado haijawalipa fidia wananchi walioombwa kupisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, wananchi hao walielezwa kupisha ujenzi wa barabara hiyo mapema mwezi Januari, 2012 na viongozi wa Serikali kuwa wasiendeleze maeneo yao hadi hapo watakapolipwa fidia na kuondoka barabara itakakopita. Hadi sasa bado wananchi hao wanadai fidia ya nyumba, viwanja, mazao na mali nyingine katika maeneo yote ambayo barabara hiyo mpya inatarajiwa kupita. Kipindi hicho ni muda mrefu sana kwa mtu kutofanya shughuli yoyote katika eneo lake, lakini pia ucheleweshaji wa fidia hiyo utawatia hasara

wananchi kwa kuwa gharama za vifaa vya ujenzi na vitu vingine muhimu zinazidi kupanda kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote hicho wameandika barua kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za Serikali (Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Waziri wa Ujenzi) lakini hadi sasa hakuna majibu ya kuridhisha yaliyotolewa na viongozi hao. Wananchi hao wana wasiwasi kama ujenzi huo utafanyika kwa wakati kwa upande wa Tanzania kwa kuwa suala la kuwaondoa wananchi katika maeneo yao linahitaji muda wa kutosha na pia fedha za fidia kabla ujenzi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo iwapo Serikali itapuuza malalamiko hayo ambayo wananchi hawa wameyawasilisha ngazi mbalimbali wanaweza kuchukua hatua za kisheria kwa kuzuia ujenzi huo mahakamani ili wapate haki yao na hivyo kupelekea ujenzi huo kwa upande wa Tanzania kuchelewa kuanza na kurudisha maendeleo nyuma pamoja na juhudi nzima zilizowekwa. Wananchi hao wana haki ya kulipwa fidia ya nyumba na mali zao kama sheria inavyoelekeza na Serikali inapaswa kuzingatia haki yao hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 kifungu cha 49 Sura ya Tatu inaeleza umuhimu wa mwenye ardhi haki ya kulipwa fidia pale ardhi yake inapochukuliwa kwa matumizi mengine. Serikali kama msimamiaji namba moja wa sheria inapaswa kuwalipa wananchi hao tena kwa haraka fidia ya fedha kwa nyumba na mali nyingine ambazo zitaathirika na zimefanyiwa tathimini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada zake kubwa sana za kuhakikisha barabara nyingi zinakuwa katika kiwango cha lami na kupitika kwa wakati wote wa mwaka. Kazi hiyo pamoja na mikakati hiyo ya Serikali inakabiliwa na changamoto mbalimbali, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na miradi mingi kutokuisha kwa wakati, miradi kukamilika ikiwa chini ya viwango, ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, Serikali kutenga kiasi kidogo cha fedha katika bajeti na hivyo kutokuwezesha miradi mingine mipya kuanza. Hali hiyo kwa kiasi fulani imekuwa ikirudisha nyuma maendeleo hasa kwa maeneo yale ambayo yamekuwa hayapitiki kabisa na yale ambayo huwa yanapitika kipindi cha kiangazi tu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutenga fedha za kutosha katika miradi mipya ya barabara na ile ya zamani ili kuiwezesha kuisha na kufanikisha azma ya kuiunganisha mikoa kwa mikoa kwa kuweza kupitika kwa njia ya barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali kuwa kuna wakandarasi wengine wamekuwa hawana viwango vya kuridhisha kiasi ambacho miradi yao inapoisha huwa chini ya kwango, najiuliza ni utaratibu gani uliowezesha kupatikana kwa wakandarasi kama hawajafikia viwango vinavyohitajika? Wakandarasi hawa wamekuwa wakichelewesha maendeleo kwani miradi yao imekuwa ikichukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuzidisha umakini kwa wakandarasi kama hawa ili kuepusha kurudishwa nyuma kwa juhudi mahsusi zilizowekwa na Serikali za kuleta maendeleo nchi nzima kwa kujenga barabara zenye viwango. Naiomba sasa Serikali pindi inapogundua wakandarasi kama huo ni vema wamalizapo miradi hiyo watangazwe kwenye vyombo vya habari ili wasije kuomba kazi sehemu nyingine katika taasisi za Serikali na ikiwezekana wafungiwe kabisa kufanya shughuli za ukandarasi.

Mheshimiwa Spika, siku si nyingi tumekumbana na mvua kubwa ambazo zimenyesha mfululizo na kuleta mafuriko pamoja na maafa kwa wakazi mbalimbali na pia kusababisha uharibifu mkubwa katika barabara zetu na kubomoa madaraja yetu mengi, barabara kukatika, kingo za barabara kuharibika na kusababisha miundombinu hiyo kuharibika kabisa na

kupelekea baadhi ya maeneo kutopitika takribani kwa siku kadhaa na hivyo kuzorotesha shughuli za kijamii na kiuchumi katika maeneo hayo. Ilichukua siku kadhaa kuweza kurudisha hali hiyo ya kurejesha barabara kupitika na kukarabatika maeneo hayo na kuyarudisha katika hali ya kawaida, baadhi ya maeneo mpaka hivi leo bado hayapitiki na hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, matukio kama haya yanatufundisha mambo mengi sana, mojawapo ni jinsi gani tunaweza kujiweka tayari kukabiliana na hali ya majanga kama hayo, kwani sehemu nyingi zilizokubwa na uharibifu huo zilichukua muda ili kurejeshwa katika hali ya kawaida ingawa Wizara iliagiza wataalam wake kuwepo maeneo yote yaliyoharibika ili kuhakikisha barabara hizo zinarudi katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kusema ukweli hatuna budi kuipa pongezi Wizara kwa jitihada ilizozionyesha katika kurejesha miundombinu hiyo katika hali yake ya kawaida, nazishauri Wizara nyingine kuiga mfano huu ulioonyeshwa na Wizara hii wa kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kuwa kila kitu kinarudi katika hali yake ya kawaida na hivyo magari kuweza kupita tena.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kidogo kuhusu Mkoa wa Dar es Salaam kwani mkoa huu unatuhusu wote kwa kuwa ndiyo shughuli nyingi za Serikali hufanyika. Mkoa wa Dar es Salaam una jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 3,262.74 ikiwa za lami kilometa 736.9, changarawe/udongo ni kilometa 2,525.84 kati ya hizo kilometa 600.97 zipo chini ya wakala wa barabara yaani TANROADS na kilometa 2,661.77 ni Halmashauri za Manispaa (Ilala kilometa 804.37, Kinondoni kilometa 811.1 na Temeke kilometa 1046.3) lakini ukiangalia kiwango cha barabara ambazo zipo katika kiwango cha changarawe ni kikubwa sana ukilinganisha na Dar es Salaam kuwa ni Jiji kubwa hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuifanyia kazi changamoto hiyo ili kuleta uwiano unaolingana na hadhi ya Jiji lenyewe. Katika sekta hii mafanikio makubwa yamepatikana tangu mwaka 2005 hadi Disemba, 2013 kwani kulikuwa na jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 444.21 zikiwa ni barabara za lami (Ilala kilometa 79.85, Kinondoni kilometa 178.8 na Temeke kilometa 169.3) na kilometa 1,009.36 za changarawe/udongo. Kwa ujumla barabara za lami zimeongezeka kwa kiasi cha kilometa 292.69 sawa na asilimia 39.7.

Kwa upande wa madaraja mwaka 2005 kulikuwa na madaraja 28 hadi kufikia Disemba, 2013 kulikuwa na madaraja 133 ambayo ni ongezeko la asilimia 79, kwa hatua hiyo hatuna budi kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kuzingatia ubora na uhitaji wa miundombinu.

Vilevile naomba nigusie pia suala zima la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Msongamano wa magari katika Jiji Dar es Salaam unaweza kuongelewa kwa namna nyingi. Ukweli ni kuwa kila anayeishi Jiji la Dar es Salam ana maelezo yake kuhusu anavyoathirika na msongamano wa magari. Maeneo sugu ya foleni ni yale ya makutano ya barabara kubwa na sehemu nyingine ni zile ambazo huathirika wakati mvua zikinyesha.

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alieleza kuwa katika kipindi chake hiki atahakikisha Jiji la Dar es Salaam linapata barabara za juu maarufu kama *flyover* kwa mujibu wa Rais Kikwete. Barabara hizo zitajengwa katika maeneo ambayo yanakutanisha barabara mbalimbali na maeneo yanayokabiliwa na msongamano mkubwa. Barabara zinazopewa kipaumbele katika ujenzi wa *flyovers* ni zile za Mwalimu Nyerere na Morogoro, lakini hizo bado ni kauli tu ama ambazo hazijaanza utekelezaji hali inayofanya kuendelea kumomonyoka kwa uchumi wa Taifa na wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la wazi kuwa idadi ya magari inaongezeka kwa kasi Jijini Dar es salam, hali hii inaonyesha kwamba watu kumiliki magari sio tena kitu cha anasa bali inatokana na uduni wa usafiri wa umma. Ofisi nyingi za umma zimejengwa eneo moja hali inayowafanya wakazi wa jiji hili kuwa na uelekeo mmoja kila asubuhi na jioni.

Pia barabara za Jiji ni za zamani sana hivyo haziendani na kutanuka kwa Jiji. Sambamba na hilo, ubora wa miundombinu sio wa kuridhisha hasa wakati wa mvua. Pia kumekuwepo na matatizo ya mipango miji ambapo huduma zinazofanana hupatikana sehemu moja ikiwa ni pamoja na makazi ya watu wengi kuwa mahala pamoja. Sababu zinazopelekea kuwepo kwa msongamano mkubwa wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Miongoni mwa vyanzo vya msongamano ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokuwa na barabara za kutosha na zilizopangiliwa vizuri.

(ii) Uchakavu wa magari.

(iii) Uduni wa huduma za usafiri wa umma.

(iv) Kutokuwa na mpango mji unaoeleweka.

(v) Ofisi za Serikali na huduma nyingine kuwa katika eneo moja.

(vi) Kuongezeka kwa idadi ya watu Jijini tofauti na miji mingine nchini.

(vii) Kutokuwa na mfumo wa kutoa huduma za jamii kwa saa 24 za siku.

(viii) Usimamiaji mbaya wa sheria za barabara.

Mheshimiwa Spika, athari zitokanazo na msongamano wa magari ni nyingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira. Imebainisha kwamba misongamano ya magari inachangia kwa kiasi kikubwa kuporomosha uchumi wa watu binafsi wa Taifa na hata kuendeleza umaskini baina ya wananchi. Wananchi wanalazimika kutumia kiasi kikubwa cha mafuta (fedha) kutembea mwendo mfupi, angalia muda unaopotea barabarani na petroli/dizeli na mafuta mengine ya kulainisha mitambo inayopotea bure hasa ukizingatia kwamba vyote hivi tunaagiza nje ya nchi, "ni hifadhi ya fedha za kigeni kiasi gani Benki Kuu inatumia kununulia bidhaa hizi?"alihoji Festo Maro.

Vilevile athari zingine zilizoainishwa ni pamoja na uharibifu wa mazingira kutokana na hewa ukaa inayotolewa na magari yanayotumia muda mrefu njiani yakiwa yanaunguruma bila kutembea. Vilevile watumiaji wa magari hayo hufika katika sehemu zao za kazi na hata majumbani mwao wakiwa wamechoka na hivyo kutokufanya shughuli zao ipasavyo. Kuna namna ya kukabiliana na msongamano huu uliopo. Ziboreshwe njia za pembezoni mwa barabara ili kuwezesha watumiaji wa barabara kuweza kuwa na mbadala wa njia za kupita badala ya kufuata njia kuu. Vilevile msongamano ukizidi sana Serikali kuruhusu hata daladala kuchepuka ili kuwawaisha wananchi makazini mwao, hali hiyo itasaidia kuharakisha shughuli za watu na hivyo kuendelea kunyanyua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzungumzia hali ya Jimbo la Kibaha Vijijini. Tuna changamoto nyingi sana zinazohusiana na miundombinu, kwani baadhi ya barabara nyingi zimekuwa hazipitiki kwa msimu mzima na zile zinazopitika basi ni kwa kipindi cha kiangazi tu, ila ikitokea masika inakuwa kero kwa wananchi kwani shughuli nyingi za kiuchumi husimama kutokana na maeneo mengi kutokupitika kabisa.

Naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu ya barabara kutoka Mlandizi mpaka Mzenga zitajengwa na zitakamilika lini, pia barabara ya Korogwe, Soga, Kisarawe nashauri zingepandishwa hadhi kuwa barabara za mkoa ili kuwezesha kuhudumiwa ipasavyo. Vilevile barabara za Vigwaza, Kwala na Dutumi hadi Kisarawe nazo pia zipandishwe hadhi kuwa barabara za mkoa.

Hata hivyo barabara za Chalinze, Gwata, Magindu, Lukenge hadi Morogoro Vijijini, barabara hizi zimeunganisha Wilaya tatu, zikiwa katika kiwango cha lami tutakuwa tumefikia lile lengo la kuunganisha Wilaya hadi Wilaya na kuwafanya wananchi wa Wilaya hizo kufanya shughuli zao za kibiashara kwa urahisi na kukuza uchumi wa Taifa letu. Naomba Wizara ituangalie kwa jicho la huruma katika barabara hizo ili kusaidia kunyanyua uchumi wa Kibaha Vijijini kwa kukamilisha miradi hiyo na ile ambayo haikuanza basi watutengee fedha ili kazi ianze mara moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali, njia mojawapo itakayosaidia kupunguza msongamano Jijini Dar es Salaam. Kwanza kabisa Serikali lazima iwe na mkakati wa utanuaji na uboreshaji wa miundombinu, ni jambo litakatopunguza kero hii, inaonekana kuwa mbinu hii ni ya muda mfupi ila itasaidia sana. Uboreshaji wa miundombinu yaani njia za maji taka, barabara kuu na zile zinazounganisha mitaa unaweza kufanyika lakini bado tatizo hili la msongamano likaendelea kuwepo baada ya siku chache.

Vilevile bado kuna haja ya kujenga barabara za juu maarufu kama *flyovers* hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile Magomeni, Ubungo, Tazara, Morocco na kadhalika. Nazishauri Manispaa za Jiji kuhakikisha zinakarabati barabara zote zinazounganisha mitaa *(ring roads)* ili kupunguza msongamano katika barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikitafakari namna ambavyo miradi mingi inavyoendeshwa, naomba kuwashirikisha Wabunge wenzangu juu ya *potential white elephant* iliyotengenezwa kwenye mradi wa mabasi yaendayo kasi yaani *DARTS,* je, ni kweli *DARTS* ilikuwa ndiyo njia pekee ya kuondokana na kupunguza msongamano Dar es Salaam na kuwa ndiyo kipaumbele cha kwanza cha kutatua kero hii *(in terms of cost, efficiency and priorty)?*

Mheshimiwa Spika, je, hizi nyumba za kusubiria wasafiri zilizojengwa zilikuwa zina ulazima gani wa kujengwa kwa gharama kama ilivyofanyika hivi sasa, je, namna ambayo barabara zimejengwa itapunguza foleni kweli? Ni lazima tujiulize ama tungejiuliza kabla ya kufanya maamuzi ya mradi huu, kwani kwa maoni yangu, *I stand to be corrected DARTS* haitapunguza msongamano na huenda ikaongeza na kama kweli mradi huu ulijadiliwa kwa mapana yanayostahili basi ungeonyesha mapema kuwa unatija.

Mheshimiwa Spika, kama ningekuwa mimi ningeanza na kujenga *fly overs* kwanza halafu barabara za pembezoni kwanza na kama fedha ingewekuwepo ya kutosha basi ningeimarisha usafiri wa reli ndani ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na kuimarisha uchukuzi wa mizigo kutokea Bandari ya Dar es Salaam kwa kuweka bandari ya nchi kavu *(dry port)* maeneo ya Ruvu au Mlandizi. Ukiziwekea lami barabara za Kinyerezi – Mbezi Loisi, Makongo Juu, Goba Tangi, Bovu - Morogoro, Mbagala - Kipawa/Banana/Ukonga utapunguza msongamano kwenye barabara ndani ya Jiji la Dar es Salaam kwa kiwango kikubwa na kwa gharama ndogo kuliko huu mradi wa *DARTS* ambao sidhani kama utasaidia kupunguza msongamano uliokuwepo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kulikuwa na sababu ya kufuata ama kuiga njia nyingine ambazo nchi jirani wamezitumia na kuweza kupunguza misongamano kwa namna walivyotengeneza miundombinu yao ambayo ni endelevu kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TEMESA, hili ni wakala wa kutengeneza magari ya Serikali na wakala hawa wapo kila Mkoa lakini karakana hizi hazifanyi kazi badala yake wanapokea magari na kuyapeleka kwenye *garage* za watu binafsi na kupelekea magari kutengenezwa kwa bei ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, swali ni kwa nini Serikali isitenge fedha kwa ajili ya kununua mashine za kisasa na kupeleka wale mafundi mafunzo *(training)* ili tuweze kuokoa fedha hizi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu magorofa yaliyojengwa chini ya kiwango Dar es Salaam, pamekuwepo na majengo kubomoka au kuporomoka na Tume zimeundwa kuchunguza mpaka leo Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Edward Lowassa na ile ya majengo ghorofa mbili imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa magari Dar es Salaam, mara nyingi tumesema ili kupunguza msongamano Dar es Salaam ni lazima zile barabara za *ring road* zikarabatiwe vizuri hata kwa kiwango cha changarawe ziweze kupitika, kwa kiasi kikubwa itapunguza sana foleni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matuta kwenye barabara kuu, haya matuta kwa kiasi kikubwa yanachangia ajali barabarani, isitoshe matuta haya hayana *standard,* mengine ni makubwa mno na mengine hayana alama kwa nini matuta kwenye *motorway* yasiondolewe?

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Serikali zilizobinafsishwa na kubadilisha matumizi kwa mfano Oyesterbay nyumba nyingi zilizokuwa za viongozi na kuzinunua zimegeuzwa kuwa *garage* za kuuzia magari nyingine zimegeuzwa kuwa baa! Je, Serikali ina mikakati gani ya kuzirudisha nyumba hizi zirudi Serikalini kwa kuwa waliozinunua wamevunja masharti ya matumizi?

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza kwa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa dhati kabisa kwa kuamua kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara kutoka Kinyanambo (A) Mafinga mpaka Igawa - Rujewa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali ikaanza kutengeneza kwa kiwango cha lami hata kwa kilometa mbili au tatu kila mwaka kuliko kuendelea kutengeneza kwa kiwango cha changarawe. Barabara hazidumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali kumalizia ujenzi wa kilometa 0.6 ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali kuanza kuangalia ujenzi wa barabara pale Mafinga Mjini kwa kiwango cha lami ambayo ni Halmashauri ya Mji.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA**: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi nzuri hususani walivyojitahidi kurudisha mawasiliano katika maeneo yaliyokumbwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa fedha za *road fund* kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Gizgiz katika Kata ya Kimote kwenda Mkuyuni. Pamoja na kupata shilingi milioni 200 napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kuongeza kiasi cha shilingi milioni 100 ili hilo daraja lijengwe kwa kiwango kizuri zaidi, ujenzi uliahirishwa kwa sababu ya mvua na mto kufurika sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kukumbushia ahadi ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwamba Wizara isaidie pia ujenzi wa daraja la Kisanga stendi kuvuka Mto Ruvu. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kujenga daraja hili kwani wananchi wanaendelea kupoteza maisha kutokana na kushambuliwa na mamba wanapovuka Mto Ruvu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja hili naomba Wizara ya Ujenzi iagize Injinia wa *TANROAD* Morogoro asaidie kuchora daraja hili kwani Halmashauri haina wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba Wizara ikubali kuchukua barabara ya Ngerengere Tomunguo - Magogoni kuwa barabara ya mkoa. Halmashauri imeshapeleka maombi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi yangu matatu ambayo naomba sana Wizara izingatie na inikubalie, napenda sasa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu awabariki Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigoma -Kidahwe - Kibonde kupitia Kasulu kuelekea Nyakanazi, natambua juhudi za Serikali kujenga miundombinu nchini. Barabara ya Kidahwe hadi Nyakanazi imebaki bila lami, najua mkataba umeshasainiwa kati ya Serikali na mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali toka mwaka 2005 nilipoanza kazi hii ya Ubunge mpaka sasa bado naomba Serikali iijenge kwa kiwango cha lami ni kilio cha muda mrefu. Kwa hatua hiyo basi naomba Serikali itoe fedha kwa wakati na zile fedha za miaka ya nyuma zilizopangwa bila kutolewa naomba zitolewe ili barabara hiyo iende kwa kasi. Barabara ile ni muhimu sana kwa uchumi wa Kigoma na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile barabara ile ni muhimu sana kwa kuwa hatuna reli yenye uhakika na usafiri wa treni hauaminiki kabisa na ndege ni usafiri ambao unatumiwa na wachache. Nasisitiza barabara hii ni muhimu sana kwa walipa kodi wa Kigoma na mikoa jirani.

Mheshimiwa Spika, mwisho nasisitiza Serikali itoe fedha kwa wakati ili barabara hiyo ya Kigoma - Kidehwe Nyakenazi ikamilike kwa kiwango cha lami. Na tabia ya kutenga fedha bila kuzitoa isiendelee tena kwani mnawakatisha tamaa wananchi, maana wanasilikiza bajeti, wanasikia barabara itajengwa, imetengewa fedha lakini mwisho wake hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika ujenzi wa barabara za lami na za changarawe nchi nzima. Pamoja na pongezi hizi ninayo maoni yafuatayo:-

(a) Ahadi ya ujenzi wa barabara ya lami katikati ya Mji wa Manyoni, naishukuru Wizara kwa niaba ya wananchi wa Manyoni kwa kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, ombi ni kwamba mkandarasi awezeshwe kutekeleza mradi huu kwa ufanisi. Hivi sasa mkandarasi amesimamisha kazi kwa vile bado hajalipwa *certificate* hata moja tangu aanze kazi. Naomba alipwe ili kazi ianze tena.

(b) Ujenzi wa barabara ya Makongolosi - Rungwe – Mkiwa, barabara hii imo kutika ahadi za Ilani ya Chama Tawala na imekwishafanyiwa upembuzi lakini ujenzi haujaanza ombi la Wanamanyoni ni kwamba ujenzi uanze mwaka huu wa fedha 2014/2015.

(c) Nyumba za TBA za Dodoma, nyumba hizi zimesaidia sana kupunguza tatizo la nyumba kwa watumishi na viongozi wa Serikali lakini tangu zijengwe takribani miaka kumi iliyopita hazijafanyiwa ukarabati, hivyo zimeanza kuchakaa. Lakini pia kwa upande wa wapangaji nao hawalipi kodi ili fedha zipatikane zitakazowezesha gharama za ukarabati.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Wizara iingie mikataba na waajiri wa watumishi hao ili kodi ya nyumba hizo zikatwe moja kwa moja kwenye mishahara yao na kulipwa TBA. Hali hii itafanya kodi zote zilipwe kila mwezi na kuwezesha ukarabati wa nyumba hizo ufanyike. Aidha, barabara nyingine za Dodoma Mjini zimewekwa lami, lakini barabara zinazoenda katika nyumba hizo zipo mbili moja inaingilia Mbuyuni na ya pili inayoenda eneo la FFU, zote mbili ni za vumbi na ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni haya narudia kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Bagamoyo na la Chalinze kwa kupoteza ndugu zao kutokana na ajali ya mafuriko. Pia wananchi wanaokwenda maeneo yote nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pili nikupongeze na kukushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo umeendelea kuifanya, kwa ufupi wananchi wa Jimbo langu na la Bagamoyo tunashukuru sana. Kwa kuwa imekuwa ni wimbo wa muda wote juu ya ujenzi wa barabara inayotoka Mbwewe kwenda Misha (Mlandizi, Mvomelo).

Naomba kujua toka kwa Mheshimiwa Waziri ni mipango gani ambayo Serikali inayo juu ya ujenzi wa barabara hii inayounganisha Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Mvomelo, Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, pia kuna ujenzi uliopangiwa mipango toka daraja la Makofia, hadi Mlandizi, Kisarawe, Mkuranga kuwa ingejengwa kiwango cha lami. Je, ni nini kinaendelea juu ya ukamilifu wa ujenzi wa barabara hii inayounganisha Wilaya nne za Mkoa wa Pwani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER L. M. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu barabara ya kutoka Ramadi kwenda Bariadi hadi Mwigumbi.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo inaunganisha mikoa mine ya Mwanza, Mara, Simiyu na Shinyanga, Mheshimiwa Waziri, ujenzi wa barabara hiyo unasuasua.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe ujenzi wa barabara hiyo ili iweze kutusaidia wananchi wa Simiyu. Wananchi wa Simiyu ni wakulima wazuri wa pamba, wakati wa msimu magari yanahangaika, hayana pa kupita, barabara ni mbovu sana. Lakini pia ajali nyingi zinatokea kwa ajili ya ubovu wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Wilaya ya Itilima, Wilaya hiyo ni mpya, barabara nyingi ni mbovu yaani hazipitiki wakati wa masika, cha kusikitisha mpaka muda huu Wilaya hiyo haina mtalaam.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali naiomba Serikali ipeleke haraka mhandisi ili barabara ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri anayofanya. Barabara ya Igawa - Rujewa - Mafinga kilometa 146 ni ahadi ya muda mrefu sana ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Mbarali, pia ipo kwenye Ilani ya CCM kwa muda mrefu mno. Toka wakati wa Mheshimiwa Edmund Mjengwa (Kanali), Mheshimiwa Estherina Kilasi zaidi ya miaka 29 kwa sasa lakini utekelezaji wake bado.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tumepangiwa ukarabati kiwango cha lami, sijaelewa vizuri ukarabati huu kiwango cha lami ni ukarabati wa namna gani? Maelezo yaliyopo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 54 inaoyesha fedha zitatoka *World Bank* na Serikali ya Tanzania lakini bila kuonyesha ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa kazi hiyo naomba ufafanuzi. Barabara hii ilikwishafanyiwa upembuzi yakinifu muda mrefu, kilichobaki ni utekelezaji tu.

Mheshimiwa Spika, TANAPA waliomba kuchepusha barabara hiyo ili isipite karibu na hifadhi mpya iliyounganishwa na *Ruaha National Park* kwa upande wa Mbarali japo haipo ndani ya hifadhi. Katika kikao hicho walichokaa waliahidi kuwa kabla ya kazi ya ujenzi kuanza kazi hiyo ingekuwa imekamilika yaani mwaka 2011. Lakini toka mwaka huo hadi leo kazi hiyo haikufanyika, kwa hiyo kazi ya ujenzi ikianza nisingependa kuwekewa vikwazo. Mwaka 2011 - 2014 ni muda mrefu sana, nilileta taarifa Wizarani nikionyesha kuwa sitakubaliana kwa kukwamisha kazi ya ujenzi wa barabara hiyo kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ambayo inatoka/inaanzia Igawa - Rujewa -Madibira Mafinga ni kiungo muhimu kwa kusafirishia mazao kutoka Madibira kwenda Rujewa na Mafinga na inakopita kuna wakulima wengi wanaotegemea barabara hiyo ambayo inaunganisha makao ya Wilaya ya Mbarali na Mafinga.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Igawa - Rujewa - Ubaruku kilometa nane bado kukamilika kiwango cha lami nyepesi. Hii ni barabara muhimu sana kwa usafirishaji wa mchele kwenda sokoni maeneo mbalimbali ya nchi hadi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii Mheshimiwa Waziri aliniahidi kumalizia kipande hiki cha Igawa - Rujewa - Ubarukwe.

Mheshimiwa Spika, naomba ahadi hii itimie, mimi nimekwishawaambia wananchi wa Mbarali juu ya ahadi yako. Lakini fedha zilizotengwa kwa barabara hii ni kidogo sana sasa itakuwaje? Naomba unapohitimisha utamke ahadi yako hii kwa wana Mbarali wasikie. Ahsante.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya barabara iliyotengewa fedha kwa mwaka 2013/2014 mingi haijakalimika na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watu wa maeneo husika. Hii husababisha vikwanzo katika uendeshaji wa shughuli nyingine muhimu za uchumi. Kwa mfano barabara ya Dodoma - Iringa, Nzega - Tabora, Tabora – Itigi - Manyoni ni moja kati ya miradi ambayo imetengewa fedha lakini haijakamilika kwa wakati na bado Wizara haifanyi jitihada ama juhudi za msingi katika kuhakikisha miradi hii si tu kuwa inakamilika kwa wakati bali pia inakamilika kwa ubora uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu watumishi wa mizani wamekuWa wakilalamikiwa kujihusisha na rushwa kutoka kwa madereva wa magari makubwa wanaokiuka sheria za barabara. Haya hufanyika kwa watumishi kushirikiana na madereva pamoja na walinzi wa mizani kuyaruhusu magari hayo kupita mizani hata baada ya kugundulika na makosa mbalimbali kwa utaratibu ulio nje ya mfumo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida magari yanayozidisha uzito au yanayokutwa na makosa ya kuharibu barabara huingizwa kwenye uzio wa mzani husika baada ya kupima uzito na huruhusiwa kutoka kwa *gate pass* au risiti ya faini iliyolipwa lakini cha kushangaza yapo mengine yamekuwa yakiruhusiwa na watumishi au walinzi wa mizani bila kufuata taratibu hizi kwa makusudi, ili kusaidia kuwanasa watumishi wapenda rushwa ni lazima vituo vyote vya mizani kutengewa bajeti ya kufunga kamera za CCTV zitakazokuwa na uwezo wa kuyaona magari yote makubwa yanayopita katika barabara kuu zitakazopiga picha za magari hayo kabla na baada ya kupima mzani. Hii itasaidia kuzisimamia barabara hizi kuwa na ubora unaotakikana, kuepuka matengenezo ya barabarani mara kwa mara, kukusanya mapato zaidi yanayotokana na faini na kukomesha mianya yote ya rushwa.

Aidha, ni lazima kwa Wizara kufanya kazi kwa ukaribu na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufanya uchunguzi wa mara kwa mara katika vituo vya mizani.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza mwaka 2010, Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alitoa agizo kwa kutoa maelekezo kwa Serikali Kuu na taasisi zake pamoja na Serikali za Mitaa, kutoagiza tena magari ya kifahari bila kupata kibali maalum kutoka ofisini kwake. Waziri Mkuu alirudia tena kusisitiza usitishwaji wa Serikali kununua magari ya kifahari mwaka 2012, wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge, kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Hivi karibuni kumeibuka utata kuhusu uamuzi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe kununua gari la kifahari kwa shilingi 142,510,000/= kwa matumizi ya Mkurugenzi wake na kupuuza agizo la Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda la kupiga marufuku ununuzi wa magari ya kifahari (mashangingi). Lakini vilevile, taasisi za Serikali nyingi bado zimeendelea na ununuzi wa magari ya kifahari na kupuuza kauli ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tunaiuliza Wizara hii kwa kupitia TEMESA imeshakagua taasisi ngapi za Serikali ambazo hazijafuata agizo la Waziri Mkuu na hatua gani zimechukuliwa kwa watendaji ambao wamekiuka agizo hilo?

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, suala la maafisa wa Serikali pamoja na viongozi waandamizi wa Serikali wakiwemo Mawaziri kuendelea kupangishwa nyumba za binafsi na wengine wakiishi mahotelini, wakati wa Serikali ya awamu ya tatu waliziuza nyumba za Serikali, ni kitendo cha matumzi mabaya ya fedha za walipa kodi. Kwa muda mrefu Wizara hii imeendelea kusema kuwa inaendelea na ujenzi wa nyumba nyingine kwa ajili ya makazi ya viongozi wa Serikali lakini miradi hiyo inachukua muda mrefu na Serikali ikiteketeza fedha kwa kulipia kodi za viongozi.

Mheshimiwa Spika, je, Waziri anatoa kauli gani ikizingatiwa kuwa tumeshauri kwa muda mrefu kuzirudisha nyumba hizo katika mikono ya Serikali ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha za umma ukizingatiwa kuwa kuna ulanguzi wa thamani halisi ya nyumba wanazokaa viongozi hao ambao kodi hulipwa kuliko kiwango cha kawaida?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. PINDI CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naipongeza Serikali kwa kuikumbuka barabara ya Njombe - Ludewa - Itoni.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 26 wa hotuba umeelezea Daraja la Ruhuhu - Ludewa kuwa usanifu unaendelea, ningependa kufahamu lini litaanza kujengwa? Fedha za usanifu na ujenzi ni za ndani au nje? *Donor* ni nani?

Mheshimiwa Spika, maeneo ya mizani nashauri barabara zake ziwe zinaenda pembeni kiasi cha kutoa *space* kwa barabara kubwa kwani huleta foleni sana mfano Kibaha foleni, Morogoro foleni na Makambako foleni sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma - Iringa pamoja na kuanza lini pia kumalizia? Ni muhimu sana kuanza lami pia kumalizia ni muhimu sana. Hivi mbona Tanzania hatufikii kujenga *flyovers* (barabara za juu)? Idadi ya watu inaongezeka, bora kuanza kulifikiria hilo.

**MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli (Mb), nampongeza sana kwa kazi nzuri anayofanya kwa kushirikiana na kamanda mashuhuri mchapakazi asiyechoka ambaye umemuambukiza tabia zake za kufanya kazi bila kuchoka, ujasiri wa kutukuka na mcha Mungu, Mheshimiwa Lwenge.

Mheshimiwa Spika, aidha nimpongeze kwa hotuba nzuri. Kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nawashukuru sana kwa kututekelezea ilani kwa asilimia 87, mabasi yote yanafika, wagonjwa hawafii njiani kwani kuna magari ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kilio chetu kikubwa sasa hivi pamoja na kazi nzuri iliyofanyika hapo awali baada ya mvua hizi kubwa za juzi katika Wilaya zote za Tanga, Kilindi imeathirika sana. Nashukuru kwa *commitment* ya kututengenezea barabara zote na madaraja yaliyoathirika.Hata Meneja *TANROADS* Mkoa, Bwana Ndumbaro, amenihakikishia suala hilo. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba unisamehe lakini nieleze masikitiko yangu kama mwakilishi wa watu wa Kilindi. Wilaya inakaribia miaka 17 tangu ianzishwe kutoka Handeni, lakini pale makao makuu tuliahidiwa lami kilometa tano, zaidi ya miaka saba mfululizo, kweli hata

kilometa mbili tu zimeshindikana, hivi wananchi wa Kilindi hawana haki ya kuona lami hata nusu kilomita. Kweli inatunyong'onyeza, uchaguzi unakuja, ahadi tumetoa, nabaki na aibu. Naomba mnisaidie hili mwaka huu ili mwakani niwe nina la kujivunia.

Mheshimiwa Spika, barabara zote kwenye kitabu chako cha hotuba ni tatu tu ambazo nazo ni *rehabilitation,* hata ile ambayo ilikuwa Handeni - Kibirshi - Songe - Lengatai - Kijungu iliyofanyiwa *feasibility study* na kupimwa mwaka juzi ili iwekwe lami hadi leo na hata bajeti hii sitendewi haki. Inauma sana.

Mheshimiwa Spika, Handeni barabara zote lami, hasa Mkata - Handeni lami, inauma sana japo sitakiwi kuelezea ya wengine, lakini hawa tunapakana nao, na wananchi wangu wanasema mbona kura za CCM tumeongoza Mkoa wa Tanga kwa Rais, Mbunge na Madiwani, lakini Serikali yetu inatutenga? Inaumiza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi hata barabara moja ya lami, hizi barabara zinazotengewa kila mwaka na kubomoka kila mvua zinaponyesha inabidi tuanze upya naona tunaonewa. Kwa jinsi ninavyojituma kulinda heshima ya Serikali yangu, nadhani nastahili a *better treatment* hasa ukizingatia barabara kwangu ni siasa. Naomba, naomba, naomba nifikiriwe.

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara nazo ziwe *considered*. Watu wangu wanalima sana, ila hakuna barabara za kutoa mazao shambani, sisemi hatujapatiwa ila naomba nifikiriwe upya hasa ambapo sasa usafiri uliopo ni pikipiki, baiskeli au baadhi ya matrekta.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ule mtaa wa Galu Ada Estate ambayo haina nusu kilometa inayochepuka kutoka kwenye lami nzito inayopita kwa juu kuzunguka hadi kurudi maghorofani, basi kale kamchepuo ambako kuna Ofisi, Star Tv na kadhalika tupate lami, siyo *fair* kabisa mitaa ya ndani ndani ina lami, ila wewe kwa mara ya chache unazofanya mazoezi unalazimika kupita barabara mbovu na imejaa tope. Natanguliza shukrani.

Mheshimiwa Spika, Mungu awape mioyo ya huruma ili muweze kuwatendea Watanzania mambo mema ambayo mwisho wa siku yataacha kumbukumbu njema kwenu na kwa utukufu wa Mungu.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa utendaji mzuri, wewe ni jembe, wewe ni mfano wa kuigwa, kila Wizara unayoongoza ufanisi unaonekana. Kiwango cha barabara kwa wingi na ubora kilichotengenezwa katika kipindi hiki ni kikubwa sana kutengeneza katika historia ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua barabara ya Katoma - Kanyigo itakamilika lini? Kuna barabara inayotoka Katoma kwenda Kashozi - Kabango hii ni pale tangu miaka ya 1960. Ni barabara iliyo na madaraja kama 12, Halmashauri haiwezi kuitengeneza hii barabara. Ni ngumu sana sababu ya madaraja ya pale Kyamato, barabara hii itatumika na watu wanaotoka Karagwe, Misenyi, Bukoba Vijijini kuelekea kwenye Ziwa Victoria kwenye mpaka wa Uganda. Naomba ukubali kuichukua na kuitengeneza.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza ajali kwenye barabara kuu mfano barabara ya kutoka Dar es Salaam - Dodoma inabidi kuwe na barabara mbili zinazojitegemea, barabara ya kwenda tu na barabara ya kurudi tu.

Mheshimiwa Spika, magari mengi yanagongana *(head on collition)* wakati yana *overtake*. Lakini barabara ya kwenda na ya kurudi zingekuwa tofauti haya yasingetokea. Kwenye miji mingi na nchi nyingi zilizoendelea barabara zao zipo kwenye mtindo huo. Je, Tanzania tuna mpango gani wa kuwa na mfumo huu wa barabara?

Mheshimiwa Spika, Dodoma ni Jiji linalokua haraka sana. *Traffic* kubwa imeanza hasa nyakati za asubuhi na mchana. Ili Dodoma isije ikawa kama Dar es Salaam ni linin a kuna mipango gani ya kudhibiti msongamano wa magari Dodoma?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Waziri/Naibu Waziri na watendaji katika Wizara ya Ujenzi. Tunshukuru kwa barabara Loliondo - Mto wa Mbu (kilometa 213) tunaamini ujenzi huu utaaanza mara moja baada ya bajeti hii kupita.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iangalie uwezekano wa *ring roads* katika Jiji la Arusha Mjini ambalo linakuwa kwa kasi na kuwa na foleni kubwa sana. Tusije tukasubiri tukafikia kama ilivyo kwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi wa nyumba elfu kumi (10,000) naomba Wizara kupitia TBA katika ujenzi wa nyumba zake Arusha isikosekane, kama tunavyofahamu Arusha ni mji unaokuwa kwa kasi, nyumba 40 mlizotupangia ni kidogo na mji ule unakuwa kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Monduli Mjini kwenda Monduli Juu Enguiki, nayo iwekwe kwenye mpango wa kuwekwa lami, wakati wa mvua hali ya barabara inakuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Benki ya Dunia wa barabara za miji katika Mji wa Arusha zimefanyika lakini zipo barabara kama za Themi Nane Nane, Njia ya Ngo'mbe, Mbauda, Kijenge ya Juu, Mushono na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na napongeza kazi nzuri ambazo Wizara hii imefanya.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, hongera Waziri kwa kazi nzuri mpaka unakonda, pole, nina mambo haya:-

Mheshimiwa Spika, Kibiti – Lindi itaisha lini? Jibu vinginevyo nitaondoa shilingi kama majibu hayaridhishi.

Mheshimiwa Spika, kuunganisha barabara za Mkoa kwa Mkoa wa Lindi tunazo, tunaomba zifunguliwe, ilani ya mwaka 2005 barabara ya Liwale – Mpigamiti kwenda Mbuga - Morogoro tunaomba ifunguliwe na kuwekwa changarawe, barabara ya Liwale - Nachingwea Kilimarondo kwenda Mkoa wa Ruvuma - Tunduru, barabara hizi mbili zifunguliwe kwa kiwango cha changarawe, ahadi ya ilani ya mwaka 2005 ilisema.

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro ya wananchi wa Kiwawa Lindi Vijijini. Wanataka barabara yao ya asili itokayo Milola kwenda Mandawa kupitia Milola Namkongo – Mchichili –

Mputwa – Kiwawa – Mandawa barabara hiyo ndiyo wanaitaka kwani kuna shule, zahanati, mazao, watu wengi, lakini Serikali wamechepusha barabara hiyo kisiasa wakapeleka Mlola – Nahoro – Mandawa hii hawaitaki.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro sana kwa kuwa wananchi wa Lindi Vijijini Rais analijua na aliagiza viongozi wa Lindi waliangalie hilo ili walifanyie ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kupandisha hadhi barabara Sheria Na. 13 ya mwaka 2007 iliyofanyiwa marekebisho, barabara za Wilaya inapobidi zipandishwe hadhi (madaraja) tunomba barabara hizi zipandishwe hadhi:-

(i) Nyengedi – Rondo – Mandawa;

(ii) Mchunga – Kijiweni Jiwe la Mzungu;

(iii) Liwale Kilimarondo – Tunduru; na

(iv) Nachingwea – Chiola Ruangwa barabara hizo zipandishwe daraja kuna madini, utalii, mbao, gypsum, gesi na ina watu wengi.

Mheshimiwa Spika, barabara za Liwale hazina pacha lazima utoke Liwale - Mwanza ndipo uende mji mwingine na kuna kata 21 ni mfumo wa kikoloni wa kumbana mtu anaenda wapi, lazima aanzie Liwale Majini, tunaomba ibadilishwe ipitie nje kwa nje.

Mheshimiwa Spika, tunataka kivuko kiwepo cha Lindi kwenda Kijiji cha Kitunda, kuna watu wengi na mazao mengi huko, kuwepo na Kivuko. Tunaomba kivuko cha Lindi – Kitunda ambayo ni ahadi za Rais, kuwa na lami katika makao makuu ya Wilaya Mkoa wa Lindi kuna Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea, Ruangwa na tupatiwe lami kilomita mbili, barabara za Dodoma - Kisasa nyumba za Magufuli 300 zikarabatiwe, tunaomba nyumba zikarabatiwe pia barabara zile zipigwe greda ni mbaya sana ni vichaka tu. Ahsante

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kwa kifupi kabisa nichangie juu ya Wizara hii, napenda kujua *status* ya barabara za Wilaya ya Tarime na Rorya ambazo ni barabara zilizo kwenye *TANROADS* na ni ahadi za Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu barabara ya kutolea Rorya (Nyamasanda/Ikoma) kupitia Tarime yaani Susuni – Kabiterere, Remagwe – Sirari Nyabisaga – Nyantira - Muriba Mangacha – Kegonga ambayo ni *security road* inapakana na nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, Waziri amekuwa akiahidi kujenga kwa kiwango cha lami nyepesi/au molamu nzito. Ni muhimu sana kwa mustakabali wa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini hii barabara haifanyiwi matengenezo ya mara kwa mara kwa molamu nzito ili kuimarisha usalama wetu?

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusiana na barabara ya Nyamwaga inayoanzia Tarime Mjini - Nyamwiga Kamaorere - Nyamwaga - Nyamango hadi Mto Mara kuunganisha na Wilaya ya Serengeti, hii barabara ni muhimu sana katika uchumi wa Wilaya hizi mbili na mkoa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, nashangaa ila kwa nini uwekaji lami unasuasua? Napenda kujua itachukua muda gani kukamilisha uwekaji lami kwenye barabara hii?

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna barabara ya Nyamanga - Muriba na ile inayounga na *security road* ya Masanga hadi Gibaso kwa nini hazifanyiwi marekebisho ya mara mwa mara? Ikimbukwe Mkoa wetu unajishughulisha na kilimo na mazao ya aina mbalimbali hivyo tunahitaji miundombinu ya barabara imara, ili wanunuzi wa mazao waweze kufika kwa urahisi na hivyo kupandisha thamani ya mazao ya wakazi wa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, pili kwa maana ya Wilaya ya Rorya ni juu ya barabara ya Mika hadi Shirati au Utegi hadi Shirati ambayo pia ni ahadi ya Rais. Mliahidi kuwa mwaka huu ingekuwa kwenye bajeti lakini sasa naona haipo. Napenda kujua ni lini sasa ahadi itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, tatu na mwisho kuhusu Mkoa wa Mara ni barabara ya Makutano – Nata. Hii barabara ya Nata inasuasua sana, kiukweli nashindwa kujua dhamira ya Serikali juu ya barabara hii licha ya umuhimu wake, mwaka huu naona imetengewa shilingi bilioni tisa tu jamani kwa barabara yenye kilomita zaidi ya thelathini.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Waziri wazingatie haya malalamiko yangu na wayape uzito na kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuzungumzia utumiaji mbovu wa barabara na hasa barabara kuu. Utakuta gari limeharibika lakini hamna alama yoyote inayoashiria kuna gari bovu na hii ni hatari hasa wakati wa usiku, lakini pia utakuta kwa upande mwingine unakuta wameweka ishara ya matawi, mawe au matairi kwa kuzuia magari mengine au kitambulisho kuwa kuna gari bovu. Mara gari lao linapotengemaa huondosha gari zao na kutekeleza hayo mawe, matairi na matawi kitu ambacho husababisha ajali kwa gari zingine hasa kama mawe makubwa yametumika.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwepo sheria au kanuni/waraka itakayoambatana na jina ili kukomesha adha hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni juu ya magari yaliyopata ajali au kuharibika, nashauri tuwe na *recovery vehicles* kwenye barabara kuu *(high ways)* ambazo zitakuwa zikiyatoa haya magari barabarani mara moja bila kusababisha ajali zingine na misongamano isiyokuwa na tija na *service* ya *recovery* inaweza kuwa inafidiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara na hasa barabara kuu kuwa na mashimo/*plot holes* ambazo si tu zinaharibu magari bali husababisha ajali. Nashauri kuwe na matengenezo ya mara kwa mara na uangalizi wa hali ya juu.

Vilevile matuta makubwa barabarani ni kero kubwa sana na huchangia ajali nyingi na hasa pale unapokuta hamna alama yoyote barabarani ambayo vinaainisha kuwa mbele kuna tuta au kona kali au upepo mkali, najua vibao vingine huibiwa lakini mnaweza kuweka *materials* ambazo haziibiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa ninaomba nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi na Waziri wake Mheshimiwa John Magufuli kwa kutazama Ludewa kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Itoni – Ludewa – Manda ni uti wa mgongo kwetu na *sincerely* nimefarijika kuona kuwa imetengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami. Mimi kama Mbunge na mwakilishi wa wananchi na wananchi wangu tunakuombea Waziri Magufuli, *CEO* wa *TANROADS, Engineer* Mfugale wawe na afya njema na uzima ili mfanye kazi zenu kama mlivyopanga. Sisi Ludewa tunakupenda Mheshimiwa Magufuli.

Mheshimiwa Spika, ninatumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe, *Engineer* Mazana. Mazana ni mtu muadilifu, msikivu na mchapakazi, Mungu ambariki sana *Engineer* Mazana.

Mheshimiwa Spika, mwisho namuomba Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Magufuli aje Ludewa atutembelee. Mbona maeneo mengine Mheshimiwa Magufuli unaenda/unafanya ziara? Sisi Ludewa tunakupenda njoo ututembelee tufurahie pamoja matunda hayo ya uhuru (lami).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, niungane na mwenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote. Pia pole ya ajali ukiwa katika kutekeleza majukumu ya kitaifa Mwenyezi Mungu ashukuriwe, Amina.

Mheshimiwa Spika, juhudi za ujenzi wa barabara tunaona lakini maeneo mengine unasuasua hii kutokana na uhaba wa fedha, ni mkakati gani uliokuwepo ili kuhakikisha ujenzi unakwenda kwa wakati na pia kuhakikisha ahadi za Mheshimiwa Rais inakamilika kabla hajamaliza kipindi chake?

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo katika barabara za Mkoa wa Pwani kwani kuna ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi toka mwaka 2005 hadi leo hazijaisha nazo ni Kisarawe – Maneromango – Mlandizi – Makofia – Kisarawe – Vikumbulu – Mloka na zile zote ambazo umezielezea.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kama fedha ulizotenga zitaweza kukamilisha hizo kazi. Naomba ofisi yako iweze kutimiza na kukamilisha ujenzi kwa wakati. Pia uangalie uwezekano wa kufufukua barabara ya zamani Mzenga – Morogoro ili kupunguza msongamano na kutumia njia moja tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wasiwasi wangu katika ukamilishaji wa ujenzi wa barabara, napenda nikupongeze kwa ujenzi wa barabara za Bagamoyo – Msata naomba ujenzi wa madaraja uharakishwe. Napongeza ujenzi wa Daraja la Kigamboni, Daraja la Malagalasi na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, tujue fedha za nje zinatoka wapi na kujua kama zitafika kwa wakati, vinginevyo tutafute njia mbadala za kupata fedha za ndani ili kuweza kujenga barabara zetu ambazo ndiyo zinazotusaidia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Mwanangu angalia barabara za wazazi wako.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la uharibifu wa barabara kwa maana ya kujengwa chini ya kiwango na kupelekea kuwa na mabonde, je, tatizo hili ni kutokuwa na wakandarasi wasiofikia kiwango au mtaalamu wa upimaji na uchanganyaji udongo na kupima kiwango cha lami? Nini hasa kinachoharibu barabara?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la barabara ya Ndundu - Somanga mbona hapa ahadi yako haikamiliki? Tatizo la fedha haliwezi kuwa ndiyo sababu kwani ni zaidi ya miaka kumi vipi ahadi haikamiliki na kila mwaka kuna kuwa na bajeti? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, kuna kero kubwa sana kwenye barabara inayotoka Hoteli Tatu kwenda Kilwa Pande, hii barabara inaleta kero kubwa sana kwa wananchi wa huko kiasi cha wakati wa msimu wa mvua wananchi hao kutengwa na kuwa na hali ngumu ya usafiri. Naomba Serikali ione ni jinsi gani watasaidia kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, napongeza kazi nzuri ya *TANROAD* chini ya *Engineer* Mfugale kwa kazi nzuri anazozifanya. Ili kazi zake ziwe na ufanisi zaidi maana baada ya barabara zilizo chini ya *TANROAD* kuwe na chombo ambacho kitasimamia barabara za vijijini kwa usimamizi wa Halmashauri zetu hauna uwezo wa kutosha. Ni vyema sasa Serikali ikawa na uamuzi wa kuanzisha Kitengo cha Barabara za Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi ni kwa sababu ya utekelezaji mzuri wa mipango ya maendeleo. Kwa miaka yote katika Wilaya yangu ya Geita barabara zote za Mkoa zipo katika hali nzuri sana pamoja na kuwepo kwa magari mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya shughuli za uchimbaji madini lakini barabara hizi zipo safi mwaka mzima. Hata wananchi wenyewe wanafurahia na kupongeza kwa juhudi zinazofanyika za utengenezaji barabara. Katika Wilaya ya Geita zipo barabara ambazo tumeomba zipandishwe hadhi kutoka Halmashauri ziwe barabara za Mkoa. Kwa mfano katika Jimbo la Busanda ipo barabara inayojulikana kwa jina la Katoro – Nyakamwaga – Kamena – Mwingiro – Kharumwa *(Mang'ombe road)*, barabara hii muhimu sana ya kiuchumi. Barabara inaunganisha Wilaya ya Geita Vijijini na Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, taratibu zote zimefuatwa na kupitisha ombi hili, hivyo ninaomba Wizara iniangalie kwa huruma na pia iwatizame wananchi wa Wilaya hizi mbili kwa huruma kwa kupandisha hadhi barabara hii muhimu ya kiuchumi kwa wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Spika, barabara ya pili ni ile barabara ya Geita – Bukoli – Kahama. Barabara hii ni ahadi ya Rais kuwekewa lami na ni barabara iliyopo ndani ya Ilani ya CCM ya mwaka 2010 2015, sasa utekelezaji utaanza hivyo naishukuru Wizara.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa utekelezaji ambao utaanza kwa ujenzi wa barabara ya Katora – *Bukombe road* kwa kiwango cha lami. Vilevile nashukuru kwa ujenzi wa kilometa 0.6 za lami katika mji wa Geita.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo machache ninaamini kuwa kilio chetu cha kupandisha hadhi kwa barabara ya Katoro – Nyakamwaga – Kamena – Mwingiro kitafikiriwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza Waziri, pamoja na Naibu wako kwa kazi kubwa na nzuri mnayofanya tangu mlipokabidhiwa Wizara hiyo ambapo inafananishwa na mishipa ya damu kwa vile inajenga miundombinu inayochochea kasi ya maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na kuwepo baadhi ya watu katika nyadhifa mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wabunge na kadhalika, nakushauri usikate tamaa kwani ukubwa wa mafanikio yako unapimwa kwa ukubwa wa jitihada zako, ukubwa wa ndoto zako na namna unavyoweza kuvumilia kukatishwa tamaa.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa niaba ya Wanamwibara kwa kuwajengea barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 51 kutoka Kisorya – Bulamba. Pamoja na ujenzi huo Wanamwibara tunaomba muendelee kutenga fedha ili barabara yote Nyamiswa - Bunda - Kisorya - Nansio ijengwe lami. Aidha leo Wanamwibara wanataka kukusikia wewe mwenyewe ni lini utakuja na Mheshimiwa Rais kuzindua ujenzi wa hiyo barabara? Wananchi wa Mwibara wanakupenda na wanakuita Magufuli ni jembe letu na hivyo wanahamu ya kukuona na kusikia.

Pia bajeti ya mwaka juzi na katika swali langu Bungeni niliomba tupatiwe Boti ya Mv Ukara huko Mwibara kuhudumia wananchi wa visiwa vya Mwibara, kuhudumia wananchi wa visiwa vya Nafuba/Sozia na Nansio na nchi kavu. Hadi leo Serikali haijatupa majibu juu ya ufumbuzi wa tatizo la usafiri kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme Wizara yako unafanya kazi kubwa na kwa kasi kubwa na hivyo kuonyesha kwamba wananchi wataweza kusafiri kwa Bajaj kutoka Mtwara hadi Mtukula unakuwa wa kweli, chapa kazi na sisi Wabunge tuko nyuma yako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa hotuba nzuri sana. Ila nimepata na homa kali ya ghafla kwani barabara niliyotegemea ujenzi wa lami kuanza kwa mwaka huu Kisarawe – Maneromango (kilometa 54) imetengewa shilingi milioni 84 tu. Sio siri kiongozi wangu umeniweka katika mazingira magumu sana, kwa sababu hii kutoanza ujenzi wa lami. Chondechonde fanya iwezekanavyo ili uninusuru.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Kwa Sadala– Masama kilometa 12.5 bado haijapata maelezo ya kina ni nini hasa kinafanyika na kwa utaratibu gani? Wakati wa uzinduzi wa barabara hii Mheshimiwa Rais alikubali ombi la ku-*extend* barabara hii kuunganisha barabara ya Sanya Juu katika Kijiji cha Mashua mpaka barabara ya Machame Kijiji cha Wavi. Serikali haijatoa kauli yoyote kuhusu namna hii inavyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bomang'ombe - Rundugai - TPC ni ndefu na muhimu imeombewa kupandishwa daraja toka Wilaya kwenda Mkoa. Vikao vyote vya Mkoa vimepitisha ombi hili, Wizara ina kauli ipi kwa ombi hili la barabara hii inahusisha daraja la Mnepo lililopo Kata ya Machame Weruweru ikiunganisha Wilaya za Hai na Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, barabara ya *Machine Tools – Machame gate* ni chakavu na ya muda wa zaidi ya miaka 40 na ni nyembamba sana isiyo katika makazi ya watu wengi na ina magari mengi. *Repair* ndogo ndogo huwa zinafanyika lakini hazitoshelezi. Naomba kauli ya Wizara.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya utekelezaji wa mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya mwaka wa fedha 2014/2015 naomba Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Waziri Mkuu watoe majibu kuhusu masuala yafuatayo yanahusu mradi wa mabasi ya haraka ya *(BRT)* unaotekelezwa na mkandarasi Starbag kwa usimamizi wa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na wataalam wa mabasi ya haraka *(DART)*.

Mheshimiwa Spika, mosi kiwango cha fedha kilichotumika mpaka sasa kwa ujenzi kuanzia Kimara mpaka Magomeni na ujenzii wa maeneo mengine ikilinganishwa na kiwango kilichopangwa awali kwenye mikataba ya mradi. Nilitoa wito kwa Mkurugenzi wa DART kutoa nakala ya ripoti ya utekelezaji kwa Ofisi ya Mbunge ziada ya taarifa fupi ambazo huwa tunapatiwa kwenye Bodi ya Barabara na Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC), hata hivyo DART haikufanya hivyo. Kutokana na DART kutofanya hivyo nitaomba baada ya mkutano huu wa Bunge sio tu kupatiwa ripoti bali pia mikataba tuangalie kwamba mradi huu ni mkubwa na una mchango mkubwa kwenye deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizonazo mpaka sasa umetumia dola milioni 290 ni muhimu, pamoja na nyongeza inayotaka kuombwa ya zaidi ya bilioni 109 zingine kutoka Benki ya Dunia (WB), Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* afanye ukaguzi maalum wa matumizi mpaka sasa aweze kutoa mapendekezo ya kuboresha ufanisi na matumizi mazuri ya thamani ya fedha *(value for money)* katika hatua zinazofuata za mradi katika awamu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pili yamekuwepo malalamiko ya wafanyakzi ambayo yamesababisha migomo mara mbili mwaka 2013 na 2014 dhidi ya kampuni ya Starbag. Wafanyakazi wamerudi kazini, sio kwa hiyari bali ni kwa kutishiwa kufukuzwa kazi. Hali hii inaweza kuendeleza migomo baridi yenye athari kwa mradi kwa hali hiyo, Wizara ya Ujenzi ieleze imeshirikiana vipi na Wizara ya Kazi na Ajira na Ofisi ya Waziri Mkuu kuwezesha ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, tatu ujenzi unaoendelea hivi sasa umefunga baadhi ya barabara muhimu mfano Kimara kwenda Bonyokwa na pia inaathiri miundombinu ya maji taka Manzese, Makumbusho na Magomeni. Nimetuma Madiwani mara kwa mara kukutana na *DART* na *TANROADS* lakini ufumbuzi haujapatikana, ni lini marekebisho yatafanyika?

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya utekelezaji mwaka wa fedha 2013/2014, Bodi ya Mfuko wa Barabara unapaswa kutoa maelezo ya ziada juu ya makusanyo na matumizi ya fedha za mfuko kutoka vyanzo vyake vya kisheria kufuatia kifo cha Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) aliyokuwa akisimamia masuala ya mafuta. Habari zimeanza kujitokeza kwamba kuna utofauti wa maelezo baina ya EWURA na Mamalaka ya Mapato *(TRA)*.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara kupitia kwa Waziri wa Ujenzi itoe maelezo Bungeni ukweli ni upi hasa?

Mheshimiwa Spika, aidha kwa kiwango cha fedha kilichokusanywa kuna kulichotajwa katika hotuba ya Waziri naomba maelezo kutoka kwa Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kwa nini haijatoa fedha za nyongeza na za kutosha kwa Manispaa ya Kinondoni kufanya matengenezo ya dharura ya barabara na madaraja baada ya madhara ya mafuriko.

Mheshimiwa Spika, suala hili nimelihoji kwenye kikao cha Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC) na katika vikao vya Manispaa ya Kinondoni vilivyofanyika kabla Mkutano huu wa Kumi na

Tano wa Bunge, hata hivyo nimebaini wazi kwamba kwa fedha za uhamisho wa ndani na fedha za Halmashauri na vyanzo vya ndani haviwezi kumudu mahitaji ya dhamira yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, maombi yameshawasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, hivyo, naomba katika majumuisho nipate majibu ni lini matengenezo ya dharura yatafanyika kwa ushirikiano baina ya Bodi ya Mfuko wa Barabara, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge - Maafa), Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, mosi barabara ya Mbezi – Bwaloni kwa Msuguri – Kwa Msigwa hasa kukatika kwa madaraja na *culverts* katika maeneo mawili na hivyo kukatisha mawasiliano ya wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, daraja na *culverts* linalounganisha eneo la Makoka katika Kata ya Makuburi Manispaa ya Kinondoni na Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, pamoja na barabara ya kuelekea eneo hilo. Sehemu hiyo pia mwasiliano yamekatika.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara ya kutoka Sinza Kijiweni mpaka Tandale ambayo ina mchango mkubwa kwenye kupunguza foleni kwenye barabara Morogoro na sasa iko hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi ina wakala na taasisi nyingi za ujenzi ambao zinapaswa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwezesha mpango maalum wa maendeleo ya makazi Jijini Dar es Salaam na nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kiwango cha kazi kilichofanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015 na makadirio ya mwaka 2014/2015 hazionyeshi dhana, dhamira na dira ya Wizara hii kuwa kiongozi katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, idadi ya nyumba zilizojengwa na Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) ni kidogo sana. TBA inapaswa kuongeza nguvu na kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa kusukuma ujenzi wa nyumba na makazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata *commitment* ni nyumba ngapi TBA imeenda kujenga kwa upande wa Jimbo la Ubungo na lini na wapi zitajengwa? TBA imeweza kuwasiliana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupata viwanja katika mradi wa mji pembezoni wa Luguruni (*Luguruni Settlement Town*) kwa kushirikiana na mwendelezaji mkuu aliyeteuliwa. Kama Wizara haina dhamira ya kupata viwanja katika eneo hilo, TBA ipanue wigo wa mradi wake wa Mabwepande ambao uko katika Kata za Mbezi Luis, Kibamba na Kwembe katika maeneo ya pembezoni yenye nafasi ijenge nyumba za watumishi wa umma. Kama Serikali haiongezi kasi ya TBA kujenga nyumba za Serikali na za watumishi wa umma basi, Wizara ya Ujenzi irudishe nyumba za Serikali zilizouzwa.

Aidha, siridhishwi na utendaji wa TBA hapa Dodoma, kama kwa miaka mitatu 2011, 2012 na 2013 TBA imeshindwa kupata nyumba moja tu kwa Mbunge kwa ajili ya kukodi ambayo nimeomba itakuwaje kwa watumishi wengine wa kawaida?

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Baraza la Ujenzi na vikosi vya ujenzi, Chuo cha Ujenzi na Chuo cha Matumizi ya Teknolojia ya Nguvu kazi kwa pamoja unapaswa kushirikiana na TBA kuandaa mpango maalum wa makazi Dar es Salaam nilitaja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ya Ujenzi iongeze mgao wa fedha na ufanisi katika mamlaka na taasisi zingine zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi kwa kuwa sasa mkazo upo zaidi *TANROADS* na Bodi ya Mfuko wa Barabara pekee wakati taasisi na mamlaka zingine zilizo chini ya Wizara hii nazo zinaweza kutoa mchango mkubwa sana katika sekta ya ujenzi, ukuaji wa uchumi wa nchi na maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha katika utekelezaji kwenye mwaka wa fedha 2014/2015 na majumuisho ya mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 naomba mamlaka/taasisi hizo zitoe majibu juu ya masuala yafuatayo ambayo nilihitaji pia katika mijadala ya Bajeti za mwaka 2011, 2012, 2013.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi niliziomba zishirikiane katika mchakato uliokuwa ukiendelea wa mpango mkuu mpya wa Jiji la Dar es salaam *(master plan)*.

Mheshimiwa Spika, tunapaswa kama Taifa kufikiria Dar es Salaam ya zaidi ya 2061.

Mheshimiwa Spika, hii itapunguza gharama kubwa ya fidia katika ujenzi wa barabara na miundombinu mingine Jijini kutokana na kutoweka na mfano mwanzoni wa mwaka 2000 barabara ya Morogoro ilipanuliwa na kubomolewa na kujengwa sasa inabomolewa na kujengwa tena kupitia mradi wa BRT/DART.

Mheshimiwa Spika, aidha maofisa kama wa Wizara ya Maji kama TANESCO na Wizara ya Maji yatavunjwa karibuni kwa kuwa ni eneo la barabara. Aidha, Wizara ieleze hatua ambazo imechukua kutekeleza mapendekezo kuhusu kuondoka kwa majengo marefu Jijini Dar es Salaam pamoja na kuwa mamlaka ya Halmashauri za Manispaa za Kinondoni, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) yapo mambo ambayo ni chini ya bodi zilizo katika Wizara hii ambazo ni muhimu yatolewe maelezo, Wakala wa Umeme na Ufundi (TEMESA) kwa kuwa kwenye masuala ya uendeshaji wa vivuko umepanuka ni muhimu mabadiliko ya kimuundo yakafanyika na kuainisha na yale ya vyombo vingine vilivyo chini ya Wizara ya Uchukuzi.

Aidha, Wizara ya Ujenzi irejee ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kuondaoa udhaifu uliojitokeza kuhusu matengenezo ya magari ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimefanya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka tajwa, nimepitia kitabu cha hotuba ya Waziri juu ya barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam (kilometa 109.35).

Pamoja na kushukuru kwa kusainiwa kwa baadhi ya mikataba katika mwaka 2013/2014 na nyongeza kidogo ya bajeti kwa mwaka 2014/2015, sijaridhika na ucheleweshaji wa utekelezaji wa kiwango kidogo cha fedha kinachotengwa kinyume na ratiba ya utekelezaji iliyopitishwa na Bunge kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano mwaka 2011 sanjari na viwango vya fedha vilivyokadiriwa katika mpango tajwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge kutaka udhaifu uliopo uondolewe, Wizara ya Ujenzi irejee michango yangu wakati wa bajeti kuu, bajeti za Wizara ya Ujenzi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais kwa miaka ya 2011, 2012 na 2013. Maelezo ya Wizara yanakuwa yanajirudia rudia

yakifanana kwa miaka mingi mfululizo, viwango vya fedha vilivyotengwa katika bajeti zilizopita bila ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Goba na maeneo mengi yaliyofanywa kwenye aya 49 ya 167, aya 168 na aya 169 wamesikiliza hotuba ya Waziri na hawaridhiki na ahadi nyingine za nyongeza bila ya utekelezaji wa ahadi zilizopita. Ieleweke kwamba hali ya barabara hizo baada ya mafuriko ni mbaya, *TANROADS* wasifanye pia matengenezo ya mpito.

Mheshimiwa Spika, hivyo iwapo Waziri katika majumuisho hataeleza hatua ambazo atachukua kuwezesha ujenzi wa barabara hizo kuharakishwa na pia viwango vya fedha kuongezwa kukidhi mahitaji, nitalazimika kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri kueleza kutoridhika.

Aidha, pamoja na hatua hiyo, kwa kuwa mipango ya maendeleo inaandaliwa na Tume ya Mipango ambayo Mwenyekiti wake ni Rais na bajeti ya Taifa inaletwa Bungeni na Waziri wa Fedha kwa niaba ya Waziri nitalazimika kutumia njia za Kibunge na za nje.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa utendaji wake mzuri wa kazi na pia nampongeza sana kwa msimamo wake wa kusimamia Sheria Na. 30 ya mwaka 1973 na Kanuni Namba 30 ya mwaka 2001 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Tangazo Namba 30 la Tarehe 9 Februari, 2001 iliyoanza kutumika tarehe 24 Januari, 2001 inayofafanua uzito wa magari unaotakiwa. Sheria hiyo inayoeleza magari yote yenye uzito kuanzia tani 3.5 na kuendelea na aina ya makosa ya uzidishaji uzito ambapo kifungu cha 2, 3 na 4 vinafafanua matumizi ya uzito uliozidi asilimia tano.

Mheshimiwa Spika, Magufuli nampongeza sana kwa kusimamia sheria hii ambayo imevunjwa na Waziri Mkuu kwa kuruhusu magari mazito yapite katika barabara ambazo matokeo yake zimeharibika kwa kiasi kikubwa na kuitia Serikali hasara ya mamilioni ya fedha za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuruhusu magari haya kupita na ni kuitia hasara Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichangie kuhusu nyumba za TBA ambazo ni za Wizara ya Ujenzi. Nyumba hizi ni nzuri ila zina matatizo madogo madogo kama vile mabomba ya maji ni vyema kushughulikiwa ili zisiendelee kuharibika kwani usipoziba ufa utajenga ukuta.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara hii nikiwa na unafuu wa afya yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuweza kuchangia bajeti ya Wizara hii nikiwa na unafuu wa afya yangu. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wa Wizara na jopo zima husika la Wizara hii kwa kazi nzuri na njema lakini zaidi kwa Waziri Mheshimiwa John P. Magufuli kwa juhudi zake, wakati huo huo nikimshukuru kwa ombi la mwaka jana la kuhusu Daraja za Nangoo (Mto Mbwinji) na Nanganga - Mto Miki.

Mheshimiwa Spika, naamini mwenyewe anakumbuka jinsi nilivyomshukuru nikimwambia, bahati mbaya sina mtoto wa kike (msichana) ningempa amuoe. Hakika sisemi tu kwa vile alinitimizia ombi lile tu, bali hata wewe Spika utakuwa shahidi kuona jinsi Wabunge wengi wanavyompongeza, mnyonge mnyongeni ila haki yake mpeni.

Mheshimiwa Spika, mimi nathubutu kusema kati ya Mawaziri wote wa Baraza la Mawaziri sijui kama kuna zaidi yake kiutendaji, kimsimamo na kiujasiri.

Mheshimiwa Spika, kuna kero ya Ndundu – Somanga ambayo bado wengi tunalalamikia ni kwa kuwa imebidi.

Mheshimiwa Spika, nimuombe tu Mola aliyemuweza wa yote ili azidi kumpa afya njema na kumuwezesha pia kuyashinda magumu anayokumbana nayo. Mungu huyo huyo amfanyie magumu hayo yawe mepesi, ampiganie na amshindanie, kila palipo na mafanikio maadui lazima wawepo. Hivyo nachukua nafasi hii nikienda kinyume na hila zote za hao maadui. Hawana nafasi wala mamlaka, nguvu zote za uchafu na pepo wabaya na ziteketeza kwa moto ushukao toka mbinguni, namfunika kwa damu takatifu ya Yesu Kristo mwana wa yule alie hai. Nasema haya nikiomba na kuamini ya kwamba Mungu atatenda amina.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri kwa kazi na hasa hii ya kutetea bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Buzuruga – *Airport* ni *superb* na wala haina matatizo, kama yapo basi Mbunge ayasimamie. Hiyo ndiyo barabara yangu nikiwa mkazi wa Buzuruga, *so* najua ninachosema.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wizara kwamba barabara ya Sumbawanga - Tunduma sasa inapitika vizuri isivyo kawaida na huko ndiyo kwenye mazao mengi lakini *cement* kwa wingi toka Mbeya - Sumbawanga na tunategemea mizigo mizito toka DRC - Mbeya – Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, swali mna langu mpango gani wa kuweka *Weighbridge* kwani hata sasa inaonekana mabasi toka Sumbawanga hujaza mizigo mizito kwenye *boot* kwa sababu basi likifika Tunduma hufaulisha abiria kwenye *coaster* wakivuka mizani *then* abiria hurudi kwenye basi kubwa na wakaendelea Mbeya.

Mheshimiwa Spika, mnasemaje kuhusu mizani ya Tunduma - Sumbawanga – Tunduma?

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Chaya - Nyahua kilometa 89 (sehemu ya barabara ya Dar es Salaam - Kigoma) barabara hii mwaka jana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete aliahidi kuwa Emil Sabbah Al Sabaah, Mfalme wa Kuwait amekubali kutupa mkopo wa *Kuwait Fund* ili barabara hii ijengwe kiwango cha lami. Ni sehemu iliyobaki changarawe kati ya barabara kutoka Dar es Salaam - Kigoma. Je, *Abu Dhabi Fund* nao tumewaomba? Kwani akiba yake *(Soverign Wealth Fund)* ni zaidi ya US$ 600 bilioni, sitoeleweka kwa wapiga kura kama mwaka huu wa fedha barabara hii haitajengwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari Dar es Salaam (Jiji) mapendekezo ya barabara pete *(ring roads)* na barabara lishe *(feeder roads)* yazingatiwe katika kupunguza msongamano Jijini Dar es Salaam. *DART* iliposanifiwa na kupangwa haikuzingatiwa uhitaji wa

mpango chanya *(mult-model design)* ili kutoa nafasi kwa kutumia barabara ile ile mabasi yaendayo kasi ikajengwa reli nyepesi *(light rail)* zikapita *trains* pamoja na mabasi yanayotumia umeme na hivyo kupunguza hewa ya ukaa jijini.

Pia usanifu na kupanga *fly overs* uzingatie uwezekano wa nguzo kujengwa kwa ajili ya treni ndogo ndogo ziendazo kasi *(rapid transit trains)* kwa utaratibu, *transport mult-model simulation system* kwa miaka 50 ijayo. DART walisema usanifu ulilenga mahitaji ya jiji mpaka mwaka 2030, yaani miaka 16 ijayo, ushauri huu wa JICA haukuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, Majiji yote duniani yanapanga kwa kuzingatia njia mbalimbali za usafiri pamoja na *sea buses* na treni kasi *(rapid trains)* hata kuchoronga reli chini ya maji hadi Kigamboni tutakapoanza kujenga baada ya kupata mfuko wa fedha za ziada za gesi kwa miundombinu kama hii *(sovereign wealth fund)* mipango iangalie miaka 50 mpaka 100.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Miswaki - Loya - Igunga inahitaji *Road Fund* itusaidie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tena hotuba ya Waziri asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nyongeza kwa mchango wangu wa jana kuhusu kutatua msongamano wa magari Jiji la Dar es Salaam na Majiji mengine kama Arusha, Mwanza, Mbeya baadaye Wizara za TAMISEMI, Ujenzi na Uchukuzi zishirikiane katika hatua zote za miradi yote katika kutatua msongamano wa magari Dar es Salaam, hiyo itasaidia kupunguza gharama na ubora na kiwango cha juu na ufumbuzi chanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chalinze *toll road,* barabara ya Dar es Salaam - Chalinze ya *toll* ishirikishe Wizara ya Uchukuzi ili *transport economics* ikae vizuri katika uwekezaji katika mabehewa na injini zipangwe kwa kupeleka mizigo sehemu mbalimbali nchini Zambia, Malawi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango kwa hoja hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Isyonje hadi Makete ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Halmashauri ya Mbeya. Kutokupitika kwa barabara hii hasa wakati wa masika huwafanya wakulima wengi kukosa soko la mazao yao hasa viazi na kadhalika. Aidha, eneo la milima ya Mporoto ni eneo ambalo hupata mvua kwa wingi kwa mwaka na hivyo kuzifanya barabara zote kutokupitika kwa wakati huo. Mwaka huu fedha zilizotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi ya barabara. Naomba Serikali ifikirie upya kutenga fedha za kutosha kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuna wawekezaji wengi wangependa kuwekeza katika eneo la Kitulo lakini kikwazo kikubwa ni barabara. Naomba Serikali iangalie na kuongeza fedha kwa ajili ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mvua nyingi ambayo inanyesha kwa wingi mwaka huu imesababisha barabara nyingi kuharibika, kwa kweli bado sijaona kama Serikali imetenge fedha za kutosha kukabili hali hii. Halmashauri hazina mapato ya kutosha ili kukabili hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wako pamoja na timu yake ya Wizara kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya hasa kwa barabara nyingi zinazojengwa nchi hii. Mungu awabariki sana na awapatie kibali cha kutekeleza kazi zenu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi nichangie hotuba ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii imefanya kazi nzuri kwa kufungua sehemu zote za nchi. Ni ukweli ulio wazi kuwa Mikoa na Wilaya sasa zinafikika karibu wakati wote wa mwaka. Hali hii imechangamsha uchumi na kuchochea maendeleo ya wananchi katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, muhimu katika ujenzi wa barabara hizi baada ya kumaliza hatua ya kufungua ambayo ni muhimu na uamuzi ulikuwa sahihi, Serikali sasa ijielekeze katika ubora na utunzaji wa miundombinu hii, itoshe kusema kuwa baadhi ya barabara zimejengwa kwa viwango ambavyo havimudu matumizi yetu. Ipo haja kuwa barabara zetu zinaharibika kwa kuwa magari yapitayo yana uzito wa GTW 55. Hivi ni kweli kuwa Afrika ya Mashariki hakuna barabara zinazohimili uzito huo au zaidi? Au utaalam wetu hauwezi kutuwezesha kujenga barabara za kuhimili uzito huo kwa tija?

Mheshimiwa Spika, mifano ya nchi za Ulaya zinazotengeneza au kuweka kikomo cha uzito pungufu si sahihi kulinganishwa na Tanzania. Kama Taifa, mtandao wetu wa reli uliharibika na sekta ya barabara (malori) ikaingia kuokoa jahazi. Kanuni za uchumi zinaeleza kuwa pindi njia ya usafiri iliyorahisi (nafuu) itakapopatikana kulingana au kuzidi mahitaji, njia ambayo ni ghali itajiondoa yenyewe.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali weledi wana mapenzi na faida wala si shughuli, makampuni ya mafuta yaliyokuwa yanavuna nchini, wamiliki wake sasa wanaelekeza mitaji yao katika kokoto na saruji, wale wanaoona hapo hakuna tija wanaondoka na kwenda mataifa mengine au kuwekeza katika sekta nyingine, mifano ya *BP, CHEVRON, ESSO, CALTEX* kwa kutaja baadhi wamekimbia soko.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kuwa tujenge barabara imara za kuhimili uzito wa GTW 55, wale watakaozidisha uzito tuwape adhabu kali sana. Barabara imara zitapunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara na barabara zitadumu kwa muda mrefu. Lakini upande wa pili Serikali ijenge mtandao wa nchi wa kisasa unafika sehemu nyingi za Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, niweke wazi kuwa mimi ni mtaalamu wa masoko *(PDM)* na nimefanya kazi ya usimamiaji wa usafirishaji wa mafuta kwa malori. Nimewahi kuwa mtafiti msaidizi wa timu ya Benki ya Dunia iliyotafiti juu ya madhara ya malori ya mafuta kwa usalama wa barabara, ubora wa barabara ni sehemu iliyonyooshewa mkono.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio kupitia Mfuko wa Barabara ambao kimsingi huchangiwa na wananchi kupitia tozo ya mafuta. Ushauri wangu ni kuwa yawepo mawasiliano ya karibu kati ya wadau wakuu wanaotumia mfuko huu, hawa ni TANROADS, Wizara na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, lengo la michango ya wananchi kwa fedha wanayohitaji sana ni kujenga barabara. Isitoshe kusema fedha inayoelekezwa kwenye Halmashauri kupitia TAMISEMI

kwa sababu ni dhahiri matumizi yake hayana tija. Naishauri Serikali ipitie upya usimamiaji wa fedha hizi, na basi ikibidi ianzishwe mamlaka moja tu itakayoshughulika na barabara nchini kote.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara ya Muhutwe - Kamachumu - Nshamba mpaka Muleba umbali wa kilometa 53. Serikali niipongeze imekuwa ikitenga fedha kuhakikisha kuwa barabara hii inapitika. Bajeti ya mwaka 2014/2015 inaonyesha dhahiri kiasi kikubwa kilichotengwa kuhakikisha barabara hii ya changarawe inakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni kiungo cha maeneo ya uzalishaji mkubwa na makazi ya wananchi wengi na barabara kuu itokayo Bukoba kwenye Biharamulo. Pamoja na jitihada za Serikali za kuhakikisha barabara inapitika wakati wote, tuliomba na tunaendelea kuomba barabara hii yote iwe kiwango cha lami. Hatua hii itapunguza matumizi katika matengenezo ya mara kwa mara kutokana na ukweli kuwa ukanda huu una vilima vingi na kupata mvua nyingi kwa kipindi kirefu cha mwaka hali ambayo inasababisha uharibifu.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuomba barabara ya Muhutwe - Kamachumu - Nshamba mpaka Muleba ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nipongeze jitihada zinazofanywa na Wizara hii, ningependa kupata ufafanuzi kuhusu barabara ya Mpanda/Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, naomba kurejea hotuba ya Waziri ukurasa wa 130 ningependa kufahamu ni barabara ipi itajengwa ni Kibaoni - Sitalike - Mpanda au Kizi - Sitalike – Mpanda? Barabara zote hizi mbili zinafika Mpanda. Ujenzi unaoendelea ni Sumbawanga - Kanazi - Kizi - Kibaoni. Sasa ili kufika Mpanda Wizara itaendelea toka Kibaoni - Sitalike - Mpanda au toka Kizi - Sitalike - Mpanda ni barabara ipi inayokusudiwa naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, wakati wote nimekuwa na naendelea na kuamini fidia ni haki ya msingi kwa namna yoyote ile kwa nchi inayojali haki za raia, Wizara yako inawaongezea sana umaskini wananchi wengi ambao nyumba na mali zao zimebomolewa kupisha ujenzi wa barabara bila kuzingatia sheria. Maendeleo ni gharama, hatuwezi kukwepa gharama za fidia kwa kisingizio cha kuongezeka kwa gharama ya mradi. Wapeni haki zao wote ambao wamepisha maendeleo ya ujenzi wa barabara. Kutokuwalipa wananchi hawa ni dhuluma inayofanywa na Serikali dhidi ya watu wake.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata maelezo lini sasa mtawalipa fidia wale wote walioathirika na maamuzi ya kutowalipa.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi kwa umahiri wake katika kuiongoza Wizara hii muhimu na ya kimkakati. Nimpongeze Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo nimeipokea hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa masikitiko makubwa. Katika bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba upembuzi yakinifu na *detailed design* ya barabara ya Nyakahura, Rulenge hadi Murugarama kilometa 86 ingekamilika katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 na kwamba ujenzi kwa kiwango cha lami ungeanza katika mwaka ujao 2014/2015.

Nimesikitika kuona upembuzi yakinifu na *detailed design* havijakamilika na ujenzi au kwa kiwango cha lami hautafanyika katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri upembuzi yakinifu na *detailed design* vikamilike haraka na kama itawezekana barabara hii ambayo ni ahadi ya Rais tangu mwaka 2010 itengewe fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika *mid-year review*, nitashukuru sana. Na Mungu akubariki mimi nitaendelea kufuatilia ahadi ya Rais wa *ADB* - Dkt. Donald Kaberuka kuhusu barabara hii.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Naanza kwa kumpa pole ya ajali Waziri Mheshimiwa John Magufuli pamoja na wote waliopata ajali ya helkopta pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mimi nawashukuru na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya kurudisha mawasiliano ya barabara kwa kipindi kufupi cha siku tatu baada ya mafuriko kuharibu madaraja yote yanayounganisha Dar es Salaam na mikoa yote Kaskazini na Kusini. Ari hiyo na kasi hiyo iendelee hata katika utekelezaji wa majukumu mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Salender Bridge* nimeona kwenye kitabu cha Waziri hotuba yake ameelezea vizuri sana mipango mingi mizuri ya kutatua msongamano wa Jiji la Dar es Salaam. Kwa kiwango kikubwa ameangalia maeneo yote niliyozungumza mwaka jana, kama Daraja la Gerezani, barabara za juu, lakini pia barabara za mzunguko *(ring roads),* lakini nakubaliana na ununuzi wa boti itakayokuwa inatoka *ferry* hadi Bagamoyo itasaidia sana wakazi wa Kunduchi, Mbweni, Bunju, Kiromo na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, hii ni mara yangu ya tatu nasimama/naandika kwenye Bunge lako Tukufu juu ya msongamano wa Daraja la Salender. Hii boti siyo ufumbuzi wa msongamano wa *Salender bridge*, hivi hiyo boti itawasaidia wa Msasani, Mikocheni, Kijitonyama, Sinza, Mbezi, Kawe, Makongo na Mlalakuwa?

Kitabu kizima hakuna hata *mention* ya *Salender bridge*. Hii ni dharau kupuuzwa na kukebehiwa kwa watumiaji wa daraja hili. Umuhimu wake hakuna asiyeuona, sasa ni kwa nini Wizara haijatoa neno lolote kwenye kitabu kizima? Na hawezi kusema kuwa kuna mpango wakati haupo kwenye mipango wala maelezo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na kuwa ni mkazi wa Dar es Salaam lakini ni mtu wa asili ya Mikoa ya Kusini. Ni haki kweli barabara ya Ndundu - Somanga miaka 50 ya uhuru haijamalizika kujengwa hata mara moja wakati kuna barabara zimerudiwa mara tatu? Huku ni kuwapuuza watu wa Kusini. Serikali itoe tamko ni lini barabara hii itamalizika, hakuna maelezo yoyote mengine yatakayokubalika.

Napongeza ujenzi wa nyumba kwa kukopesha wafanyakazi. Wakala wa Majengo wana viwanja vizuri sana maeneo nyeti sana, nashauri wayatumie maeneo hayo hasa yaliyopo mijini kujenga nyumba za ghorofa ndefu ili nusu ya nyumba hizo wauze, lakini nusu wapangishe wafanyakazi hasa wa Serikali na hasa vijana ili wawe karibu na kazini, lakini pia zitawapunguzia adha ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya makandarasi, niiombe Serikali imalize haya madeni ya Wizara ili fedha inayotengwa kila mwaka ifanye kazi zile zilizopangwa kwa mwaka

ule. Hali ilivyo sasa fedha nyingi zinatumika kulipa madeni lakini pia kunakuwa na kulegalega katika kumaliza miradi kwani makandarasi wanakuwa na *certificates* ambazo hazijalipwa hivyo kushindwa kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwanakamati na Kamati ya Kudumu ya Miundombinu hivyo naunga mkono hotuba hii, ila tu nitakwazwa iwapo sitapata jibu la kuridhisha juu ya *Salender bridge*.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nashauri kuhusu barabara ya Tunduru - Songea iishe mwaka huu ili kuwasaidia wananchi hao wa Tunduru kupata urahisi wa usafiri.

Mheshimiwa Spika, nashauri barabara ya Dar es Salaam - Lindi kipande ambacho bado, kiishe mwaka huu ili kuenzi jitihanda za Rais Mstaafu Mzee Benjamin Mkapa. Ahsante.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. Tunamuomba Mungu aendelee kuwapa hekima na nguvu ili wafanye zaidi. Tunashukuru pia kwa ujenzi wa barabara ya Peramiho - Mbinga.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara iziangalie barabara zifuatazo:-

(a) Ahadi ya Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete:-

(i) Mbinga – Litembo, hii ni inafika katika eneo la hospitali kubwa ya Litembo, barabara hii ni chafu na wakati wa mvua haipitiki.

(ii) Nyoni – Mkoka, barabara ya Mbinga - Mbambabay inawekwa lami. Nyoni ni *junction* kwenda Mkoha ni eneo lenye uchumi mkubwa utokanao na kahawa.

(iii) Ahadi ya Waziri Mkuu kuhusu Kitai - Ruanda - Ntanduwao mpaka Lituhi. Hapa ni kijicho cha Mgodi wa Makaa ya Mawe, bila kuweka lami barabara hiyo kwa dharura basi mradi huu wa makaa ya mawe unaweza kufungwa kwa sababu yale malori makubwa yanatimua vumbi sana na hivyo kuhatarisha afya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni Litumba Nyoni – Kuigole, barabara hii ni mbaya sana, naomba fedha zake ziongezwe. Mbinga - Litembo - Mzuzu eneo la kutoka Litembo - Mzuzu halijatengenezwa muda mrefu sana, naomba fedha iliyotengwa ikafanye kazi hii.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, wasaidizi na watendaji wote kwa kazi nzuri za ujenzi wa barabara za taifa na barabara za mkoa katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi madhubuti juu ya utendaji wa makandarasi wa ujenzi wa barabara, kama Mheshimiwa Waziri alivyokataa kupokea *Kilwa Road,* kutokana na ujenzi kuwa chini ya kiwango na kwa gharama zake ndiyo mfano wa usimamizi bora na uuendeleze.

Mheshimiwa Spika, matokeo mengine mazuri ni pale mkandarasi aliyekuwa anatengeneza barabara ya kutoka Boza (Pangani) hadi Muheza na Muheza - Amani alipoondolewa. Mkandarasi mpya amefanya kazi nzuri na kwa muda mfupi, ninawashukuru sana. Sasa mtazameni mkandarasi anayehukumiwa kila siku barabara ya Somanga - Fungu zile kilometa 65 barabara ya Kilwa kwenda Lindi - Mtwara. Nini kinaweka ugumu wa maamuzi sahihi ya kumuondoa?

Mheshimiwa Spika, upandishaji wa barabara za Wilaya kuwa za Mkoa, miaka mitano iliyopita Wilaya ya Muheza iliomba kupandishwa daraja barabara kuwa za Mkoa. Baada ya ukaguzi barabara zifuatazo zilikosa vigezo. Kigezo kikubwa kutokuwepo muendelezo wa barabara iliyopo kuunganisha na eneo la pili la barabara hiyo:-

(a) Barabara ya Kilulu - Mtindiro - Mbambara - Kwafungo - Bagamoyo. Eneo dogo toka Kwabada - Mbambara - Kwafungo sasa limefunguliwa na kutimiza kigezo pungufu.

(b) Barabara ya Bombani - Mashewa - Kimbo - Potwe Ndondondo - Maguzoni, eneo la kutoka Kimbo - Potwe Ndondondo - Maguzoni limeshafunguliwa kutumiza kigezo pungufu.

Kamati ya Maendeleo ya Mkoa (RCC) imeridhia maombi haya mapya na kuomba barabara hizo mbili sasa zipandishwe daraja kuwa barabara za Mkoa. Barabara (a) inapita eneo kuu la uzalishaji wa machungwa Wilayani Muheza, zipo zahanati nne, shule za sekondari tatu, shule za msingi zaidi ya nane na kuunganisha barabara ya Mkoa Boza - Muheza na barabara kuu ya Taifa Segera – Tanga. Tunaomba ukaguzi mpya ufanyike na zipandishwe daraja.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliyorudia mwezi Machi 2014, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi hiyo mwaka 2005 na kurudia tena mwaka 2010 na tena mwaka huu 2014 mwezi Machi, 2014. Niliona vema kukuandikia juu ya ahadi hiyo kwani Mheshimiwa Rais alisema barabara itajengwa mwaka 2014/2015 ndani ya muda wake wa Urais Kikatiba. Barua yangu ina Kumb. Na. MB./IMZ/999/5/14 ya tarehe 20/05/2014.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni fupi kilometa 34 tu, inaelekea Tarafa ya Amani ambapo yapo mashamba makubwa ya chai yanayoingizia Taifa letu fedha za kigeni kwa mauzo ya chai nje ya nchi. Pia magari makubwa yanasafirisha miwa kutoka Amani - Muheza - Dar es Salaam na pia hiliki.

Mheshimiwa Spika, hifadhi kubwa ya msitu wa Amani ni kivutio kikubwa cha utalii na kupatia Taifa fedha za kigeni. Mwezi Machi, 2014 ratiba ya ziara ya Mheshimiwa Rais, Wilaya Muheza ililenga kumpeleka Tarafa ya Amani kuzindua miradi mikubwa ya Kituo cha Afya, *high school* ya Shebomeza, *SACCOS* kuu ya wananchi Misalai na kuona jinsi wafugaji wanavyosaidia upatikanaji mkubwa wa maziwa yanayotumika kuendesha kiwanda cha maziwa cha *Tanga fresh*. Ni matarajio yangu kwamba mradi huu sasa utatekelezwa kwani upembuzi yakinifu umefanyika na bila shaka sasa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili fedha zipatikane na kuongezeka ili kuwezesha miradi mingi zaidi kukamilishwa mwaka 2014/2015.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wa Wizara hii katika uchapaji kazi wao. Nawasisitiza waongeze kasi zaidi katika kazi ili kuliletea heshima Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala la uharifibu wa barabara kwa kuzidisha mizigo na hivyo kupelekea barabara zetu kuharibika. Je, Wizara hadi sasa imechukua hatua zipi za dharura ili kuhakikisha kuwa inazuia tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, rushwa katika mizani, je, Wizara na watendaji wake wote wanafahamu kuwa kuna rushwa katika mizani ambapo kuruhusu malori na magari yaliyozidisha mizigo na hivyo kuipelekea kuharibu barabara zetu? Ni hatua zipi zimechukuliwa au zinazokusudiwa kuchukuliwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtandao wa barabara Wilayani Tarime, kwa masikitiko makubwa napenda kuwasilisha kupitia kwako malalamiko jinsi Wizara hii kupitia Waziri Magufuli na Naibu wake na hata watendaji wake wasivyoitendea mambo mazuri Wilaya ya Tarime.

Kwanza Wilaya ya Tarime ipo mpakani mwa nchi ya Kenya hivyo ina *security road* inayoanzia Wilaya ya Rorya kupitia Sirari, Remagwe - Nyabisaga - Nyantira - Muriba - Kegonga - Masanga hadi Gibaso. Barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi yetu ya Tanzania. Swali, ni kwa nini barabara hii haifanyiwi matengenezo ya mara kwa mara ili kuimarisha suala la ulinzi katika Wilaya ya Tarime na Mkoa wa Mara kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuiwekea lami barabara hii ili kurahisisha mawasiliano kwa watu wa Tarime na Mkoa wa Mara kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, pili, kuna barabara ya Nyamwaga inayoanzia Tarime Mjini kupitia Nyamwigura - Nyamwaga - Nyamongo - Mto Mara hadi Serengeti yenye urefu wa kilometa 53.

Swali ni kwa nini ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unasuasua? Je, itachukua muda gani kuikamilisha hii barabara ikiwa kwa mwaka mzima ujenzi wake huchukua kilometa moja?

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu ujenzi wa kiwango cha lami aliyoitoa mwaka 2010 imefikia wapi? Hii barabara ndiyo nguzo kuu ya uchumi ya Mkoa wa Mara kwani inapitisha watalii na mazao ya chakula na biashara, hivyo naiomba Wizara iangalie upya suala la barabara hii kwa kuipatia kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuna barabara ya Nyamwaga - Muriba. Hii barabara haifanyiwi matengenezo ya mara kwa mara na hivyo kupelekea usumbufu katika Wilaya ya Tarime hasa katika Kata za Nyamwaga na Muriba katika Tarafa ya Ingwe. Namshauri Waziri aiangalie barabara hii kwa jicho la huruma kwani huleta mateso makubwa kwa wananchi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za Serikali Wilayani Tarime, napenda kumkumbusha Waziri kuhusu ahadi yake aliyotoa ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa Serikali katika Wilaya zilizo pembezoni ikiwemo na Tarime.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshmiwa Spika, nampa Waziri hongera kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, suala la *Law School* (Chuo cha Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo) kilichopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, kipo eneo la Sam Nujoma - Dar es Salaam, Chuo hiki kipo ½ kilometa toka barabara ya Sam Nujoma, ila ni ya vumbi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba msaada kwa Waziri kujengewa barabara hii muhimu kwa kiwango cha lami (½ kilometa), hatukutengewa fedha. Tutashukuru endapo itawezekana.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, hali ya msongamano katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa ni tatizo sugu, naipongeza Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara za pembeni ili kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itilie maanani jambo hili kwa kuhakikisha barabara hizo zinajengwa pamoja na ile ya Kigogo - Dampo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikutumia fedha nyingi kwa ajili ya kununua, kutengeneza, mafuta na kadhalika kwa magari ya Serikali hasa *Land Cruiser* ambazo ni ghali kununua na zina gharama kubwa ya matengenezo, ni kwa nini Serikali isiangalie namna ya kuacha kununua magari hayo ambayo ni ghali sana na kununua aina nyingine ya magari ambayo hayana gharama kubwa kama *Land Cruiser* au *Prado?* Ni kwa nini tusiige Kenya ambao wameacha kutumia magari hayo ya *Land Cruiser* na kuamua kutumia magari yasiyozidi cc 3000 na tena ya aina nyingine tofauti na Toyota?

Mheshimiwa Spika, haingii akilini Waziri atumie V8, Naibu Waziri V8, Wakurugenzi nao hivyo hivyo hadi Wakurugenzi wa Halmashauri wanatumia aina hiyo hiyo ya magari, haya ni matumizi mabaya kwa fedha za umma. Naomba sana Serikali iliangalie jambo hili kwa umakini ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii, pamoja na kuunga mkono nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu ambayo kwa kiasi kikubwa miundombinu ya nchi imeathirika sana kutokana na mvua kubwa iliyonyesha mwaka huu, maeneo mengi ya nchi yetu, barabara nyingi zimeharibika na fedha nyingi zinahitajika ili kurudisha barabara hizo ziweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rufiji, Wilaya ambayo kwa kiasi kikubwa mafuriko yameathiri kwa zaidi ya miezi miwili sasa barabara nyingi si tu za TANROADS bali za Wilaya na za Vijijini. Hadi sasa maeneo mengi ya vijijini hayafikiki na wananchi wanatembea kwa miguu kwenda vijiji jirani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa kiasi kikubwa iongeze fedha ili kuhakikisha kuwa mawasiliano ndani ya Wilaya hii yanakuwepo. Kwa fedha zilizowekwa hazitasaidia hata kidogo kuzirekebisha na kurudisha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bungu - Nyamisati yenye urefu wa kilometa 42 imetengewa shilingi milioni 16 tu. Barabara hii ambayo ni ya TANROADS na ni kiungo muhimu baina ya Mafia na Rufiji kwa kiasi kikubwa imeharibika na ina mashimo makubwa sana. Kwa kiasi kilichowekwa hakitaweza hata kidogo kurudisha mawasiliano katika eneo hilo hali ambayo italeta matatizo makubwa sana kwa wananchi wa huko. Naiomba Serikali iongeze fedha ili kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara hiyo kuna barabara ya Kibiti - Utete - Nyamwage barabara hii ni ya muhimu sana kwani inakwenda makao makuu ya Wilaya. Barabara hii kwa pande zote mbili yaani Kibiti - Utete na Nyamwage - Utete zote zilikuwa hazipitiki kwa mwezi mzima kutokana na mafuriko na imeharibika vibaya naomba pia barabara hii iongezewe fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Ujenzi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe - Makete ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi kujengwa kwa kiwango cha lami fedha zilizotengwa ni ndogo ukilinganisha na urefu wa barabara hii, wana Njombe tunaomba fedha iongezwe ili kuweza kukamilisha ujenzi wa barabara hii ya Njombe - Makete.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe Iyayi - Mbeya ipo kwenye upembuzi yakinifu, tunaomba upembuzi yakinifu ukiisha tu barabara hii ianze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Waziri na Naibu Waziri wa Ujenzi pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanya kwenye ujenzi wa barabara nchini. Barabara ya Manyoni - Itigi - Chaya (kilometa 89) inajengwa kwa kiwango cha lami na tayari kilometa 40 kutoka Manyoni - Itigi zimekamilika, wananchi wamefurahishwa na hatua hii, wanatarajia sehemu iliyobakia kutoka Itigi - Chaya ikamilishwe mwaka huu wa 2014.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri na Naibu wake wapokee pongezi za wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi.

Mheshimiwa Spika, barabara kutoka Mkiwa - Itigi - Rungwa - Makongolosi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ijengwe kwa kiwango cha lami. Tangu Bunge la Tisa barabara hii inazungumziwa na majibu yamekuwa yakitolewa kuwa barabara inafanyiwa upembuzi yakinifu na sasa barabara hiyo inafanyiwa usanifu. Nyumba kando kando ya barabara hii zilishapigwa alama ya X, tena alama nyekundu. Naomba nipatiwe majibu ya kina kuhusu hii barabara ni lini itaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida ulishapeleka mapendekezo yake Wizara ya Fedha kwenye miradi ya MCC kuwa barabara hii ya Mkiwa - Itigi - Rungwa iingizwe kwenye mradi wa MCC kama mradi wa Mkoa baada ya kutakiwa wapendekeze mradi mmoja wa MCC. Napenda kujua kama mradi huo umekubaliwa kwenye miradi ya MCC?

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Mkiwa - Itigi - Rungwa hadi Makongolosi ilikuwa barabara ya *East African Road Services* mpaka Mbeya. Nyumba zilizojengwa kando kando ya barabara hii ziliidhinishwa kwa kuzingatia viwango vya upana wa barabara za Jumuiya hiyo kote Afrika Mashariki. Je, ni kwa nini zipigwe alama X nyekundu badala ya X ya kijani ili wananchi wafidiwe kihalali. Naomba majibu kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nyumba 300 zilizojengwa kisasa lazima barabara za uhakika. Mfano ni ile inayotoka Mbuyuni kwenda nyumba zilizojengwa na Magereza ni mbaya na hazieleweki kama ni barabara halisi.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara ya uhakika ijengwe kwa kiwango cha lami na nyumba zinazozuia barabara hiyo zivunjwe kupisha njia. Inasikitisha kuona barabara inayokwenda kwenye nyumba za viongozi wakiwemo Mawaziri inatelekezwa na wala haina hadhi yoyote ni kama uchochoro wakati barabara za lami zimejengwa nje ya mji huu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu ujenzi wa barabara kupitia kando ya Ziwa Tanganyika kwa kuwa katika Mkoa wa Kigoma barabara kutoka Kigoma mpaka mwisho wa Mkoa yaani kijiji cha mwisho kabisa kunajengwa barabara yaani ya TANROADS siyo Halmashauri, sasa katika Mkoa wa Katavi na Rukwa mwambao mwa Ziwa yaani kuunganisha vijiji hakuna barabara iliyopita barabara kando ya Ziwa Tanganyika yaani inapoishia Kalya ije mpaka Kasanga kupitia vijiji vya Karema, Ikola, Kabwe, Korongwe, Kazovu, Isaba, Chongo, Kirando, Kipili, Karungu, Kisambala, Namasi, Ninde, Msamba, L'yapinda, Kizumbi, Wampembe, Mwinza, Izinga, Tundu, Kala, Mpasa, Kipanga na Kasanga.

Mheshimiwa Spika, barabara itasaidia sana kuinua hali ya wavuvi kando ya Ziwa Tanganyika uwezo wa Halmashauri hawawezi kujenga barabara hiyo kwa ufinyu wa fedha kutegemea usafiri wa Ziwa ni vigumu sana kutokana na hali ya pepo za Ziwani. Vijiji nilivyovipigia mstari havina njia kabisa. Pia ni ulinzi kwa nchi yetu maana vijiji vyote vinapakana na DRC Congo kwa mpaka wa Ziwa Tanganyika.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naipongeza hotuba na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, barabara kutoka Kamanga - Katunguru hadi Sengerema ipo katika mpango wa mwaka *(budget)* upi kuwekewa lami baada ya *feasibility study* na DD kama hoja inavyosomeka? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, suala la *flyover* kituo cha Furahisha, eneo hili ni la muhimu sana kufunguka kwa sababu zifuatazo:-

(i) Uwanja wa mpira Kirumba una barabara kupitia hapo.

(ii) Soko kuu wa kimataifa linajengwa maeneo hayo.

(iii) Uwanja mkubwa wa wazi wa mikutano ya hadhara unafanyikia hapo.

(iv) Makanisa makubwa ya madhehebu mbalimbali yamezunguka eneo hilo.

(v) Hospitali mbalimbali aina za watu binafsi na madhehebu zipo pale.

(vi) Ni barabara kuu iendayo uwanja wa Mwanza *(airport)* unaotarajiwa kuwa wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, je, kwa sababu hizo kwa nini *flyover* zisijengwe? RCC imeshapitisha tayari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuifungua Mwanza:-

(i) Usagara - Kisesa naomba pakamilike.

(ii) Buhongwa hadi Igoma kilometa 13 tu (changarawe)

(iii) Makuyuni hadi Mwatex kilometa 10 tu (changarawe)

Mheshimiwa Spika, barabara zote hizi zikiimarishwa pamoja na kuwa hizo changarawe zitasaidia kwa sababu Mwanza ni pafinyu sana. Zipandishwe*(to) TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, natoa hongera sana kwa Waziri kuifungua nchi hii kwa barabara zinazounganisha mikoa mbalimbali na Mungu atawatia nguvu. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Ndundu - Somanga, naiomba Serikali kwa heshima na taadhima kuimaliza barabara hii kwani imekuwa kero wa wananchi wote wa Kanda ya Kusini, nashauri Serikali ifanya juu chini ikamilishe isije ikapatikana laana, kwani kila siku wananchi wanalaani.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Magufuli (Mb) na *Engineer* Gerson Lwenge (Mb) kwa kazi nzuri ya kutukuka. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kukamilisha barabara yangu ya Mwanga - Kikweni - Lomwe kwa kiwango cha Lami laini ya *otta seal*.

Mheshimiwa Spika, aidha nawaomba watusaidie barabara ya Lembeni - Kilomeni - Lomwe ipande daraja ili ihudumiwe na *TANROADS* Kilimanjaro.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni barabara ya Kalambanzite – Ilemba kupandishwa kuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, yapata miaka miwili imepita tangu barabara hii kuombewa na RCC - Rukwa kupandishwa iwe ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, wataalam kutoka Ofisi ya Wizara walikuja na kuridhishwa kuwa barabara hiyo inafaa kupandishwa daraja kuwa ya Mkoa. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri ni lini barabara hiyo itapandishwa daraja? Naomba majibu wakati wa ufafanuzi.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru jitihada za kujenga barabara ya Tanga - Pangani - Saadani - Bagamoyo kwa kiwango cha lami. Barabara hii itahusisha *bypass* ya kupitia Nguvumali ambako tathmini za nyumba zitakazobomolewa hazijulikani hivyo zinawapa kigugumizi wenye nyumba hizo. Naomba tathmini za nyumba na majengo yote yanayohusika na barabara hizi zipangwe mapema.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuamua kuwafidia waliokuwa wanadai fidia. Hata hivyo inaonyesha kuwa fidia nyingine ya shilingi milioni 130 imetengwa kwa malengo mengine. Ningependa kujua fedha hizo ni kwa wananchi wangapi na tathmini zao zikoje?

Mheshimiwa Spika, kituo cha mabasi Tanga kimekamilika, hivyo *TANROADS* watekeleze jukumu lao kwa kuboresha barabara inayopita mbele ya kituo hicho ili kurahisisha uingizaji wa mabasi kituoni.

Mheshimiwa Spika, matuta kwenye barabara kuu yaondolewe.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache katika hotuba hii ya bajeti ya ujenzi. Nianze na nyumba zinazomilikiwa na ujenzi zilizopo hapa Dodoma *Area D.* Nyumba hizi kwa muda mrefu hazijafanyiwa matengenezo vitu, vingi vimechakaa vinahitaji kubadilishwa. Ukienda kwenye ofisi zao wanadai hawana fedha za matengenezo je, wapangaji wafanyeje wakati wanalipa kodi wakitegemea kupata huduma za matengenezo pale yanapotokea matatizo katika nyumba hizo?

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa wapangaji katika nyumba hizo, tumekuwa tukifanya matengenezo madogo madogo katika nyumba hizo baada ya kuona hakuna hatua zinazochukuliwa na Wizara hii, sasa napenda kujua ni lini Wizara itaona umuhimu wa kutengeneza nyumba hizi?

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni mizani. Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wasafirishaji kuwa mizani imekuwa ikitoa taarifa ambazo si sahihi kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine. Ningependa kujua ni kitu gani kinasababisha tofauti hiyo kutokea za kuongezeka kwa uzito?

Suala la tatu ucheleweshwaji wa wananchi kulipwa fidia baada ya kufanyiwa tathimini hili limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa Serikali kushindwa kulipwa fidia hiyo na hii kusababisha kutofahamu nini kinachoendelea na tunawapa wakati mgumu sana wananchi wetu wanashindwa kuendeleza maisha yao. Hivyo naomba Serikali ichukue hatua za haraka pale tathimini inapofanyika wananchi walipwe ili miradi hiyo iweze kuanza kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru, naomba niliyoandika yafanyiwe kazi.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri naomba sana mambo yafuatayo yafanyiwe kazi kwa haraka sana kwani ni kero kubwa kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mizani ya Singida, imekuwa tabia ya watu waliopo kwenye mizani ya Singida kuomba rushwa, cha kushangaza ni kwamba maeneo mengine yote yenye mizani magari yanapita na kuonekana mizigo haijazidi lakini ifikapo tu Singida ni lazima mzigo uonekane kuwa umezidi na baada ya kutoa rushwa kuanzia 20,000/= mpaka 50,000/= malori hayo ya mizigo huachiwa. Inawezekana mizani imechezewa ili kuweka mwanya wa kuomba rushwa. Hata magari ya *transit* yanasumbuliwa sana, hii inavunja heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za lami Tabora kwa miezi kadhaa kazi ya ujenzi wa barabara Tabora - Ndono - Urambo, Tabora - Kigwa - Kizengi, Tabora - Puge - Nzega ilikuwa imesimama kutokana na Serikali kutowalipa wakandarasi lakini kwa sasa kazi imeanza isije ikawa kwa ajili ya kipindi hiki tu cha kupitisha bajeti na baadaye kazi ikasimama tena! Hayo yametukuta mwaka jana lakini sasa naomba isije kutokea tena kwa sababu barabara hiyo ni heshima kwa Rais wetu aliyetoa ahadi ya kukamilisha barabara kabla ya muda wake kuisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa Mheshimiwa Waziri kumpongeza yeye na watendaji wa Wizara ya Ujenzi na Bodi zote hasa Bodi ya Barabara na *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika,sasa nachangia kama ifuatavyo nikianza na *Closed Circuit TV* (CCTV). Ili kuokoa *road asset* inayoharibiwa na madereva wazembe nashauri CCTV ziwekwe kwenye majiji makubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya lami Karatu - Mbulu - Haydom - Sheluu barabara ya Karatu - Mbulu – Haydom, Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi siku ya kuzindua barabara ya Minjungu – Singida, baada ya hapo Naibu Waziri wa Ujenzi mwaka 2013 alijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mbulu, Mustapha Akunaay alisema mwaka wa fedha 2013/2014 upembuzi yakinifu *(feasibility study)* utafanyika na mwaka 2014/2015 itafanyika upembuzi wa kina *(detailed design)* tarehe 22 Aprili, 2014 ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kuwa inakuwaje kwenye bajeti hakuna fedha zilizopangwa kwa ajili hiyo labda fedha hizo zitapatikana kwenye vyanzo vingine? Mheshimiwa Waziri naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Mbuyu Germani - Mbulu nashukuru kuna fedha angalau kidogo zimepangwa. Je, shilingi milioni 240 kwenye Daraja la Magare itafanya nini? Ule mpango wa *Millenium Development Account* kuhusu mradi huu umekuwaje? Wakati fedha zikitajwa naomba Daraja la *Berrer* liwekwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naishukuru Serikali kwa uamuzi wa kuweka *concrete slab* kwenye barabara hiyo, lakini barabara haina mifereji *(calvets)* za kuhamisha maji. Nashauri *TANROADS* Mkoa wa Manyoni warekebishe jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upanuzi wa barabara katika Mji wa Mbulu mpango huu utazamwe upya ili barabara kuu inayoingia mjini kutoka Majora ibadilishwe kukwepa bomoa bomoa nyingi, kituo cha mabasi inapendekezwa kujenga nje ya mji wa upande wa barabara ya kutoka Karatu. Ahsante.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la mfereji/mitaro pembeni ya barabara, hii imekuwa ni kero ya muda mrefu sasa na tatizo hili lipo katika sehemu mbili, (a) Mifereji kuwepo lakini kwa sababu ya uzembe na kutoisafisha mara kwa mara inasababisha kuziba na hivyo mvua zinapoanza inasababisha mafuriko katika barabara zetu ambayo yanapelekea foleni ya magari na uharibifu mkubwa wa miundombinu na kupelekea tatizo kubwa kwa wananchi wanaokaa eneo husika.

Mheshimiwa Spika,mfano katika eneo la Sakina kata ya Elerai – Arusha Mjini kumekuwa na tatizo hili kwa muda sasa, zaidi ya wananchi 600 wamekabiliwa na tatizo hili na kusababisha maji kuingia katika makazi yao kutokana na mkondo uliopo katika makazi yao, kama mifereji ingekuwepo tatizo hili lisingetokea.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari kwenye Majiji kama Arusha, kunatokana na ongezeko kubwa la watu katika Miji yetu na hasa ile inayokua sasa kama

Arusha, inabidi litafutiwe suluhisho mapema sana kabla hali ya msongamano haijawa mbaya kama ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mpangilio mbaya wa mipango Miji tayari napendekeza *solution* iwe ni *flyovers* na hili lifanyike mapema tofauti na ilivyofanyika katika hali ya ucheleweshaji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Magole - Turiani nasikitika sana kwa namna barabara hii inavyosuasua kujengwa. Kwa taarifa nilizonazo baada ya kukaa vikao viwili na wasimamizi wa mradi toka *TANROAD* Makao Makuu ni kwamba mkandarasi amesimama ujenzi kwa sababu anadai fedha shilingi bilioni zaidi ya sita kwa kazi zilizokamilika na kuhakikiwa kupitia bajeti iliyowasilishwa leo ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetega shilingi 6, 156,840,000/= maana yake fedha hizi ni za kulipa deni la mkandarasi wa fedha anazodai. Swali langu mkandarasi ataendeleaje na kazi kama fedha ni za kumlipa deni kwa kazi alizofanya tu? Naomba ahadi ya Rais itimie ya kukamilishwa kufikia kipindi cha 2010 hadi 2015. Naomba majibu hii barabara itakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, kupandishwa daraja barabara ni miaka mitatu, nimeomba kupandishwa daraja barabara zifuatazo:-

(1) Dakawa - Dihombo.

(2) Mhonda - Ubiri - Pemba.

(3) Langali - Nyandira - Kikeo.

Mheshimiwa Spika, kikao cha *Road Board* mwaka 2011 na RCC vilishawasilisha Wizarani na Katibu Mkuu kukiri kupokea lakini mpaka sasa na hata bajeti yako haionyeshi majibu. Naomba majibu kuhusu maombi haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi maalum ya ujenzi wa madaraja, kutokana na mvua za mwaka huu kumetokea madaraja mawili kusababisha kukosekana kwa mawasiliano ya vijiji katika Kata ya Bunduki. Naomba fedha, maombi maalum kuwaokoa wananchi wangu Kata ya Bunduki na Mgeta

(i) Daraja la Mgeta limeonyesha nyufa ni hatari sana.
(ii) Daraja la Bunduki katika Kijiji cha Bunduki.

(iii) Daraja la kuunganisha Bunduki na kijiji cha Vinile na Maguruwe.

Aidha naomba daraja kuunganisha Njeula (Mziha) na Kibindu (Jimbo la Chalinze) na kijiji cha Pandambili (Kata ya Kibati) na Kilindi. Naomba Wizara yako na TAMISEMI kupokea maombi haya maalum kwani Halmashauri ya Mvomero haina uwezo wa ujenzi wa madaraja hayo, naomba sana Waziri atusaidie wana Mvomero kwa hili.

Mheshimiwa Spika, natumaini maombi yangu yatapokelewa na kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kujenga nyumba za watumishi kupitia Wakala wa Majengo Tanzania. Hapa Dodoma nyumba zilizojengwa zenye kujulikana kama nyumba 300 zipo katika mazingira machafu sana. Ni kweli kwamba wateja wanaoishi katika nyumba hizo wana *background* tofauti za maisha.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa nyumba hizo na mazingira yake kutasaidia sana nyumba hizo zidumu na pia usalama kwa wateja na kuzuia mazingira rafiki kwa wadudu waenezao magonjwa kama vile malaria, dengue na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza masharti ya utunzaji na usafi wa mazingira yapewe kwa wale wote wanaotaka kuendelea kuishi katika nyumba hizo na hata katika miji mingine. *Estate Managers* wapite angalau mara moja kwa mwezi ili kuhakikisha kwamba nyumba hizo zinatuzwa na zipo katika mazingira safi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wana ile tabia ya kusema ni mali ya Serikali jambo ambalo hupelekea kutojali, kutowajibika na kuacha tu nyumba hizo ziharibike.

Mheshimiwa Spika, nyumba hizo zifanyiwe *maintenance*/ukarabati pale inapostahili ili zidumu na hivyo kutumika kwa muda mrefu zikiwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa juhudi zake kwa ajili ya miradi mingi inayofanyika kwenye Wizara yake. Wizara yake ina bahati kubwa kutokana kuwa na timu nzuri kuanzia Wizarani mpaka Mikoani, hasa Mhandisi wa Mkoa wetu wa Arusha ni mchapakazi wa kuigwa.

Napenda kuelezea mambo machache ambayo yanasababishwa na uharibifu wa barabara zetu. Kwanza ni magari mazito zaidi ya kiwango, ni afadhali jambo hili lifuate sheria kwani kabla ya barabara kumalizika inaanza kubonyea, mfano barabara ya Arusha - Namanga imebonyea sehemu mbalimbali, napenda kueleza barabara hii iangaliwe kwani wanajenga chini ya kiwango kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Sanya Juu - Kamwanga, barabara hii imepangiwa fedha kuanzia mwaka 2009/2010 mpaka leo haikuanza matengenezo, niliwahi kuzungumzia kwamba naomba barabara hii ianze kutokana na uharibifu wa barabara iliyopo kuharibika kila mwaka kutokana na udongo kuwa mbovu sana. Kutokana na bomoa bomoa huko Kamwanga baadhi ya wananchi wamelipwa lakini kuna wengine hawakulipwa. Naomba walipwe wale ambao hawakupata malipo yao.

Mheshimiwa Spika, lingine wale wote waliowekewa X na wengine wamesimamisha majengo yaliyokuwa yanaendelea. Malipo yao yaanze kulipwa mapema.

Mheshimiwa Spika, napenda kufikisha shukrani za wananchi wa Longido kwa kupandishwa barabara za Longido - Sanya Juu Siha kuwa barabara ya Mkoa, wanakushukuru sana pamoja na Mhandisi wa Mkoa Bwana Kakoko. Vyakula kutoka Sanya vinaletwa mpaka masoko yote ya Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba ujenzi wa barabara ya Ketumbeine - Gilay - Lengai ifunguliwe, watalii toka Kenya kwenda Mlima Lengai na *Lake Natron* wanapita.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze na kuwapongeza Mawaziri wa Wizara pamoja na watendaji wote kwa kuleta bajeti yao hapa Bungeni ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara niendelee kuwapongeza kwa kazi nzuri za ujenzi wa barabara nchini zikiwepo za Mkoa wetu wa Iringa na hasa ile ya Dodoma - Iringa tunaamini itakamilika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua vigezo vinavyotumiwa na Serikali kwa ajili ya kuanza hii miradi ya barabara, kwa sababu katika Mkoa wa Iringa zipo barabara za kiuchumi ambazo muda wote zimekuwa hazipatiwi kipaumbele, mfano barabara inayokwenda *Ruaha National Park,* barabara hii nilishauliza swali hapa Bungeni niliambiwa kuwa upembuzi yakinifu unafanyika na nikaambiwa mradi huu kuna fedha toka Marekani, ningependa kujua kwa sasa ni lini barabara hiyo itapewa kipaumbele na upembuzi yakinifu huchukua kipindi gani mpaka kujengwa barabara?

Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara hiyo pia zipo barabara za Kilolo - Idete, na zile zinazokwenda katika msitu wa *Sao Hill* - Mufindi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya miradi ya ujenzi wa barabara, kumekuwepo na malalamiko makubwa sana ya makandarasi kuidai Serikali mpaka kutishia migomo, na kiukweli hawa makandarasi wengi wao wanakuwa wana mikopo benki. Ningeomba kujua mkakati uliowekwa na Serikali katika kumaliza tatizo hili na kujua endapo makandarasi hawa watafilisiwa dhamana zao kwa ajili ya mikopo waliochukua benki, Serikali ipo tayari kuwafidia?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa masuala mtambuka ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara niipongeza Serikali katika ushirikishwaji huo ambao tunaamini kuwa utawajengea pia uwezo wanawake kuweza kushiriki katika miradi hii ya barabara. Tunaomba Serikali iwe inaweka vigezo vinatumika katika kuwajengea uwezo wanawake hao na iweke wazi vikundi ambavyo vimejengewa uwezo ili tuwajue kama ni wa mikoa gani wanawake wamejengewa uwezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TEMESA niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanyika kupitia wakala hii, ningependa kujua ni mkakati gani umewekwa na Serikali kuhakikisha magari yote ya Serikali yanatengenezwa kupitia wakala hii. Katika bajeti za Wizara za Serikali kumekuwepo na bajeti kubwa sana zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya magari kama fedha hizo zingepelekwa katika Wakala huo ingesaidia sana.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2013 niliuliza katika swali langu la msingi ni lini barabara ya Dodoma - Mayamaya kilometa 43 itakamilika?

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri alijibu kuwa barabara hiyo itakamilika ifikapo mwisho wa mwezi Septemba. Sasa ni miezi minane barabara hii haijakamilika. Je, sasa barabara hii itakamilika lini?

Namshukuru Mheshimiwa Waziri alitualika katika hafla ya uwekaji wa saini kati ya Serikali na Wakandarasi CHICO na *China Seventh Group* kwa ujenzi wa barabara ya Mela - Mayamaya kilometa 99.35 na Mela - Bonga kilometa 88.80. Pamoja na kuwa miezi mitatu ya *mobilaization* imepita bado kazi ya ujenzi haijaanza. Je, kazi hii itaanza lini kwani miezi 33 waliyopewa kukamilisha kazi inaweza kuisha kabla ya kazi kukamilika. Aidha Wakandarasi wafahamishwe

kuwachukua wananchi katika maeneo husika katika kazi wanazozimudu ili nao wanufaike badala ya kuchukua watu wa maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Mheshimiwa Rais aliahidi kupandishwa hadhi barabara ya Ntundwa - Hurui - Kash na kuchukuliwa na *TANROADS*. Mpaka sasa barabara hii haijapandishwa hadhi pamoja na maombi hayo kupitishwa katika ngazi zote husika. Aidha barabara zifuatazo zimeombewa kupandishwa hadhi lakini mpaka sasa hazijachukuliwa na *TANROADS* pamoja na kuwa zinatoka Wilaya ya Kondoa na kuelekea Wilaya za Mkoa jirani wa Manyara.

(i) Mnenia – Kikore – Galapo;

(ii) Senya – Beleko – Babati; na

(iii) Kinyasi- Majengo – Chubi – Babati.

Mheshimiwa Spika, je, zitapandishwa hadhi lini kwani ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Munguru lililopo katika Kata ya Senya linakaribia kufunikwa na mchanga. Je, ni lini mchanga huo utaondolewa, kwani daraja lipo katika hatari ya kuvunjika.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbande - Kongwa inaendelea kujengwa kilometa tano kwa lami pale Kongwa Mjini. Itakuwa vema na haki mkimalizia kilometa 11 zilizobakia kutoka Kongwa kwenda Mbande. Barabara hii ni muhimu sana kwa watu wa Kongwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, kule Vunjo Mheshimiwa Waziri unatengeneza barabara mbili za kwenda vijiji vya Marangu - Kilima Sokoni na Kawawa - Nduoni Kata ya Kirua Magharibi.

Pia kuna barabara ya Himo - Kilema Hospitali, barabara hii inapita kwenye taasisi muhimu za kidini na shule. Nimeambiwa kwa maandishi kuwa DED ameiombea fedha kutoka *Millenium Challenge Account* nisaidie kujua kama hizo fedha zinaweza kupatikana maana itakuwa ni mwokozi wetu.

Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa kazi nzuri na utumishi uliotukuka.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa John Magufuli kwa kazi nzuri anazofanya kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kuona kwamba pamoja na ahadi za Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikweke na wewe Mheshimiwa John Magufuli kwamba barabara ya Makutano (Musoma) - Butiama - Ikuzu hadi Serengeti itapewa kipaumbele kujengwa. Leo ni miaka 13 nasimama hapa Bungeni nikiomba kujua ni lini barabara hii itajengwa?

Mheshimiwa Spika, nashangaa kuona Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli anatoa ahadi mbalimbali kwangu mimi binafsi na Wabunge wenzangu kutoka Mkoa wa Mara kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami haraka iwezekanavyo. Leo pia naona

kwa masikitiko makubwa kwamba hakuna *seriousness* yoyote inayofanywa kuhusu ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu Azimio la RCC Mkoa wa Mara kwa kauli moja walishauri kwamba hao makandarasi wanaojenga barabara hii wafukuzwe kwa sababu hawana uwezo wa kumudu ujenzi wa barabara hii. Naona ushauri huu umepuuzwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu Jimboni Butiama wamenituma niseme kwamba kama barabara imeshindikana Serikali iseme wazi wazi kwamba barabara ya Musoma - Butiama - Serengeti kamwe haitajengwa na Serikali inayoongozwa na CCM.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo nasema iwapo sipati sababu za kuniridhisha kuhusu barabara hii sitaunga mkono hoja hii.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nianze na suala la vita dhidi ya rushwa. Wizara ihakikishe inatoa elimu kwa watumishi kama Wakandarasi, Wakurungenzi na Wahandisi kuhusu athari za rushwa jinsi rushwa inavyorudisha nyuma maendeleo hasa wakati wa utoaji wa *tender* kwani *tender* zinapotangazwa kumekuwa na michezo michafu, kwa waombaji *tender* kutoa *percent* fulani katika fedha zilizopangwa katika mradi ili muomba *tender* apewe *tender* hiyo.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo huitia hasara Serikali na kusababisha miradi kujengwa chini ya kiwango na kazi kuwa za kurudiwarudiwa, sijui Wizara inasemaje kuhusu hili? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara na madaraja Serikali ihakikishe inamaliza kero zinazosababisha kukwama kwa miradi mingi ya ujenzi ya barabara na madaraja kama vile ucheleweshwaji wa fedha za miradi ya barabara hivyo kupelekea kutotengenezwa kwa wakati, Wakandarasi kutolipwa fedha zao kunafanya utendaji kazi kuwa mbovu na wa chini ya kiwango na barabara nyingi kutengenezwa chini ya kiwango kunafanya barabara kutodumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii yenye dhamana kuhakikisha upungufu wote huu unafanyiwa kazi ili tupate barabara na madaraja kwa wakati na imara kwa manufaa ya Watanzania wote kwa maendeleo safi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha taarifa yangu kwa maandishi kwa uchungu kuona Mkoa wangu wa Katavi barabara nyingi vijijini hazipitiki na hivyo kusababisha usumbufu wa kupitisha mazao msimu huu wa mavuno. Hivyo basi naiomba Serikali kupitia Wizara kuhakikisha inapeleka fedha katika Halmashauri kwa wakati ili miradi ya barabara na madaraja yajengwe kwa wakati uliyopangwa. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, barabara zetu zinatengenezwa kwa fedha nyingi sana ambazo ni kodi za Watanzania tena wengi ni maskini. Hili ni jambo la ajabu kwamba tunazo sheria na kanuni za kulinda barabara zetu lakini viongozi wakuu wamekuwa wanatetea malori yanayozidisha mizigo na kuharibu barabara.

Mheshimiwa Spika, sisi wote ni mashahidi barabara zote zina migongo na hata kusababisha ajali barabarani. Barabara zimejaa mashimo na mibonyeo. Serikali ieleze Bungeni kauli iliyotolewa na Waziri Mkuu kuruhusu magari yanayozidisha mizigo kuendelea kuharibu barabara zetu inalenga nini hasa kwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, tangu kutolewa kwa kauli ile malori sasa yanasanya mizigo ya mikaa, mahindi na mazao mengine juu ya mizigo waliobeba. Kwa nini Waziri Mkuu amevunja sheria?

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2008 mpaka 2010 vikao vya RCC Mkoa wa Tabora tulijadili na kuomba Serikali iziweke barabara mbili chini ya *TANROAD* ambazo ni barabara ya Kaliua - Ulyankuru (Makazi - Uyowa na ile ya kutoka Kaliua kwenda kilometa 90 kupitia Kangeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubali barabara hizi kuwa chini ya *TANROAD* lakini mpaka sasa bado imeachwa kwa Mkoa wa Tabora. Mkoa na Halmashauri ya Wilaya na Kaliua zinakosa fedha ya kutosha kutengeneza barabara hizi na hivyo wakati wote wa mvua hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali hizi barabara zihudumiwe na *TANROAD* kwani hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwenye hotuba ya Waziri aliliambia Bunge kwamba barabara za Mkoa wa Tabora zinakamilika mwaka 2013/2014 ambazo ni:-

(i) Manyoni - Itigi - Tabora.

(ii) Nzega - Tabora.

(iii) Tabora - Urambo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na vilio kwa wananchi kubomolewa nyumba zao pale ambapo Miji inaboreshwa kwa barabara. Wananchi wamebaki maskini na hivyo kushindwa kujenga tena nyumba bora za kuishi. Serikali itumie utaratibu uliotumika hapa Dodoma, barabara zimejengwa tena pana bila kubomoa nyumba za wananchi wala vibanda vya biashara.

Mheshimiwa Spika, alama za barabarani zimeendelea kung'olewa kwa sababu ya vyuma chakavu, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, ipo kasumba ya wananchi katika baadhi ya maeneo kutupa takataka kwenye mitaro ya barabara na kufanya ni dampo. Matokeo yake mitaro inaziba, inafunika na wakati wa mvua barabara zinafunika maji. Elimu itolewe na zaidi adhabu kali iwekwe kwa wale wanaokiuka taratibu za ulinzi wa miundombinu za barabara.

Mheshimiwa Spika, TEMESA ni wakala wa kutengeneza magari ya Serikali, kila Mkoa kuna karakana ya TEMESA lakini magari ya Serikali yanatengenezwa kwenye *garage* za watu binafsi. Gharama kubwa zinatumika kupeleka magari haya huko *garage* binafsi wakati wapo mafundi wazuri wa TEMESA ambao hawatumiki vizuri. Serikali ina mpango gani kuboresha karakana za TEMESA mikoani ili kuokoa fedha za Serikali zinazokwenda nje?

Mheshimiwa Spika, kuna mwongozo gani umewekwa na Serikali ili magari yote ya Serikali yatengenezwe na wakala wa Serikali?

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara kwa hotuba nzuri. Pongezi pia kwa jitihada na matokeo yanayoonekana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa ni muhimu sana kiuchumi na itachochea kukua kwa uchumi wa Mikoa ya Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro na Taifa kwa ujumla. Nashauri mwekezaji apatikane haraka na ujenzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ngapito (Kiteto), Kimotorok hadi Babati iandaliwe ifanyiwe upembuzi yakinifu na hatimaye ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kijungu - Simya hadi Dongo ipewe usimamizi wa karibu. Pia mitaro ya maji iwekwe ili kuhakikisha kuwa barabara inadumu.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya muda mrefu ya kilometa saba za lami katika mji wa Kibaya itekelezwe.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara, kuanzia kwa Waziri, Naibu Waziri, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hasa *TANROADS* Morogoro ambaye anajitahidi sana kusimamia barabara zinazomhusu ingawa fedha zinazotengwa ni kidogo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo mimi langu ni swali kwa Serikali ni lini na ni sababu gani barabara ya Dar es Salaam - Lindi kipande cha Ndundu - Somanga haikamiliki kwa miaka karibu ishirini sasa? Kweli inasikitisha kwa vile kuna barabara nyingi mpya zinaanzwa na kumalizika na hii ya Ndundu - Somanga imekuwa donda ndugu, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo upembuzi yakinifu unaendelea kwa muda mrefu ni ile ya Mtwara - Newala - Masasi ya kilometa 209. Barabara hii ikifunguliwa kwa lami itanufaisha wananchi kwa kusafirisha mazao yao kama korosho, karanga, ufuta na kadhalika kuelekea Mtwara Bandarini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kwamba barabara Mtwara - Mingoyo - Masasi ifanyiwe ukarabati mkubwa kabla haijamalizika kujenga upya kwa vile barabara yenyewe ilijengwa miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu mfupi naunga mkono hoja kwa matumaini kwamba haya niliyoshauri yatafanyiwa kazi.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara isikie kilio changu cha muda mrefu cha kupandisha daraja, barabara muhimu sana inayohudumia majimbo manne barabara hiyo ni kutoka Mlalo - Jimbo la Mlalo kwenda Ngwelo - Mlola Makanya - Jimbo la Lushoto kwenda Milingano Jimbo la Bumbuli hadi Mashewa Jimbo la Korogwe. Barabara hiyo ni ya uchumi kwa maeneo na majimbo yote inakopitia.

Mheshimiwa Spika, naomba sana barabara ya Lushoto kwenda Magamba imechukua miaka nane tangu imeanza kujengwa. Barabara ile ni kilometa 5 - 10 inatengewa fedha kidogo sana. Umuhimu wa barabara hii ni kwamba inakwenda Ikulu ndogo, ni aibu kwa viongozi wetu wanapotembelea Lushoto. Naomba itengewe fungu kamili/dharula kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, ipo barabara mbadala ya kwenda makao makuu ya Wilaya ya Lushoto, barabara ni ya mkato kutoka Mombo kwenda Lushoto kupitia Dochi. Barabara hii ni

muhimu kama barabara mbadala ikitokea dharula kwa kuharibika barabara ya kawaida ya Mombo - Soni Lushoto. Tunaomba kutengeneza barabara hiyo maana imeharibiwa na mvua za masika ya mwaka huu, Halmashauri haiwezi kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo si kwa umuhimu naunga mkono wazo la kuundwa Shirika/Wakala wa Ujenzi wa Barabara Vijijini, jambo hilo ni muhimu kwa kuongeza ufanisi katika ujenzi na utengenezaji barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zangu za dhati kutoka sakafu ya moyo wangu kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, namkumbusha upandishaji daraja kwa ahadi yake barabara ya Mlalo, Ngwelo - Mlola - Makanya hadi Milingano - Mashewa, naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli.

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya lami kutoka Lushoto hadi Magamba naomba Waziri anisaidie. Ahsante.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Njiapanda -Karatu) - Mangola - Lalago katika uchaguzi wa mwaka 2010, katika kampeni za mgombea Urais wa CCM, ahadi ilitolewa kujengwa kwa kiwango cha lami barabara husika, majibu ya Serikali imekuwa ni usanifu na mchakato unaendelea. Hata hivyo katika bajeti ya mwaka jana ya Wizara hii mlituahidi kuwa mtaanza matengenezo na fedha zimetengwa na hadi sasa hakuna kilichofanyika.

Mwaka ujao wa fedha hakuna fedha mlizotenga, je, ni kwa nini mliwadanganya wananchi ili hali hakuna dhamira ya kufanya hivyo? Je, ahadi hiyo ilikuwa ya kisiasa zaidi? Kama sivyo ni kwa nini hamkutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami? Je, ni lini sasa ujenzi utaanza? Tunahitaji majibu ya kweli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahadi nyingine iliyotolewa ni ujenzi wa kilometa moja kwa kiwango cha lami katika Mji wa Karatu. Ahadi hii iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ila hakuna kilichotekelezwa na wakati wa ziara ya Rais tarehe 22/04/2014 Wilayani Karatu alikumbushiwa ahadi hiyo hiyo kutoa msisitizo kuwa ahadi hiyo itatekelezwa. Lakini katika bajeti hii hakuna fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo. Je, ni kwa nini fedha hazikutengwa na je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kupandishwa kwa hadhi ya barabara nitakazoziainisha hapa chini toka ngazi ya Halmashauri na kuhudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ambazo ni barabara kutoka:-

(i) Ntungwa - Chilumo - Mkulwe - Kamsamba (kilometa 51.1);

(ii) Kakozi - Kapele - Namchinka - Longa (kilometa 50.6); na

(iii) Ivuna - Mkomba - Songwe (Chunya) kilometa 24.4.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni ndefu na haziwezi kuhudumiwa na Halmashauri na zinaunganisha Wilaya moja na nyingine, zinauzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zilipitishwa katika vikao vya RCC tangu mwaka 2011 na 2012 lakini mpaka sasa hatujapatiwa majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kupatiwa majibu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, *few things to be answered, Nelson Mandela Road* wakati tunazindua Taasisi ya Nelson Mandela Arumeru *(Nelson Mandela Institute)* Mheshimiwa Rais aliahidi ile barabara ingetengenezwa kwa kiwango cha lami *financial year* 2012/2013 *of which last year* imetengwa bilioni 1.3 pekee, ni kilometa tatu peke yake zilizotengenezwa tena kwa kipande kidogo tu cha katikati. Kutoka Tengeru kilometa tatu *to Nelson Mandela Road* bado kwa namna hii hata hizo kilometa tatu hazina maana kama hatujaunganisha na Arusha Mjini au na Tengeru.

Mheshimiwa Spika, barabara ya mzunguko *(by pass) high way* ya Arusha - Meru barabara hii imekuwa ni wimbo, fidia haijalipwa, hatujui italipwa lini na kwenye *rates* zipi. Pili mradi utaanza lini bado haijulikani?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibaoni King'ori kwenda mpaka Longido ni rai yangu kwamba sasa hii barabara ipande hadhi. Kwa mtu anayetoka Kenya hakuna sababu ya kupita Arusha Mjini badala yake ingekuwa rahisi kutumia njia hii. Lakini pia kwa watalii wanaokwenda *Arusha National Park* ingekuwa rahisi zaidi. Vilevile barabara hii ni fursa nzuri ya kufanywa *business pattern* hususan kwa biashara ya nyanya na pia ni kiunganishi kizuri kwa Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Vilevile shukrani nyingi kwa *Regional Manager* wa *TANROAD* Arusha kwa ushirikiano mzuri anaowapatia wananchi wa Mkoa wa Arusha.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Masimba kutokea Mangamba tuliombea fedha (ombi maalum) la RCC na *TANROADS* bado ili iwe ya lami kutokana na umuhimu wake kwenye bajeti sioni kitu. Una taarifa zozote maana nitachangia hilo.

**SPIKA:** Sasa namwita mtoa hoja wa kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 20!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo mengi ambayo amenitendea ikiwa na pamoja na kunipa afya njema na pia kwa namna anavyolibariki Taifa hili kuwa na ustawi mkubwa wa maendeleo na kuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Njombe Magharibi, Wilaya ya Wanging'ombe kwa namna wanavyochangia maendeleo. Hivi sasa wameweza kujenga Ofisi na kukarabati Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya kwa kujitolea na jana wamemkabidhi Mkuu wa Mkoa. Hili ni jambo moja zuri la kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna anavyonisaidia, tunavyoweza kuongoza hii Wizara kwa pamoja na kwa namna alivyowasilisha Bajeti hii. Kazi yetu ni ngumu, ni kazi ambayo inahitaji kwa kweli tushirikiane pamoja na Waheshimiwa Wabunge katika kujenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba ndugu Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono. Ni kweli kila mmoja anahitaji barabara nzuri, barabara ya lami, inawezekana tukawa hatujafikia, lakini hivi sasa

Serikali inajenga kilomita 11,154 nchi nchi nzima. Ni kazi moja kubwa. Ukienda kwa takwimu ya fedha maana yake unahitaji karibu trilioni 11,000. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imedhamiria kufanya kazi hiyo. Naamini kabisa tutafikia huko tunakokwenda, tuombeane kuliko kubeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezitoa, lakini zile ambazo hatutajibu tutawaletea kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, kwanza ameipongeza Serikali na sisi tunasema tunashukuru kwa pongezi. Pia angetaka kujua fidia kwa wananchi walioathirika na mradi wa Arusha-Holili, upande wa Arusha umechelewa sana toka mwaka 2012, malipo yatalipwa lini?

Mheshimiwa Spika, jibu ni kwamba, fidia za mradi zimeanza kulipwa. Fidia ya sehemu ya Sakina hadi Tengeru imeshalipwa jumla ya Shilingi milioni 810 na sehemu ya pili ya *Arusha Bypass* itaanza kulipwa mwaka huu wa fedha ambayo tayari tumeiweka kwenye bajeti, ukiangalia Kasma 4118 ukurasa wa 202.

Mheshimiwa Spika, pia, ametaka kujua uwiano wa barabara za lami na za changarawe katika Jiji la Dar-es-Salaam uongezeke ili kulipatia hadhi Jiji.

Mheshimiwa Spika, jibu ni kwamba, ushauri tunaupokea na Serikali itaendelea kujenga barabara za lami katika Jiji la Dar-es-Salaam kama tulivyoonesha kwenye ukurasa wa 125 hadi 127 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameongelea pia, suala la msongamano wa Dar-es-Salaam kwamba, tuanze kujenga *fly-overs.* Majibu ni kwamba, ujenzi wa *fly overs* katika Jiji la Dar-es-Salaam umeshaanza kwa maana ya usanifu umekamilika. *Fly Over* ya *TAZARA* inategemea kuanza mwezi Septemba mwaka huu, 2014 baada ya Serikali ya Japani kuongeza fedha ambayo ilikuwa inahitajika kwa ajili ya kazi hiyo. Pia Serikali inaendelea na maboresho katika maeneo ya Daraja la Salander, makutano ya Mwenge, Moroko, Magomeni, Chang'ombe, *KAMATA,* Uhasibu na Tabata - *Mandela Road.* Haya tumeyaeleza katika ukurasa wa 133 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika, yeye ametaka kujua fedha imekuwa ikitengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi katika Jimbo la Ubungo miaka mfululizo toka mwaka 2011, 2012 mpaka 2013, lakini hakuna ujenzi wowote wa barabara ulioanza?

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba, katika kujenga barabara kuna hatua mbalimbali ambazo ni lazima zifanyike, ikiwa kwanza lazima barabara hizi zifanyiwe usanifu. Kazi hii imeshafanywa na sasa hivi baadhi ya barabara tayari tumeshaanza kuzijenga.

Mheshimiwa Spika, ametaka kujua barabara zilizioathirika na mvua kama zitafanyiwa matengenezo ya dharura. Barabara zote ambazo zimeathiriwa na mvua, mafuriko yaliyotokea tutazijenga na tutatumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo, fedha zipo na kazi hiyo itafanyika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Henry Shekifu, yeye ametoa pongezi kwa Waziri; tunazipokea pongezi hizo. Lakini pia anakumbusha ahadi ya kupandisha daraja barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya. Jibu ni kwamba barabara hiyo itapandishwa baada ya Kamati Maalum ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria hii ya Barabara kupitia na kuona kama inakidhi vigezo viliavyoainishwa kwenye Sheria hiyo. Kwa hiyo, ikishapitisha, basi tutaipandisha barabara hiyo.

Vile vile Mheshimiwa Shekifu alitaka ujenzi wa lami kutoka Lushoto hadi Magamba ukamilishwe. Mwaka wa Fedha 2014/2015 ujenzi wa kiwango cha lami utakamilishwa kilometa mbili zilizobakia. Kwa hiyo, ahadi hiyo tutaikamilisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, yeye ametaka kujua ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya Chaya – Nyahua, kilometa 89 kwa kutumia ufadhili wa *Kuwait Fund* umetekelezwa?

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba barabara hiyo itaanza mara tu baada ya usanifu wa kina kukamilika. Hii ilikuwa ndiyo *condition* ya Wafadhili. Japokuwa usanifu ulikuwa umefanywa, lakini wakasema tutatoa fedha baada ya kufanya usanifu tena. Kwa maana Mfadhili, kila mmoja anakuja na *condition* yake. Kwa hiyo, sasa hivi kazi hiyo imeshafanyika, tunasubiri *no objection* kutoka *Kuwait Fund* ili kazi hiyo iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, pia ametaka kujua wakati *DART,* hii barabara ambayo inajengwa kwa ajili ya Dar-es-Salaam – *BRT:* Je, walizingatia *mult model design* inayohusisha mabasi yaendayo kasi, reli nyepesi na *trams* na hivyo kupunguza kukaa Jijini?

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba, mfumo wa *BRT* unajengwa kwa kuhusisha usafiri wa mabasi pekee bila kuhusisha usafiri wa treni na *tram.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Herbert James Mntangi aliuliza: ni mpango upi wa kutekeleza ahadi ya Rais kwa barabara za Muheza, kujenga barabara ya lami kutoka Muheza mpaka Amani katika mwaka wa fedha 2014/2015?

Mheshimiwa Spika, mpango upo katika Kitabu cha Bajeti ukurasa wa 251. Kwa hiyo, ahadi ya Rais inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luckson Mwanjale ametaka kujua kwa nini fedha zilizotengwa barabara ya Isionje hadi Makete ni kidogo? Serikali ifikirie upya ili kutenga fedha zakutosha.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 124.092 ambazo zitatumika kufanyia matengenezo yaliyopangwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwanjale pia alisema mvua zimeharibu barabara nyingi za Halmashauri na kwamba, Halmashauri haina uwezo. Tunaagiza Halmashauri husika kwamba, itumie fedha za Mfuko wa Barabara kutengeneza mahali ambapo barabara hizi zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini alitoa pongezi, tunashukuru kwa pongezi. Lakini alitaka barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Mshamba ijengwe kwa kiwango cha lami kupunguza gharama za matangenezo kutokana na kwamba inapita kwenye vilima vingi na mvua nyingi.

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba, ushauri tunaupokea. Juhudi za ujenzi zimeanza kufanywa katika vilima vya Kasiko, Kamachumu, kwa kutenga fedha kila mwaka mpaka Serikali itakapopata fedha zakutosha ili tuweze kukamilisha barabara yote. Barabara hiyo imekamilika kwa kilometa nane kwa kiwango cha lami. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 tutaendelea kujenga kilometa moja nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda, alitoa pongezi kwa Wizara ya Ujenzi. Tunashukuru kwa pongezi hiyo, lakini pia anaomba maelezo juu ya barabara

ya Sumbawanga – Mpanda; ukurasa wa 130 wa hotuba. Ujenzi unaendelea sasa sehemu ya Sumbawanga – Kanazi – Kizi – Kibaoni: Je, hii itafika Mpanda? Ujenzi unakusudiwa kuendelezwa hadi Kibaoni – Stalike - Mpanda au toka Kizi – Stalike – Mpanda?

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba, ujenzi unakusudiwa kutoka Kizi – stalike hadi Mpanda.

Mhshimiwa Spika, pia anasema ni lini Serikali itawalipa fidia wale wote walioathirika na ujenzi wa barabara?

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba malipo ya fidia yatalipwa kwa wenye stahiki baada ya tathmini kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius Aloyce Ntukamazina, yeye ametoa pongezi, tunashukuru kwa pongezi. Lakini amesema katika hotuba ya 2013/2014 Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba barabara ya Nyakahura – Rulenge – Mrugama yenye kilometa 86, ingefanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba taratibu za ununuzi wa kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea na Mhandisi Mshauri anatarajiwa kupatikana Mwezi Juni, mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zarina Madabida naye ametoa pole kwa Mheshimiwa Waziri kwa ajali ya. Tunashukuru kwa pole hiyo. Vile vile ametoa pongezi kwa Wizara kwa kushughulikia mafuriko haraka; tunashukuru pia kwa pongezi hizo. Anataka upanuzi wa Daraja la salander.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, majibu ni kwamba, Serikali ya Korea imekubali kufadhili kufanya usanifu wa sehemu hiyo ya *Salander*. Kwa hiyo, tatizo hilo Mheshimiwa Madabida litashughulikiwa baada ya upembuzi kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Madabida na Wabunge wengi wameongea kwa kirefu sana kuhusu kumaliza kwa kipande cha barabara ya Ndundu – Somanga.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, ni kweli, ni nia ya Serikali, kama ilivyoanza kujenga zile kilometa 60 zilizobakia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kazi hiyo itakwisha. Sasa hivi tatizo lilikuwa Mfadhili wetu aliyekuwa amefadhili, *Kuwait Fund,* hakutoa fedha ambazo alikuwa ameahidi. Sasa hivi ameshaleta fedha. Kwa hiyo, Shilingi bilioni tano ambayo tumeiweka kwenye bajeti yetu na fedha ambazo ameshaleta, niwahakikishie kwamba kazi ile itakamilika. Tumemwita Mkandarasi, tutafanya Mkutano; mimi na Mheshimiwa Waziri tutafuatilia kwa karibu sana kuhakikisha barabara hii inakamilika, wananchi wa Kusini watapata barabara ya lami na hicho kipande kitakamilika. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na ushauri kwamba Serikali imalize kulipa madeni ya Makandarasi ili fedha zilizotenga zitumike kwa kazi zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, tunaupokea ushauri. Serikali itajitahidi sana kulipa madeni kwa kazi ambazo zimeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema, alitoa pongezi; tunashukuru kwa pongezi. Vile vile alisema anaomba barabara ya Himo – Kilema – Hospitali na kwamba fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka *Millenium Challenge Account* Waziri asaidie?

Mheshimiwa Spika, tutafuatilia maombi haya kutoka *Millenium Challenge* kupitia Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya Miundombinu ni kwamba matuta ya barabarani yaondolewe kabisa, yarekebishwe kulingana na viwango vilivyokubalika na wananchi waelimishwe kuhusu matumizi bora ya barabara.

Mhesimiwa Spika, ushauri tunaupokea na tumetoa maagizo kwamba matuta yote ambayo hayako kwenye kiwango ambacho kimewekwa yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo imeshaanza, lakini tunakwenda kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa sababu, hii pia ina gharama yake. Kwa hiyo, tutaendelea kufuatilia na kuhakikisha matuta yote ambayo yamejengwa, kama alivyosema mmoja, kwamba matuta mengine yako kama mgongo wa tembo, tutayaondoa matuta hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri kwamba Wakala wa Majengo ujihusishe na usanifu wa majengo, uchoraji ramani na uendelezaji wa viwanja vyake, ili kuongeza makusanyo ya Wizara. Ushauri tunaupokea. Wakala tayari ameshaanza kufanya kazi hiyo na tutaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inataka Wakala wa Majengo uzingatie lengo na madhumuni ya uwepo wake kuwapatia watumishi wa Serikali makazi bora.

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba, ushauri tunaupokea, lakini sasa hivi Wakala umeanza *program* maalum ya ujenzi wa nyumba za Serikali 2,500 na mpaka sasa kuna nyumba 155 zimekwishajengwa katika eneo la Bunju 'B' na hizi nyumba tutawauzia wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inataka Bodi ya *Archtect Quantity Surveyors Registration Board* itengeneze ramani ya majengo ya kisasa kwa mahitaji ya wananchi ili kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Bodi ya Usajili ni kutoa leseni kwa wabunifu majengo na wakadiriaji majengo kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, ushauri tunaupokea na tutaendelea kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati imetaka utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kwamba Hadi mwezi Aprili fedha za ndani zilizotolewa ni asilimia 85 ya bajeti wakati fedha za nje zilikuwa zimetolewa asilmia 30.

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba Serikali inazidi kuongeza kiasi cha fedha zake za ndani. Hata mwaka huu fedha ni nyingi zaidi kuliko ilivyokuwa bajeti iliyopita. Tutakuwa tunawendelea kuongeza kwa namna jinsi Serikali itakavyokuwa inajenga uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na ushauri kwamba Serikali itafute fungu maalum kwa ajili ya kutatua msongamano wa magari ya Dar-es-Salam badala ya fedha kidogo kidogo inayotengwa. Ushauri huo tunaupokea na tutaangalia namna bora ya kuutekeleza ushauri wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, nijibu hoja moja tu kutoka Kambi ya Upinzani kwamba, wametaka kuweka hizi *Cameras* kwenye mizani ili kupunguza ule msongamano.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeshaanza kufunga *CCTV Camera* mizani ya Wenda – Iringa na ipo katika hatua za mwisho kumpata mzabuni wa kuweka *CCTV Camera* katika vituo vya

mizani vya Mikese, Mkuranga na Msata. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Shilingi bilioni 1.62 fedha za Mfuko wa Barabara kuweka *CCTV Camera* katika vituo vingine 15 vya mizani nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *TEMESA* itoe maelezo, kwa nini ilifanya ununuzi wa Kivuko cha *MV. Malagarasi* ambacho kilikuwa kwenye Mpango wa Mwaka wa Fedha 2013 na hivyo kuashiria udhaifu wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba, Wizara kupitia *TEMESA* katika mipango yake ya mwaka 2013 ilipanga na kuanza ununuzi wa Kivuko cha *MV. Malagarasi* na kukamilisha ujenzi wake katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara ieleze ni kiasi gani kimeokolewa kwa manunuzi ya magari tangu agizo lililotolewa na Waziri Mkuu? Majibu ni kwamba, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi, wakati Serikali ilikamilisha mpango huo, Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kutoa maelekezo juu ya ununuzi wa magari ya Serikali ambapo magari ya Serikali yanayonunuliwa kwa sasa ni yenye injini isiyozidi *CC* 3,000. Mipango hii inalenga kupunguza gharama za ununuzi na usawazisho wa magari – *Standardisation.*

Mheshimiwa Spika, kuna mapendekezo, wengi wamechangia kuhusu kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara Vijijini? Ushauri huu tunaupokea na tutaona namna bora ya kuutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi kuhusu hifadhi ya barabara: Je, nyongeza ya hifadhi ya barabara kutoka meta 45 hadi 60 na meta 7.5 kila upande zilichukuliwa kwa kufuata Sheria?

Mheshimiwa Spika, jibu ni kwamba, Wizara kwa kupitia *TANROADS* imeweka alama kwa ajili ya kuwafahamisha wananchi mpaka wa hifadhi ya barabara ya meta 60 kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007. Kwa hiyo, tulifuata Sheria.

Vile vile kulikuwa na swali: Je, uthamini wa mali za wananchi ulifanyika na kuwalipa fidia?

Mheshimiwa Spika, uthamini utafanyika pale tunapotaka kufanya maendelezo ya barabara hii. Kwa sababu huwezi ukafanya uthamini nchi nzima.

Kwa hiyo, kwanza unatoa taarifa kwamba hapa ulipo uko kwenye hifadhi ya barabara. Lakini pale unapohitaji sasa kutwaa eneo lile na kupanua barabara, tunafanya uthamini na tunalipa pale ili kusudi tuweze kufanya kazi ya kufanya upanuzi. Huo ndiyo utaratibu ambao tunaendelea nao.

Mheshimiwa Spika, nadhani maelezo njiliyokuwanayo nimemaliza. Naomba tena niunge mkono hoja hii, ili nimwachie Mheshimiwa Waziri aendelee na yale ya kisera. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru wewe, lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa pande zote; Wabunge wa *CCM* na wa upande wa Vyama vya Upinzani kwa michango yao mizuri waliyoitoa. Lengo letu kubwa kwa sababu, Serikali kwa ujumla inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi inaamini maendeleo hayana Chama, lakini maendeleo ya kweli yataweza kutekelezwa na Chama cha Mapinduzi. Nilitaka nianze na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na kutoa historia kidogo ili kusudi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania waelewe tulikotoka, mahali tulipo na mahali tunakoenda. Wajerumani walipochukua nchi yetu, tangu enzi za akina Carl Peters kwenye miaka ya 1884 wakaitawala nchi hii na baadaye wakaja Waingereza nao wakatawala karibu miaka 41. Walipokuwa wakiondoka Tanzania waliacha nchi ya Tanzania ikiwa na kilometa 1,330 za lami. Kwa hiyo, unaweza ukaona katika watu waliotutawala katika miaka 76, waliweza kutengeneza kilometa 1,330 tu.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 50 iliyotoka, Tanzania ikawa imetengeneza karibu kilometa 7,500. Katika Awamu hii ya nne chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kilometa ambazo zinatengenezwa ni zaidi ya kilometa 11,154. Zipo zilizokamilika na zipo nyingine ambazo ziko katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ni lazima tutambue kwamba hii ndiyo *challenge.* Nilijaribu kuangalia kwenye *website* kuona ni nchi ngapi ambazo angalau hata zimeweza kukamilisha kupata kuwa na kilometa za lami tu katika maeneo yao, nimekuta sisi Tanzania tuko mbele sana. Kwa mfano, Bangladesh, wana *network* ya kilometa 21,269 wana kilometa 1,063 tu za lamii. Benin wana *network* ya kilometa 16,000 wana kilometa 1,400 tu. Brazil wana *network* ya kilometa 1,580,964 wana kilometa 212,798 tu, kilometa 1,368,166 ni changarawe. Burundi wana kilometa 1,286, Cambodia wana kilometa 4,108 za lami peke yake, *DRC* pamoja na kwamba wana *network* ya kilometa 153,497 wana kilometa 2,794 tu za lami. *Cote D Ivoire* wana *network* ya kilometa 81,996 lakini wana kilometa 6,502 tu za lami.

Mheshimiwa Spika, Ethiopia wana kilomita 6,000, Gabon wana kilomita 1,000, Ghana wana kilomita 13,787 pamoja na kuwa na *network* ya 109,515. Kenya wana *network* ya 160,878, wana kilomita 11,189 za lami.

Mheshimiwa Spika, najaribu kujenga hoja ili kusudi hata Mbowe aendelee kutupongeza tu CCM kama ambavyo imekuwa kawaida yake. Namibia wana kilomita 6,000; Nigeria wana kilomita 28,000 pamoja na kwamba wana-*network* ya kilomita 193,230; Rwanda wana kilomita 1,209 na kadhalika.

Ukiangalia, kwa watu ambao wanataka wakacheki kwenye mtandao. Wakasome kwenye mtandao wa *https//www.cia.gow/librarypublication/the world fact book field 281.html* kwa ushahidi. Mtaangalia nchi nyingi, mtakuta hata nchi ya Japan ina barabara za changarawe. *(Makofi)*

Nilitaka niliweke hili ili Watanzania na Waheshimiwa Wabunge na hasa ambao wanazungumza kwamba tumetengeneza kilomita ndogo sana, wajue *challenge* kwamba Tanzania *we are better* katika dunia hii. Tumetengeneza mpaka sasa hivi kilomita 7,500 ambazo zinatengenezwa chini ya awamu ya nne, ni kilomita 11,154. Unaweza ukazungumza mahali popote toka hapa Dodoma nenda Iringa, kilomita 261, kuna makandarasi watatu wanajenga. Toka hapa Dodoma nenda Babati kule utakuta kuna makandarasi watano. Kuna wale wa Bonga - Mayamaya, Mayamaya kwenda mpaka zile kilomita 19 za kwenda Bonga mpaka Babati, yaani kila mahali.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukazungumza hata mpaka kwa Mheshimwia Mbowe kule kuna makandarasi. Kuna kilomita 12 kule na mikataba ilisainiwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbowe, wewe ni mtakatifu kwa sababu ulimpongeza Rais Jakaya Kikwete kwa kazi nzuri anazofanya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *count anywhere!* Sasa hivi ukitoka Songea, nenda mpaka Masasi kuna Shilingi bilioni 68 zimewekwa, kuna makandarasi watano wanafanya kazi. Zungumza kila sehemu ya Tanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kueleza kwamba tulitoka pabaya, tunaelekea pazuri. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wa pande zote, bila kujali itikadi za Vyama tuipitishe haraka sana hii bajeti ili kilomita 11,154 ambazo zimewekwa kwenye ilani ya uchaguzi ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jukumu hili la mtandao mkubwa wa barabara zinazojengwa kwa kiwango cha lami karibu katika kila sehemu ya nchi, ieleweke pia kwamba asilimia 99.3 ya mizigo yote inayosafirishwa katika nchi hii, inapita kwenye barabara. Asilimia 0.7 ndiyo inapita kwenye reli, ndiyo inapita kwenye maji, ndiyo inapita kwenye ndege. Kwa hiyo, sisi Wabunge wote kwa pamoja, bila kujali itikadi zetu za Vyama, sasa tujenge hoja; katika mipango mingine inayokuja na mimi ni Mbunge, tuweke fedha nyingi kwa ajili ya kuweka *investment* kwenye reli ili mizigo yetu iweze kusafirishwa kwa urahisi zaidi kwa sababu kusafirisha mizigo yote kwenye barabara saa nyingine ni *bad economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona nianze na hili lakini niseme na mengine kwa ujumla. Katika masuala ya barabara limezungumziwa suala la uzito wa mizigo. Kwanza nataka kulithibitishia Bunge hapa kwamba hakuna mtu anayevunja Sheria namba 30 ya mwaka 1973 inayohusu uzito. Kinachotakiwa, wote tutekeleze Sheria. Ndiyo maana hata ukienda sasa hivi, utakuta magari bado yanapimwa, mizani bado ipo na hatua zinachukuliwa. Lakini labda nieleze tu kwa suala la jumla kwamba katika nchi zote duniani ambazo zinasimamia barabara zake kama ambavyo na sisi tunavyofanya kazi, suala la mizani limekuwa likizingatiwa.

Tanzania kwa mfano tuna mizani 28, Ghana wana mizani 14 wakati *network* yao ni kilomita 13,367, sisi ni kilomita 35,000 zinazohudumiwa na *TANROAD*. *South Africa* wana mizani 25 wakati *network* ni 16,000; Calfornia wana mizani 60; Florida wana mizani 21; *North* Carolina mizani 8; Kenya mizani 13, na ile *portable* minane; *England* wana mizani zaidi ya 47; *Scotland* mizani 21; Wales mizani 23 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zote duniani, jukumu la kulinda usalama wa barabara limekuwa likizingatiwa na hata sisi Tanzania tumekuwa tukizingatia suala la kusimamia uzito wa barabara.

Kwa hiyo, pasitokee mtu akaanza kuchonganisha hivi; tulizuiliwa, tulifanywa nini. Hakuna cha kuzuiliwa, wote tunafanya kazi hiyo na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ni *supporter* mzuri sana wa kusimamia Sheria. Hicho ndicho tumekuwa tukikifanya. Kwa hiyo, pasitokee watu wa kuanza kutuchonganisha hivi kwa masuala ambayo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamezungumziwa juu ya suala la *traffic jam* katika Jiji la Dar es Salaam.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mkaangalie, katika Miji 10 duniani ambayo *traffic jams all the days* ambayo *the ten worst traffic cities in the World,* kuna Millan Italy, kuna *Detroit Michigan USA*, kuna *London* Uingereza, kuna Brussels Belgium na wanasema hivi, *is the evil traffic jam around the global.* Nendeni mkasome kwenye mitandao. Kuna San Fransisco Calfornia, USA; kuna Paris, Ufaransa; kuna Dallas, kuna Los Angles, kuna Rotterdam Netherlands, haimo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nazungumza haya *with fact.* Ukienda katika Miji ambayo ni *five traffic congested cities in Africa* wanazungumzia Joharnesburg, kuna Nairobi, kuna Lagos, kuna Accra, kuna Cairo. Dar es Salaam haimo hata katika zile tano. Lakini kwa kutambua suala hili ni *global* na kwa kutambua kwamba Miji yetu imekuwa ikikua siku hadi siku, ndiyo maana Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi tumeanza kuchukua hatua za kupunguza misongamano katika Majiji yetu. Dar es Salaam kwa mfano kuna zaidi ya kilomita 109 ambazo zinashughulikiwa ambazo kwa bahati nzuri nimezifafanua vizuri katika hotuba yangu, nisingependa kuzirudia hapa.

Katika Mikoa mingine ambayo pia nayo barabara zimeanza kupata msongamano, kwa mfano, Dodoma na maeneo mengine, hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa katika kuhakikisha kwamba suala la misongamano katika Jiji letu zinatatuliwa. Nisingependa kuzirudia hizi zote kwa sababu nilieleza kikamilifu katika hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumziwa kwa ujumla na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu barabara ya Ndundu somanga. Barabara ya Ndundu - Somanga yenye jumla ya kilomita 60, nataka niwaeleze na ninawaeleza kwa dhati kabisa na ukweli kabisa na wananchi wa Mtwara wote wasikie, Serikali ina nia kubwa sana ya kuhakikisha kile kipande cha kilomita kumi kinakamilika. Ni Serikali hii iliyoanza kujenga barabara hii yote kwa kilomita 504.

Bahati nzuri nakumbuka wakati tukisimamia hii barabara tulianza na daraja la Mkapa likakamilika. Daraja hili ni refu kuliko madara yote katika Afrika Mashariki na Kati. Tukaenda Nangurukuru Mwemkulu, kilomita 95 na tulitengeneza kwa Tanzania *mode of standards* ambayo ni *design and construct method,* kilomita 95 zikajengwa kwa fedha zote ambazo zilitolewa na Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukaingia Mbwemkulu – Mingoyo, kilomita 95, nazo zimekamilika na Mkandarasi aliyetengeneza pale ni Karafi. Baada ya hapo, tukatengeneza Somanga – Matandu kilomita 35 kwa fedha za ndani, nayo ikakamilika ikawa imebaki hii sehemu sasa ya Ndundu – Somanga. Palitangazwa tenda chini ya ufadhili wa *Kuwait Fund,* Mkandarasi akapewa kazi ya kuanza kuifanya kazi ile. Akafanya *mobilization* yake katika kipindi alichopewa cha miezi sita, akaanza kufanya kazi. Alipoanza kufanya kazi, tatizo la kwanza ambalo tulianza kulipata; nami nataka niwaeleze vizuri na kwa ukweli kabisa, kwa sababu msema kweli ni mpenzi wa Mungu.

Mheshimiwa Spika, Kuwait ambao walikuwa wamepanga kuufadhili ule mradi hawakutoa fedha. Wamekaa kwa zaidi ya miaka minne hawajatoa fedha. Baadaye mazungumzo yakaendelea, wakawa wameamua sasa kuanza kutoa fedha kidogo kidogo. Fedha zote zilizokuwa zikitolewa katika mradi ule ikabidi Serikali iwe inatoia fedha zote asilimia mia moja. Wakati kazi zile zikiendelea, yule mkandarasi ambaye ndiye alikuwa *owner* ya Kampuni ya Karafi, akafariki dunia. Nyinyi wote Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, mnafahamu madhara ya kufiwa. Unaweza ukafiwa ulikuwa na nyumba umebakiza kuweka milango tu, watoto wakashindwa kuweka hata milango.

Kandarasi huyu Karafi alipofariki, ile Kampuni ikatetereka, *actually* ikafilisika ikawa *destabilized.* Tulipokuwa tukijaribu kutoa fedha, zile fedha zinapitia kwenye mkono mwingine kwa sababu zilikuwa zinatumika kulipa madeni mengine akashindwa ku-*perform* pale katika kazi. Tukambana, wakati huo alikuwa amejaribu kutafuta hata *guarantee* ya Benki akaikosa.

Tumekaa katika hiyo hati hati na baadaye tukaenda kule tukaona tunaweza tukatumia njia mbili; njia ya kwanza ilikuwa ni kumfukuza Mkandarasi. Nami kufukuza, tena huwa nashangilia; lakini kwa yule kwa sababu alikuwa amekufa, nikaona sasa nikimfukuza na amefiwa na Kampuni yenyewe, nitafanya dhambi kwa Mungu. Huruma ya ubinadamu na mimi

ikaja, tukaona ngoja tumvumilie ili kusudi ajitengeneze vizuri, matanga yake yaishe aendelee kutengeneza ile barabara. Amejikongoja, akamaliza karibu kilomita 50, madaraja yote akamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na hiyo *process,* tukamwomba *guarantee;* hili nazungumza kwa ukweli kabisa! Nikamwomba *guarantee* ya Benki ili kusudi kila anapo-*produce certificate* yake alipwe. Hakupa *guarantee* kwenye Benki yoyote. Alikuwa anatudai Shilingi bilioni 5.5, ikabidi kwa sababu ni mtu ameingia kwenye matatizo na amebakiza kipande kidogo, tukamwambia sasa hela yako ya *guarantee* ni lazima ukatwe. Ilikuwa ni Shilingi bilioni 4.08 akalipwa Shilingi bilioni 1.5 ili kusudi aweze kujisogeza na akaweka *sub-contractors* kwa sababu yeye ameshafilisika.

Mheshimiwa Mama Anna Abdallah anafahamu maana ya kuweka *sub-contractors.* Kwa sababu hata *contractor* wa daraja la Mkapa walifilisika, tukaweka *sub-contractors* ndiyo wakamaliza lile daraja. Wakati tukifanya hizo *process, Consultant* ambaye ni Kampuni ya Michael Pattman ya Uingereza pamoja na *ECG Engineering of* Kuwait aliyekuwa *Director* wa pale, Ndugu Andrew Handson, *Project Director,* akafa. Nataka niwaeleze *the fact!* Baada ya kufa ambaye ndiye msimamizi wa mradi, tukawa tumekosa *Consultant and Engineer* wa kuweza kuusimamia ule mradi.

Mheshimiwa Spika, mtu akishakufa huwezi ukasema nakufukuza kwa sababu alikufa *Director.* Tulivumilia, tukasema hii ni mipango ya Mungu. Wakataka kukimbia ile *site,* tukazungumza nao, wameleta mtu mwingine. Wakaanza kujipanga. Walipokuwa wakijipanga, tumeendelea kuzungumza na *Kuwait Fund,* bahati nzuri Mheshimiwa Rais mwenyewe alizungumza na watu wa *Kuwait Fund* fedha zikaanza kuja. Ninapozungumza hapa, kuna zaidi ya Shilingi bilioni 16 ambazo zimeletwa na *Kuwait fund* kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, walipoanza kuleta, mafuriko yakatokea, kandarasi hakuweza kwenda kutengeneza barabara wakati wa mafuriko, tukahangaikia mafuriko ya Dar es Salaam na maeneo mengine na siku tulipokuwa tumejiandaa kuzungukia Dar es Salaam pamoja na pale Kibiti, Helkopta ikaanguka, nami nilikuwemo! *(Kicheko/Minong'ono)*

Nataka niwaeleze ukweli! Ikabidi nimtume Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ajili ya kwenda kushughulikia masuala ya kukomboa barabara ile. Amekaa kule siku tano! Wananchi wa Kusini ni mashahidi.

Sitaki nieleze haya yote, lakini nataka kuwaeleza ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, barabara hii tutaimaliza. Naomba mnisikilize; tumepanga mkakati, yule kandarasi kwa kushirikiana na *sub-contractors* waliopo pale, *actually* tumeshateua *Engineer* wa Wizara ya Ujenzi, atakwenda pale, atakaa masaa yote, Mkandarasi yule anaponunua lami, tunalipa hela; akileta greda, mafuta tunaleta hela; nataka kuwahakikishia, haiwezi ikazidi zaidi ya miezi miwili barabara hii itakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza kilometa nyingi katika nchi hii, mimi Magufuli siwezi nikashindwa kilomita saba. Kilomita saba Serikali haiwezi ikashindwa! Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, msizuie hela, mturuhusu na hizi tulizozipanga katika Serikali zitakwenda kumalizia hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya mafuriko yametokea katika nchi hii, zaidi ya Mikoa 14 ilipata matatizo. Palipotokea mafuriko Dar es Salaam, njia zote tatu zilikuwa zimeshajifunga, ilikuwa imebaki baada ya siku tatu, siku nne Dar es Salaam waanze kulia njaa, lakini Mikoa yote

ya Tanzania ianze kukosa mafuta, na nchi nyingine ambazo ni *land locked countries* saba kwa sababu mafuta yote yanatoka Kigamboni.

Napenda niwashukuru wahandisi kupitia *TANROAD* wakiongozwa na Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa jinsi walivyokesha kwa siku tatu wakihangaika kufungua hizi barabara na ndiyo maana pongezi mlizokuwa mkizitoa kwa Wizara, *actually* wao ndio wanastahili kupata pongezi zaidi kwa sababu walifanya kazi za ziada na wakawa wanalala kwenye Vituo huko. Mimi nililala *of course* sehemu fulani fulani, kwa mfano pale nililala pale Dumila, lakini ni kwa sababu nilikuwa na Watendaji wazuri ambao wameweza kuisimamia ile kazi.

Mheshimiwa Spika, barabara zimezinduliwa lakini kuna eneo moja la Ifakara, pale maji yalijaa zaidi ya kilomita 10. Tumeanza kutengeneza tuta, lakini nataka kuwahakikishia Wabunge wote maeneo yote ambayo yaliathirika sana na mvua, tutayaridisha katika hali yake ya kawaida kwa sababu katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha za kutosha za kuhakikisha yale maeneo yote yanarudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nina muda wangu mfupi, lakini niende kwa haraka haraka sasa angalau kujibu hata hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao ni zaidi ya 35 waliochangia hapa na wengine wamechangia kwa maandishi, inawezekana muda hautatosha sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu imetupongeza, tunazingatia ushauri wao na suala la makandarasi linashughulikiwa na Serikali. Lakini nieleze kitu kimoja, Mkandarasi anapopewa kazi, huwezi ukamlipa fedha pale. Anachotakiwa kulipwa ni *advance payment* peke yake. Atakuwa analipwa kadiri anapo-*produce* kazi; zinaitwa *IPC*.

Kwa hiyo, kwa mkandarasi yeyote, madeni ni kitu cha kawaida. Mkandarasi anapo-*produce certificate* ndio analipwa. Lakini ielewe pia, hata Mkandarasi anapomaliza kazi halipwi fedha zote ni lazima akae kati ya mwaka mmoja na miaka mitatu, fedha zake zile zimewekwa kwa ajili ya kuangalia uharibifu wa barabara utakaojitokeza ndani ya kipindi kile cha mkataba. Kwa hiyo, tunapozungumzia madeni ya makandarasi, haina maana kwamba Serikali sasa imeshindwa kulipa haya madeni, kwa sababu Serikali ina uwezo wa kulipa haya madeni. *(Makofi)*

Hata hivyo, hata Mkandarasi anapo-*produce Certificate,* kwanza ni lazima ile *Certificate* ipitiwe na kupitishwa na *Consultant* anayemsimamia kazi. Ikishatoka kule, inapitishwa na *TANROAD*, inakuja Wizarani inapitishwa na Wizara ya Fedha. Huwa tuna kipindi cha miezi 56, hii ndiyo kawaida ya mikataba.

Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia kuhusu uharibifu wa barabara, barabara ina *life span* yake. Ni kama tunavyokunywa madawa ya hospitali, unaambiwa *expiring date* ni siku fulani. Barabara ambazo zimejengwa kwa *surface dressing, expiring time* yake ni kati ya miaka 15 hadi 20. Kwa barabara ambazo zinajengwa kwa *asphalt concrete, expiring time* yake inaweza ikafika mpaka miaka 30 ambazo ni *very expensive,* wanajenga Wamarekani. Barabara zetu ni *surface dressing.*

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ilianza kufanyiwa *design* na kujengwa kwenye miaka 1968 ikakamilika kwenye miaka ya 1972. Barabara ya kutoka Morogoro kuja Dodoma, imekamilika kwenye miaka ya 1983; barabara ya Tanzam *Highway,* imekamilika kwenye miaka ya 1972. Ukijumulisha *life span* ya miaka ile ni miaka 40. Sasa miaka 40 huwezi ukaona barabara inatoboka ukasema ma-*engineer* hawa hawafai. Hawa wanajisikia vibaya sana hapa! *Combination* ya ma-*engineer* hawa nikiwataja, *they are really highly qualified. (Makofi)*

Kwa mfano, nimkitaja hapa Mwenyekiti wa *National Construction Council* ni Profesa Mhamila, ambaye ndiyo Mkuu wa Chuo cha Mandela University. *Chief Executive* wake alikuwa *Lecturer* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alipata *first class* Japan, Eng. Leonard. Mwenyekiti wa *Engineers Legislation Board, Profesa* Lema. *Nimwashe shingapi esaoshonkorentiani,* ndio yeye! Ni lugha ya kisukuma kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, najaribu kuzungumza hivi katika kuonyesha kwamba kufeli kwa barabara ni kutokana na *life span* yake. Kwa hiyo, mtu anapo-*compare* kwanini hii barabara haijapita, hii barabara mbona haijaharibika, tuangalie *life span* yake na ndiyo maana kuna fedha za *maintenance* ambazo tunahangaika nazo. Tungekuwa na uwezo, tungetengeneza barabara kila baada ya miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ndiyo maana kuna mizani na ndiyo maana kuna Sheria namba 30 ya mwaka 1973.

Lingine ni *traffic* inayopita kwenye magari haya. Katika *research* iliyofanyika kwenye mwaka 2010 *traffic* ya magari yanayopita kwa kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro ni zaidi ya magari 56,000 *per day.* Kwa sasa hivi inawezekana yatakuwa yameshafika hata 70,000 *per day.*

Katika *projection* ikifika mwaka 2018 kama hatutakuwa tumechukua hatua zozote hapa magari yataumana kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro bila *space.* Ndiyo maana Serikali kwa sasa hivi ina *involve PPP* kwa ajili ya kujenga barabara *six line* kwa njia ya *PPP*. Tunafanya hivi na tutafanya katika maeneo mengine mbalimbali, katika kuhakikisha kwamba misongamano na barabara zetu zinakuwa *secured* kwa kusafirisha magari mengi. *(Makofi)*

Sasa niende haraka haraka, najua nina dakika chache. Nilikuwa najaribu tu hiyo kama *preamble*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu imetoa ushauri mzuri, tumeuzingatia, imezungumzia pia Ndundu – Somanga, nimeshatoa maelezo yake. Napenda niseme kwa dhati kwamba ushauri wao tunauzingatia.

Kambi ya Upinzani wamezungumzia majukumu ya Wizara ya Ujenzi, wakazungumza mambo mengine kwamba Serikali inajikwaza wakati ni asilimia 21 tu. Nimetaja *data* hapa, najua kama atafanya *calculation* atajua ni asilimia ngapi. Lakini Serikali haijikwezi, inafanya yanayotakiwa kufanywa na tunapozungumza wananchi wa Tanzania wanafahamu kwa sababu barabara hizo wanazipitia na makandarasi wanawaona katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Ila wamezungumzia mambo ya *CCT Camera* na mengine mengi, lakini mwishoni Mheshimiwa Mkosamali alisema atapenda sana kushirikiana na mimi, nami napongeza kwa hilo kwa sababu ukimwona kijana ambaye ameingia kwenye siasa anapenda kushirikiana na Mbunge wa CCM, ni mambo mazuri yanakuja. Mimi napenda kukuthibitishia Mheshimiwa Mkosamali tutaendelea kushirikiana kama ambavyo tumekuwa tukishirikiana ili ujifunze zaidi na kuielewa zaidi Wizara jinsi inavyoenda. *(Makofi)*

Pia umezungumzia kuhusu barabara ya Kigoma na hilo ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Machali, nataka kukuhakikishia, tulishasaini mikataba kwa kilomita 50 na upande ule wa Nyakanazi kwenda Kibondo kilomita 50. Ukishasaini kandarasi, moja kwa moja ni kwenda kuripoti. Kwa taarifa tulizozipata, makandarasi wale wameshakwenda kuji-*introduce* kwa viongozi kwa ajili ya kuanza *mobilization* na watajenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Kwenye hilo hilo wamekuwa wakizungumza, tumekuwa tukipanga fedha kila mwaka kila mwaka; barabara hutengenezi kama chapati au maandazi unayachemsha tu unayaweka mle. Barabara *you have to start with feasibility study,* unakwenda *detail design,* ndipo unakwenda kwenye *construction*.

Kwa hiyo, hata ile *feasibility study* na *detail design* na *construction*, ile ni kazi! Kwa hiyo, katika kipindi chote cha nyuma tumeanza na *feasibility study* tukamaliza, tukaingia na *detail design,* baadaye sasa tumeingia kwenye *construction.*

Nataka kuwathibitishia wananchi wa Kigoma, Kigoma tunaipenda; ndiyo maana hata barabara za Kigoma zimekamilika; ndiyo maana barabara ya kutoka Mwandiga - Manyovu imekamilika kilomita 60 wakati upande wa Burundi hakuna lami;ndiyo maana barabara ya Kigoma - Uvinza, kilomita 76.6 imekamilika; ndiyo maana hata daraja la Kikwete na mabilioni ya fedha limekamilika. Kwa hiyo, hii barabara nayo tutaikamilisha. *(Makofi)*

Naomba mtuamini kwa sababu tuna nia hiyo. Hata zile fedha za mwaka 2013 ambazo zilitengwa, kwa sababu bajeti hii haijaisha, zile nazo zinahusika kwa ajili ya kulipa *advance payment* kwa Mkandarasi. Kwa hiyo, ni kama tumeongeza kingine ili kusudi barabara hizi ziweze kukamilika mapema.

Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mbunge wa Mufindi, ametoa pongezi nyingi na sisi tunampongeza, nami namshukuru kwa pongezi kwa barabara zake. Ameelezea mambo mengi, kwa ujumla ushauri wake wote tumeupokea.

Mheshimiwa Jafo amezungumzia kuhusu *concern* ya barabara yake ya Kisarawe kwenda Mwanarumango - Mikumburu, anasema barabara hii ni vizuri ikatengenezwa kwa kiwango cha lami. Napenda kukuhakikishia kabisa, zile barabara ambazo umezizungumza Mheshimiwa Jafo, nazungumza na *Hansards* inarekodi, tutazitangaza kwa ajili ya kuzitengeneza kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Madabida amenipa pole, amezungumzia juu ya barabara ya *Salendar Bridge*. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Madabida, *Salenda Bridge* itatengenezwa na bahati nzuri wale waliotengeneza daraja la Kikwete ambalo ni refu zaidi, lina zaidi ya kilomita 2.75, ndiyo wamejitokeza tena ambao ni *South Korea* kwa ajili ya kutengeneza daraja la *Salenda Bridge***.**

Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia hilo daraja nalo litatengenezwa. Vile vile Mheshimiwa Maabida amezungumzia pia kuhusu barabara ya Ndundu-Somanga, nimeshaielezea. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Pamba ametoa pongezi, lakini akataka kuhakikishiwa kama kivuko cha *Pangani one* kipo. Kwenye bajeti ya mwaka huu, tumetenga fedha kwa ajili ya kivuko *Pangani one* ili vishirikiane na Pangani *two*.

Mheshimiwa Deo Sanga, ametoa pongezi, amezungumzia juu ya barabara zake, lakini amezungumzia pia matatizo katika mzani wa Makambako. Tunaushughulikia, tutauhamisha mahali hapo. Lakini kwa sasa hivi wakati tunadhibiti hili suala tutaendelea kukaa pale kwa ajili ya kushughulikia. Tatizo la foleni saa nyingine ni kutokana na madereva, huwa wanasubiriana njiani na wanafika pale wana-*jam* wenyewe, halafu baadaye siku nyingine panakuwa hakuna foleni. Lakini haya yote tunayashughulikia.

Mheshimiwa Susan Kiwanga, alizungumzia barabara za Mkoa wa Morogoro. Nimemsikia Mheshimiwa. Nataka kumhakikishia kwamba barabara hizi kama nilivyozungumza kwenye

hotuba yetu, tunazishughulikia. Bahati nzuri *USAID*, pamoja na *European Union* wamejitolea kwa ajili ya kuhakikisha barabara hii inafunguliwa. Haitafunguliwa tu, inataka ifunguliwe mpaka Songea, kwa sababu barabara hii ni muhimu katika maendeleo ya wanachi wa Morogoro.

Kwa sasa hivi, tatizo hili la kivuko na mvua; mvua hazikuletwa na Mheshimiwa Dkt. Kikwete, hazikuletwa na Mheshimiwa Magufuli, wala hazikuletwa na CCM. Tusubiri ziiishe, baadaye tutarudi kwenye kazi. Ndiyo maana hata yule mtengenezaji wa daraja, aliona akiliacha lile daraja la *temporary,* lingepotea. Akaona ali-*withdraw* ili baadaye kazi zianze kuwekwa, kwa sababu kuna Shilingi bilioni 53 zimetengwa pale.

Vile vile kumezungumziwa kuhusu Halmashauri kufungua *account* kwa ajili ya fedha za *USAID*. Mimi hilo sina tatizo. Hilo ni suala la Halmashauri, wakiamua, *we have no problem.*

Mheshimiwa Kimwanga amezungumzia juu ya msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, nimeshaeleza sana. Kwa sababu magari yote ya *turns goods* yanatoka kwenye *destination* moja ya Bandari, msongamano hatuwezi tukaukwepa kwa sasa hivi. Lakini hatua mbalimbali zinachukuliwa, ikiwemo hatua za kufufua reli, Mheshimiwa Mwakyembe atakuja aelezee. Masuala ya msongamano yako kwenye hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba yanatatuliwa. Ndiyo maana tunanunua kivuko, tunafanya nini; haya yote, tumechukua barabara zaidi ya kilomita 86, tukaziweka kwenye mpango wa *TANROAD.* Kwa hiyo, haya yote yatashughulikiwa.

Tulishauriwa vile vile kwamba Barabara ya Nyakato - Kayenze iliyochongwa, nayo sasa ingefaa ichukuliwe ijengwe kwa kiwango cha lami. Dada yangu Mheshimiwa Kimwanga, nimekusikia, ngoja tutakaa na wataalam wangu tuangalie. Lakini tulichukua barabara ya Nyakato kwenda kule, lakini hili nalo tutaangalia. *Problem* kubwa ya barabara hii, watu wamejenga mpaka kwenye *road reserve*. Kwa hiyo, tutakapoamua kuichukua hii, wananchi wa pale wajiandae kubomoa nyumba zao na ukatusaidie.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, hata zile fedha tunazozituma za *Road Fund* katika Halmashauri ile, ile Halmashauri ya Ilemela, waache kuwa wanabishana; mara *Mayor*, mara nani; watatue matatizo yao ili kusudi fedha zinazotumwa za *Road Fund* ziweze kushughulika kwa ajili ya kutengeneza barabara za Halmashauri.

Mheshimiwa Machali, amesema pongezi, anasema barabara ile ya Kigoma kwenda Nyakanazi, nimeshakueleza mdogo wangu, barabara ile tunaitengeneza. Usiwe na wasiwasi, nenda ukawaeleze wananchi wa Kigoma, kwamba Serikali ya CCM inatengeneza barabara ya kutoka Kigoma hadi Nyakanzi. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Machali amezungumzia juu ya *Rural Road Agency.* Kwa sababu zile barabara ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya, nafikiri ni ushauri mzuri sana. Inawezekana tukianzisha *Agency* kama ilivyo *TANROAD*, tutapunguza hata haya maneno ya kila Mbunge kuomba barabara za Halmashauri kurudi *TANROAD*. Mimi nafikiri, hiyo kwa mujibu wa sheria namba 30 ya mwaka 1997, wenzetu Serikali tutalijadili na tuone ni namna gani tunaweza tukaanzisha hiyo *Road Agency* kupita TAMISEMI.

Mheshimiwa Agness Hokororo, dada yangu, ametoa pongezi na amezungumzia kuhusu barabara ya Ndundu – Somanga. Nimeeleza kwa kirefu dada yangu Hokororo, naomba usitoe Shilingi, tuachie tuimalize hii barabara kwa sababu nimezungumza kwa dhati, na nimesema jua linawaka ili kusudi hili eneo nalo tulimalize, lakini matatizo ni kama nilivyoyazungumzia.

Barabara ya Masasi - Newala - Mtwara, tumeweka zaidi ya Shilingi bilioni 2.5 kwa mwaka huu. Kama yule *Consultant* anayefanya *design* anaweza akachelewa kazi, na nitazungumza na watu wangu baadaye, tunaweza tukaamua, tujenge ile barabara kwa *design and construct method,* kutoka Masasi – Newala – Mtwara. Ila nitaomba sasa wananchi wa eneo hili na Mheshimiwa Hokororo na Waheshimiwa wengine, Mheshimiwa Njwayo na wengine, mnieleze nianzie wapi? Kwa sababu hilo nalo linaweza likawa ni tatizo. Mkae, mtuambie kwamba tuanzie wapi kutangaza, sisi tutaanza kufanya kazi kwa sababu katika bajeti ya mwaka huu tumeweka fedha.

Mheshimiwa Spika, barabara za Lupaso kwa Mhehsimiwa Mkapa na kadhalika, haya yote tutayaangalia kwa sababu ndiyo jukumu letu.

Mheshimiwa Ezekiel Maige amezungumzia pongezi, ameoa ushauri wa suala la vipaumbele kwa baadhi ya barabara, tumeuzingatia ushauri wake, tutauangalia, lakini barabara zinaharibika kwa sababu ya rushwa; sababu ni nyingi, hatuwezi tuka-*generalize*, lakini katika rushwa za barabarani, nimeshaeleza zaidi ya wafanyakazi 400 na kitu, tuliwafukuza kazi waliyokuwa wanafanya kwenye mizani.

Tushirikiane wote katika kuhakikisha kwamba rushwa haipo, uzidishaji uzito haupo, na masuala mengine ya mtambuka.

Mheshimiwa Mhita ametoa pole kwa ajili ya ajali ya ajali, ametoa shukurani kwa barabara ya lami Kondoa; anaomba barabara ya Mayamaya ikamilike na ametoa shukrani kwa barabara ya kutoka Mayamaya - Bonga zaidi ya kilomita 188.8. Nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa maeneo hayo, barabara hizo zinajengwa, na Wakandarasi wako kule, na mfadhili ni *African Development Bank.*

Mhehsimiwa Shah, amezungumizia kuhusu eneo lake. Kwanza, nianze kwa kumpa pole sana Mheshimiwa Shah kwa msiba wa mama yake, na roho ya Marehemu ipumzike kwa amani. Pia amezungumzia suala la mvua zilizoathiri maeneo hayo, amezungumzia malipo ya fidia kwa watu walio ndani ya *road reserve,* tatizo la shimo kwenye uwanja, anaomba kivuko kwa ajili ya Mafia – Kilindoni na Nyamsati. Sasa tutaangalia *distance* ya pale, kwa sababu kivuko nacho hakitakiwi kitembee *distance* ndefu.Haya yote uliyoyazungumza Mheshimiwa Shah, tunayachukua, tuyaangalie na wenzangu tuone namna ya kuyafanyia kazi. Vile vile umeomba tena baadhi ya watalaam wangu uende nao. Tutapanga hiyo safari ili hata wataalam wangu niweze kuwatuma mwende nao kule. Ila tutapanga siku ambayo munaweza mkaenda kule tukaangalie uharibifu katika Wilaya yako.

Mheshimiwa Zungu ametoa pongezi nyingi na ameunga mkono na ametoa pongezi kwa makandarasi wazalendo, amesema miundombinu ya Dar es Salaam ikifa, nchi itapata shida. Nami nakubaliana na wewe kwa sababu tuliyaona ilipokufa tu siku tatu. Tunashukuru hiyo miundombinu ilifufuka baada ya siku tatu. *Otherwise* nchi ingepata shida.

Vile vile umezungumza pia, kwamba kwa Dar es Salaam ni vizuri pawepo na *special fund* ili iweze kutengeneza barabara zake zote ambazo ni muhimu na ambazo zinaweza zikatatua suala la msongamano. Kwa sababu hili ni suala mtambuka, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesikia, viongozi wa Serikali tumesikia, nasema kwa dhati kabisa kwamba ushauri ule ni mzuri. Hata barabara yako ya Uhuru, tutaishughulikia na nataka kukuhakikishia kwamba tutaimaliza, pamoja na zile kilomita 0.5 ulizoomba kwa maandishi, zile zote tutashughulikia.

Napenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam, tunafanya juhudi kubwa katika kuhakikisha kwamba tunarudishae mawasiliano na kuhakikisha

tunatengeneza barabara nyingi, lakini saa nyingine uwezo hutufikia *limit*, kwa sababu kila mahali kuna matatizo. Unahangaikia barabara hii, unasikia pametokea ugonjwa wa *dengue* na kadhalika. Kwa hiyo, hizi ndizo changamoto katika utawala na hizi ndizo changamoto katika Uongozi na katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mipata ametoa pongezi, anasema barabara ya Sumbawanga – Kizi – Kibaoni: Je, zitakamilika lini? Mheshimiwa, napenda kukuhakikishia barabara hizi tutaendelea kuzitengeneza na ndiyo maana katika bajeti hii tumezitengea fedha ili barabara hizo nazo ziweze kukamilika, kulingana na ahadi za Mheshimiwa na ahadi zilizotolewa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mipata amezungumzia pia ahadi za Mheshimiwa Rais kuhusu barabara ambazo ziko chini ya Halmashauri. Juzi juzi tulijibu swali hapa. Mheshimiwa Mipata, tutaliangalia hili tujue ni namna gani tunaweza tukazishughulikia hizi barabara angalau hata ikiwezekana tuzitengeneze kwa kutimia fedha za *Road Fund* ili ahadi ya Rais iweze kukamilika. *(Makofi)*

Wanasema Mipatwa? Unajua majina ya Wafipa saa nyingine ni magumu sana, nafuu angeitwa Magufuli nisingepata shida, watani zagu hawa, lakini basi ni Mipata. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mdee, amezungumzia kuhusu barabara za vijini, uangaliwe utaratibu huo, amezungumzia kuhusu *concern* ya barabara zake, ambazo anasema angeomba sasa ziweze kutengenezwa kwa sababu tumezizungumza siku nyingi.

Nataka kumweleza Mheshimiwa Mdee kwamba hizi barabara tumeshasaini mikataba. Zote, hata kwa Mheshimiwa Mnyika na barabara zote zile za kupunguza msongamano. Ukishasaini mkataba, ile ni *commitment,* na mikataba inajulikana. Nataka kukuhakikishia, baada ya kusaini tu mikataba, Wakandarasi wanatakiwa waanze kufanya *mobilization* kwenye maeneo husika kwa ajili ya kutengeneza barabara. Barabara hizo ni za Watanzania wote, hata mimi nazipita, hata wengine wanazipita. Kwa hiyo, ni muhimu kwa ajili maendeleo ya Dar es Salaam na kwa Taifa kwa ujumla.

Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia kwamba barabara hizo zitatengenezwa. Miaka ya nyuma tumekuwa tukitenga fedha hizo kwa ajili ya *detail design* na *feasibility study,* sasa umeshafika wakati wake kwa ajili ya kuanza kuzijenga kwa kiwango cha lami. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam, kwa barabara hizi ambazo tumeweka mikataba, ambazo nyingi zilikuwa ni za Halmashauri za Wilaya, tuwashauri wananchi wasiendelee kujenga kwenye *road reserve* kwa sababu wataanza kukwamishwa maendeleo ya ujenzi wa barabara hizi ambazo ni muhimu katika kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Halima Mdee pia amezungumzia suala la *DARTS* Jangwani pale, maji yanajaa. Mvua za mwaka huu zilikuwa siyo za kawaida. Hili pia tumeliweka kwenye *consideration.*

Kambi ya Upinzani pia walizungumza, kwa nini *DARTS* mliomba tena hela nyingine za *World Bank?* Mimi nilifikiri Mheshimiwa Mkosamali ungeipongeza Serikali kwa kuomba hela nyingine kwa ajili ya mradi wa *DARTS*, kwa sababu ule mradi uko kwenye *phase.*

*Phase* ya kwanza ni kilometa 21, *phase* ya pili itahusisha Mwenge kwenda Tegeta; *phase* ya tatu itahusisha barabara ya kwenda *Kilwa Road* na kadhalika. Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali itaendelea kuwaomba wafadhili na tunawashukuru sana wafadhili wa *World Bank* ambao siku zote wamekuwa mstari wa mbele katika kusaidia mradi huu ambao pia unasaidia kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Haroub Shamis ametoa shukurani na kusema kwamba Dar es Salaam ndiyo uso wa nchi. Nami nakubaliana naye, hataki kuamini kama Wizara haina wataalam; ina wataam, barabara ya *BIT* haina nafasi ya magari, hasa magari yanayoharibika. Magari yatakayopita mle ni yale ambayo hayataki kuharibika. Tumechoka kukaa, kuletewa mikweche ya kuharibika barabarani na kuziba.

Kwa hiyo, tunawaomba wasafirishaji wawe wanaleta magari ambayo hayaharibi hovyo na likiharibika linabebwa na *winch,* anapigwa *fine* ya Shilingi milioni moja na kadhalika kwa mujibu wa sheria namba 13 ya mwaka 2007. Kwa hiyo, tusiwaendekeze watu wenye magari yanayoharibika, wakae nayo mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, tulishauriwa kwamba hatua zichukuliwe kwa Wakandarasi na *Consultants;* tumekuwa tukichukua na tumekuwa tukifukuza. Mkandarasi yule wa Kusini tulimfukuza akatupeleka Mahakamani tukamshinda, aka-*appeal* tukamshinda. Kwa hiyo, tumekuwa tukichukua hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha amezungumzia pongezi kwa Wizara, na alizungumzia daraja la Mto Mombo. Mwaka 2013 tulitenga Shilingi bilioni mbili na mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni mbili. Tutaanza mwaka huu kulitengeneza lile daraja, kwani ni muhimu kwa kuunga Mikoa hiyo yote miwili, nataka kukuhakikishia.

Amezungumzia pia barabara ya Nyakatundu Starike, Tendo, Munze na maeneo mengine. Ushauri wako wote tumeupokea, tutauzingatia katika kuhakikisha barabara hizo zinatengenezwa.

Mheshimiwa Highness Kiwia amezungumiza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ndiyo ameanza nao na baadaye akaja na msongamano wa Arusha na baadaye akamalizia na msongamano wa Mwanza. Mimi nitajibu msongamano wa Mwanza kwa sababu yeye anatoka Mwanza.

Nataka kumhakikishia kwamba tumeendelea kuushughulikia msongamano wa Mwanza na ndiyo maana tumejenga pale Daraja la Mabatini. Tutajenga daraja lingine la wapita kwa miguu pale kwenye barabara ya kwenda kwenye uwanja wa CCM. Napo tutajenga daraja la waenda kwa miguu kwa ajili ya kupunguza msongamano. Lakini nataka kumhakikishia kuwa katika Nyamagana tumekuwa tukipanga pia fedha za *Road Fund* na mwaka huu nafikiri kuna Shilingi bilioni 1.09 ambazo zinaweza zikatumika kwa ajili ya kutengeneza baadhi ya barabara zilizo chini ya Halmashauri yake.

Mheshimiwa Deo Filikunjombe ametoa pongezi, lakini na mimi nichukue nafasi hii kumpa pole sana kwa kifo cha Marehemu Baba yake Mzee Filikunjombe, Roho ya Marehemu ipumzike kwa amani, lakini huko ndiko kukua. Namshukuru pia kwa pongezi zake nyingi, ametoa pongezi kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mama Tunu alivyokuwa anampelekea chakula Mzee wake. Ndiyo hivyo, Wanyamwezi huwa wana huruma sana na ndiyo maana Mzee Pinda akaenda akaoa Mnyamwezi kwa sababu ni watu wenye huruma na upendo mkubwa hasa kwa wagonjwa. Kwa hiyo, yale aliyoyazungumza yote tumeyazingatia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Njwayo nimeshaijibu. Mheshimiwa Mchungaji Natse ametoa shukurani, nami namshukuru sana; amezungumzia kuhusu barabara kwenye Mji wake ule. Tutaliangalia ili tuangalie namna ya kulitengeneza kwa kiwango cha lami ile sehemu kwa kutumia fedha za *Road Fund*.

Mheshimiwa Said Mtangi, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe amezungumzia *concern* ya sehemu yake na hasa daraja la Kavuu. Nimeyapokea maelezo yako haya tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mnyika amezungia kuhusu barabara hizo ambazo tumezirudiarudia, ndiyo utaratibu. Kuna *feasibility study*, kuna *detail design* na *construction*. Sasa ni *construction,* amini barabara zile zinajengwa kwa kiwango cha lami. Ukishasaini, Mkandarasi anatakiwa kuripoti kwenye *site*. Kwa hiyo, pitisha tu hizi hela, sisi tumfuatilie Mkandarasi akaripoti kwenye *site* ili tupite kule tunajidai, hata na mimi nitapita mle, nitasema CCM oyee! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mikidadi ametoa pongezi, anasema barabara ya Liwale – Kibiti – Lindi kuhusu migogoro ya barabara; Barabara ya kupandishwa; amezungumzia *concern* ya barabara nyingi; naambiwa nimebakiza dakika mbili hivi.

Mheshimiwa Nimrod Mkono amezungumzia barabara yake, kuna Kandarasi ya *JVC* ambayo imeanza kazi pale kwa Kilometa kumi na katika bajeti ya mwaka huu tumeweka fedha. Mheshimiwa Nimrod Mkono naomba usitoe Shilingi, Mkandarasi yupo na barabara yote mpaka Mto wa Mbu tumeweka zaidi ya Shilingi bilioni tisa.

Naomba utuelewe na barabara ile itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Pia, hata barabara nyingine umesema Musoma hakuna hata lami moja Mzee wangu; zipo! Musoma kuja mpaka wa Simiyu ni lami. Tunatengeneza sasa hivi kwenda Kisorya. Mheshimiwa Nimrod Mkono naomba hiyo Shilingi usiitoe ili kusudi barabara zile zitengenezwe.

Mheshimiwa Paul Lwanji amezungumzia kuhusu barabara zake na barabara inayounganisha kule; na Mheshimiwa Mtanda amezungumzia.

Mheshimiwa Dkt. Mponda amezungumzia *concern* ya daraja lile; Mheshimiwa Bungala naye amezungumzia kuhusu eneo lake lile na nimeshalielezea; Mheshimiwa Mtutura ameelezea na Mheshimiwa Katagira amezungumzia kuhusu barabara za kwenda mpaka Lwamnunka na Mheshimiwa Gregory Teu amezungumzia barabara za Mpwapwa. Nakuhakikishia zile barabara za Mpwapwa zitajengwa. Tumeshaanza kutengeneza kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye amekuwa ananisadia sana. Nawashukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wenyeviti na Wahandisi wote ambao siku zote wamekuwa wakijitoa katika kazi zao kwa ajili ya miradi hii ya barabara.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na nasema kwa dhati kabisa kutoka moyoni mwangu, michango yao ni mizuri, tumeizingatia, tutaifanyia kazi, sisi ni watumishi wenu.

Tutaendelea kufanya haya yatakayowezekana, lakini nataka kuwahakikishia kwamba michango yao hatukuidharau na yote tutaitolea majibu, kabla ya Bunge hili tutawapa taarifa zote kuhusu Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na wengine hata kwa kusema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, kwa sababu muda ni mdogo, ningependa nitoe maelezo hata kwa masaa matatu, basi niwaruhusu Waheshimiwa Wabunge watafakari Roho ya Bwana iwaguse, waamue kwa ukamilifu kwa wema kwa kuangalia changamoto tulizonazo na maslahi ya Taifa hili katika kuhakikisha tunatengeneza barabara ili waweze kuunga mkono hoja niliyoitoa kuanzia jana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!(Makofi)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Hatua inayofuata Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Bado naomba wito, anapokuja huyu mnakaa kimya. Unakuta wengine wananong'onezana, wengine wanaongea na wengine wanafanya nini, sivyo inavyokuwa. Kwa sababu tusipokuwa na utaratibu ndani ya nyumba, basi tunakuwa hatuna utaratibu. Katibu!

**Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management … … … Tshs*. 2,926,467,347/=

**MWENYEKITI:** Sasa si ni mshahara wa Waziri hapo? Tuanze na Waziri Kivuli. Wewe unataka kugawana nini? Nimepata majina. Mheshimiwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nasimama kutaka kupata ufafanuzi na uhalisia wa bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Naomba Waziri atuletee, hata kama siyo leo, lakini atuletee orodha, kwa sababu hapa kuna miradi mingi nimeeleza hapa, zaidi ya Kilometa 11,000 ziko kwenye Ujenzi.

Sasa kama hii bajeti ni ya uhalisia tupate ratiba, kilometa hizi 11,000 zitakamilika lini? Tusije tukawa tuko hapa tunajisifu kwamba awamu ya nne imeanzisha miradi mingi ambayo itakamilika miaka 20 ijayo.

Naomba watuambie kwa ratiba yao hii miradi ambayo wameanzisjha kila mahali ambayo mingine imetengewa Shilingi bilioni mbili, Shilingi bilioni moja, Shilingi bilioni tatu, itakamilika lini? Pia tuambiwe, kwa sababu Wizara hii ina deni la zaidi ya Shilingi bilioni 400. Ni fedha kiasi gani katika bajeti hii zinakwenda kulipa madeni, ili tujiridhishe kwamba kweli kuna kilometa hizi zinazosemwa zinakwenda kujengwa?

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Licha ya kwamba kuna hatua mbalimbali za ujenzi wa barabara, lakini kuna barabara nyingine zimekuwa zinaandikiwa na nimeeleza hata kwenye hotuba yangu kwamba ni ujenzi, siyo *feasibility study*.

Ujenzi utaAnza, lakini hauanzi. Sasa Waziri atueleze, kwa sera ya Wizara yake, hii miradi yote mingi sana, isije ikawa ni miradi ya kututumainisha tu hapa Wabunge tunapiga makofi. Ratiba zinakamilika lini hizi kilometa 11,000 isije ikawa kama ambavyo nimesema tunakuwa na miradi mingi, barabara inajengwa kwa miaka kumi, baada ya miaka 15 ameeleza hapa ndiyo *life span* ya barabara. Kule ilikoanzia ilishaisha, mnaendelea kumalizia huku. Kwa sababu inachukua miaka 10, au 15. Sasa tunataka uhalisia wa bajeti hii, na kama yuko tayari kutupa ratiba kamili ya ujenzi kwa kila barabara. Nisiporidhika nitatoa Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asipotoa hiyo ratiba leo hapa? Hapa haitoki. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Mkosamali kwa kueleza kwamba anataka ratiba ya miradi yote inayotekelezwa na

Serikali kuhusu barabara. Kwa sababu ameomba hiyo ratiba, nitampa Ilani ya Uchaguzi ya CCM akasome ukurasa wa 72 hadi 82 ambapo miradi yote ya barabara iliyomo kwenye kitabu humu hatua za ujenzi, hatua za *feasibility study* na hatua za *detail design* zimeorodheshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempenda Mheshimiwa Mkosamali kwa sababu anapenda kujua ratiba ya miradi inayotekelezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hongera sana Mheshimiwa Mkosamali, kwa sababu hicho ndicho nilitaka nimweleze. Bahati nzuri nilijua hili swali Mheshimiwa Mkosamali anaweza akauliza. Nimekuja na kitabu hapa nitakikabidhi kwako nimpe Mheshimiwa Mkosamali, akasome vizuri ukurasa wa 72 hadi wa 82 ataiona miradi yote inayotekelezwa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, amezungumza kuhusu madeni. Nilipokuwa nikitoa ufafanuzi hapa, nimeeleza kwa ukamirifu kabisa kwamba katika miradi ya barabara na kwa sababu miradi ya barabara inachukua miaka mingi, ipo inayochukua miaka miwili, ipo inayochukua miaka mitano, ipo inayochukua miaka sita.

Ni vigumu kusema kwamba leo umekata kabisa kwamba hutakuwa na madeni. Mkandarasi anapopewa *site*, kitu cha kwanza huwa analipwa *advance payment.* Akishalipwa *advance payment* halipwi *Certificate* inayoitwa *IPC* mpaka a-*produce* kazi. Asipo-*produce* kazi, hawezi akalipwa hata kama fedha imetengwa kwenye bajeti. Kwa hiyo, ina *depend* na *speed* ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mkandarasi alitengeneza barabara ya Kagoma - Lusahunga, kilometa 154. Siku Mheshimiwa Rais anakwenda kuweka jiwe la msingi barabara ile alikuwa amebakiza mita 500 kumaliza. Kwa hiyo, ina-*depend* na Mkandarasi na *speed* yake. Kwa hiyo, kila *Certificate* anapo-*produce* ndipo analipwa fedha. Akisha-*produce* ile *Certificate* ni lazima ikae siku 56 kabla haijawa fedha. Kwa sababu ni lazima iwe *verified* na *Consultant* aliyeko kule, *TANROAD*, Wizara pamoja na Wizara wa Fedha. Kwa hiyo, madeni haya yaliyopo tuna uhakika kwamba italipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa uhakika kwa sababu hata Mkandarasi anapokabidhi kazi halipwi fedha zote. Ana-*produce Certificate* anakuwa na adai fedha zile tunazishikilia ili kusudi mradi ule umalize ile *grace period* yake, ndipo anaweza akalipwa fedha. *Grace period* huwa ni kati ya mwaka mmoja na miaka mitatu. Kwa hiyo, ukishaona kwamba Mkandarasi yule anadai madeni, haina maana kwamba tumeshindwa kulipa madeni.

Nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Mkosamali, fedha za kulipa madeni zipo na ndiyo maana tumekuwa tukilipa. Nimezungumza juzi tu, zaidi ya Shilingi bilioni 212 zimetolewa na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba hilo lisiwe tatizo, tatizo sisi ni miradi kukamilika kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mkosamali pia amezungumza kuhusu barabara kwamba nyingine zinasainiwa tu, fedha zinakuwa hazipo. Nimeeleza katika maelezo yangu kwa uzuri kabisa kwamba Ujenzi wa barabara unaanza na *feasibility study,* ni lazima uweke fedha; inakuja *detail design,* ni lazima uweke fedha; inakuja *construction,* ni lazima uweke fedha; unapo mu-*involve Consultant* au *Engineer* kwenda kufanya *feasibility study* ni lazima umlipe, ni lazima utenge kwenye bajeti. Unapomwambia *Consultant* kwenda kufanya *design,* ni lazima umlipe fedha, lazima utenge kwenye bajeti. Anapokwenda kwenye *construction* ni lazima utenge kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mkosamali alitoa mfano wa barabara ya Kigoma kwenda Nyakanazi ya Kilometa 310. Tumetenga katika kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya *feasibility*, *detail design* na

mwaka 2013 tulitenga kwa ajili ujenzi na mwaka huu tumetangaza, tumesaini na *contractor,* wameenda kule kwa ajili ya kuanza *mobilization* na mwaka huu tumeongeza tena Shilingi bilioni kumi nyingine kwa ajili ya kuanza kazi.

Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mkosamali na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itaendelea kulipa Wakandarasi kama ambavyo imejipanga lakini kuhusu orodha ya miradi iliyopo, nitashukuru sana Mheshimiwa Mkosamali akienda kusoma Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, sasa unaondoa Shilingi na mjadili hoja, *unless* umeridhika unatoa!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Eh!**

**MWENYEKITI:** Kama umeridhika, unarudisha Shilingi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Aah, sirudishi Shilingi, naiacha iendelee kuwepo.
**MWENYEKITI:** Haya!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Bado naihitaji kuondoka nayo niipeleke Kibondo kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amenielekeza kwamba nisome Ilani ya Chama cha Mapinduzi…

**MWENYEKITI:** Hiyo ni hoja. Unachodai siyo Ilani, unachodai ni nini? Kusudi tuwe na *item* moja tu tunayojadili sisi wote.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri amenijibu!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna Wabunge wengine mtu akisimama, wenyewe maneno, maneno, sivyo tunavyokaa. Sisi wenyewe tunatumia akili kusikiliza kinachosemwa. Kwa hiyo, ninachomwelekeza huyu, ndiyo utaratibu wa Shilingi. Uwe na hoja mahususi ambayo sisi tutachangia. Mheshimiwa!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba tunatakiwa tupewe ratiba na majibu yake amenieleza kwamba nisome Ilani ya CCM ndiyo ratiba ilipo. Sasa mimi ninavyofahamu, hii Ilani ya CCM ni ya miaka hii mitano inayoishia mwaka kesho.

Barabara ambazo ziko hapa kwa mfano barabara ya Ndundu - Somanga imetengewa Shilingi bilioni tano. Hii fedha haitoshi kukamilisha pale. Barabara nyingi zimetengewa fedha kidogo kidogo, *unless* watuambie kwamba hii Ilani ya CCM imeahidi mpaka Rais atakayechaguliwa mwaka kesho na wengine. Tunachotaka sisi hapa, ni ratiba ya ujenzi wa kila barabara.

Pili, hajatuambia kiasi gani? Swali langu halijajibiwa; kwenye bajeti hii, fedha kiasi gani zinakwenda kulipa madeni? Hilo bado.

Mmesema kuna madeni zaidi ya shilingi bilioni 450, ni kiasi gani cha fedha kinakwenda kulipa madeni? Kwa sababu miradi ni mingi na Wabunge kweli wanashangilia, wanashangilia, lakini kwenye Ilani, hapajaandikwa ratiba kwamba barabara fulani itakamilika tarehe fulani, hawajaandika hivyo. Naomba anifafanulie na ajibu vizuri, tusiwe na miradi mingi, hii miradi mingine ipo tangu mwaka jana, mingine iko tangu mwaka juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulivyojipanga kwenye UKAWA, unaweza ukashangaa mwaka kesho tunaingia madarakani, sasa hatuwezi kuendelea kutekeleza Ilani hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ondoa maneno yako UKAWA, ondoa maneno yako ya UKAWA tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize, hapa Bunge tunatambua Kambi Rasmi ya Upinzani, ndiyo jina lenu! Maneno mengine mnatuletea ya kazi gani hapa. Mheshimiwa Mkosamali ondoa neno lako ama huendelei. Ondoa neno lako, ni Kambi Rasmi ya Upinzani.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kwa Bungeni Kambi Rasmi ya Upinzani.

**MWENYEKITI:** Sawasawa, hiyo ni safi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa aje atujibu ili Kambi Rasmi ya Upinzani tutakapochukua nchi, badala ya kujenga reli na maeneo mengine ili barabara zisiharibike, tukajikuta tunalipa madeni na kumalizia barabara zaidi ya miaka hata 10, 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka ratiba ieleweke, naomba jambo hili lijadiliwe, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Niangalie ambao hawajasema, Mheshimiwa Nassari, sijawahi kumsikia safari hii.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Mkosamali amezungumza vizuri sana. Mimi kule kwangu kwa mfano tu nina mradi wa barabara ya Nelson Mandela ambayo inaanzia *Usa River* inakwenda mpaka Arusha Mjini kuunganisha kule *Masai Camp*. Kwa mwaka jana peke yake haikutengewa shilingi, nilipopiga kelele hapa na kwa sababu alipozindua Chuo cha Nelson Mandela, aliahidi mwaka jana akasema lazima iwepo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha uliopita tayari, siyo huu ambao tupo leo, lakini mwaka jana haikupangiwa, nilipopiga kelele wakatoa shilingi bilioni 1.3 lakini ni barabara yenye kilomita karibia 18. Sasa unapotenga shilingi bilioni 1.3 kwenye barabara kama ile, maana yake kimetengenezwa kipande cha kilomita tatu peke yake, tena haikutosha imeongezewa milioni 500 ndiyo wakatengeneza kilomita tatu, tena katikati. Kwa hiyo, huku mwisho hakuna kitu, huku mwisho hakuna kitu, katikati kilomita tatu za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme tu kwamba, tunahitaji kupata ratiba, kwa sababu kwa mfano mwaka huu ile barabara haiko kwenye bajeti, lakini mwaka jana imepewa 1.3. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba inaweza ikachukua miaka 30 kutengeneza kilomita 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mkosamali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Msakamali, ya Mkosamali, samahani Mheshimiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila sababu ya Serikali kuja na ratiba maalum jinsi ya kukamilisha barabara zetu. Kwa sababu tunafahamu barabara inavyojengwa kwa muda mrefu kwanza kuna hasara kwa Serikali kwa sababu Mshauri Mwelekezi anaendelea kupewa hela wakati barabara haitengenezwi, lakini pia wale wakandarasi wanaoweka vyombo barabarani bila barabara kutengeneza wanalipia, kwa hiyo, ni hasara kwa Serikali, pia kuna *fluctuation* ya *price* ya *materials,* kwa hiyo, barabara ikijengwa kwa miaka kumi gharama ya barabara inakuwa ni kubwa. Mfano mmoja ni barabara za Mkoa wa Tabora. Ni miaka mingi tunapiga kelele hapa Mkoa ule haujafunguliwa na barabara ambazo zimeanza mwaka 2007 mpaka leo miaka nane, bado ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja tu, barabara ya Nzega-Tabora, ukiangalia hotuba ya Waziri ya mwaka jana, ni *copy and paste* na mwaka huu. Mwaka jana barabara ilitengewa kilomita 15 shilingi milioni 13,169.34, mwaka huu hivyohivyo, kwa maana nyingine hakuna kilichofanyika kwa mwaka mzima. Wakati huohuo Waziri alituambia kwamba mwaka huu wa fedha barabara za Tabora zote zitakamilika, leo tunazungumza hapa hazijakamilika! Kwa hiyo, lazima kuwepo na *time frame,* barabara ikitengewa pesa, kama ujenzi umeanza muda fulani, Waziri atuambie Wabunge wajue barabara yangu imeanza muda fulani, itakamilika muda fulani, wananchi wajue na kuokoa pia fedha za Serikali ambazo zinakuja kupotea bila utaratibu. Naunga mkono wazo la Mheshimiwa Mkosamali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa Kambi Rasmi, akishasema yeye wote mnakaa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mkosamali kwa sababu mbili zifuatazo:-

Kwanza, ni siri iliyo wazi kwamba ujenzi wowote unapofanyika kwa *speed* unaokoa gharama kubwa sana.

Pili, ni ukweli usiopingika kwamba Serikali imeji-*commit* kwenye kujenga barabara nyingi, lakini barabara hizi hazijengwi kwa wakati na zimesababisha usumbufu mkubwa siyo tu kwa wananchi bali hata kwa wakandarasi ambao wanajenga barabara hizi kwa sababu wanashindwa kuzimaliza kwa muda na jambo hili linapelekea gharama za ujenzi wa barabara kuwa kubwa sana kuliko ambavyo pengine ingestahili kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ya Mheshimiwa Mkosamali ya kutaka uwepo wa ratiba ni mojawapo ya mbinu pengine za kuitaka Serikali iwe inatekeleza *commitments* zake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano rahisi Mheshimiwa Magufuli aliuzungumza hapa mapema wakati akiwasilisha, alizungumzia barabara ambayo tuliizindua, barabara ya Kwa Sadala-Masama ambapo katika uzinduzi ule na Mheshimiwa Rais tulikubaliana vilevile pale kwamba iweze kuongezwa iunganishe Machame- Barazani - Machuwa. Barabara ya awali ilikuwa na urefu wa kilomita 12.5, barabara hii imejengwa kuanzia mwaka 2009. Barabara ya kuanzia mwaka 2009 mpaka leo 2014 haijakamilika pamoja na kwamba mkandarasi wa kwanza alikuwa na matatizo, ni dhahiri kwamba kungekuwa kuna *commitment* ya kumaliza barabara kama hizi zingeweza zikamalizwa mapema zikaokoa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono sana hoja ya Mheshimiwa Mkosamali na nikitegemea kwamba Waziri atakapotupa majibu hayo katika hili ataweza vilevile kuzungumzia hiyo *extension* ambayo Mheshimiwa Rais aliizungumza kwa sababu haiko kwenye bajeti, lakini Masama - Kwa Sandala imetengewa shilingi bilioni moja tu mwaka huu, fedha ambayo kwa vyovyote vile haitaweza kuimaliza barabara ile. Ni barabara fupi sana kama mkandarasi anakaa *site* miaka mitatu au miaka mitano kujenga kilomita 12 kwa vyovyote gharama zinakuwa kubwa bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nimeshasema akisema mkubwa wenu wengine wote mmemaliza. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaelewa sana Waheshimiwa na hoja ya Mheshimiwa Mkosamali lakini nafahamu Mheshimiwa Mkosamali na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii wanafahamu kazi ya barabara. Barabara wanapoweka mkataba huwa kuna *contract limit,* kama ni miezi 36, kama ni miezi 24, kama ni miaka minne, kila mkataba wa barabara hata wa barabara ya kwake Mheshimiwa Freeman ile ya Kwa Sadala mkataba umewekwa pale. Sasa ukiniambia mimi nitengeneze *frame work* kwamba itaisha lini na wakati Mheshimiwa Freeman Mbowe amezungumza pale, kandarasi aliyekuwepo wa kwanza tulimfukuza, maana yake nikishaweka *frame work* pakitokea matatizo ya makandarasi wa kufukuzwa kama tulivyomfukuza wa kwake na tukatangaza tenda nyingine, *frame work* hiyo itakuwa *useless! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mwingine, katika mikataba tulipoweka kwa mfano ya Tunduru, kuna kandarasi *progressive,* ambaye tulimpa *packages* tatu kwa ajili ya kutengeneza kwa kiwango cha lami ndani ya mawasiliano na makubaliano ya *African Development Bank.* Kandarasi yule amekaa mwaka wa kwanza haku-*perform*, mwaka wa pili haku-*perform*, ikabidi tuingie makubaliano na *African Development Bank* kwa ajili ya kumfukuza, tukamfukuza. Katika nchi inayoheshimu utawala wa Sheria akatupeleka Mahakamani tukasubiri, tukamshinda, aka-*appeal,* tukamshinda baada ya kumaliza kumshinda tumetangaza tenda nyingine tumeweka makandarasi wengine. Leo unaniambia niweke *time frame work, time frame work* iliyopo kwa mikataba yote ya barabara ni mikataba tuliyosaini na makandarasi ambayo iko kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kwanza ya fedha kiasi gani zinakwenda kulipa madeni hajaifafanua kabisa wala hajaijibu.

**MWENYEKITI:** Hoja ni moja hiyo mengine ilikuwa mifano, hoja yako ni ratiba.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye hoja ya ratiba, ni kwamba tungependa sisi Waheshimiwa Wabunge, kama hiyo mikataba ipo na inaelezea muda ndiyo ratiba yenyewe tunayoitaka sisi, aende angalie kila mkataba wa barabara tupatiwe. Kwa nini tunasema hivi, ni sawa na barabara hii anayoisema, barabara za Tabora zina zaidi ya miaka sita, miaka nane barabara hazijakamilika, *life span* ya barabara ni miaka 15. Kwa hiyo, maana yake kama itakamilika baada ya miaka minane ijayo ni kwamba huku nyuma barabara inatakiwa ianze tena kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nachosisitiza hapa ni kwamba tupewe ratiba na ile ratiba itakuwa na *notice,* itaeleza kwamba barabara hii imechelewa kwa sababu moja mbili, tatu, barabara hii ina tatizo kwa sababu mkandarasi ametupeleka Mahakamani, ratiba itafafanua *in detail.* Kwa sababu hapa Wabunge wanachanganyikiwa miradi hii ni mingi mno

na fedha nyingine zinatengwa shilingi bilioni mbili kilomita 100, shilingi bilioni tano kilomita, hii miradi kama imeahidiwa mwisho wa kukamilika kwake au hakuna, haifahamiki, itajengwa hata miaka 30 ijayo, basi mimi naomba tupige kura lakini najua hata Wabunge wa CCM wananchi wenu wanatamani kujua barabara hizi zitakamilika lini.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MWENYEKITI:** Sema ya kwako Mkosamali unachokoza watu bure, wewe jibu ya kwako. *(Kicheko)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Nilikuwa nasema wananchi wa vyama vyote wanatamani kupata hii ratiba maana wana hamu sana ya hizi barabara. Kwa hiyo, mimi niwaombe wasikatae hoja hii kwa sababu hata wananchi wao wanatamani hii ratiba kujua kwamba hizi barabara zitakamilika lini maana wamekuwa wanawaambia na wamekuwa wanawaahidi. Kwa hiyo, naomba waniunge mkono kwa sababu ni mambo ya muhimu sana kwenye Majimbo yao na ni mambo ya muhimu kwenye nchi.

**MWENYEKITI:** Jamani eeeh, mkifanya anavyofanya Mkosamali ninyi mtakuwa mnafanya kazi gani? Kila Mbunge ana wajibu wa kufanya kazi katika eneo lake na kuuliza hizo ratiba anazosema kwa barabara yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu ni hoja ni lazima tufanye maamuzi, kila Mbunge afanye kazi yake, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, waliokataa hoja hiyo wameshinda, kila Mbunge aombe ratiba kwa barabara yake na atapewa. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala zima la *TAMESA*.

**MWENYEKITI:** Naomba tumsikilize mwenzetu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na ufafanuzi huu uwe wa kina na wenye mashiko juu ya utendaji wa Taasisi au Wakala huyu *TEMESA*. Wizara ya Ujenzi kupitia *TEMESA* ina wajibu wa kusimamia magari ya Serikali, lakini vilevile pamoja na manunuzi, usajili na matengenezo ya magari ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelezo na maelekezo juu ya manunuzi ya magari ya Serikali na akaielekeza Serikali na Taasisi zake juu ya ununuzi wa magari ya kifahari, kwa maana ya mashangingi, lakini vilevile akairejea tena kauli yake mwaka 2012. Kama hilo halitoshi, hivi sasa inaonekana *TEMESA* imeacha kufanya shughuli zake za msingi kama ambavyo inatakiwa kufanya. Sasa hivi gari za Serikali zinaonekana kutengenezwa katika gereji bubu au gereji za nje bila ya ukaguzi ama kibali kutoka *TEMESA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi ni hivi karibuni tumepata taarifa kwamba Serikali kwa kupitia *TanTrade* walinunua magari 11, magari ambayo hadi leo hii hayajulikani yalipo. Magari ambayo hata usajili wake yalisajiliwa kwa nambari za watu binafsi.

**MWENYEKITI:** Naomba tuelewane kidogo hapa, hatujaelewa unajadili ama? Maana unapofika kwenye mshahara wa Waziri ni *issue* moja ya kisera.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Ndiyo ninayoiongelea.

**MWENYEKITI:** Ngoja nielewe vizuri na wewe utulie chini. Nielewe vizuri, ni ununuzi wa magari au utengenezaji wa magari au sijui kitu gani, uwe na hoja moja, ndiyo wakati wa mshahara wa Waziri, siyo kila kitu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, Wizara ya Ujenzi kwa kutumia kitengo chake cha *TEMESA* kina wajibu wa ununuzi wa magari ya Serikali, kina wajibu katika kutengeneza magari ya Serikali lakini vilevile kina wajibu katika kusajili magari ya Serikali. Kwa hiyo, hiyo ni hoja moja tu. Sasa nachokitaka ni ufafanuzi wa kina kutoka kwa Waziri juu ya utendaji wa taasisi hii ambayo iko chini yake ya *TEMESA* na kama sikupata majibu ya kuridhisha hasa kutokana na kauli hizi ambazo vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu amezieleza basi nina nia ya kutoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, anachouliza ni kwamba utendaji wa *TEMESA* haufai au haufanyiki.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mheshimiwa Rajab na mimi nitashangaa sana kama atatoa shilingi kwa sababu akitoa shilingi maana yake Wajomba zake kule watakwenda kufa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kumwelewesha Mheshimiwa Rajab, *TEMESA* ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.30 ya mwaka 1997 na ilipoanzishwa, majukumu yake yameainishwa kwenye Sheria hiyo. *TEMESA* ilipokuwa ikifanya kazi, siku za nyuma haikuwa na Bodi kwa sasa hivi ina Bodi na Mwenyekiti wake wa kwanza alikuwa Profesa Msholo ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Ardhi na kwa sasa ameteuliwa Balozi Mlango aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kumwelewesha Mheshimiwa Rajab, majukumu ya *TEMESA* yanaendelea kutekelezwa vizuri, tunashughulika na kusimamia magari na kwa sasa hivi *TEMESA* imeimarishwa, ofisi zake katika Mikoa yote 25 pamoja na Mikoa mipya ambayo imeanzishwa, tunaanzisha ofisi zao, tuna Mameneja na *TEMESA* sasa hivi itakuwa *agency* kama inavyofanya *TANROAD* ili kusudi magari yote yanayokwenda kutengenezwa yawe yanatengenezwa kwenye ofisi za *TEMESA* zilizoko Mkoani lakini *with exception* kwa sababu kuna magari mengine ambayo yana *specification* na *dealers* labda yanatengenezwa Toyota au yamenunuliwa mapya ambao muda wake wa kufanyiwa *service* yanatakiwa yapelekwe kwenye *agency* nyingine au ya Ikulu na mambo mengine, kwa hiyo, pale *TEMESA* huwa wanatoa vibali maalum. Kwa hiyo, yale ambayo yalikuwa yamezoeleka ya kwenda kutengeneza kwenye gereji bubu hayatakuwepo, nataka kuhakikisha hilo. Ndiyo maana hata katika ripoti ya *Control And Auditor General,* ninayo hapa Wizara ya Ujenzi imepewa *clean certificate.*

**MWENYEKITI:** Bado unataka kuuliza Rajab, kwa sababu alitoa *indication* anataka kutoa shilingi ndiyo maana namrudia, sio kwamba ni kila mtu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yangu ya kutoa shilingi bado iko palepale. Pamoja na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri amejaribu kuyaeleza na kusema kwamba Wizara yake imepata hati ambayo haina mashaka kutoka kwa Mkaguzi lakini Mkaguzi huyohuyo katika taarifa yake anaeleza kwamba, pia ilibainika kuwa Wizara ya Ujenzi

haina orodha ya karibuni ya magari ya Serikali kama chombo cha kufuatilia matengenezo ya magari ya Serikali. Umezungumzia habari ya karakana, katika ziara yao CAG anasema kwamba katika kutembelea karakana za *TEMESA* zilizopo Dar es Salaam, *depot* ya Vingunguti, ilibanisha kuwa karakana hizi zilikuwa na vifaa vichakafu, kwa hiyo, hizi karakana hazifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli majibu ya Waziri hayakuridhisha kwa yale ambayo nilitegemea yatakuwa ni majibu halisia. Bado naendelea kubana shilingi yangu na kama kuna uwezakano niwape nafasi na wengine wachangie katika hili.

**MWENYEKITI:** Ulikuwa haueleweki hoja yako sasa ni ipi, maana tukiingia kwenye shilingi ni hoja moja tu, kwa sababu ukitaka kila mtu azungumzie magari yaliyoko huku na ya kwao tutakuwa hatufiki, sasa uwe *very specific*.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni utendaji wa TEMESA. Hiyo ndiyo hoja yangu kuu, nilitaka ufafanuzi juu ya utendaji kazi wa taasisi ya TEMESA.

**MWENYEKITI:** Si amekueleza kwamba iko ndani ya sheria.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Nakubaliana na yeye kwamba iko ndani ya sheria na kwa sababu sheria hizohizo ndizo zinazovunjwa, ndiyo maana mimi nikahoji sasa, kwa sababu uvunjaji huu wa sheria upo, sheria zipo lakini zinavunjwa.

**MWENYEKITI:** Tunachojaribu kuona hapa tusiwe tumefungua *Pandora's box* ya hoja yako, kwa sababu wewe umesema kwa mfano *audit report* ya sasa kwamba magari hayajulikani yako wapi, ndiyo hoja hiyo peke yake na wengine watoe mfano? Yaani tunapochukua shilingi ni hoja, kama umesoma kile kifungu ni hoja na utuweke sisi wote tuzungumzie ile hoja yako, si kila mtu anazua ya kwake na mwingine ya kwake, aah, aah, bado hujawa *very clear* na hoja yako.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko *very clear*, lazima tukubali kwamba suala la magari ni suala ambalo vilevile linatumia fedha nyingi za taifa, matumizi mabaya ya magari ya Serikali. Magari ya Serikali yametungiwa sheria, sawa na TEMESA imepewa jukumu na Serikali kushughulikia magari ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Serikali imekataa kufanya hivyo?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Kwa hiyo, Serikali inavunja sharia. Sasa ndio nilitaka maelezo ya kina kutoka kwa Serikali, ni kwa namna gani sasa TEMESA imeshindwa kufanya kazi zake, ndio ufafanuzi niliouomba.

**MWENYEKITI:** Basi naomba Waziri rudia, wala siyo hoja hiyo, ni *very specific*, si suala la sera.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa ufafanuzi vizuri sana lakini katika maelezo yake tena kasema mitambo ya *TEMESA* ni mibovu, sasa inawezekana kweli ni mibovu, ndiyo maana nimeleta bajeti ya *TEMESA* hapa tupitishe tukanunue mitambo mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akazungumzia tena magari, kazi ya *TEMESA* imeelezwa vizuri kwenye Sheria Na.30 ya mwaka 1997 na kazi yake kubwa nyingine ni kufanya *registration*, inafanya *registration* na ndiyo maana katika magari yote yanayokuwa *registered*, PT mpaka ya Magereza, STJ yanafanyiwa *registration* na *TEMESA*. Sasa anaposema magari yanatumika vibaya, angekuwa *specific*, kwa sababu kazi ya *TEMESA* si kwenda kukagua barabarani magari

yaliyo kwenye *bar* na ndiyo maana nimemtajia Sheria Namba 30 ya mwaka 1997 iliyoanzisha *agency* ya *TEMESA*. Mheshimiwa Mbunge angeisoma vizuri angeelewa kwa hiyo asingeipa majukumu mengine *unless* tulete mabadiliko ya sheria hapa tukaiongezee majukumu mengine *TEMESA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa asitoe hiyo shilingi, aturudishie, tukafanye kazi. Hiyo mitambo chakavu si ndiyo maana tumeomba hapa bajeti ya *TEMESA* tukanunue, tufanye kazi, tufanye udhibiti, rudisha tu hiyo shilingi rafiki yangu.

**MWENYEKITI:** Anakuomba umrudishie shilingi swali lako sio *specific*, *it is too direct.*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Shemeji niko tayari kukurudishia shilingi lakini Mheshimiwa inaonekana hili suala kama linataka kupigwa danadana hapa ndani kwa kweli. Ni suala ambalo kwa kweli lina uzito wake na linaathiri uchumi wa taifa na ni mambo ambayo tayari yalishatolewa maelezo ambayo inaonekana ufuatiliaji wake basi pia haukufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ndiwe Mwenyekiti, uamuzi ni wa kwako, mimi nilitaka wenzangu wapewe nafasi wachangie katika suala hili.

**MWENYEKITI:** Tutafungua *Pandora's box* kwa sababu haukuwa *very specific,* inawezekana ulikuwa na hoja nzuri lakini ilivyoulizwa inatoa maneno mengi sana. Tunaendeelea Mheshimiwa Augustine Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka tu kumbukumbu zinazotokana na Naibu Waziri wa Ujenzi ziwekwe sawa na niweze kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ombi langu la maandishi barabara niliyoitaja na ambayo amekubali kwamba atanisaidia, yeye amesema ni Himo kwenda Kilema Hospitali, lakini barabara niliyoiandika kwenye kumbukumbu alizonazo ni Kilema Pofo kwenda Kilema Hospitali. Mimi nakupongeza sana kwa kukubali kwamba ule Mfuko wa *Millenium Challenge Account* utasaidia barabara hiyo. Kwa hiyo, mimi sitoi shilingi, ningekuwa nayo ningekuongezea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa moja kwa moja na pia katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuna hoja imetolewa kuitaka au kuishauri Serikali angalau iunde Wakala wa Barabara Vijijini na Wabunge wengi wamezungumzia sana masuala ya barabara vijijini. Ukiangalia vyakula vingi au vifo vingi vya akina mama ni kutokana na kwamba wanakaa vijijini na wanashindwa kufika Makao Makuu ambako ndiko ziliko Hospitali za Wilaya. Kwa hiyo, barabara hizo hata Wabunge tunaposimama huwa tunajenga hoja lakini kama Waziri anashindwa kuzielewa. Kwa mfano, kule Kilombero, mimi nimezungumzia tu barabara tena ya *TANROADS* kutoka Ifakara - Mlimba - Madeke - Njombe lakini hakuitaja kabisa. Hata hivyo katika mfululizo wa bajeti miaka yote anasema ataijenga kiwango cha lami na changarawe, lakini leo hakuitaja kabisa. Sasa sielewi anasahau na wananchi huko wanatuma meseji wanauliza. Kwa mfano, kuna Kata moja pale Namowala kwenda Kata nyingine ya Mofu kuna daraja kubwa. Kwa mfano kuna barabara na Waziri Mkuu anaijua kutoka Chita - Melela inatakiwa karibu Sh.2,000,000,000, barabara hizo bado ni za Halmashauri za Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hoja ya Kambi ya Upinzani imesema kwamba sasa wakati umefika Serikali iunde Wakala wa Barabara Vijijini ili mamlaka hiyo sasa iweze kuwa inaangalia barabara za vijijini ndani ya nchi yetu ili barabara hizo zipate chombo cha

kuzisimamia. Tofauti na sasa hela nyingi zinakwenda kwenye Halmashauri na kwenye Halmashauri kuna matatizo makubwa, kuna ulaji mkubwa wa pesa hizo za barabara. Wanatenga hapa shilingi lakini mbili, hapa laki tatu, hapa kufukia mashimo, wanasema kwenye vitabu changarawe kule unakuta udongo, kule unakuta vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najenga hoja kwamba sasa umefika wakati, kwa sababu matatizo ni mengi nchi nzima kuhusu barabara za vijijini, sasa kuwe na mpango na Serikali inipe majibu, wa kuunda Wakala wa Barabara Vijijini. Kama hoja yangu hii haitapata majibu na naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono, barabara ni zetu, akina mama wanakufa, mazao hayafiki katika barabara kuu, kwa hiyo ni muhimu sasa Mamlaka hiyo ikiundwa ili fedha nyingi zinazokwenda kwenye Halmashauri zisimamiwe na Mamlaka hiyo ili tupate barabara vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kutoa shilingi kwa mara ya kwanza kama sitapata majibu ya uhakika kuhusu uundwaji wa chombo hiki ambacho kitakuwa mkombozi kwa barabara za vijijini. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa ufafanuzi huu, kwanza, napenda nimueleweshe Mheshimiwa Mbunge, Wizara ya Ujenzi inahusika na kilometa 35,000 katika nchi nzima ambapo inahusisha na barabara za *trunk roads* na *regional roads*. Barabara nyingine zilizobaki ziko chini ya TAMISEMI. Katika michango iliyotolewa hapa na wala haikutolewa tu na Kambi ya Upinzani, imetolewa hata na wa CCM, kwamba wakati umefika sasa tuangalie ni namna gani tunaweza tukaanzisha *agency* ya barabara za vijijini. Mimi kwa niaba ya Serikali, nikasema hili tutaliangalia, kwa sababu Sheria ya kuanzisha *agency* yoyote ambayo tuliipitisha hapa Bungeni ni kupitia Sheria Namba 30 ya mwaa 1997. *TANROADS* imeanzishwa kwa Sheria hiyo, *TBA* imeanzishwa kwa Sheria hiyo, *TEMESA* imeanzishwa kwa Sheria hiyo, *agency* zote zilizoko hapa Tanzania zimeanzishwa kwa Sheria hiyo. Nikasema kwamba hili litaangaliwa na Serikali ili lifanyiwe kazi ili kama itaanzishwa *agency* kupitia TAMISEMI zile fedha zinazokusanywa za *Raod Fund* na kadhalika zikafanya kazi kule za vijijini. Sasa unataka kutoa Shilingi, kwanza nataka kukueleza sitishiki na kutoa Shilingi kwa sababu mshahara wangu ni wa Ubunge, ukitoa utatoa za Uwaziri, nitakwenda kupokea fedha za Ubunge wa Chato lakini nakuomba mtani wangu usitoe Shilingi ili tulifanyie kazi hili litatuliwe kwa sababu ni michango ya Watanzania wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwanga nadhani umesema vizuri na Waziri ameelewa.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na Waziri kunielewa lakini mimi bado nilikuwa nahitaji kuambiwa ni lini, kwa umuhimu wa barara za vijijini na vifo vya akina mama, jamani akina mama wanakufa, afadhali ungekwenda huko ukaona, watoto wafia njiani, barabara hakuna na hela zinaliwa, lini mchakato unaanza wa kupata hiyo Wakala wa Barabara Vijijini. Ni vyema Wakala ya Barabara Vijijini ikaingia hapa kwenye *Hansard* ili tunapokwenda tuone sasa ni namna gani ya kuifuatilia Serikali, kwa sababu hapa ulipojibu umejibu jumla jumla na ndiyo maana Wabunge wengi wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nimesema Waziri kuna barabara za Wilaya ya Kilombero ameziahidi tangu mwaka wa juzi lakini mpaka leo hakuna chochote kinachoendelea, sanasana tunamwagiwa vumbi, watu wanazidi kufa, maisha yanazidi kuwa magumu. Haiwezekani mtu anasafiri kilometa tano analipa nauli Sh.50,000, haiwezekani, ni matatizo! Ndiyo maana tunasema hebu aende huko akaone wananchi wanavyoteseka. Simu zinajaa meseji ni lini mchakato utaanza ili hiyo *agency* ya *Rural Road* ipatikane.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwanga, mtu mzima ameshaelewa ushauri wa Kambi ya Upinzani na ushauri wa Wabunge hapa kwamba labda muangalie namna ya kuanzisha *agency* na sikuona kama wanasema kwamba hawataangalia.

**WAZIRI WA UJENZI:** Na wala halipo kwenye Wizara yangu.

**MWENYEKITI:** Sasa tukibishana tu kwa sababu ya kubishana haisaidii. Mheshimiwa Waziri sema mara ya mwisho.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa ufafanuzi vizuri sana. Kwanza hizo barabara za vijijini anazozungumzia haziko chini ya Wizara ya Ujenzi. TAMISEMI walieleza hapa, hakusimama wala hakuuliza, leo amemuona Magufuli hapa anataka kumuonea. Hata hivyo nikazungumza kwa kumheshimu Mheshimiwa Kiwanga kwamba Serikali tutakaa, Serikali ni moja, Waziri Mkuu anasikia, Waziri wa TAMISEMI anasikia, yeye ananiambia niseme lini, sisemi lini. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, Serikali iko hapa. Mimi natoa shilingi ili uwape nafasi Wabunge wajadili, naomba kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Nimekataa hiyo shilingi kwa sababu hili ni suala la sera, hambishani, hakuna anayekubishia wewe, Serikali haijakataa wala wewe hujabisha. Hoja hapa ni kwamba tujaribu kuona hili suala tunalimalizaje. Hilo tumelimaliza, mimi napima, nasema hakuna hoja kwa sababu hakuna anayepinga hoja hii. Tukipiga kura Kiwanga ujue kwamba tunakataa ile hoja yako, kitu ambacho si lazima. Mimi sitaki hoja hii ipingwe kwa sababu ni hoja ya kweli. Sasa tuendelea, Mheshimiwa Njwayo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati wa mchango wangu asubuhi nilieleza suala la barabara ya kutoka Mtwara, Tandahimba, Newala hadi Masasi kuwa ni ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Pia Mheshimiwa Rais alipopita kwenye maeneo hayo aliwaahidi wananchi wanaoishi maeneo yale kwamba kabla hajatoka ataweka jiwe la msingi la kuanza ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadiri muda unavyokwenda, pesa zinazotengwa kwenye eneo hilo zinaonekana hazitoshi. Kwa mfano, kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba shilingi bilioni tatu zilizokuwa zimetengwa mwaka wa jana kwenye barabara hiyo kwa ajili ya usanifu kazi inaendelea, wakati sisi tunaoishi kule hatujawahi kuwaona wataalam wakiwa *field* wala hatujaona ndege ikiwa angani ikifanya shughuli hii. Sasa inaonekana kuna dalili hapa za funika kombe mwanaharamu apite, jambo ambalo silitarajii sana na kwa sababu Mheshimiwa Waziri namheshimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika maelezo yake hapa ametutaka watu wa Mtwara, Tandahimba, Newala tukubaliane tuanzie wapi? Busara ya kawaida ni kuweka wakandarasi watatu katika sehemu tofauti tofauti ili kazi hiyo ifanywe kwa muda mfupi. Nimesimama ili kutaka uthibitisho kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, utayari wa kuanza ujenzi na uhalisia, tusiletelete maneno, tupate mkakati uliopo wa kuanza kazi hiyo sambamba na kuweka jiwe la msingi kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tatizo hili linaleta athari kweli kwa wananchi kwa sababu watu wanalalamika sana lakini hatumuweki vizuri Rais wetu mpendwa kwa wananchi kwa sababu inaonekana kama anababaishwababaishwa, ilikuwa ubabaishaji

tu. Kama nilivyosoma *message* hapa wakati ule nachangia, Mtanzania mmoja katuma *message* hapa, anasema hivi ile ahadi ya Rais tumewekewa mbuzi kwenye gunia? Ni hayo tu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Juma Njwayo ni *issue* ya msingi. Barabara ya Masasi - Newala - Mtwara iko kwenye Ilani ya Uchaguzi. Mwaka jana tulitenga fedha na mwaka huu tumetenga fedha. Napenda kumhahakikishia Mheshimiwa Njwayo ndugu yangu pamoja na Waheshimiwa wananchi wa eneo hilo, barabara hii tutaijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *consultants* ambao wako kule, nataka kukuhakikishia na naomba *Hansard* zichukue, kama *consultant* ata-*delay* kufanya kazi ya *design* na wataalam wangu wote wananisikiliza hapa, tutaitengeneza barabara ile kwa njia ya *design and construct*, kama tulivyofanya Nangurukuru-Mbwemkuru na Mbwemkuru-Mingoyo. Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia tutatangaza tenda, tunaomba usitoe hii shilingi kwa sababu itachelewesha kazi hii, ili tuweze kusimamia kazi hii kadiri Mheshimiwa Rais alivyoahidi. Mimi nataka kukuhakikishia leo na wananchi wa Mtwara, barabara hii Mheshimiwa Rais ataiweka jiwe la msingi kabla hajamaliza muda wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zarina Madabida, hakutoa shilingi, hakusema hivyo, Mheshimiwa Madabida.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa kuzungumza pamoja na maandishi nilikuwa nimezungumzia kuhusu suala la daraja la *selander* na umuhimu wake katika kuondoa msongamano na sisi wote hapa ndani tunajua jinsi adha iliyoko pale *selander bridge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri lakini tatizo langu ni kwamba majibu haya humu kwenye vitabu hayamo na kwenye kitabu chake cha *speech* kuna shilingi milioni mia mbili ndizo zimetengwa lakini huku kwenye kitabu cha maendeleo zimechanganywa tu hela za *construction of bridges*, nimeiona, haipo yenyewe lakini nimeona ile jumla yake. Pia amesema kwamba kuna hawa Wakorea ndio ambao watakuja kujenga hili daraja lakini kwenye hiki kitabu cha maendeleo, kwenye hela za nje imewekwa *dash*, sasa mimi nikawa najiuliza, hivi Mheshimiwa ananiambia ukweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi sitaki kuchukua shilingi, mimi ni Mjumbe wa Kamati na hili nililiuliza tokea kwenye Kamati, nilikuwa nafikiri baada ya kuliuliza kule basi huku ningepata *commitment*. Huku ndani hakuna hata mahali pamoja palipoandikwa hayo aliyosema. Sasa mimi naomba nipate *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba haya aliyoyasema humu ambayo yameingia kwenye *Hansard* ndicho kitakachotokea kwa *selander bridge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Madabida nilieleza kwamba daraja la selander tunafahamu ni muhimu sana katika kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam. South Korea wameonesha *interest* kubwa sana ya kutengeneza daraja lile. Sikutaka kuweka hapa *commitment* ya fedha kwa sababu inaweza ikawa ni *grant* na mara nyingi katika fedha ambazo zinatolewa inaweza ikawa msaada, huweza ukaanza kusema kwamba ni kiasi fulani. Tumeiweka *open* na ndiyo maana katika fedha ambazo tumeziweka hapa, katika ukurasa wa 119 na ukurasa wa 205, fedha zile za *selander bridge* zitakazohusika pale tumeziweka. Pia katika upanuzi wa barabara ambao utatoka Mwenge hadi Morocco ambao unafadhiliwa na Wajapani, pia nao walikuwa wana-*interest* ya daraja hilo. Sasa hatukutaka kuyazungumza haya kwa kuwagombanisha wafadhili. Naomba Mheshimiwa Madabida aamini

kwamba lile daraja la *selander* ni muhimu katika kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam na ndiyo maana na sisi tumelieleza na hata haya ninayoyaeleza yanakuwa *recorded* kwenye *Hansard*. Kwa hiyo, achukue hizi *Hansard* nazozungumza leo kwamba Serikali iko *serious* kulipanua daraja *selander.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia juu ya kusuasua kwa barabara za Mkoa wa Katavi. Mkoa wa Katavi ndiyo Mkoa pekee ambao hauna barabra hata moja ya lami. Namuomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina, ni lini ujenzi wa barabara Sumbawanga – Kanazi – Kizi – Kibaoni – Stalike – Mpanda utakamilishwa kwa ujenzi wa lami? Pia naomba nipate ufafanuzi wa kina, ni lini barabara ya Mpanda – Mishamo - Uvinza itaanza kutengenezwa? Ni lini barabara inayofungua Mkoa wa Katavi kwenda Mkoa wa Tabora, barabara ya Mpanda – Inyonga - Koga – Sikonge –Tabora itajengwa? Naomba anipe majibu ya msingi vinginevyo kama sitopata majibu ya msingi, nakusudia kutoa shilingi ya Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu niliyoisoma jana nilieleza kwamba katika barabara ya kutoka Sumbawanga – Mpanda – Uvinza, zimetengwa shilingi milioni 28,858.72. Nilieleza shilingi milioni 8,850.94, ni kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga – Kanazi, shilingi milioni 8,850.94 ni kwa ajili ya sehemu ya Kanazi – Kizi – Kibaoni na shilingi milioni 6,617.63 ni kwa sehemu ya Kizi – Stalike – Mpanda na shilingi milioni 4,539.21 ni kwa ajili ya sehemu ya Mpanda – Mishamo na nikaeleza tenda zimetangazwa wiki iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa akitoa shilingi maana yake hizi shilingi bilioni 28.858 zikosekana kwa watu wa Mpanda ambapo Serikali imeanza kufanya kazi? Mheshimiwa Kakoso, naomba ujikosoe hizi fedha usizitoe ili kusudi ziende zikafanye kazi mtani wangu kule kwa wananchi wa Mpanda. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, amekuwa kila mara anatoa majibu mazuri lakini utekelezaji unakuwa tatizo. Nimeeleza huu ndiyo Mkoa pekee ambao hauna barabara hata moja inayounganisha Mkoa hadi Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ni fundi sana wa kuelezea, mimi nataka anihakikishie na awahakikishie wananchi wa Mpanda, wana matumaini makubwa sana na wewe lakini katika utekelezaji umekuwa wa shida, naomba nipate maelezo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile anihakikishie barabara ya kutoka Mpanda – Inyonga ambayo haina fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami, kupitia Koga – Ipole – Tabora ni lini itaanza kujengwa? Barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi na kwa Mikoa mingine ya Mwanza, Shinyanga na hata Geita ambako na yeye yupo, wanakuja kuchukua bidhaa kutoka Mpanda lakini barabara yenyewe haipitiki vizuri. Naomba anipe maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Halafu urudishe shilingi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kakoso, pamoja na Waheshimiwa wananchi wa maeneo hayo kwamba Serikali imejipanga kwa ajili ya kutengeneza barabara hizi. Kuna baadhi ya maeneo wakandarasi wapo. Ndiyo maana nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba barabara ya kutoka Mpanda – Mishamo, kandarasi ameshapatikana. Kwa ile barabara ya kutoka Mpanda - Tabora kilometa 359, mwaka huu tumeweka fedha ambazo zitahusika kulipa *compensation* mara kandarasi atakapotangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amekuwa mstari wa mbele kuzungumza na *African Development Bank* ambao wameonyesha nia kubwa sana ya kutaka kutoa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Ukitoka Tabora hadi Sikonge, tumeshasaini kandarasi na yuko kule kwa ajili ya kufanya *mobilization* kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie wananchi wa maeneo haya kwamba Serikali ime-*determine* kwa ajili ya kuzitengeneza barabara hizi kwa kiwango cha lami. Mimi nimepanga, ikiwezekana hata baada ya Bunge hili, nitaenda kule ili nikazungumze na watani zangu Kifipa namna ya kutekeleza hiyo barabara na Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika barabara husika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye mchango wangu wa maandishi, nilimwomba Waziri anieleweshe barabara tatu, moja nilikuwa ninazungumzia barabara ya kutoka Iringa - Msembe, ambayo inakwenda *Ruaha National Park* na tukizingatia kwamba tunataka kukuza Utalii lakini alipokuwa anajumuisha hakuitaja.

Barabara hii ni muhimu sana kwa wakazi wa Mkoa wa Iringa na Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka pia maelezo ya barabara ya kutoka Musoma – Busekelea - Makojo – Bwasi. Barabara hii iko katika Wilaya ya Butiama, imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi kwa sababu ni eneo la uvuvi na barabara hii inategemewa sana na wananchi hasa magari makubwa na inategemewa pia na Wilaya ya Ukerewe, wananchi wanaokwenda kwenye visiwa vya Ilugwa wanapita barabara hiyo, barabara hiyo pia inaunganisha Wilaya ya Bunda. Sikupata maelezo yake, nimeona ziko fedha kidogo ambazo zimeandikwa kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia Barabara ya tatu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hapana, unazungumzia suala moja tu.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Ya wapi sasa, ile ya Iringa au barabara ile nyingine, ni suala moja tu.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Basi naomba nizungumzie barabara ya utalii ambayo imewekwa muda mrefu lakini hizo nyingine pia azizingatie ziko kwenye maandishi.

**MWENYHEKITI:** Haya Mheshimiwa.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatanieleza vizuri, nitatoa shilingi yake leo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Mheshimiwa Mng'ong'o ataishukuru Serikali kwa kutengeneza barabara ya kilometa 261 kutoka Dodoma – Iringa ambayo ilikuwa *The Great Northern Road* ambayo imetumia mabilioni ya fedha badala yake ameshatishia kutoa shilingi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nachotaka kumueleza, barabara ya Iringa - Msembe, kwa Mheshimiwa Lukuvi, ile barabara tumeipandisha hadhi hivi karibuni. Kuna barabara nyingi za kitaifa kutoka Tabora hadi Ipole, kutoka Songea kwenda Masasi, ambazo ni *trunk road* lakini hazina lami. Mheshimiwa Mng'ong'o ameona barabara ya kwenda Iringa ambayo ni *trunk road* tumejenga kwa lami, anataka kila barabara sasa tujenge kwa lami. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimueleze na mimi nasema ukweli Mheshimwia Mng'ong'o, hii barabara tutaendelea kuitengeneza ili iendelee kupitika kwa kipindi chote. Tukifanikiwa tukapata fedha za kutosha hasa fedha za *Road Fund,* kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii kwa sababu ni ya utalii, tutaitengeneza kwa kiwango cha lami polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata barabara ile ya Musoma – Busekela - Makojo, ile barabara kwa bajeti ya mwaka huu, tumeweka fedha kwa ajili ya kuanza kufanya *design* kwa kiwango cha lami. Tumeanzia pia Musoma kutengeneza kwa kiwango cha lami polepole ili barabara hii nayo itengenezwe na ni muhimu sana katika maendeleo ya wananchi wa kule.

Mheshimiwa Mng'ong'o, naomba usichukue shilingi yangu dada yangu. Irudishe hii shilingi ili tumalize hata barabara hii ya Iringa itakuwa inakusaidia kwenda kutalii vizuri kule unakokwenda. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa rudisha shilingi maana yake…

**M,HE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia Bajeti ya Waziri Mkuu, niliipongeza barabara ya Iringa kwenda Dodoma, ndiyo maana sikurudia kufanya hivyo, nimeshapongeza ni kitu kizuri. Nachokizungumza ni kukuza utalii katika Mikoa yetu.

Hatupati watalii wanaokwenda kwenye *National Park ya Ruaha* na *Ruaha National Park* ndiyo *National Park* kubwa katika nchi zote za Afrika ya Mashariki lakini hatuna watalii, labda sisi Mkoa wa Iringa na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hoteli kubwa zingejengwa kama barabara hiyo ingekuwa imejengwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri akiniambia barabara ya Dodoma – Iringa imeniridhisha, mimi napongeza kabisa lakini naomba niambiwe hii barabra itajengwa lini kwa sababu hii barabara ndiyo itakayoinua uchumi. Nipewe jibu ni lini na sisi tutapata watalii ili mji wa Iringa ukue na wananchi wote tufaidike na Mikoa ya Njombe na Iringa nayo ifaidike. Aniambie ni lini kwa sababu tulishaambiwa *feasibility study* inafanyika itakamilika lini? Mimi akinipa jibu hilo sina shida, nitarudisha shilingi, Njombe pia tutapata nyumba nzuri, watalii watakuwa wengi, tutapata tedha na Iringa tutakuwa pia sawa na Mikoa mengine ya Kaskazini inayopata watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiniridhisha hilo, mimi ninamrudishia shilingi yake lakini sitakubali bila kupata jibu la uhakika.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uhakika Mheshimiwa Mng'ong'o dada yangu atanirudishia shilingi kwa sababu katika ujenzi wa barabara ni lazima uanzie

mahali, ndio maana nimezungumzia barabara ya Dodoma kwenda Iringa ambayo kwa sasa hivi kuna wakandarasa watatu wanaijenga kwa kiwango cha lami. Ile sehemu waliyoitengeneza ya barabara ya kutoka Iringa kwenda Msembe, ni barabara ndogo sana. Ndiyo maana tumeweka fedha za kufanya *design* kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Sasa akinizuia maana yake hata hizo fedha za kufanya *design* ili kuijenga kwa kiwango cha lami nayo itashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mng'ong'o, *one step at a time,* huwezi ukajenga kilometa zote hizi kwa wakati mmoja. Hata angekuwa yeye ndiyo yuko hapa asingeweza. Kwa hiyo, avumilie, ajue kwamba tunaanzia mahali, tunamaliza mahali, tunafanya hivi, huku una *design* huku unafanya *feasibility study.* Mheshimiwa Mng'ong'o, naomba shilingi yangu uirudishe ili kusudi tumalize hata hii kazi ya *design* na barabara hizi ziendelee kutengenezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mng'ong'o, naomba rudisha hela ili tuendelee na kazi.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa lakini naomba wazingatie na sisi tunataka watalii ili miji yetu ikue.

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. DKT. PUNDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kupata ufafanuzi. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa majibu yake ya kuridhisha ambayo ameweza kumjibu kaka yangu Kakoso, kwa jitihada zake na kusema sasa wana mazungumzo na *ADB,* kwa maana sasa napata matumaini na kuona namna gani Wizara kupitia Serikali inaweza sasa ikafanya jitihada za makusudi ili waweze kupata hizo pesa na barabara hii ya Tabora - Mpanda, iwe imekamilika kwa wakati na sisi tuweze kuona rangi nyeusi katika barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hajajibu kuhusu daraja la Kavuu amesema analichukulia *into concern,* sasa sijaelewa *concern* ipi. Kwa sababu leo hii, lile daraja ndilo linalounganisha wananchi wa Tarafa ya Mpimbwe na Tarafa ya Inyonga. Wanalazimika kuja mjini, mji wetu wa Katavi umekaa kama pweza ili utoke Mpimbwe kwenda Inyonga lazima uje Mpanda mjini. Sasa pale ndio kivuko kinachoweza kuwasaidia wale kwenda Makao Makuu ya Wilaya, kwenda hospitali kuu ya Wilaya, shughuli zote za Serikali ziko pale. Kwa hiyo, naomba, kwa sababu mkandarasi yule hajafanya lolote pale, kwanza wananchi hawamtaki, sasa uwapatie majibu wananchi wa Inyonga na Mpimbwe, waone ni kwa namna gani itawarahisishia kupunguza gharama zao za maisha.

Mheshimwia Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandaraasi yuko pale, ameeleza wananchi hawamtaki. Sasa hawamtaki kwa sababu hafanyi kazi au hawamtaki kwa sababu ya sura yake au hawamtaki kwa sababu gani? Nataka nimuahidi Mheshimiwa Dokta Kikwembe, nitakapokwenda Rukwa, nitakwenda pia kumkagua mkandarasi na kwa sababu hapa nina *Contractors Registration Board,* nitaomba tukishamaliza bajeti hii, waende wakamkague yule mkandarasi ana matatizo gani. Kama ananisikia basi abadilike sasa hivi ili wananchi wa pale wampende ili aweze kutengeneza daraja lile linalohusika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkono.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi na pia kwa kusema, nilizungumzia hofu tuliyonayo kuhusu mkandarasi aliyeko kwenye *site* kwenye barabara ya kutoka Makutano - Serengeti. Sijapata maelezo mazuri lakini wananchi wameniomba nieleze na *RCC* pia ilikaa ikaona kwamba huyu mkandarasi hafai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, fedha zilizotengwa ni kiasi kidogo sana kuweza kukidhi mahitaji ya Butiama kwa sababu moja, Butiama sasa imeanza kuvutia watalii, Butiama sasa imepata Chuo na watu watakuwa wanakuja wengi sana pale Butiama. Bila kupata barabara ya kuweza kuwaunganisha hawa watu kutoka kwenye *junction* ya Makutano kwenda Mbugani na kuunganisha na watu kutoka Majita, wanaokuja pale, inakuwa ni kazi bure kuweza kuendelea na huyo mkandarasi aliyepo pale *site*. Bila kupata maelezo mazuri, nilisema nitatoa shilingi lakini nasita kutoa shilingi kwa sasa kwa sababu Serikali imeweka fedha kujenga Chuo pale cha Mwalimu, nikitoa shilingi pengine hata fedha za kwenda kwenye Chuo zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakusihi sana umshawishi Waziri wa Ujenzi aje kwenye *site* pale, amtimue yule mkandarasi, alete mkandarasi mwingine na tuweze kufanya kazi mapema iwezekanavyo. Kama sipati maelezo ya kutosha, basi nitatoa shilingi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Eeeh, haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilifurahia kweli maneno ya mwanzo ya Mheshimiwa Mkono alipoanza kusema kwamba anasita kweli kutoa shilingi. Mimi naomba huohuo moyo wa kusita uendelee kukaa kwenye dakika hizi mbili zilizopo ili asije akatoa ile shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni iliyopo pale ni *GV* ambayo imeanza kufanya *mobilization*. Mkandarasi yeyote anapo-*sign* mkataba na mikataba hii huwa ni ya Kimataifa, muda wa kufanya *mobilization* huwa ni miezi sita. Namuomba Mheshimiwa ajue kuwa yule mkandarasi anafanya kazi na ni mkandarasi huyu ndiye ametengeneza daraja la Mbutu ambalo Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi amepitia pale na limejengwa kwa *standard* nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuahidi Mheshimiwa Mkono, yule ni mkandarasi mzalendo, ukimfukuza maana yake tunakosa na sisi uzalendo. Jambo ninalotaka kukuhakikishia sisi tutamsimamia ili kazi nzuri aliyoifanya katika daraja la Mbutu, daraja ambalo lilikuwa lijengwe kwa zaidi ya shilingi bilioni 25 akalijenga kwa shilingi bilioni 13, aendelee kufanya kule kwa kutumia uzalendo wao kwa sababu ni *combination* ya wazalendo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Mkono atupe muda, zile kilometa 50 za kutoka Makutano - Zanzate ambazo zinajengwa na mkandarasi yule zitatengenezwa. Niamini ndugu yangu hiyo barabara itatenngenezwa na mimi nitapanga muda mzuri au Naibu Waziri, tutaenda kule. Nakumbuka pale Makutano ndiyo siku tulipoweka jiwe la msingi na Mheshimiwa Makamu wa Rais tulipokuwa tukitengeneza kilometa 85 za barabara za lami kutoka Musoma kuelekea mpaka wa Simiyu ambayo nayo ni barabara nyingine. Nakuomba rudisha hiyo shilingi, ule moyo wa kusita ule, usite kweli na Mungu akubariki kweli kwa kusita kwa sababu tunazihitaji hizo hela kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkono, haya rudisha shilingi.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimerudisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina.

**MHE DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mimi sina tatizo na Wizara hii, mimi pamoja na wananchi wa Ngara tunamheshimu sana Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake ila nataka atoe ufafanuzi kwa hoja yangu ambayo niliitoa kwa maandishi, Mheshimiwa Naibu Waziri alijaribu kutoa ufafanuzi lakini hakujibu hoja yangu na wananchi wa Ngara wana hamu ya kumsikia sana Waziri akifafanua yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa ni kwamba tangu bajeti ya mwaka jana, Waziri alihidi kwamba barabara ya Nyakahura – Rulenge - Murugarama ambayo inaunganisha Tanzania na Burundi na ambayo ni muhimu kwa mgodi wa *Kabanga Nickel* ambao ni wa pili duniani, tutakapoanza kuchimba *nickel* barabara hii ndiyo itasaidia kusafirisha *nickel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka jana wakasema, mwaka huu watafanya upembuzi yakinifu na *detailed design* na kwamba mwaka kesho yaani 2014/2015 wataanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Sasa katika kitabu hiki bado barabara hii ambayo ni ahadi ya Rais ya mwaka 2010 iko kwenye *level* ya upembuzi yakinifu na *detail design.* Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi na wananchi wa Ngara wana hamu ya kumsikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nyakahura – Rulenge - Murugarama ambayo kwa bahati nzuri hata Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika Mkoa wa Kagera aliamua kuacha kupita barabara ya lami na akapita hiyo barabara ya vumbi na akafanya mkutano wa hadhara ambapo watu wengi walihudhuria pale Rulenge, aliahidi kwamba barabara hii inafanyiwa *feasibility study* pamoja na *detail design* kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Pia Mheshimiwa Rais aliagiza kwa sababu madini ya *nickel* yako pale na kwa sababu inawezekana reli ikachelewa kutengenezwa, Wizara tuchukue hatua za haraka kwa ajili ya kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Wizara tumeshaanza kuchukua hatua, tunafanya *feasibility study,* tunafanya *detail design,* tumeandika barua kupitia Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuomba fedha kutoka *African Development Bank* na barua tulimpa Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wananchi wa Rulenge na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais na kwa sababu pia ni maeneo ya uwekezaji, itatengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Said Mtanda!

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *at last!* Nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioni hii wakati nikichangia hapa nilielezea hofu yangu na adhabu ambayo wananchi wa Lindi tunapata kwa sababu ya kutokamilika kwa kilomita 12 za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwa sasa ni gumu sana kwa sababu Serikali kupitia vitabu na majibu yaliyoletwa hapa, kwenye vitabu hivi vinaonyesha tumetengewa shilingi bilioni tano lakini mkandarasi yule anaidai Serikali shilingi bilioni 45 na ili barabara hii kwa

awamu hii iweze kujengwa ni lazima zipatikane shilingi bilioni 16 jumlisha hii shilingi bilioni tano iliyoandikwa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi na kama sitaridhika, nitatoa shilingi na ningekuomba jambo hili lijadiliwe humu Bungeni kwa sababu Serikali katika majibu yake imetueleza hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema, Serikali tayari imepata fedha shilingi bilioni 16 kutoka Kuwait Fund. Nia yangu ni kuiuliza Serikali, fedha hizo ziko wapi kwenye vitabu hivi ambavyo tunavisoma na kupitisha bajeti leo kwa sababu toka mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu tunaambiwa Serikali tayari imeshapata fedha ya Kuwait Fund lakini inapokuja kwenye utekelezaji fedha hiyo inaonekana haikutolewa. Kwa hiyo, nataka kupata ufafanuzi, je, shilingi bilioni 16 zilizoahidiwa zipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, Mheshimiwa Waziri wakati wa majibu yake amesema kwamba tuvute subira wananchi wa Kusini, Lindi na Mtwara kwa sababu katika kipindi cha miezi miwili kutoka sasa barabara hii itakamilika lakini mimi binafsi nilivyofanya mazungumzo na mkandarasi Yule, tumekwama wananchi zaidi ya 400 tunakwenda Jimboni, mkandarasi huyu anasema itatumia siku 130 kuweza kukamilisha ujenzi wa kipande hiki endapo atalipwa fedha yake shilingi bilioni 45. Nataka ufafanuzi kutoka Serikalini na nakusudia kushika mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashangaa Mheshimiwa Mtanda kujua mkandarasi anadai shilingi bilioni 45, kwa sababu mpaka sasa hivi mkandarasi yule ameshalipwa zaidi ya shilingi bilioni 45. Sasa anatengeneza kilomita 60 halafu anakwenda anamweleza Mbunge kwamba anadai shilingi bilioni 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nachotaka kusema ni kwamba mkarandasi alichokuwa anadai kwa sasa hivi kwa *certificate* yake kutokana na *report* ya *consultant* anayemsimamia kazi ni shilingi bilioni 1.5 na shilingi bilioni 4.08 tumezishikilia kwa sababu alikosa *guarantee* ya benki. Kwa mujibu wa Sheria, huwezi ukamlipa mkandarasi bila kuwa na *guarantee* ya *bank* na tungekuja kuulizwa hapa na kuhukumiwa. Kwa hiyo, alipokosa *guarantee* ya benki na amekosa *guarantee* ya benki kwa muda wa miaka miwili kwa sababu hakopesheki. Sasa namshangaa mkandarasi ambaye amefilisika anazunguka anasema anadai shilingi bilioni 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni kwamba mkandarasi huyu yuko chini ya mkataba wa *TANROAD* ambao unalindwa kwa mujibu wa sharia, akishindwa kutekeleza kama tunavyozungumza, tunamfukuza na wala sisi hatushindwi kumfukuza mkandarasi, tumefukuza wakandarasi wa kila aina. Kwa hiyo, nachosema ni kwamba naomba Mheshimiwa Mtanda aamini kauli hiyo nayoizungumza, ile barabara ni muhimu. Baada ya mimi kufanya ziara pale, Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri pia walifanya ziara na sisi tumeshapata maelekezo kutoka Serikalini na kwa Mheshimiwa Rais mwenyewe kwamba ni lazima ile barabara tuimalize. Mimi ndiyo maana nimeahidi hapa kwamba ile barabara ni lazima tuimalize mkandarasi afanye au asifanye lakini barabara hii tunaimaliza. Mkandarasi akiboa tunamfukuza ili kusudi aende Mahakamani tutakutana kule Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mtanda, nimeahidi hapa mbele jua linawaka kwamba Serikali haiwezi ikashindwa kutengeneza kilomita saba zilizobaki wakati tumetengeneza kilomita maelfu katika nchi hii. Mheshimiwa Mtanda atuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia hizo shilingi bilioni 16 zimetoka wapi, nimeeleza katika maelezo yangu ya msingi kwamba mradi huu tulipoanza tulipata matatizo mfululizo. Kwanza tuliposaini mkataba ulikuwa ufadhiliwe na *Kuwait Fund* lakini hawakutoa fedha kwa

zaidi ya miaka minne. Baadaye katika mazungumzo ambayo yameanza juzijuzi ndiyo wametoa fedha. Wakati nakuja bajeti hapa nimemuuliza *Chief Executive*, wametoa milioni 10 *point something USD dollars*. Kwa hiyo, hizi zote tutazikusanya na zile tulizoziweka kwenye bajeti hapa zikafanye kazi, tukamsimamie mkandarasi. Kilomita saba zilizobaki hata kama zingekuwa zinatengenezwa kila kilomita shilingi milioni 1,000 zingetumika bilioni saba, sasa bilioni 45 zimetoka wapi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda!

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niseme maelezo niliyoyatoa ni sahihi na maelezo haya pia yalitolewa na mkandarasi kwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Lindi juzi. Kwa hiyo, maelezo hayo niliyoyatoa ni sahihi lakini pili, nachotaka kusema ni kwamba yule mkandarasi anadai bilioni 16 na kwa kuwa *certificate* zake nyingi hakulipwa *plus interest* ndiyo inayofikisha shilingi bilioni 45. Mimi ninaiamini sana Serikali na ninamwamini sana Mheshimiwa Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri anasema katika kipindi cha miezi miwili barabara itakamilika na yeye anasema ni kilomita saba, kwa sisi tunaopita ni kilomita 13 na kwa muda wa miaka sita barabara hii yenye urefu wa kilomita 60 imejengwa, maana yake ni nini? Ni *ratio* ya kwamba kila mwaka ni kilomita 10, kwa hizi kilomita 13 kwa mtindo huo wa miaka sita kwa kilomita 60 maana yake ni mwaka mmoja. Nataka tu nijiridhishe na Waziri awathibitishie Watazania wanaoishi Lindi na Mtwara kwamba katika kipindi hiki atawezaje kumaliza jambo hilo wakati hata kwenye bajeti humu fedha hizo hazipo na kama fedha hizo bilioni 16 zipo kutoka kwa *Kuwait Fund* kwa nini hazijaonyeshwa kwenye vitabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu! *(Makofi)*
**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba umalizie tu!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi yeyote ukimuuliza kwa sababu wako *after profit maximization* anaweza akakuambia anadai hata bilioni 50 au 60. Kila *claim* ya mkandarasi inakuwa *certified* na *consultant* aliyepo kule na ndiyo maana huwa tunaajiri ma-*consultant* na consultant wa mradi huu anaitwa Partman pamoja na *CG Engineering* ya *Kuwait Fund*. Mkandarasi yeyote akifanya kazi ni lazima a-*verify* ametumia *material* gani, ametumia lami kiasi gani, ametumia mafuta gani na ndiyo maana huwa kuna *consultant* anayekaa kwenye *site* kwa ajili ya kumwakilisha *client*. Sasa katika madai sisi tunayoyajua kuna *claims* zake ambazo hazijawa *certified.* Kwa hiyo, hawezi akaenda akazungumza kwamba tunadai kiasi hiki cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mtanda aniamini, nachokizungumza ndiyo hicho. Sisi kama Wizara sio mara ya kwanza kumsimamia kandarasi Kharafi. Tanzania tuna *registered contractors* zaidi ya 7000 na wote tumekuwa tukiwasimamia na makandarasi ukienda vibaya unaumia na ndiyo maana wakandarasi wengine tumekuwa tukiwarudisha kwenye *site*. Mkandarasi wa Kajima katika barabara ya Kilwa ilibidi arudie kwa kutumia fedha zake, mkandarasi CHICO ilibidi arudie barabara ya Sekenke atumie zaidi ya bilioni 15. Kwa hiyo, tunafanya hivi na huyu kumdhibiti ili asije akaona hapa ni mahali pa kufanyia biashara. Alifilisika *of course* palikuwa na matatizo, Baba yake alifariki, kampuni ikaingia kwenye mufilisi, tunacheza naye ili kusudi tuhakikishe eneo letu lile linakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mtanda aniamini kwamba tutamsimamia mkandarasi yule na hasa kuhakikisha kwamba ile barabara inakamilika kwa

kiwango cha lami. Ile barabara madaraja yote ameshamaliza, *subbase* ameshamaliza, *prime* kuna sehemu nyingine ameshamaliza, lami ameshaweka zaidi ya kilomita 50. Kwa hiyo, ukijumlisha eneo lililobaki hasa ukipunguza yale madaraja ambayo ameshayamaliza pamoja na *subbase* na base aliyoitengeneza na *CCR,* tunajua sisi ni kilomita saba lakini ukijumlisha zile ambazo hazijaweka *prime* ndipo zinafika mpaka kilomita 11 au 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba tutaitengeneza ile barabara iweze kupitika kwa sababu ni muhimu na iko kwenye Ilani ya Uchaguzi. Tumetengeneza kilomita 504 za kwenda mpaka Somanga, hatuwezi tukashindwa kutengeneza kilomita saba, niamini Mheshimiwa unirudishie hiyo shilingi tukamsimamie vizuri na hizi fedha zilizopo tukafanye kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda!

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Waziri ninamwamini sana sina tatizo naye lakini pili ningependa *commitment* kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza, tumwamini nani sasa, Waziri anasema miezi miwili barabara itakwisha na huu ni mwezi wa tano, kwa hiyo, mwezi wa saba itakwisha lakini Mjenzi mwenyewe anasema siku 130 ambazo ni sawa na miezi minne. Sasa nataka kupata *commitment* ya Serikali, ni lini sasa *specific* mwezi gani barabara hii itakwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kwa kuwa fedha hizi nyingine zilizotajwa na Naibu Waziri hazionekani kwenye vitabu, hizi dola milioni 10, napenda jambo hili ili nimrejeshee shilingi tulipeleke kwenye Kamati ya Bajeti ili pia jambo hili lisomeke kwenye vitabu kama *commitment* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tumalize hili!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mtanda aniamini mimi kwa sababu mimi ndiye nimemwajiri mkandarasi, mkandarasi ni kibarua wangu kule na mimi ndiye ninamsimamia, kwa hiyo, aniamini mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu zile *commitment* ya zile zilizorudishwa kutoka *Kuwait Fund* kutokana na zile fedha zilizolipwa na Serikali, *I have no problem* na naomba zichukuliwe kwenye *Hansard* kwa sababu ninazungumza hadharani na kwenye *records* zinakuwa *recorded*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda tumalize sasa maana muda wetu umekwisha.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimalize lakini jambo hili ulifahamu, nataka tu kauli moja ya Mheshimiwa Waziri sasa, ni kipindi gani?

**MWENYEKITI:** Hapana, amesema miezi miwili na yeye ndiye msimamizi.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameahidi katika kipindi cha miezi miwili kutoka sasa kilomita 13 zitakwisha, kwenye hili nakubali kumrejeshea shilingi lakini pia jambo hili tulipeleke Kamati ya Bajeti kama nilivyoshauri awali.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) naongeza nusu saa, tuendelee!

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*........Tshs. 764,603,837/=

Kif. 1003 - *Policy and Planning Division*……Tshs. 732,495,339/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit*..............................................Tshs. 320,795,110/=
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*...............................................Tshs. 281,543,220/=
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit*………………...Tshs. 233,488,884/=
Kif. 1007 - *Legal Service Unit*…….................Tshs. 192,323,260/=
Kif. 1008 - *Information Communication Technology*……..............................Tshs. 200,972,108/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2002 - *Technical Service Division*……Tshs. 10,608,016,370/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 270600, *Current Grant to Non-Financial Institution*, kifungu hiki kina kasma vilevile kwa ajili ya fedha za Wakala wa Majengo kwa maana ya *TBA* na Wakala wa Ufundi kwa maana ya TEMESA, bilioni 4.2 na bilioni 6.8 kwa kila mmoja. Kifungu hiki mwaka huu kimeongezeka kwa milioni 700 *plus* na sina tatizo na nyongeza hiyo na sina dhamira ya kuondoa shilingi lakini kwenye mchango wangu wa maandishi niliomba ufafanuzi kuhusu nyongeza hii kwa sababu ni ya matumizi ya mishahara pamoja na mengineyo kwa ajili ya vyombo hivyo viwili nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba ufafanuzi iwapo kwa nyongeza hii, miundo ya kiutendaji ya Wakala wa Ufundi na Umeme itafanyiwa marekebisho ili kuweza kutekeleza majukumu mapana kama ambavyo niliainisha kwenye taarifa yangu? Vilevile niliomba ufafanuzi kama nyongeza hii ya fedha itakwenda kuongeza fedha za matumizi mengineyo kwa Wakala wa Ujenzi wa Nyumba ili kuweza kutekeleza mpango maalum mpana zaidi wa ujenzi wa nyumba kuliko ulivyoainishwa? Sasa napenda kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba hii nyongoza ya sasa ni ya nini hasa na kama itatekeleza yale ambayo nimeishauri Wizara kwenda kuyatekeleza.

**MWENYEKITI:** Mmeiona kwenye randama?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili ni kwa ajili ya mishahara kwa watumishi wa *TBA* na *TEMESA*.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba atoe ufafanuzi tu sina dhamira ya kuondoa shilingi. Kifungu hiki ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, amejibu kama vile kifungu hiki ni kwa ajili ya mishahara peke yake. Kiwango kimeongezeka, atueleze hiyo nyongeza ni kwamba mishahara imeongezeka peke yake au matumizi mengineyo yameongezeka? Kama matumizi mengineyo yameongezeka yanaelekezwa kwenye maeneo gani? Ndiyo jambo nililoomba ufafanuzi, hajajibu kuhusu matumizi mengineyo.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara imeongezeka pia kwa watumishi wa *TEMESA* na *TBA,* kwa hiyo ndiyo maana fedha hizo zimeongezeka.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2005 - *Roads Development Division*...................................Tshs. 540,608,368,510/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru! Nitaomba ufafanuzi na kwa sababu majibu hayatolewi ya kuridhisha, asipotoa majibu ya kuridhisha kwenye hili nitaomba kuondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kasma 270800, *Current Grant to Non-Financial Institution* ambapo mwaka jana kulitengewa shilingi bilioni 353 na mwaka huu ni shilingi bilioni 527, kwa hiyo bilioni nyingi kidogo zimeongezeka. Nimepitia randama ya Wizara na vitabu mbalimbali, hapa kuna fedha za Bodi ya Barabara na ruzuku nyingine, kwa hiyo, ni kiwango kikubwa sana cha pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba ufafanuzi kuhusu masuala kadhaa. Kwenye vyombo vya habari kumejitokeza migongano ya kikauli kati ya *EWURA* na *TRA* na hata waliitwa mbele ya Kamati ya Bajeti na baada ya hapo kukatokea kifo cha Mkurugenzi wa Mafuta wa *EWURA*, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, juu ya kiwango cha fedha ambacho kinaelekezwa kukusanywa kutokea kwenye barabara kwenda kwenye umeme na Mfuko wa Barabara. Safari hii kiwango cha fedha kimeongezwa. Napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya nyongeza hii kama ni kufidia ule upungufu uliojionesha kwenye mwaka wa fedha uliopita ambao Kamati ya Bajeti iliuelekeza au ni nyongeza kwa ajili ya miradi ya maendeleo? Kama ni nyongeza, tungependa kupata *clarity* ya hii miradi iliyoongezeka, kuna maombi ambayo nimepeleka hapo ya mafuriko na maeneo mengine, kama ni kwa ajili ya kushughulikia masuala kama hayo kupitia Bodi ya Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Aah, kwamba ni maendeleo haiwezekani, wewe uulize tu kwa nini zimeongezeka ili waeleze huku, nadhani mengine yote yalikuwa siyo.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya *Amendment Act*, Na. 2 ya mwaka 1998 na mabadiliko yake ya mwaka 2006**.** Mfuko wa Barabara ulipoanzishwa kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge hili, mwanzo kabisa makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 57, yameenda yameongezeka na mwaka jana fedha zilizopitishwa hapa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara zilikuwa shilingi bilioni 504, mwaka huu makusanyo ni shilingi bilioni mia saba na kitu. Nilitegemea kabisa Mheshimiwa Mnyika angepongeza juhudi hizi za Serikali za kukusanya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika fedha zilizowekwa hapa, mwaka jana fedha za Mfuko wa Barabara zilikuwa shilingi bilioni mia tatu na kitu, mwaka huu ni shilingi bilioni mia tano na kitu na ndiyo zilizoongezeka hizi. Katika fedha hizi ambazo zitatumika kwa ajili ya Mfuko wa Barabara ndiyo zimefafanuliwa vizuri katika viambatisho Na. 5A mpaka 5E vya fedha zitakazotumika kwa ajili ya Mfuko wa Barabara kutengeneza barabara *including* barabara za Mheshimiwa Mnyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni jambo la kutambua kwamba kiwango cha fedha kimeongezeka ni kwa sababu ya hatua ya kuongeza kodi kwenye mafuta ya taa ili kupunguza uchakachuaji, ni kiwango ambacho kimeongezeka kwa gharama za walipa kodi wanaonunua mafuta ya taa. Kwa hiyo, ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya walipaji wa gharama hizi ni wananchi wa Dar es Salaam wanaotumia magari na wanaoingia gharama vilevile za mafuta ya taa pamoja na maeneo mengine nchini. Pamoja na nyongeza hii, gharama za ujenzi wa barabara za pembezoni za Dar es Salaam, iwe ni ya Goba, Marambamawili, Kilungule, Msewe, barabara zote hizo kwa ujumla zimetengewa shilingi bilioni 28 peke yake pamoja na nyongeza hii. Kama kuna nyongeza kubwa namna hii tungeielekeza hii nyongeza kwenye kuhakikisha tunatatua matatizo ya barabara siyo Dar es Salaam tu na maeneo mengine ya nchi kwa sababu ni nyongeza kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hivi viambatisho vyote, nitaomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, kutokana na nyongeza hii sasa, hiki kifungu kipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti ili miradi ambayo ni *strategic*, miradi ambayo Serikali iliji-*commit* lakini haijatengewa fedha za kutosha, Bodi ya Barabara iagizwe ielekeze kwenye miradi hiyo. Kwa sababu nyongeza hii ya mabilioni ni kubwa sana lakini ukiangalia kwenye michanganuo viwango sasa kwa miradi ambayo ingesaidia kwa maana ya kupunguza hata foleni Dar es Salaam ni vidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba kuna mradi wa *DART* pale na nini, lakini hii miradi yote inatumia mabilioni ya Benki ya Dunia, bado haitatui tatizo la msingi la kuifungua Dar es Salaam maeneo ya pembezoni na kupunguza foleni. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja na siyo kwa ajili ya Dar es Salaam, bali na wananchi wa maeneo mengine kwa sababu huu ndiyo Mfuko wa Barabara, fedha zimeongezeka tuangalie miradi iongezewe fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba jambo hili lijadiliwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Siyo katika *stage* hii. Katika *stage* hii yeye atuambie hizi fedha zinafanya kazi gani, lakini kwamba tunafungua *discussion* kwa fedha zilizoko kwenye randama, hapana! Naomba Waziri ueleze hizi fedha zinafanya kazi gani, siyo tunaanza kufungua *Pandora's box* jipya hapa, hapa siyo mahali pake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninasikitika sana Mheshimiwa Mnyika hajasoma hii hotuba yangu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA UJENZI:** Naomba nimueleweshe aelewe.

**MBUNGE FULANI:** Subiria.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Amesema kwamba sijasoma hotuba yake.

**WAZIRI WA UJENZI:** Ndiyo umeisoma hujaielewa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Labda useme sijaielewa lakini usiseme kwamba sijaisoma.

**WAZIRI WA UJENZI:** Basi pole sana siku nyingine uwe unasoma unaelewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mnabishana wenyewe, naomba mkae wote.

**MBUNGE FULANI:** Mwenzio kakuvumilia.

**MWENYEKITI:** Mimi nimesimama ninyi mnabishana, naomba mkae. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizoongezeka za Mfuko wa Barabara zimegawanywa katika Mikoa 25 na nimezifafanua vizuri kwenye viambatisho hapa kuanzia Kiambatisho Na.1 mpaka Na. 5E. Kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Mnyika akasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu Dar es Salaam, zile shilingi bilioni 28 zilizotengwa ni *issue* ambayo ni *special* kwa ajili ya kupunguza msongamano wa Dar es Salaam lakini si fedha hizo tu zilizotengwa kwa ajili ya kupunguza msongamano kwa jiji la Dar es Salaam, kuna shilingi bilioni 88 kwa ajili ya barabara ya Mwenge – Tegeta, kuna shilingi bilioni karibu 100 ambazo zitahitajika kutengeneza barabara ya kutoka Rangi Tatu – Gerezani pamoja na *fly over* ya Dar es Salaam, kuna shilingi bilioni 214 ambazo mradi wake unaendelea ka ajili ya kutengeneza daraja la Kigamboni na miradi mingine mingi. Mbali ya hivyo tukachukua hizi barabara za pembezoni ambazo katika bajeti ya mwaka huu tumeziwekea shilingi bilioni 28 wakandarasi wanaanza na mwaka jana tuliziwekea fedha ambazo jumla yake ni karibu kilomita 109, tutaendelea tena katika mwaka mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akizungumza hizi fedha za *Road Fund* ambazo zingine zimegawiwa Njombe, Geita, Ruvuma na wapi zitolewe zote zipelekwe Dar es Salaam, *is unfair*. Akizungumza kuhusu miradi ya *BRT* kwamba ni ya *World Bank*, Tanzania tumekopa, maana yake ni kwamba hata wa Kigoma watalipia, hata wa Njombe watalipia, hata wa Kilimanjaro, hata wa Ilembura watalipia, hata wa kule Rukwa ambako wamekosa barabara ya lami watalipia kwa ajili ya miradi ya *BRT*, fedha ambazo zinauja kutengeneza Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mnyika awe *fair* kwa Watanzania wengine ambao wamezaliwa hawajawahi kuona lami. Hizi fedha zinapopatikana hizi za *Road Fund* zinakwenda kusaidia kazi kule. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa anachokisema hapa hiyo siyo *debate*, suala kubwa ni kwamba hizi fedha zinafanya kazi gani. Hilo ndiyo suala la hapa, siyo suala la kwamba mnaanza kutoa fedha hapa mnapeleka sijui wapi, sivyo! Wala hakuna hoja, Mheshimiwa Mnyika jibu, hakuna hoja ya kuendelea, maana tutaingia kwenye *guillotine* sasa hivi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi sikusema hizi fedha ni kwa ajili ya Dar es Salaam peke yake, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri asipotoshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili hasara ya kutopunguza msongamano Dar es Salaam ni kwamba Taifa linapoteza kwa sekta binafsi na sekta ya umma shilingi trilioni 1 (bilioni 1000) ambazo kama tukiharakisha kutatua tatizo la foleni Dar es Salaam tutaweza kuharakisha kwa muda mfupi sana kujenga barabara za nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nachoomba kupata ufafanuzi ni kwamba, kama kuna nyongeza kubwa hivi ya fedha, ukipitia kwenye vitabu vya mgawanyo wa fedha hata vya Mikoani, mgawanyo haulingani na nyongeza iliyoongezeka. Ndiyo maana mimi rai yangu ni kwamba, sehemu hii kwa sababu fedha imeongezeka kwa mabilioni mengi, Kamati ya Bajeti ikafanye mapitio ilinganishe kati ya orodha siyo ya Dar es Salaam tu bali ya Mikoani na kwingineko na hii nyongeza hapa ili tuhakikishe kwamba fedha zinakwenda kweli kujenga barabara za mijini na vijijini kupitia Bodi ya Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo rai yangu, naomba jambo hili liamuliwe.

**MWENYEKKITI:** *Budget Committee* itafanya kazi yake na iko kazini huko, kifungu kinaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 5002 - Safety and Environment Division......................................Tsh. 614,495,015/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

*Kif. 1003 - Policy and Planning Division ……….……….................Tsh.539,701,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2002 Technical Service Division……...Tsh.15,294,000,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murji.

**MHE. HUSNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 2002, item 4125, Ferry, Ramps and Vending Machines*. Nilitaka kujua, tulikuwa na ahadi ya kivuko cha kutoka Mtwara kwenda Msanga Mkuu, lakini hapa sasa naona hizi fedha zilizotengwa mwaka 2013 na mwaka 2014 zinafanana na hiki kivuko bado hakijaisha. Nataka kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kivuko gani hicho?

**MHE. HUSNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko cha kutoka Mtwara kwenda Msanga Mkuu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko cha Msanga Mkuu ambacho kwa sasa hivi kinatengenezwa katika Bandari ya Dar es Salaam kitakamilika hivi karibuni na kwa sasa hivi tumeshatengeneza *Ramp* kwa maeneo hayo, baada ya kukamilika tu tutakipeleka kule kwa ajili ya kufanya kazi katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hizi fedha siyo zenyewe?
**WAZIRI WA UJENZI:** Ndiyo, zenyewe ilikuwa ni katika bajeti ya mwaka jana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hii siyo fedha yenyewe. Kulikuwa na Mheshimiwa mwingine alisimama, Mheshimiwa Mponda.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Subvote* 2002, kifungu 4144, hizi fedha zilizotengwa shilingi bilioni 2 zimejumuisha na ukarabati wa MV. Kiu pale Mto Kilombero. MV. Kiu kwa mujibu wa *Road Board* ya Mkoa wa Morogoro mwaka 2013 ilikuwa *disposed for sale*. Boti hii kazi yake kubwa ilikuwa kusukuma kivuko ambacho hakina mashine ya kujiendesha yenyewe (jenereta au injini). Sasa nashangaa hizi fedha kwa nini zimewekwa tena kukarabati MV. Kiu wakati ilikuwa *disposed for sale?* Naomba kama inawezekana fedha hizi zisitengwe zipelekwe kukarabati au kuongezea ujenzi wa daraja la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Hizi fedha ni za kitu gani, naomba utuambie.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizotengwa ni kwa ajili ya MV Magogoni shilingi milioni 660, MV Mwanza, shilingi milioni 500, MV Kiu shilingi milioni 400 na MV Pangani shilingi milioni 472. Kwa hiyo, hizo shilingi milioni 400 za MV Kiu tuliona itengenezwe kwa sababu kutokana na utafiti wa wataalam *(mechanical engineers)* wa *TEMESA* wameona hii feri inaweza ikatumika kwa ajili hata ya uokoaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi, maji mengi yanapita kwa *speed* kubwa, tumesimamisha kivuko cha MV Kilombero kwa sababu ni hatari. Hii ni kutokana na sababu kwamba hatuna hata kivuko kingine ambacho kingeweza kutumika kwa ajili ya uokoaji kama matatizo yangeweza kutokea. Ndiyo maana tukasema tutenge shilingi milioni 400 kivuko hiki cha MV Kiu kitengenezwe kiendelee kufanya kazi pamoja na kivuko cha MV Kilombero lakini pia na ujenzi wa lile daraja la Kilombero ambalo lina-*cost* shilingi bilioni 53.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2005 - Roads Development*
*Division ……….……............Tsh.640,278,990,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer, atafuatia Mheshimiwa Cheyo na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho cha 2005, kifungu kidogo cha 4115, Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga/Sanya.

**MWENYEKITI:** Naomba urudie tena tuwe pamoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Kifungu hicho cha 2005, kifungu kidogo cha 4115 Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga/Sanya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni mwaka wa nne sasa imekuwa ikitengewa fedha lakini hakuna kinachofanyika. Naomba kujua kwamba, hizi fedha zitakwenda kufanya kazi ya kujenga barabara hiyo au itakuwa ni maandishi tu kama miaka mingine iliyopita? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Laizer kwamba fedha hizi zitahusika katika kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Barabara mpaka Kamwanga kule juu ni kama kilomita 75 na tumeshatangaza tenda kwa ajili ya kutengeneza kwa kiwango cha lami. Barabara hii inamhusu Mheshimiwa Laizer pamoja na Mheshimiwa Mwanri, ambayo wameipigania sana kwa ajili ya wananchi wa kule kwa sababu sehemu ile ndiyo sehemu pekee iliyobaki kwa ajili ya kuunganishwa barabara ikatokezee kwa Mheshimiwa Selasini. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ile barabara inatengenezwa kwa kiwango cha lami na ndiyo maana katika mwaka huu tumetenga hizi fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer ulikuwa unauliza tu na kama unauliza tu haurudii mara mbili. *Unless* kama umetoa shilingi ndiyo unarudia lakini kama umeuliza tu ndiyo basi. Haya Mheshimiwa Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kasma 4162 ambayo ni mradi wa Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi Road. Tangu mwaka 2005 tunazungumza juu ya mradi huu. Nimeona na tunashukuru kwa kidogo kilichowekwa na sasa shilingi bilioni 10. Sasa kweli ndugu yangu shilingi bilioni 10 zitalipa madeni yaliyopo na kuanza kujenga kutoka Mwigumbi kupita Maswa kupita Luguru mpaka Bariadi na – Lamadi, itawezekana kweli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inaanzia Lamadi – Bariadi - Maswa - Mwigumbi. Katika upande wa kutoka Lamadi – Bariadi kilomita 71.9, mkandarasi anafanya kazi, Mheshimiwa Rais ameshakwenda kuweka jiwe la msingi, madaraja yote yamekamilika mpaka daraja kubwa la Bariadi liko kwenye hatua nzuri za kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kutoka Mwigumbi – Maswa – Bariadi ambako kuna karibu kilomita 100 hivi, tumetangaza tenda ya ile sehemu ya kutoka Mwigumbi – Maswa, mara ya kwanza tulipotangaza *engineers' estimate* ikawa juu kuliko ile fedha iliyokuwa imepangwa. Tumetangaza tena *last week* na tunataka tufanye *fast track* na ndiyo maana fedha zilizotengwa mwaka jana pamoja na mwaka huu ambapo zitakuwa karibu shilingi bilioni 9 katika *section* hiyo moja tu, ukiacha ile ya Lamadi – Bariadi ili tuweze kumu-*involve* kwa ajili ya kuanza kutengeneza kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Cheyo, Mzee wangu na Kaka yangu, hii ni ahadi ya Serikali hata Mheshimiwa Rais alipokuwa katika mji wa Maswa alisema hii barabara lazima ijengwe na ataiweka jiwe la msingi kabla hajaondoka madarakani. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Maswa na wa Mkoa mpya wa Simiyu kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kama tulivyoanza Lamadi – Bariadi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kwangu nilikuwa naomba ufafanuzi kwenye *item 4108* na item number…

**MWENYEKITI:** Ni moja tu.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, hizi ni barabara ambazo ziko pamoja.

**MWENYEKITI:** Sasa wewe uliza kimoja halafu utaunganisha lakini tunaongelea kifungu kimoja. Sasa rudia kile ulichosema.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa naomba ufafanuzi ni kwamba katika Ilani ya CCM…

**MWENYEKITI:** Hatukusikia vizuri ni kifungu gani?

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2005, *item 4108, DSM – Chalinze – Morogoro Express Way*. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kama

kifungu hiki kinahusu pia ile barabara inayotoka Mbwewe – Mziha kule upande wa Morogoro! Ni hilo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri Mheshimiwa Ridhiwani hataniuliza kwa sababu mtoa fedha anakaa naye karibu karibu pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nataka kumhakikishia Mheshimiwa Ridhiwani kwamba fedha zilizotengwa hapa ni kwa ajili ya kujenga kwa njia ya *PPP* barabara ya kutoka Dar es Salaam - Chalinze kwa njia sita. Ile barabara aliyoitaja itatengenezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ambazo tumeziweka kwenye Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee hajasema muda mrefu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Item 4138, *De- Congestion of Dsm Road.* Kwanza, nilitaka kumsahihisha Waziri, hizo shilingi bilioni 88 alizozisema wakati akizungumza na Mheshimiwa Mnyika kwenye barabara ya Mwenge – Tegeta hazipo hapa. Kilichopo ni shilingi bilioni 14, kwa hiyo, asitumie maneno maneno kupotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kifungu nachokizungumzia hapa kinahusu fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kujenga *ring roads*. Mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni 28 na hizo fedha za mwaka jana mpaka sasa hivi hazijatumika. Sasa kwa sababu mwaka mpya wa fedha haujaanza, bado tunatumia mafungu ya mwaka jana, Waziri anithibitishie ili tuongezee hoja ya haja ya hizi barabara kuongezewa fedha kwamba, hizi fedha ambazo tunazitenga mwaka huu hazina uhusiano kabisa na hizi fedha ambazo zilitengwa mwaka jana na ambazo Mheshimiwa Waziri amekiri hapa kwamba mikataba yote imeishasainiwa. Kwa hiyo, kama mikataba imeishasainiwa, tafsiri yake ni kwamba, kwa mafungu ya mwaka jana, wakandarasi wameshaanza kufanya kazi, kwa hiyo, hizi shilingi bilioni 28 ambazo zinaisha katika mwaka wake wa fedha tarehe 30 mwezi wa Sita, zitatumika, halafu mwaka huu sasa ambao tunauanza tarehe 01 mwezi wa Saba tuna hizi bilioni 28.9

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri akinihakikishia hapo nitajua kwamba zile barabara zetu kwa ujumla wake tuna takribani shilingi bilioni 56. Asiposema hivyo tafsiri yake ni yale maneno ambayo tumeyazungumza asubuhi kwamba Mheshimiwa Waziri analeta *figures* nyingi kumbe anachokifanya kikubwa anahamisha *figures* za mwaka huu anapeleka mwaka ujao, anajaza matumaini ambayo hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hiyo *commitment* ya Serikali na kama ikiwa haijitoshelezi tutatoa shilingi ili hii fedha yetu ya mwaka huu ije. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hakuna muda, tuna *guillotine* baada ya dakika moja tu hapa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mdee kwamba mimi huwa sizungumzi kwa kupotosha, huwa nazungumza kwa *facts*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mwenge – Tegeta, ni shilingi bilioni 88 na *contractor* yuko kwenye *site*. Kwa hiyo, hicho ndicho nilikuwa namuelezea, *the total construction cost* kwa barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu hiki alichokizungumza kuhusu barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam zilizotolewa mwaka jana ni *commitment* ya

mwaka jana na ndiyo maana tumesaini mkataba, tusingeweza kusaini mkataba bila kuwa na fedha. Kwa hiyo, za mwaka jana zitatumika kwa mwaka jana, hizi ni *new money, you can add them together to get 56. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murji, dakika mbili kwa sababu tunatakiwa kwenda kwenye *guillotine*.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Niko kwenye *subvote* 2005, item 4143, Ndundu – Somanga Road.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, amepata karibu dola milioni 10…

**MWENYEKITI:** *Sub item* gani?

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub item* 4143.

**MWENYEKITI:** Okay, endelea.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba amepata karibu dola milioni 10 ambazo ni karibu na shilingi bilioni 16 lakini hapa fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 5. Sasa ninataka kujua, je, hizo shilingi bilioni 16 zinaingia wapi au ndiyo hii itarudi kwenye Kamati ya Bajeti? Je, jumla itakuwa ni shilingi bilioni 21 ukiweka pamoja hii shilingi bilioni 5 na ile shilingi bilioni 16?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kujua hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ni wasema ukweli. Nilieleza katika tatizo la mradi wa Ndundu wakati ulipoanza *Kuwait Fund* walikuwa hawatoi fedha, kwa hiyo, tukawa tunatoa fedha *hundred percent* fedha za Serikali. Wiki iliyopita wametoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kufidia zile fedha tulizokuwa tukilipa katika mradi huu. Sasa baada ya kupata hizi, hii ni *addition* ya fedha ambazo zitatumika hapa. Nilitoa taarifa hii na ndiyo maana nataka *records* kwenye *Hansard* ijulikane hivyo, kwa sababu *otherwise* ningenyamaza tu. Kwa hiyo, hizi fedha zote zitaenda kwenye mradi wa Ndundu – Somanga.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 5002 - Safety and Environment*
*Division …….…………...............Tsh.6,121,336,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, basi naomba sasa Makadirio haya yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge lilipitisha Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa Fedha 2014/2015)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi kubwa wanazozifanya. Kama tunavyowasifia basi waendeleze hapo na sisi tunaamini kabisa nchi yetu itang'aa kama wataendelea kutufanyia kazi vizuri na Waheshimiwa Wabunge wote mna wajibu wa kusimamia miradi iliyoko katika maeneo yenu. Hii ndiyo kazi yenu kwa sababu mkifanya hivyo mtatoa changamoto kwa hawa kusimamia kazi, mkisema msubiri tu huku ndani haitoshi, nendeni hukohuko mkabanane nao na msome humu mtakuta wamefanya kazi nzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge naomba nitoe taarifa kwamba kesho kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu hakitakuwepo kwa sababu ana *medical instructions* kwamba akimeza dawa zake saa tatu hapaswi kuja huku. Kwa hiyo, hatutakuwa na kipindi hicho na tutaendelea tu kama kawaida.

Kwa hiyo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.27 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 22 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*